

Kanuni takatifu iliandikwa na Mchungaji Sun Myung Moon huko Korea. Ujumbe wake ulioandikwa kwa lugha ya Kikorea ulitafsiriwa kwa mara ya kwanza kwa Kiingereza na sasa umetafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Kanuni hii takatifu inafungua njia kwa yule anayetafuta majibu ya ukweli kwa maswali mengi ya kimsingi hii si tafsiri rasmi kwa mujibu wa baraza la Kiswahili Bakita na tunaomba kwa unyenyekevu msomaji asiwe mkali hata kidogo katika uwasilishaji na tafsiri, jambo ambalo si la moja kwa moja. kutoka Makao Makuu ya kanisa la umoja, lakini kwa wafuasi rahisi na wa kujitolea wa Baba Moon, wanapotaka kusambaza ujumbe wake kwa watu wanaozungumza Kiswahili. Tunapenda kukualika usome kwa makini kitabu hiki kitakachokupa maono mapya ya ulimwengu. na itabadilisha maisha yako yote.

## GENERAL INTRODUCTION

## UTANGULIZI KWA JUMLA

Tukonainia katika zama mpia. Tukonaingia katika nyakati zahatua haraka ya mpito ; bado, kwa mabadiliko yenye kufanyika katika maisha ya wato binafsi, ma jamaa, jamii, ma taifa, na duniani kote, wengi wekona angaika kuhusu mwelekeo wa mabadiliko haya na kuhisi ya kwamba kuna tena na baadhi ya mabadiliko ya msingi yanayo takiwa kufanyika.

Kanuni*, ambayo imetajwa katika kitabu hiki, ni maono na mwongozoinaowaletea wale ambaye wanataka kungunduwa kiini cha uhai na kuishi maisha ya uhaki. Sisi sote kwa wakati mmoja ama mwingine, tulijuliza maswali kadha za msingi kuhusu Mungu, sisi wenyewe, na ulimwengu. Tena mara kwa mara tulijiuliza siku zetu za usoni zitakuwaje. Maswali ya hivi ni ya kawaida kwa kila mtu. Hata hivyo, majibu yaliotolewa mara nyingi yalikuwa ya sio kutosha. Mu kujibu maswali haya intubidi ku yafikiria kwa kupitia mtazamo mpia ambayo itatupatia majibu yale yatakatutoshea sisi sote. *Muhtasari wa Kanuni* inaelekezwa kwenye kusudi hilo.

Kanuni ni fundisho lile Mungu alimfunulia Mchungaji Sun Myung Moon. Mchungaji Sun Myung Moon hakufundake theologia au falsafa masomoni au kwa mwalimu yeyote. Mungu alimchaguwa juu ya kuonyesha Nia Yake. Bado, ufunuo wakutoka kwa Mungu aupatikane kwa urahisi, kama maji ya mtoni juu ya maporomoko ya maji, wala inayopewa kwa mara moja. Kuna hatua kadha kwa kufungua kwayo,

na inahitaje jibu inayotakiwa toka kwa mtu juu ya kufungukiwa ile kuendelea.

Kwanza Sun Myung Moon aliitwa na Munguwqkqti alikuwa na umri wqa miaka kumi na saba.  Basi, ndivyo alitembea kupitia dunia isioonekana (dunia ya kiroho), ambayo ni dunia chanzo, akitafuta kutatua maswali ya msingi kuhusu maisha na ulimwungu. Ilimbidi kushinda wikwazo vikubwa ndani ya dunia ya kiroho.  Katika utafutaji wa ukweli, alitembea njia ya mateso na kupigana vita ya kutosha damu dhidi ya nguvu za Shetani.  Ni Mungu peke ndio anajua aina ya njia alivyosafiri.  Kwa uhuru aliwasiliana na Yesu na watakatifu katika Paradiso. Katika mawasiliano yake na Mungu, Sun Myung Moon alipokea ufunuo kuhusu vipengele vya msingi vya Nia ya Mungu kwa maisha ya mtu.

Kwa ajili ya kuweka utaratibu na kufundisha ujuzi huu, alitumia ma saa ya siokuhesabiwa katika maombi na kujifunza Biblia.  Ku mwaka 1950, alianza kufundisha rasmi wipande vya muhimu zaidi vya Kanuni kwa wanafunzi wake.  Hata hivyo, mengi katika Kanuni alivyopokea Mchungaji Moon bado isiyochapishwa.  Zaidi ya ufunuo wa Kanuni yatatolewa kulingana na hatua ya maendeleo ya nyakati na maendeleo ya kujengwa kwa msingi duniani.

___________________________________

*  Wakati inachapishwa kwa aina roman, 'Kanuni' inareejea ufunuo alipokea Mcungaji Sun Myung Moon. ( Ona tena maelezo ya chini katika ukurasa 35.)

Maandishi mawili, yenye jina *Wol-li Hae-sul [*Maelezo za Kanuni] (Seoul, Korea : Segye Kidoki=yo Tongil Shillyong Hyophwe, 1957; haijatafsiriwa) na *Wol-li Kang-ron [Majadiliano ya Kanuni]* (Seoul, Korea : Segye Kidokyo Tongil Shillyong Hyophwe, 1966,iliyochapishwa kwa Kingereza kama Kanuni za Mungu, Washington, D.C. : HAS-UWC,

1973) ilitumiwa kuwa mafundisho rasmi ya Kanisa la Umoja. Viliandikwa na Hyo Won Eu, rais wq kwanza wa Kanisa la Umoja la Korea, ambaye aliwahi kumutumkia Mchungaji Moon katika miaka mapema ya huduma wake na ambaye tena alifundishwa moja kwa moja na Mchungaji Moon peke yake.

Kwa ombi la Mchungaji Moon, mfululizo huu, *Muhtasari wa Kanuni,* iliandikwa, kwa msingi wa *Wol-li Kang-ron,* kwa kusudi la kusaidia wasomaji kuelewa Kanuni na kutumiwa kuwa muhtasari wa hotuba. Mimi* nilisoma na hotubiwa juu ya Kanuni kunapita miaka ishirini chini ya uongozo wa Mchungaji Moon. Hata hivyo nikingari na upungufu wa kuelewa kamili Kanuni na uwezo wa kuionyesa kikamilifu. Kwa kukataa kupunguza ukubwa wa thamani ya Kanuni yenyewe, niliandika kitabu hiki kwa maombi. Kama kunakuwa na fujo yoyotr katika uelezo wa Kanuni, ni uajibu wangu mimi peke.

Kulingana na Kanuni, Mungu ni chanzo cha upendo na *moyo.* Msukumo wa Mungu mu kuumba ni kutimiza lengo la upendo – kutimiza lengo lake la upendo ni Kusudi la UUmbaji. Katika dunia ambamo lengo la Mungu linatimizwa, mtu na vitu vyote wataishi katika furaha na maelewano, kwa upendo wa Mungu kuwa chemchem ya maisha na furaha yao. Dunia ambamo nyanja ya upendo timilifu wa Mungu inakamilishwa ni Ufalme wa Mbinguni. Mungu alimuumba mtu duniani, sio mbinguni. Wakati nia timilifu ya Mungu inakamilishwa duniani ndio basi inaitwa Ufalme wa Mungu Duniani. Mtu anatakiwa kuishi katika Ufalme wa Mungu dunianin na tena mtu wa kiroho wake inatakiwa kuingia katika ufalme wa Mungu katika dunia ya kiroho, ambamo ataishi milele (uhusiano kati ya dunia izo mbili unafanana na ule wa akili na mwili ya wanadamu). Ufalme wa Mbinguni ni fasi ambamo mtu binafsi ambaye anakuwa na uzoefu kamilifu wa uoendo wa Mungu anaishi kwa furaha milele katika uhusiano kamilifu wa upendo na Mungu pamoja na watu wengine.

Katika dunia la upendo timilifu ya Mungu, hakuwezi kuwa dhambi, uovu, ukosevu wa haki, ama kujizuia yoyote. Hata hivyo, mwanaume na mwnamke wa kwanza hawakukamilishe uajibu wao, na kutokana na hayo, hawakujikamilishe wenyewe, na waliiacha ulimwengu wa upendo wa Mungu. Ile ndie Anguko, na tokeo lake lilikuwa kwambz dhambi na mabaya ziliingia duniani, na Kuzimu, ambaye ni ulimwengu inje ya upendo wa Mungu, ilikuya kuwepo.

Eti Mungu angeiacha dunia hii ambayo imejazwa na dhambi, uovu, na mateso ? Hapana ; asingeweza kamwe kufanya hivyo. Vile vile alivyosema katika Isaya 46 : 11, " '…naam, nimenena, nami nitatekeleza; nimekusudia, name nitafanya.'" Mungu atamkomboa mwanadamu vile alivyoahidi katika Baraka alivyo mkabidhi baada ya kumuumba mtu (Mwanzo, 1 : 28). Kwa hivyo mpango wa Mungu kwa ukombozi ni, Mbango wa Marejesho, ambamo ataanzisha Ufalme timilifu wa upendo, ambaye ilikuwa Kusudi asilia ya Uumbaji.

________________________________

* Nakala hii iliandikwa katika luga la kikorea na Chung hwan Kwak.

Ukombozi ≡ Marejeano



Dunia la Anguko X Dunia Kamilifu

Kuzimu Mbinguni

Mungu ni mwenye kuwa hai na nguvu za kazi. Zote katika historia na kumbukumbu za watu, riziki za kazi za Mungu ziliacha alama zake. Kisha, ni nini kwa mtu, ambaye ni mtendewa wa riziki ya Mungu alie

hai ;  katika historia mtu alikuwaje ? Katika kila hatua za historia, Mungu ilimbidi kuhusiana na mtu kulingana na kiwango cha hali ya kiroho na akili zake.  Kwani mtu aliwayi kubakiya siku zote vile vile ndani yake, ama alikuwa anaendelea na kujiboresha kila wakati ? kama mtu asikuanguke, angeweza kuonyesha tabia ya Mungu (Yoano, 14 :20) na ukamilifu (Mt 5 :48), na hivyo Mungu angeweza kuwasiliana naye moja kwa moja.  Hata hivyo, Adamu na Hawa walianguka na kuwa mwili moja na dhambi na ubaya badala ya kuwa watu ambaye walikuwa fikirio halisi asilia la Mungu.  Kama tungeweza kusemea namna gani roho na akili ya mtu walioathirika kwa hali hiyo ya utengano na anguko, tungesema kwamba walipunguzwa ku hali ya chini kabisa.

Kupitia Riziki za Mungu za Marejeano, roho na akili ya watu wa anguko zilikuwa zinaboreshwa hatua kwa hatua.  Kwa vile viwango vya roho na akili ya mtu vilikuwa zinaboreshwa hatua kwa hatua katika kila ngazi, Mungu alipata uwezo wa kurekebisha ipasavyo namna za ufundisha watu na kuwasiliana nao.  Kwa mfano, nyakati za Abraham, ambamo hali ya roho na akili za mtu ilikua ikingari chini sana, Mungu alitakiwa kuwaacha watu wamkaribie kwa njia ya utolewo wa sadaka. Watu wa nyakati zile walikua wqchanga sana kuweza kujibu sheria na amri za Mungu.  Ma mia ya miaka baadae, kwa nyakati za Musa,



Abraham Musa Yesu (Yoano 6:25)

Mungu aliendelesha riziki zake za Marejeano kupitia Sheria. Katika nyakati za Yesu, badala ya kurudilia

riziki ile moja mojakupitia Sheria ama Amri, Mungu alitumika kupitia njia mpia kwa kuwakaribisha watu zaidi naye, kwa kuwapa Injili, kulingana na kukuwa kwa roho na akili za watu wa nyakati hizo.

Ukweli wa kwamba wa Yahudi, ambaye walimwamini Mungu kwa hiari, walishindwa kutambua motto wake wa pekee, Yesu, kuwa mwokozi ni hatua muhimu katika Riziki za Marejeano. Kwa sababu gani hawakukuwe na uwezo ya kumtambua ? Kw nyakati hizo, watu wa Israeli walikua wanamfwata Mungu kupitia utiifu kwa Sheria, walakini Mungu alianza kukaribia watu kwa njia ya Yesu pekeyake, kwa njia ya riziki za Injili. Kwa mwangaza wa ukweli huu wa kihistoria, tunaweza kuyaona ya kwamba kulingana na kuendelea kwa roho na akili ya mtu, kila wakati Mungu aliunda njia ya kulingana ilio sawa ya kufikia mtu. Watendewa wa Mungu alie Hai pamoja na riziki zake hawana sawa mafuta, ila tu ni watu ambaye ni wazima na wachapa kazi sana.

Basi, wakati huu wa leo ni nani lengo la mpango wa Mungu ? Aina watu wa wakati a Yesu, wala watu wa nyakati za Musa, wala mtu asiyesahilishawa mno kwa hata kurudi nyuma zaidi. Ni mtu wa kisasa,ule anaeishi hapa na sasa. Bado hatuwezi kukataa ya kama leo mengi kati ya vijana hawavutiwe tena na ma kanisa, na tena watu kwa jumla weko wanageukia mbali na ma kanisa. Mkazo wa mantiki na wa kisayansiya watu wa leo unaomba uelewa wa wazi na wa ndani zaidi wa ukweli na ufafanuzi wa ile inaonekana kuwa utata ndani ya mafundisho na mazoezi kabla y aya wao kufuata njia ya maisha ya kidini. Vile tuliona katika mchakato kihistoria ya marrejesho ya

Mungu, Mungu eko hai na ekonatumika, kwa hivyo tunaweza kujua ya kwamba dhahiri Mungu atampa mtu uelezo mpia wa ukweli, ule ambayo utaweza kuongoza watu wa wakati huu katika wokovu na nyakati mpia.

Leo, maswali mengi ya nguvu yanatokea wakati wa uchunguzi wa Biblia. Kwa mfano, uhusiano sahihi gani uliopo kati ya Mungu, Yesu na mtu ; ni nini uelewa sahihi ya Ufufuo na Siku za Mwisho ; kwa sababu gani Yesu inambidi kurudi ; na wakati gani na namna gani atakaerudi ? Jibu ku maswali haya yote ilisha tolewa kwa mifano na ishara lakini bado inatakiwa kufafanuliwa wazi wazi.

Tunasoma katika Yoano 16 :25 Yesu alisema : '' 'Hayo nimesema kwa mithali ; saa yaja ambapo sitasema nanyi tena kwa mithali, lakini nitawapa waziwazi habari ya Baba.' '' Katika Yoano 16 :12,13 tunasoma ya kwamba alisema tena, ' ''Hata bado nikali ninayo mengi ya kuwaambia, lakini hamwezi kuyastahimili hivi sasa. Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa Kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote ; kwa maana hatanena kwa shauri lake mwenyewe, lakini yote atakayoyasikia atayanena, na mambo yajayo aatawapasha habari yake.' '' Tena katika Ufunuo 10 :11 tunasoma '' 'Wakaniambia, imekupasa kutoa unabii tena juu ya watu na taifa na lugha na wafalme wengi.' ''

Kila katika mafungo haya zinaonyesha kama katika Siku za Mwisho uelezo mpia wa ukweli itapewa.

Hata hivyo, kwa vile ufunuo mpia itapewa, kutakuwa na vipengele kadha ambayo itashindwa kuelewa kwa mwangaza ya mafundisho na utamaduni ya kawaida. Kwa mfano, ingawa mafundisho ya Yesu ilikuwa na msingi wa Agano la Kale, watu wa wakati zake walifungwa katika tafsiri halisi ya Agano la Kale ku kiwango cha kutomwelewa Yesu. Ni kwa sababu hiyo Yesu alitamka kwmaba, '' '….. lakini divai

mpya sharti kutiwa katika viriba vipya.' ''(Luka 5 :38) ; alikuwa anawafundisha kwamba inawabidi kujifanya wenyewe wapya juu ya kupokea maneno ya sasa.

Tunajua kwama Mungu alitumika kwa njia ya Nuhu na Ibrahimu, na tunajua kwamba Mungu alisema kwa njia ya Musa na Yesu. Kwani mpaka Mungu mwenyewe, yule alie hai leo, hawawezi kupasha ufunuo upya ? Kanisa haitaje tafsiri ingine ya kimuntu ya Biblia. Jambo lililo na haja ni namna gani Mungu analitafsiri na tena sisi kutimiza Nia yake kwa kuyikamilisha mu maisha yetu.

Kuna sababu ingine ile watu wanahitaje uelezo wa ukweli wa sasa, na wa ndani zaidi. Tunaweza kuona kuporomoka kwa haraka ya ustaarabu wa kisasa na ili ndani ya jamii bila kuwa na badala ya kuridhisha mbele. Hisia ya utupu, upweke, na kutoridhika iliongoza katika kukata tamaa, fujo, kujitetea, na matumizi mabaya ya pombe na madawa ya kulevya. Fujo kuote katika jamii kuhusu viwango vya thamani na kufanya inasabisha mwenendo wa nguvu kwelekea ubinafsi, na kwa kiisindikiza, kuvunja kwa jamaa na kuongeweka haraka kwa uhalifu, uharibifu kwa watoto, na aina zote za uasherati, ambazo zikonatenganisha msingi za jamii na kusababisha kukosewa kwa tumaini katika siku za baadaye. Vurugu na vita, ambazo zimeenea, na ubaguzi wa rangi, usambazaji wa utajiri usiosawa, upendeleo wa madini za dunia katika uongozaji wa zama za kisasa, pamoja na upanuzi wa Ukomunisti usioamini wote wanaimarisha mashaka kuhusu matarajio ya ustaarabu wa kisasa. Hakuna hata kimoja katika migogoro hizi zote kinaweza kutatuliwa kabisa au hata kipande papo hapo. Suluhisho ya msingi na milele inaitajika. Kwa vile Mungu ni hai, dhahiri wataokoa wanadamu kutoka katika migogoro hizi kwa kupitia mbinu mapinduzi.

Ufunguo wa kutatua kweli au kuondoa hata moja katika matatizo haya ni kufahamu na kuelewa chanzo yayo. Ni kwa vile sababu azikwelewake kabisa kamwe ndio matatizo haya hazikuondoake. Kanuni hueleza sababu hizo na kuleta suluhu za wazi na kwa vitendo ambazo kwa njia ya elimu zinawawezesha watu na jamaa (ambaye ni kiini cha jamii ya watu) badili kwa uhuru na furaha mtindo za maisha.

Kwa watu wa anguko, ufahamu ni upya ya akili na roho ; ujinga ni kifo na uharibifu. Hakuna hisia za usomi zinaweza kutokea katika ujinga, wala nia na tumaini kukua ndani yake. Na ujinga na kutoelewa Mungu ndio inasabisha watu kugeuk mbali na Mungu na kukata tamaa. Kanuni ekonaesha aina paka kwamba Mungu yupo, lakini tena ekonaeleza *Roho ya Asili ya Mungu* na maelezo ya riziki zake vile zinafunuliwa katika historia.

Zaidi ya hayo, inafanya mabadiliko ya tabia kwa wale ambaye wanataka kwa dhati kumpata Mungu kwa njia ya uzoefu wa kiroho na Roho Mtakatifu. Zaidi tutakapopata uzoefu wa upendo wa kweli wa Mungu kwa njia ya Kanuni, zaidi tutakapopata uzoefu wa kuumbwa upya wetu wenyewe. Zaidi, tutanaweza kuendeleza mahusiano ya kimuntu ya kweli na waaminifu na wengine.

Kwa kupitia maendeleo katika maana ya mawasiliano na usafirishaji, na kwa njia ya mawasiliano ya kibiashara na kiutamaduni, dunia ilivutwa kiinje karibu sana ku kiwango cha kuifanya kila taifa inashawishi moja kwa moja ama kwa njia isio moja kwa moja mataifa mengine yote. Hata hivyo, undani wa msingi wa mawasiliano ya kimuntu bado ni kutoaminiana na chuki yasabishayo na ubinafsi na kujipendelea wenyewe. Kwa maneno mengine, licha ya mwenendo wa inje wa kujenga jumuiya ya dunia moja, umoja na maelewano katika hisia halisi havijafanyika. Na ni upendo wa Mungu tu inaweza kutimizisha hayo.

Kanuni ekonafundisha kwamba jamaa ni kitengo cha msingi kinachotakiwa juu ya kamilisha upendo wa Mungu. Tena Kanuni inasisitiza kwamba ni kwa njia ya kutimizisha amri nyumbani ndio upendo unaweza kupandwa ndani ya roho iliokauka ya mtu wa kisasa, na ni paka pale ndie uhusiano wa kweli unaweza kuwekwa kati ya mume na mke wake, kati ya wazazi na watoto, kati ya wandugu wanaume na wanawake, na kati ya wajirani. Upendo kati ya mume na mke wakamilifu ni sharti ya msingi kwa furaha ya wanadamu. Ni paka pale tu upendo wa ile aina unakuwa kati ya wazazi ndio watoto wataweza kuelewa na kupata uzoefu wa upendo halisi kutoka kwa wazazi wao.

Nia halisi ya Mungu ni kwa wanadamu kupenda Mungu kama mzazi wao na kuishi katika undugu kama jamaa moja iliopanuka. Kanuni ni uongozo kwa kuamka kwa upendo halisi wa mtu na kurejesha mawasiliano halisi ya kimuntu ambayo itaunda jamii ya jamaa moja duniani.




Tena, Kanuni inaelekeza ku umoja wa ukweli wa ndani, ambaye ilitafutwa na dini, na ukweli wa nje, ambaye ilitaftwa na sayansi. Sababu Kanuni inaweza ku kufikisha ku umoja ni kwamba ikiwe mmoja anaye husika na maisha ya ndani au ulimwengu, juhudi ya mtu kupata ukweli katika Uumbaji wa Mungu inahusika na Mungu, hata nidhamu na mbinu yoyote.

Dini = Ukweli wa ndani



Sayansi = Ukweli wa nje

Zaidi ya yote, Kanuni itatawala juu ya itikadi ya kikomunisti, ambaye inamkataa Mungu, na itafikisha ku mwisho vit aya kiitikadi katika historia kwa ushindi wa ngambo ya Mungu.  Kukamilishwa kwa riziki ya Ukombozi itajumuisha watu chini ya utawala wa serikali za kikomunisti.  Tena na wao wanapashwa kuwa watu binafsi ambaye watakuwa tabia kamilifu kwa njia ya upendo wa Mungu na Maneno mapya.

Kulingana na Kanuni, dini zote katika historia ambazo zilitafuta na kusisitizanjia ya maisha mwangalifu moja kwa moja au sio yalikuya kuwepo  kwa nguvu za Nia ya Mungu.  Ni kweli kwamba Ukristo unasimama katika nafasi ya kati katika ukamilishaji wa kusudi kwa ujumla la riziki za Mungu.  Hata hivyo, Mungu aliongoza watu toka mataifa mengine kwa kuweka ma dini iliofaa  kwa wakati na mazingira hasa yao kwa ajili ya kuwaandaa kupokea Masihi siku zitakujayo.  Kwa vile Yaono 3 :16 inasema, ‘’ ‘Kwa maana jinsi Mungu aliupendanulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele.’ ‘’ (mkazo huongezeka).  Mungu anamtuma Masihi aina juu wakilisto tuu, ila juu ya wanadamu wote.

Ufunuo ambao Mungu alimpa  Sun Myung Moon ilitolewa kwa kimia kule Mashariki, lakini inawapa matu wanaume na wanawake duniani kote, zaidi wa vijana, furaha na tumaini mpya na kuwapa maisha mapya ndani ya roho zao.  Vijana kutoka zaidi ya mataifa mia moja na ishirini, ambaye wenye kuwa na rangi za ngozi, usuli wa kiutamaduni,

na mitindo ya maisha ya kuachana, wote walikumbatia maisha mapya hii na walipata ,aana mpya na kufuata Nia ya Mungu kwa shauku mpya. Hapa, tunatanguliza muhtasali wa Kanuni, ambaye inakuwa na nguvu ya kuhoja ndani kabisa akili na roho ya mtu na kumbadilisha mtu mtafutaji katika mtu wa tabia mpya unaozingatia Mungu.

## THE PRINCIPLES OF THE CREATION

## KANUNI ZA UUMBAJI

Maswali ya muhimu kuhusu maisha na Ulimwengu hayawezi kutatuliwa bila kuifahamu asili ya Mungu, Muumba. Hii ni kwa sababu ili kuyaelewa na kuyatatua matatizo yahusuyo kiumbe chochote ni lazima kwanza tuelewe chanzo chake. Hivyo, ili tuweze kuyajibu maswali mengi ya msingi kuhusu viumbe vyote, ni lazima kwanza tuielewe asili ya Mungu, Muumba, na kanuni zote alizotumia kuumba Ulimwengu. "Kanuni za Uumbaji" huelezea asili ya Mungu na kanuni hizi, na hivyo basi zajibu maswali ya msingi kuhusu maisha na Ulimwengu wote.

### 1. TABIA MBILI ZA MUNGU NA UUMBAJI (Dual characteristics of God and the creation)

**A.Tabia mbili za Mungu.**

Tunawezaje kujua asili ya Mungu ambaye haonekani ? Twaweza kuijua kupitia kwa uchunguzi wa viumbe. Kama ilivyo kazi ya msanii ni udhihirisho inayoonekana wa asili isiyeonekana wa mtengenezaji wake (inabainisha fikra zake juu ya kitu anachokitengeneza), kila kiumbe katika ulimwengu ni ubainisho halisi wa asili isiyeonekana ya Mungu, Muumba wake. Kama tunavyoweza kuhisi tabia za mwandishi kupitia kazi zake, ndivyo twaweza kuijua asili ya Mungu kupitia viumbe vyake.

Kwa sababu hii , Paulo akasema,

> "Tangu kuumbwa kwa Ulimwengu asili yake isiyoonekana, iitwayo uweza wake wa milele na u-Ungu, vimeeleweka dhahiri ndani ya vitu alivyoviumba. Hivyo, hakutakuwa na msamaha…"
>
> (Warumi 1 :20).

Tutaweza kuielewa asili ya Mungu inafananaje kwa kutafuta tabia ambazo zapatikana kwa kila kiumbe chake.




**Chanzo**

**Tukio**

**Warumi 1:20**

1. ***Tabia mbili ya aina ya Sung Sang (Asili ya Ndani) na Hyung Sang (umbile wa nje)***

Tunaona kwamba viumbe vyote vina tabia isiyoonekana (tabia ya ndani) na inayoonekana (mwonekano wa nje). Sung Sang ni asili ya ndani ama tabia ya kiumbe chochote, ambapo Hyung Sang ni hali ya mada, muundo na umbo la kitu chochote. Sung Sang na Hyung Sang ni misamiati ya kikorea ambayo kiurahisi yaweza kutafsiriwa kama tabia ya ndani na umbo la nje.




Kwa mfano, katika mwanadamu kwa maana rahisi, Sung Sang ni akili isiyoonekana na Hyung Sang ni mwili wenye umbo. Katika wanyama, tabia ya hisia ya wanyama isiyoonekana ndiyo Sung Sang ambapo viungo vifanyavyo mwili wa mnyama ndio Hyung Sang. Katika mimea, uhai na tabia zingine zisizoonekana ndiyo Sung Sang yake, ambapo vitu vingine vilivyotengenezwa na chembechembe hai ndivyo Hyung Sang. Kanuni hiyo hiyo yaweza kutumika kwa viasili. Na tabia ya kikemikali kuwepo ndiyo Sung Sang ya viasili hivyo. Ambapo mada inayoonekana na muundo ndio Hyung Sang yao.

| | | |
|---|---|---|
| Mwanadamu | Roho na Akili | Mwili |
| Mnyama | Hisia ya mnyama | Mwili |
| Mimea | Uhai na tabia zingine | Mwili |
| Milekuli | Tabia asilia | Nishati / matta |
| Chembe | Tabia asilia | Nishati / matta |
| Chembechembe | Tabia asilia | Nishati / Matter |

Katika mwanadamu akili ndiyo mtenda na mshawishi wa mwili kwa hiyo mwili unaenenda kulingana na maelekezo ya akili. Vivyo hivyo, Sung Sang za wanyama, mimea, dutu, atomi na chembechembe huzielekeza na kuzimiliki Hyung Sang zao.

Mwili ambao ni Hyung Sang hudhirisha na kufanana na akili ambayo ndio Sung Sang. Ingawa akili haiwezi kuonekana na ina muundo wake na mwili ambao hutoa picha halisi na hufanana na akili, huchukua umbo la akili hizo.  Akili na mwili ni tabia za ndani na nje za mtu, ambapo akili ni chanzo katika nafasi ya mtenda dhidi ya mwili. Hii ndio sababu mtu aweza kujua vitu fulani kuhusu akili na majaliwa ya mtu mwingine, kwa kuangalia mwonekano wake wa nje.  Kutokana na hayo, twaweza kuelewa kuwa Sung Sang na Hyung Sang ni tabia za ndani na nje za kila kiumbe.  Sung Sang ndicho chanzo na husimama katika nafasi ya mtenda kwa Hyung Sang ; Hyung Sang ni matokeo na husimama katika nafasi ya mtendewa kwa Sung Sang.  Kwa maana hiyo, Hyung Sang yaweza pia kuitwa *Sung Sang ya pili*.  Kwa pamoja twaziita *tabia mbili*.

Kwa vile Mungu ndio Chanzo Asilia cha viumbe vyote na kila kiumbe kina tabia mbili za Sung Sang na Hyung Sang, Mungu lazima awe na Sung Sang na Hyung Sang (Warumi 1 :20).  Sung Sang na Hyung Sang za Mungu zipo katika nafasi ya mtenda kwa Sung Sang na Hyung Sang za viumbe vyote. Sung Sang ya Mungu, ambayo ipo katika nafasi ya mtenda kwa Sung Sang za viumbe vingine, inaitwa Sung Sang asilia, na Hyung Sang yake, ambayo ipo nafasi ya mtenda kwa Hyung Sang za viumbe vyote, inaitwa Hyung Sang asilia.  Ieleweke kuwa inasisitizwa kwamba Sung Sang na Hyung Sang asilia ya Mungu haiwezi kuwapo kama vitu vinavyojitegemea, bali katika mahusiano mema kati ya kila kimoja. Mungu ni mtenda wa uhusiano mwema wa Sung Sang ya asili na Hyung Sang ya asili, na ndiye chanzo cha mwanzo cha Ulimwengu uliopo.

### *2. Aina mbili za tabia za Chanya na Hasi.*

Tunaona kuwa katika Viumbe vyote kuna uhusiano wa kutoa na kupokea kati ya hasi na chanya. Viasili vyenyewe vina tabia za Chanya na hasi*. Kwa mfano, chembe (atoms) zinafanyika kutokana na uhusiano wa kubadilishana kati ya dutu za aina ya chanya na hasi. Chembe zenyewe zina tabia za chanya na hasi. Kwa kufuata msingi wa tabia hizo, viasili viwili ama zaidi huingia katika uhusiano wa kutoa na kupokea na kuunda dutu /milekuli. Mimea ina viasili vya kiume na vya kike. Vivyo hivyo wanyama wengi huzaliana kupitia mahusiano kati ya jinsia mbili tofauti. Wanyama na mimea vyote huwapo huzaliana kwa kupitia uhusiano/uwezo mkuu wa ndani na nje vikitegemeana katika uhusiano wa viasili hasi na chanya. Biblia inasema kwamba Mungu hakuridhika na mume peke yake (mwanzo 2 ;18) hivyo akamfanya mwanamke, Hawa mtendewa wa Adam. Ndipo kwa mara ya kwanza Mungu akaona uumbaji wake ulikuwa '……….mzuri sana'.

Uwanadamu ni wanaume na wanawake, na jamii ya mwanadamu ipo na hukua kupitia mahusiano ya Tendo la Kutoa na Kupokea kati ya mtu mme na mtu mke. Uhusiano kati ya chanya na hasi unafanana na ule ambao upo kati ya tabia za ndani/kiroho na indje/ kimwili.




| Mwanadamu | Mme | Mke |
|---|---|---|
| Mnyama | Dume | Jike |
| Mimea | Viasili vya kiume | Viasili vya kike |
| Milekuli | Chanya | Hasi |
| Chembe | Chanya | Hasi |
| Chembechembe | Chanya | Hasi |

Muundo wa nje .Uchanya na Uhasi vina uhusiano wa kutoa na kupokea wa mtenda na mtendewa, chanzo na matokeo, undani na unje ; hivyo uchanya na uhasi pia kwa pamoja vianitwa tabia mbili. Viumbe vimeumbwa katika jinsi ambayo kila kitu huwapo kwa kupitia mahusiano ya kutoa na kupokea ya chanya na hasi. Sasa ni nini asili ya tabia hizi mbili za chanya na hasi ambazo zapatikana katika viumbe vyote ? Kwa vile viumbe vyote ni matokeo, viasili vinavyofanana kutoka kila kimoja, ni lazima viwe vimetoka asili moja ya msingi, Mungu, muumba. Katika ukweli kwamba viumbe vina tabia mbili za chanya na hasi, inamaanisha kuwa mwenyewe, ambaye ni chanzo asilia cha vitu vyote, ndiye asilia ya tabia mbili za chanya na hasi. Ukweli huu unaweza kueleweka kutoka mwanzo 1 :27, ambao unasema 'Mungu alimuumba mtu kwa mfano wake…………….mtu mme na mtu mke aliwaumba'.







**‘Mtenda‘/‘Mtendewa‘**

________________________________________

***Uchanya na Uhasi, ama Chanya na Hasi, inatumika na maana ya yang-yin (yang-um, na kikorea) sawa na falsafa ya yin-yang. Haimanishi hata kidogo kuwa ni wema na mabaya, uzuri na ubaya, au kujenga = ujenzi na uharibifu.**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **CHANZO** | **Mungu** | **+** | **-** |
| **MATOKEO** | **Viumbe** | **+** | **-** |

Mungu ndiye mwenye Chanya na Hasi zenye thamani halisi ya asilia ambazo husimama katika nafasi ya mtenda kwa Chanya na Hasi zingine zote za viumbe. Tunaziita hizi Chanya na Hasi za Mungu mtenda kama Chanya Asilia na Hasi Asilia. Chanya na Hasi Asilia za Mungu zina uhusiano mzuri ndani yake ; hivyo Mungu ndiye Chanzo Asilia cha kuwapo kwa Ulimwengu na anaendelea kuwapo kama mmiliki wa uhusiano mwema kati ya Chanya na Hasi.

***3. Tabia mbili za Mungu.***

Nini uhusiano kati ya tabia mbili za aina ya Sung Sang na Hyung Sang na tabia mbili za aina ya Chanya na Hasi ? Katika viumbe vyote, tabia mbili za hasi na chanya ama za kiume na za kike, ni ubora wa asili wa Sung Sang na Hyung Sang. Hii inamaanisha kuwa ufahamu na mwili ndivyo vitu muhimu zaidi vya mtu binafsi, na tabia za kiume na za kike ni vitu vya ziada. Kwa maneno mengine Sung Sang ina ubora asilia ulio tabia za chanya na hasi, na Hyung Sang pia ina ubora asilia ulio tabia za chanya na hasi.




Na sasa tuziangalie hizi tabia mbili ndani ya mwanadamu. Kwanza katika akili au Sung Sang, kuna hisia chanya ambayo ni angavu au yenye uhai na kuna hisia hasi ambayo ni kuchanganya mawazo au kupungukiwa msisimko. Kuna akili ya ufahamu iliyo chanya ambayo ina uwezo wa kufikiria, na akili ya ufahamu iliyo hasi, ambayo haina nguvu. Kuna hiari chanya, ambayo huongoza na kuwajibika, na kuna hiari hasi ambayo imelala au haiwajibiki. Pia kuna hali za chanya na hasi katika mwili wa binadamu au Hyung Sang. Sehemu zinazoonekana au zilizotuna, ndizo hali za chanya, ambapo sehemu zilizojificha au bonyea ndizo hali za hasi. Hivyo, tunaweza kuona kuwa Uchanya na Uhasi ni ubora asilia wa Sung Sang na Hyung Sang.




Vivyo hivyo, Uchanya wa asili/Awali na Uhasi wa asili/Awali ndivyo ubora wa asili wa Sung Sang/Awali na Hyung Sang za asili/Awali za Mungu. Kwa ufupi, Mungu ndiye Chanzo cha Kwanza na mtenda mwenye tabia mbili za asili/Awali za Sung Sang na Hyung Sang zilizo katika uhusiano mzuri, na Chanya ya asili/Awali na Hasi ya asili/Awali.




Sasa, nini asili muhimu za Sung Sang na Hyung Sang za asili/Awali za Mungu ? Sung Sang Awali za Mungu ni asili ya Mungu ya kiroho na asili ya isiyoonekana ya ndani ya kila kiumbe : akili ya mtu, akili isiyo na ufahamu ya mnyama/Silika za mnyama, uhai wa mimea, na tabia za kiumbo na kikemikali za madini na viasili. Sung Sang ya asili/Sung Sang Awali ni Akili ya Mungu, ambayo inahusisha maono/hisia, ufahamu wa akili, na hiari, kama dhana na sheria. Hata hivyo, umuhimu mkubwa zaidi wa undani wa Mungu ni Moyo*.

** Moyo (Shimjung, katika luga la Kikorea) ni kiini cha Utu wa Mungu – kiini cha Sung Sang Yake Mungu. Moyo ni sehemu ya muhimu zaidi cha asili Yake, sawa na ubora zingine zote ndani yake ziko vile ziko na zinatenda vile zinazotenda kwa sababu ya ubora wake tu. Moyo ni msukumo wa kupenda na kuunganishwa katika upendo na mtendewa wa upendo wake. Kwa hivyo, Moyo inasemekana kuwa chemchem ya upendo, na kwa wakati mmoja ni sababu kuu nyuma ya upendo.Moyo wa Mungu una ndani yake sababu yake peke ; kwa hivyo ni kwa njiya ya Upendo wa Mungu, kupitiya Moyo wake, ndio Kanuni (Logos = Nembo) walionyesha na Uumbo inakuwepo na hutimiza kusudi lake.*

**Sung Sang Awali**
**Hisia, Akili wa ufahamu, Hiari**

**/Dhana, Sheria**

**Moyo**

**Hyung Sang Awali**

**Nguvu Kuu ya Ulimwengu**




Hyung Sang ya asili/Hyung Sang Awali ni ubora asilia wa nje wa Mungu na asili ya uhalisi na umbo la kila kiumbe : mwili wa mtu, miili ya wanyama na mimea, na uhalisi na muundo wa madini/mada isokaboni. Nguvu Kuu ya Ulimwengu (angalia kifungu kifuatacho) na mada ndivyo viboresho halisi vya Hyung Sang ya asili/Hyung Sang Awali.

**B.Uhusiano kati ya Mungu na Uumbaji.**

Kila kiumbe ni mtendewa halisi wa Mungu, hii ni kuwa, kila kiumbe ni muonekano na namna halisi na haiba ya tabia mbili za Mungu, ambaye yupo kama mtenda asiyeonekana. Wakati ambapo kiumbe kinakuwa mtendewa mkamilifu wa Mungu, mtenda, mapenzi ya Mungu hutimizwa kikamilifu. Kwa maneno mengine, Dunia (Ulimwengu) timilifu ni kama mwili mmoja wa kiumbe hai uliotimilifu na ambao hujongea ama hutulia kwa kuenenda na kusudi la Mungu la Uumbaji.

Japo kuwa viumbe vyote huakisi tabia za Mungu vyaweza kugawanya katika makundi mawili ; (1) Mtu, na viumbe vingine vyote. Mtu ameumbwa kuwa taswira ya Mungu, na hivyo anaitwa mtendewa halisi katika taswira (taswira ya mtendewa halisi) ya Mungu. Viumbe vingine vyote hufanana na Mungu kwa mfano, na

hivyo huitwa mfano halisi wa watendewa wa Mungu.

Mtenda

Mtendewa




Mungu

Watu / Vitu vingine

Watu Vitu

Taswira Mfano/Ishara

Mtendewa halisi yeyote mwenye tabia mbili ambazo hufanana na tabia mbili za Mungu, anaitwa mwili wa kweli. Kama tulivyoona, kila mwili wa pekee wa kweli ndani yake una Sung Sang na Hyung Sang na Uchanya na Uhasi, ambayo hutokana na Sung Sang ya asili, Hyung Sang ya asili, Chanya ya asili na Hasi ya asili iliyomo ndani ya Mungu.

Ngoja tujumlishe uhusiano kati ya Mungu na uumbaji kama inavyotazamwa katika tabia mbili. Viumbe ni mtendewa halisi wa Mungu, vikiwa na miili ya kweli ambayo ni mdhihirisho wa tabia mbili za Mungu katika taswira (mtu) na mfano (vitu vingine vyote).

Sung Sang Awali




Chanzo

Hyung Sang Awali

Madini/Mimea/Wanyama/Watu

Matokeo

Tunapomwangalia Mungu na viumbe kwa ujumla, uhusiano kati ya Mungu na kazi ya uumbaji (viumbe) hurandana na ule kati ya Sung Sang na Hyung Sang. Mungu haonekani, ni chanzo cha ndani na Sung Sang, mtenda wa kiume kwa viumbe ; Uumbaji unaonekana, tokeo la nje na Hyung Sang, mtendewa wa kike wa Mungu.

## II. MSUKUMO MKUU WA KIULIMWENGU, TENDO LA KUTOA NA KUPOKEA, NA MSINGI WA NAFASI NNE

### A. Msukumo mkuu wa kiulimwengu.

Kama Mungu alivyomwambia Musa katika Kutoka 3 :14 'MIMI NDIMI ALIYE !'. Mungu alikuwepo kabla ya muda na uwazi (nafasi na mbingu) na nyuma ya wakati ambao mwanadamu hakuwahi kuona uwazi ambao ulikuwepo awali. Mungu ni wa milele, yupo kwa nguvu zake mwenyewe na pia hakika. Kwa hiyo, msukumo wa muhimu kwa kuwepo kwake na wenyewe ni lazima uwe wa milele,upo kwa nguvuzake wenyewe na ni hakika. Msukumo huu wa asili haukuumbwa bali umekuwepo ndani ya Mungu toka mwanzo, hata kabla ya wakati wa uwazi (nafasi na Ulimwengu). Msukumo huu unaitwa Msukumo Mkuu wa (jumla) kiulimwengu ; ni nguvu za msingi za Mungu, Muumba.  Ni msukumo muhimu wa uumbaji ambao Mungu humpa kila kiumbe,  ama kiumbe cha ukweli cha pekee, wakati  ali umbwa kama mtendewa halisi wa Mungu.

### B.Tendo la Kutoa na Kupokea.

*1. Maana ya tendo la kutoa na kupokea*

Kila kitu ambacho kimeumbwa na Mungu kina tabia za muhimu za Sung Sang na Hyung Sang, na Chanya na Hasi.  Sasa, hizi tabia zipo zenyewe, zimetengana na hazina uhusiano kati yake ama zina uhusiano wa kutoa na kupokea wa aina yake ? Ingawa kila kiumbe chaonekana kuwa huru na vingine vyote, Ulimwengu wote unatokana na uhalisi wa Mungu, ambaye ni wa uhusiano mwema wa tabia mbili za Mungu.  Kwa hiyo kila kiumbe hakipo bila uhusiano na vingine, ila kimeumbwa kuishi katika mahusiano  na viumbe vingine.







Uhusiano  adilifu/bora  unakuwepo wakati mtenda na mtendewa wana uhusiano mzuri wa kutoa na kupokea. Huu uhusiano mzuri wa kutoa na kupokea kati ya mtenda na mtendewa unaanzishwa na Msukumo Mkuu wa Kiulimwengu na unaitwa *Tendo la Kutoa na Kupokea*.  Wakati hali za mtenda na mtendewa katika kiumbe na kati ya viumbe, zinakuwa na uhusiano wa *Tendo la Kutoa na Kupokea*, misukumo yote ya muhimu kwa ajili ya kuwapo, kuzaliana na kutenda kunatokea.

Hebu tuangalie mifano michache. Mwili huifadhi uhai wake kupitia tendo la kutoa na kupokea kati ya mishipa ya damu safi na mishipa ya damu chafu, na kupumua (kuvuta hewa ndani ya mapafu na kutoa hewa chafu nje). Mtu anaweza kufikia kusudi lake la kuumbwa kupitia tendo la kutoa na kupokea kati ya akili na mwili. Familia au jamii huwapo kupitia tendo la kutoa na kupokea kati ya watu binafsi na makundi. Vitu huwapo na huendelea kuwapo wakati ambapo viasili vya mtenda na mtendewa ndani ya vitu hivyo huzaa uhusiano mzuri wa mzunguko na mabadiliko ya kiumbo na kikemia kupitia tendo la kutoa na kupokea. Vyote mimea na wanyama huendeleza kazi zao kwa kupitia tendo la kutoa na kupokea katika viungo vyake mbalimbali na mifumo. Na tunakuta kwamba hata mfumo wa jua na sayari huwapo kupitia tendo la kutoa na kupokea kati ya jua na sayari katika mizunguko yake kwenye njia zake.

Akili = Mtenda




Mwili = Mtendewa




Wazazi = Mtenda

Watoto = Mtendewa

Ma Babu = Mtenda

Wajukuu/vizazi = Mtendewa

Mwalimu = Mtenda

Wanafunzi = Mtendewa




Mwajiri = Mtenda

Employee = Mfanyakazi

Kiini = Mtenda ; Jua = Mtenda

Elektroni = Mtendewa ; Sayari = Mtendewa

***2. Uhusiano kati ya msukumo mkuu wa Ulimwengu na misukumo ya Tendo la Kutoa na Kupokea.***

Misukumo ya tendo la kutoa na kupokea ni misukumo inayotokea wakati mtenda na mtendewa wana uhusiano mzuri wa kutoa na kupokea kati yao. Tendo hili huanzishwa na Msukumo Mkuu wa Ulimwengu, na hivyo huu msukumo ni chanzo na wima na upo katika nafasi ya mtenda kwa misukumo ya tendo la kutoa na kupokea, ambayo ni majumuisho na ulalo na ipo katika nafasi ya mtendewa. Msukumo Mkuu wa Ulimwengu hutoka kwa Mungu na ndiyo msukumo ambao Mungu huelekeza kwa kila kiumbe katika wakati wa uumbaji wake. Misukummo ya Tendo la Kutoa na Kupokea ni misukumo ambayo hujidhihirisha kati ya viumbe na ndani ya kila kiumbe, na ndiyo misukumo ambayo huvifanya vitu vyote kuwapo, kuzaliana na kutenda.

**Chanzo, Mtenda, Wima** **Mungu**




**Tokeo, Mtendewa, mlalo/ Nguvu za Tendo la Kutoa na Kupokea**

Ingawa Msukumo Mkuu wa Ulimwengu ndiyo kiasili cha msingi ndani ya kila kiumbe, hutokana na chanzo kimoja, Mungu. Matokeo yake, viumbe huwa na uhusiano mzuri katika idadi yake kubwa ya

maumbo, bila kujali aina zisizohesabika za Tendo la Kutoa na Kupokea, linatokana na Msukumo Mkuu wa Ulimwengu.

Kwa maneno mengine, kwa njia ya Msukumo Mkuu wa Ulimwengu, Tendo la Kutoa na Kupokea inaelekezwa/ongozwa na uhusiano wa kutoa na kupokea huelekezwa kwa kuunganisha dhumuni na kupitia uhusiano wake mzuri wa kutoa na kupokea kinasaba, hutoa misukumo ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuishi, kuzaliana na tendo la viumbe vyote, kutokea kidogo saana mpaka kikubwa kuliko vyote.

Mwelekeo na matarajio yote ya Tendo la Kutoa na Kupokea yako chini ya udhibiti wa Msukumo Mkuu wa Ulimwengu. Uhusiano wa kutoa na kupokea huwapo sio tu kwamba mtenda na mtendewa huweza kutimiza kusudi la mtu binafsi, bali pia kwa ajili ya dhumuni la kuunganisha vitu vyote. Matarajio ya kusudi la uhusiano wa kutoa na kupokea ni kuwawezesha mtenda na mtendewa kuungana na kuendelea katika kiwango kikubwa cha juu. Muungano huo ambao ni mtenda na mtendewa huwa baada ya kuungana ndipo huangukia uhusiano wa kutoa na kupokea ukiwa na muungano mwingine unaofanana nao katika kiwango hiki kikubwa na kwa kuungana bado hujengeka zaidi katika muungano wa hali ya juu. Hivyo, vitu vyote vimekuwa na makusudi yote ya kujiimarisha na kuimarisha Ulimwengu, kwa hiyo Ulimwengu waweza kuongelewa kuwa ni umbo moja kubwa kinasaba lenye makundi mawili yanayoingiliana na yenye uhusiano mzuri (hili litaelezwa zaidi kwenye kipengele cha ‘Madhumuni ya Uumbaji’)

*3. Uhusiano kati ya Mungu na Mwanadamu katika Tendo la Kutoa na Kupokea.*

Sasa tufikirie uhusiano kati ya Mungu na mwanadamu katika Tendo la Kutoa na Kupokea. Ukweli ni kwamba Mungu alimpa mtu wa kwanza amri zake (Mw. 2 :17) humaanisha kuwa mtu ameumbwa kumwitikia Mungu na kwa kuzitunza na kuziheshimu amri zake. Wanadamu kwa asili walitakiwa kuutunza uhusiano wa tendo la Kutoa na Kupokea na Mungu. Mtu huwa mtendewa timilifu wa Mungu anapofanana na utilifu wa Mungu na Mungu huwa ndani yake (Mt. 5 :48). Hivyo mara anakuwa na uhusiano kamili wa Tendo la Kutoa na Kupokea na Mungu na huwa kitu kimoja katika mapenzi ya Mungu, na Mungu huwa kitovu cha fikra zake, tabia na maisha yake (Yoh. 14 :20). Kama mwanadamu wa kwanza angekuwa na uhusiano wima na Mungu, kupitia uhusiano timilifu wa Tendo la Kutoa na Kupokea naye, ukoo wao pia ungeweza kudumisha Tendo la Kutoa na Kupokea timilifu nae. Kwa njia ya uhusiano wa Tendo la Kutoa na Kupokea wima na Mungu peke yake, watu binafsi wangeweza kudumisha Tendo la Kutoa na Kupokea timilifu kati yao, na kuishi kwa ajili wa wengine, na kwa hivyo kutimiza Ufalme wa Mbinguni duniani. Kupitia anguko la mababu zetu wa kwanza, huu uhusiano wa Tendo la Kutoa na Kupokea na Mungu




ulisitishwa, na hivyo kila mtu hajaweza kuwa na uhusiano mzuri kati yao na Mungu na kati yao na wengine.

Masihi ni mwana wa Mungu na huwa mwili mmoja na Mungu kupitia tendo la kutoa na kupokea lililokamilika. Watu wa anguko wanapaswa kuishi maisha ya imani na kumtumikia Masihi kwa kila hali kama mtenda wao mkuu. Mtu wa anguko anapaswa kuwa mtendewa ambaye anamtumikia Masihi kikamilifu, kwa sababu kwa kuwa na uhusiano wa kutoa na kupokea na Masihi mtu wa anguko huwa mmoja na Masihi ambaye ni mpatanishi kwa Mungu, na hivyo anaweza kuukomboa uhusiano wake wa kutoa na kupokea na Mungu. Kwa hiyo Yesu anaitwa 'mpatanishi' (1Tim 2 :5) na 'njia na kweli na uhai…' (Yoh 14 :6) kwa mtu wa anguko

Kama usemi wa tendo la kutoa na kupokea unavyomaanisha, tendo ni kutoa kwanza na ndipo upokee, na sio kupokea na ndipo utoe. Kutokana na ukweli kwamba Mungu aliumba inaamanisha kuwa alijitoa mwenyewe. Kwa maneno mengine, alijitoa sadaka kwa ajili ya uumbaji wake. Hivyo, ni sheria ya kimbingu kuwa kutoa kunatangulia kupokea. Hata hivyo watu wa anguko hushindwa kurudisha hata baada ya kupokea, na ndivyo njia ya maisha ambayo husababisha matatizo.

Yesu alikuja kutumikia wanadamu kwa upendo na kwa kujitoa sadaka : "…..' Mwana wa mtu alikuja sio kuhudumiwa, bali kutumikia…'" (Mt. 20 :28). Yesu pia alifundisha waziwazi, kuihusu kanuni ya kutoa na kupokea wakati aliposema, " 'usihukumu, usije ukahukumiwa. Kwa maana hukumu uitamkayo, ndiyo utakayohukumiwa nayo, na kwa kipimo kilekile utumiacho kwa wengine, ndicho kitatumika kwako". (Mt. 7 :2) na '……………..kile utakacho utendewe na watu nawe fanya hivyo kwao……………' (Mt. 7 :12).

**C. Asili- Mgawanyiko- Muungano, Dhumuni la Watendewa Watatu na Msingi wa Nafasi Nne.**

*1. Tendo la Asili – Mgawanyiko - Muungano*

Tabia mbili za Mungu, ambaye haonekani kiumbe mtenda huzaa viumbe Mtenda na Mtendewa halisi kutokana na tendo la msukumo mkuu wa ulimwengu, Mtenda na Mtendewa huunda uhusiano wa msingi wa kutoa na kupokea na kujihusisha katika tendo la kutoa na kupokea. Hatua kabla ya tendo la kutoa na kupokea ni kuanzisha uhusiano wa msingi wa kupeana. Inawezekana pale ambapo mtenda na mtendewa wanapoweka umuhimu katika kusudi la jumla zaidi ya kusudi la binafsi. Wakati ambapo mtenda na mtendewa hutekeleza tendo la kutoa na kupokea, huwa kitu kimoja, na hivyo na kuwa na muungano ambao huwa mtendewa mpya wa Mungu. Muungano huu ni uhalisi wa kudhihirisha kuwapo kusudi la jumla, ambalo mtenda na mtendewa wanalo kwa pamoja. Muungano ni tunda ama matokeo yanayotokana na tendo kwa mtenda na mtendewa la viasili vya kusudi katika msukummo mkuu wa ulimwengu. Kwa ufupi, Asili/ Mgawanyiko/ Muungano ni mwelekeo wa maendeleo (kukua) kwa msukumo ambao unaanzia kwa Mungu (Asili) kugawanyika na tena huunganika.




*2. Dhumuni la Watendewa Watatu*

Wakati ambapo kila kimoja kati ya vinne/ Asili, Mtenda na Mtendewa na zao la Muungano wao/ huchukua nafasi ya mtenda kwa vingine vitatu, kiwango cha watendewa watatu huundwa. Halafu, kupitia msukumo mkuu wa ulimwengu kila mtenda hutenda tendo la kutoa na kupokea na watendewa wake watatu na anaungana na kila mmoja akitimiza dhumuni la watendewa watatu.

Kama ilivyo kwisha fafanuliwa, msingi kwa ajili ya kuwapo kwa mtu (kitu) binafsi hauwezi kuanzishwa na huyo mtu au kitu hicho chenyewe.Msingi kwa ajili ya uhai waweza kuanzishwa tu iwapo kuna mtendewa ama mtenda halisi ambao wana tendo la kutoa na kupokea kati yao. Wakati kiumbe katika nafasi ya mtenda kina watendewa watatu kwa dhumuni la tendo la kutoa na kupokea kinakuwa na msingi kamili wa kuwapo. Hivyo, ni kwa kutimiliza dhumuni la watendewa watatu tu ndipo kutamwezesha kiumbe atekeleze dhumuni la kuwapo kwake. Kama Adam na Hawa wangekamilika na kuwa hekalu la asili ya Mungu na pia wangekuwa mtu Mme na Mke na kuzaa watoto wenye wema ndani yao, familia halisi ya wema ingekuwa imeanzishwa. Katika familia ile, Adam, Hawa na watoto wao wote kila mmoja angekuwa ametimiza dhumuni la watendewa watatu. Kila mmoja angefikiria kuwa katika nafasi zake tatu za utendewa Mungu angekuwa wa kwanza ambaye anatakiwa kuwa naye uhusiano wa kutoa na kupokea. Hii ina maana kwamba, mtendewa na mtenda waliogawanyika na muungano wao ni lazima kila kimoja angemweka Mungu katika nafasi ya kwanza ya mtendewa kati ya nafasi zao tatu za utendewa. Kwa kufanya hilo, viumbe vyote vinawekwa katika uhusiano mwema ulioungana kwa dhumuni la Ulimwengu mkamilifu na la jumla.

3. Msingi wa Nafasi Nne

Wakati mgawanyiko wa mtenda na mtendewa, na muungano wao, ambao huwapo kwa kupitia Tendo la Asili- Mgawanyiko- Muungano, wanapotimiza Dhumuni la Watendewa Watatu, wanaunda msingi wa milele wa nguvu. Msingi huu unaitwa Msingi wa Nafasi Nne. Msingi wa Nafasi Nne huundwa ambapo watu wanne - Mungu, Mtenda na Mtendewa waliogawanyika, na Muungano wao- kila mmoja hutimiza Dhumuni lake la Watendewa Watatu. Twaweza kusema kuwa msingi wa Nafasi Nne ni msingi wa uweza ambao hushirikisha mahusiano sita tofauti ya Kutoa na Kupokea.

Msingi wa Nafasi Nne adilifu huanzishwa wakati mtenda na mtendawa wanapoungana kupitia uhusiano halisi wa Tendo la Kutoa na Kupokea, ambao upo chini ya Mungu. Msingi wa Nafasi Nne ni Msingi muhimu unamwezesha Mungu kutenda kazi zake. Pia ni msingi muhimu wa wema ambao kwa huo madhumuni ya Mungu kuumba hutimizwa. Kama itakavyofafanuliwa zaidi hapo baadaye, Kusudi la Mungu la Uumbaji hutimia kupitia Baraka Tatu ambazo Mungu aliahidi kwa mwanadamu, na hili linafanywa kwa kuanzisha Msingi wa Nafasi Nne.

Wakati akili (mtenda) na mwili (mtendewa) ya mtu vinapokuwa na uhusiano halisi wa Tendo la Kutoa na Kupokea (chini ya Mungu (asili)), humfanya mtu mwadilifu, mwenye akili na mwili vilivyoungana (muungano), na Msingi wa Nafasi Nne wa mtu binafsi hutimia.




Mungu

Mtenda / Mtendewa

Muungano

Msingi wa Nafasi Nne

Wakati Mwanaume na Mwanamke wanapokuwa na uhusiano halisi wa kutoa na kupokea, huunda familia ambayo ni mtendewa timilifu wa Mungu, na kiwango cha familia katika msingi wa Nafasi Nne huanzishwa. Wakati ambapo mtu na vitu (viumbe vingine) vinapoingia katika uhusiano halisi wa kutoa na kupokea, viumbe vyote kwa ujumla huwa watendewa timilifu wa Mungu, na msingi wa Nafasi Nne kwa ajili ya utawala wa Mungu huanzishwa. Katika matukio yote, Mungu ni asili na kitovu. Hii ina maana kwamba moyo wa Mungu na nia ya wema ni kitovu. Kwa hiyo, msingi wa Nafasi Nne ni msingi muhimu wa wema ambao hutimilisha Kusudi la Mungu la Uumbaji.










Msingi wa Nafasi Nne pia ni msingi wa mara kwa mara wa tarakimu tatu, nne, saba na kumi na mbili katika Biblia na nyakati za ukombozi (angalia sura za 8/16). Msingi wa Nafasi Nne ni lazima uundwe kupitia hatua tatu za kuwepo Asili Mgawanyiko/ Tendo la Muungano kwa vile kuwapo kwa msingi

wa Nafasi Nne hupitia katika hatua tatu pia kuna hatua tatu katika kipindi cha kukua (angalia kipengele cha IVB), na tatu ni tarakimu ambayo huwakilisha ukamilifu. Kwa kuangalia muundo unaohitajika msingi wa Nafasi Nne una viasili vinne. Huu ni msingi wa tarakimu 'nne' ikiwakilisha muundo unaohitajika ili kudhihirika kwa uhalisi wa Mungu. Kwa vile msingi wa Nafasi Nne una viasili tofauti vinne na hudhihirika kupitia njia ya hatua tatu, pia ni msingi muhimu kwa matumizi ya mara kwa mara ya uwakilisho wa tarakimu 'saba' na 'kumi' na 'mbili' pia ni tarakimu ya mwelekeo tofauti katika uhusiano wa kutoa na kupokea kati ya vitu vinne vilivyomo katika msingi wa Nafasi Nne. Tarakimu 'saba' na 'kumi na mbili' huwakilisha ukamilifu ama utimilifu wa Msingi wa Nafasi Nne.

## III. KUSUDI LA UUMBAJI (The purpose of creation)

### A. Kusudi la Mungu kuumba.

Kila kiumbe kina kusudi lake la kuwapo. Kama kiumbe kitapoteza kusudi lake la kuwapo, chapaswa kutelekezwa. Kama kusudi la kuwapo ni muhimu hivyo, sasa ni nini kusudi la kuwapo kwa mwanadamu ? Kusudi la kuwapo halidhamiriwi na kiumbe chenyewe, bali kusudi lake la kweli linadhamiriwa na muumba wake. Kwa hiyo ni muhimu kujua kusudi la Mungu la uumbaji, ili kuelewa kusudi la kweli la mtu na Ulimwengu wote. Kwa nini Mungu, ambaye ni mwenye uwezo na mkamilifu, alianza kuumba ?




Hali ya muhimu zaidi ya Mungu ni moyo, moyo ni msukumo wa kumpenda mtendewa na ni chemchemi na mhamasishaji wa upendo. Ni asili ya moyo kutafuta mtendewa wa kumpenda. Asili hii ya moyo ni hamasa ya Mungu ya kuumba. Hii ni kwamba, Mungu, ambaye ubora wake muhimu ni moyo, hujisikia raha awezapo kumpenda mtendewa wake aliyemuumba. Kama mtendewa hayupo, Mungu hawezi kuurudisha msukumo wake wa kutoa uangalizi (kutunza) na kupenda (kutoa upendo), ambao hutoka kama chemchemi bila kikomo kutoka ndani mwake mwenyewe. Mungu aliumba ili uumbaji uwe mtendewa wa upendo. Awezao kuupenda.

Twaweza kuona katika mwanzo 1 kuwa alipoongeza kwenye uumbaji wake alisema kuwa ilikuwa nzuri kuangallia/ kutazamwa. Mungu alitaka viumbe vyake kuwa watendewa wa wema na furaha kwake. Sababu aliyotaka uumbaji kuwa mtendewa wa moyo wake ni ili aweze kuvipenda na furaha kwa kuridhishwa kwa kupenda.

**B.Furaha hupatikanaje?**

Tufikirie jinsi tunavyohisi furaha. Furaha haiumbwi na mtu binafsi pekee, bali kupitia kwa mtendewa ambaye huakisi hali zetu wenyewe. Raha huhisiwa kupitia msisimko ambao mtenda huhisi ambapo asili yake mwenyewe huakisiwa ndani ya mtendewa, bila kujali mtendewa anaonekana ama haonekani. Kwa mfano, msanii rangi husikia furaha vyote anapokuwa na msisimko wa maono au wazo kama watendewa wake na ambapo maono yake ama mawazo yanapokuwa mbele yake kama mchoro halisi. Furaha huja kama matokeo ya msisimko unaohisiwa kutoka mtendewa anayeakisi Sung Sang na Hyung Sang za mpaka rangi. Wazo lenyewe linapokuwa mtendewa, msisimko unaotokana na wazo hilo sio halisi ; kwa hiyo, raha




inayotokana nayo hawezi kuwa halisi (timilifu). Kwa mfano, ingawa mchoraji aweza kuhisi raha kutokana na maono au wazo alilo nalo, raha hiyo siyo kamili kama raha ambayo huhisi ambapo kazi iliyokamilika huwakilisha maono yake husimama mbele yake. Tunapokea msisimko imara zaidi kutoka mahusiano na watendewa imara au halisi. Kutokana na hali hiyo tunahisi raha kuu kutoka kwa watendewa ambao ni halisi wenye umbo. Vielelezo hivi ndani ya mwanadamu hutoka kwa Mungu. Kwa hiyo twaweza kufahamu kuwa Mungu huhisi raha anapohisi asili ya Sung Sang na Hyung Sang inayoakisiwa na Viumbe vyake.

**C. Mtu - Mtendewa wa Moyo kwa ajili ya Furaha ya Mungu,Baraka Tatu.**

Uumbaji umefanywa katika taswira ya Sung Sang ya asili na Hyung Sang ya asili. Mwanadamu ni mtendewa halisi katika taswira ya Mungu, ambapo vitu vingine vyote vilivyoumbwa ni vitendewa ambavyo ni mfano wa Mungu. Kwa hiyo mwanadamu ni mtendewa aliye na mwitikio wa kiumbe ambaye yupo karibu sana na moyo wa Mungu.

Mungu alitoa amri (sheria) kwa mababu wa kwanza wa wanadamu, Adam na Hawa, akisema '…..na ya mti wa maarifa wa mema na mabaya msile, siku mtakayokula mtakufa, (Mwanzo 2 :17)'. Hii inaonyesha kuwa Mungu moja kwa moja alitoa mapenzi yake na moyo wake wa upendo kwa mwanadamu. Hakuna sababu kuwa Mungu angetoa moyo wake kwa mwanadamu kama angekuwa amemuumba mwanadamu ambaye hawezi kuhisi moyo wa Mungu. Hivyo twaweza kuelewa kuwa mwanadamu aliumbwa mtendewa ambaye aweza kuelewa na kuitika katika matakwa ya Mungu na moyo na hivyo ni kiumbe kilicho karibu na moyo wa Mungu. Hivyo mtu aliumbwa kama mtendewa ambaye angeupokea moja kwa moja moyo wa Mungu na kumletea furaha. Mtu ameumbwa kama mwana wa Mungu.

Kama ilivyoelezwa tayari, Msingi wa Nafasi Nne ni msingi wa muhimu ambao Mungu anaweza kutenda kazi. Mtu anapotimiza Msingi wa Nafasi Nne kwa kukamilisha Baraka Tatu, chini ya kusudi la Mungu la Upendo, anakuwa mtendewa wa Moyo anarudishaye furaha kamili kwa Mungu. Kwa hivyo Dhumuni la Mungu juu ya mtu inakamilishwa. Mwanzo 1:28 inaonyesha kwa ufupi kusudi la Mungu kwa kumuumba mwanadamu katika kile iitwacho *Baraka Tatu.*




1. Baraka ya Kwanza. (1st Blessing)

Baraka ya kwanza ya Mungu ni uwezo wa mwanadamu kuwa mkamilifu kitabia. Kwa kutenda katika uhusiano mzuri wa Tendo la Kutoa na Kupokea kati ya akili na mwili wake na kuunganisha chini ya uongozi wa Mungu, Mtu huunda Msingi wa Nafasi Nne katika kiwango cha mtu binafsi na huwa hekalu la Mungu (1Wakorintho 3 :16). Wakati watu hao wakamilifu katika kiwango cha mtu binafsi wanapokuwa kitu kimoja (mwili mmoja) na Mungu na katika Moyo (Yoh 14 :20), huja kuwa na tabia ya Mungu, na kwa wakati wote huwa na Mungu katika kitovu cha mawazo yao na matendo yao.

Mtu anapoifanikisha baraka ya kwanza ya Mungu, kwa kawaida atashiriki hisia za Mungu kama zake mwenyewe. Kwa hiyo, itakuwa vigumu mno kwa mtu huyo kutenda uovu, maana kwa kufanya hivyo atahisi huzuni sawasawa kama atakavyopata Mungu. Badala yake, mtu huyo atataka kuwa mtendewa mkamilifu wa Mungu. Mtu anapotimiza ukamilifu wake binafsi, huwa mtendewa kamili wa moyo wa Mungu na huridhisha mvuto wa Mungu katika upendo. Kwa maneno mengine, Mwanadamu, alingetimiza Baraka ya Kwanza, angekuwa mtendewa wa Moyo ambaye Mungu hutamani kupenda. Hivyo angekuwa tunda la upendo wima wa Mungu.

Baraka ya kwanza




- Hekalu la Mungu
- Mmoja na Mungu
- Asili ya utakatifu

*2. Baraka ya Pili. (2nd, Blessing)*

Baraka ya pili ya Mungu ni uwezo wa mtu kupata familia adilifu. Adam na Hawa walihitajika kufikia ukamilifu wa binafsi na baadaye kuwa mume na mke na kuzaa watoto wenye asili ya wema, na kuunda familia isiyo na dhambi. Familia hii iliyo chini ya Mungu katika Msingi wa Nafasi Nne ingekamilisha Baraka ya pili ya Mungu.

Kwa kuwa mume na mke katika msingi wa kujikamilisha wenyewe kupitia upendo wima wa Mungu, Adam na Hawa wangetimiza kwa kukamilika upendo mlalo wa Mungu. Kutokana na mtazamo wa uhalisi wa Moyo, ukweli kwamba Mungu alimruhusu mwanadamu kupata watoto baada ya kutimiza upendo mlalo wa Mungu ni Baraka kuu, kwani kwa kuwa na watoto mtu aweza kuhisi upendo wima ambao Mungu huhisi kwa mwanadamu.

Baraka ya Pili




Kama Adam na Hawa wangefikia ukamilifu, wakaunda familia ya kwanza, na kuzaa watoto wenye asili ya wema, wangekuwa Baba na Mama wa Kweli (chini ya utawala wa Mungu) kwa watu hii ni kwamba, wangekuwa Wazazi wa Kweli wa milele na Mababu wa wanadamu wote, wakiuanzisha Ufalme wa Mbinguni. Kipimo cha msingi cha Ufalme wa Mbinguni ni familia ya kweli, msingi muhimu wa Nafasi Nne.

Familia ya kweli ni msingi muhimu kwa ajili ya upendo wima na mlalo wa Mungu na mtendewa mkamilifu wa Moyo wa Mungu. Kwa kuwapo familia hii ya kweli kama msingi, jamii ya kweli, taifa la kweli na ulimwengu wa kweli vingekuwa vimedhihirika. Hii ndio Nia ya Mungu. Kama Adam na Hawa wangefanya familia na ulimwengu wa namna hiyo, Ufalme wa Mbinguni ungekuwepo hapa Duniani.




- Jamii
- Taifa
- Familia ya Ulimwengu

*3. Baraka ya Tatu. (3rd Blessing)*

Baraka ya tatu ambayo Mungu alimpa mwanadamu ni haki ya kutawala viumbe vyote.  Ili Mungu apate hisia za raha, mtu kama mtendewa wa Moyo Wake, alihitajika kuwa na uzoefu wa raha maishani mwake. Kwa hiyo Mungu aliviumba viumbe vyote kuwa watendewa wa raha ya mwanadamu ili huyo mwanadamu awe na raha siku zote. Kwa maneno mengine, kwa vile viumbe vyote huakisi kihalisi Sung Sang na Hyung Sang ya mwanadamu, ni watendewa halisi wa mwanadamu na mtu aweza kuwa na raha halisi kupitia msisimko wanaotoa.

Kabla ya kumuumba mwanadamu, Mungu aliumba vitu vingine vyote kwa kufuata taswira (mwonekano /mfano) wa mwanadamu.  Kwa hiyo, miundo, uendaji, na tabia za wanyama vimo ndani ya mtu. Kwa nyongeza mwanadamu  ana umbo na tabia za mimea na madini.  Kwa vile vitu vyote hufanana na Sung Sang na Hyung Sang ya mtu, mtu aweza kuvipenda vitu vyote na kuwa na raha kupitia msisimko vinavyotoa. Utawala wa upendo wa mtu juu ya vitu vyote na kuwa na raha kutokana na vitu hivyo ndiko kudhihirika kwa Baraka ya Tatu ya Mungu kwa wanadamu.




Utawala wa Upendo




Mwanzo, 1 :28

Ulimwengu ambamo Baraka Tatu zina timizwa ni ulimwengu mkamilifu ambamo Mungu na mtu, na mtu na ulimwengu mkamilifu, viko katika maelewano (kamilifu) (uhusiano mzuri) yaliotimilika. Ulimwengu wa namna hiyo ni Ufalme wa Mbinguni hapa Duniani. Kama itakavyofafanuliwa kwa undani zaidi hapo baadaye, mtu aliumbwa ili aishi katika ufalme wa Mbinguni hapa Duniani katika maisha ya umoja na Mungu, chanzo cha uhai na wema. Mwili wake unapokufa baada ya maisha hayo Duniani, roho yake itauacha mwili wake na kwenda kwenye ulimwengu wa kiroho. Huko ataishi milele kwenye Ufalme wa Mbinguni, katika utawala wa upendo timilifu wa Mungu.

Ufalme wa Mbinguni unafanana na mtu ambaye amefikia ukamilifu. Ndani ya mwanadamu, amri za akili husafirishwa kwenda mwili mzima kupitia mfumo mkuu wa fahamu na unasababisha mwili kutenda ili kuji dumisha wenyewe.

Amri za Akili

Mwili

Watu




Mapenzi ya Mungu

Watu

Ufalme wa Mbinguni

Vivyo hivyo katika ufalme wa Mbinguni, matakwa ya Mungu hutolewa kwa asili (bila pingamizi) kwa watoto wote kupitia Wazazi wa Kweli, Mababu wa Kweli wa wanadamu, ikisababisha wote kuenenda na kuwa na uhusiano mwema kulingana na uhalisi wa Mungu. Kama ambavyo hakuna sehemu ya mwili itakayo asi amri za mfumo mkuu wa fahamu, mtu mkamilifu hatahisi uadui au uasi dhidi ya utawala wa upendo wa Mungu. Ulimwengu wa namna hiyo usingekuwa na vita/mapigano/uovu wala uhalifu/kuhasimiana.

**D. Ulimwengu ni Mwili Mmoja Uliounganishwa/ulioungana wa Viumbe Vyenye Madhumuni ya Aina Mbili ya Kutegemeana.**

Kila kiumbe kilichopo kina hali mbili : ya ndani na ya nje (Sung Sang na Hyung Sang). Vivyo hivyo, kila kiumbe kina makusudi ya aina mbili, kusudi la ndani (Sung Sang) na kusudi la nje (Hyung Sang). Dhumuni la ndani/Dhumuni la Sung Sang ni dhumuni kwa ajili ya wote, na dhumuni la nje/dhumuni la Hyung Sang (kusudi la nje) ni kusudi kwa ajili ya mtu binafsi. Kusudi kwa ajili ya wote ni kusudi linaloelekezwa kwenye kuuhifadhi, kuiimarisha, na kuendeleza wote. Kusudi la mtu binafsi ni kuhifadhi na kuilinda, na kuendeleza kuwapo kwake. Kusudi la mtu binafsi ni kulinda na kuimarisha kuwapo kwake. Kwa upande mwingine, ana kusudi la maisha kutoa mchango wa aina fulani kwa familia yake, jamii yake, na taifa lake kama mwanachama wa jumuiya hizo.

Sio tu mwanadamu, bali kila kitu kilichoko Ulimwenguni hata chembechembe ndogo sana za viasili zina madhumuni ya aina mbili.  Madhumuni ya binafsi na ya wote (ya jumla) hayajitegemei kwa kila moja kivyake, bali yanahusiana na yanategemeana.

Dhumuni la jumla ni dhumuni la ziada kwa ajili ya ubora wa mtu pia.  Dhumuni la binafsi halijatenganishwa na dhumuni la jumla, na dhumuni la wote haliwezi kuendelea kuwapo bila kuanikisha dhumuni la binafsi. Ulimwengu ni mwili wenye mfumo mmoja uliosukwa kwa madhumuni ya aina mbili.  Kwa hiyo tunauita mwili wenye maingiliano wenye madhumuni ya aina mbili.

**Aina Mbili za Mathumuni**




Kwa madhumuni yote yanayoelekezwa zaidi ya nafsi, dhumuni kuu kwa vyote ni kuhudumia mahitaji ya mwanadamu, kwa maneno mengine, kumpa raha mwanadamu, na dhumuni kuu la mwanadamu ni kumpa raha Mungu. Kwa hiyo mtu na vitu vyote kwa pamoja wana dhumuni la kumhudumia na kumpa raha Mungu.

**IV. KIPINDI CHA KUKUA KWA VIUMBE.**

Mpangilio wa uumbaji wa vitu vyote umehifadhiwa ndani ya kitabu cha Mwanzo sura ya kwanza (Mwa, 1).   Uumbaji wa Mungu ulianza kwa kuumba mwanga kutokana na ukiwa, utupu na giza, na alihitaji muda unaoelezwa kuwa ni ‘siku’ sita, kabla ya kuishia na kumuumba mtu.  Lakini kwa kuwa 2Petro 3 :8 anasema kuwa ‘…………….kwa Mungu siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja’, twaweza kuelewa kuwa hizi siku hazikuwa siku za kawaida  za ma saa ishirini na nne.  Kile kitabu cha Mwanzo sura ya kwanza (Mwa, 1) inachotueleza ni kuwa Ulimwengu mzima haukukamilika/haukukuwapo papo hapo,  kwa mara moja, bali uliumbwa hatua kwa hatua  kupitia vipindi sita.

**A. Kipindi cha kukua kwa viumbe.**

Kutokana na ukweli kwamba ilichukua muda kwa Ulimwengu kuumbwa inamaanisha kuwa kipindi cha kukua kwa kila kiumbe hufikia ukomavu ni muhimu. Kama muda haukuwa muhimu kwa kila kiumbe kufikia ukomavu, hivyo hakuna sababu kwa nini Ulimwengu ulihitaji muda katika kuumbwa kwake. Ngoja tuangalie sababu za nyongeza zinazotufanya tuseme kuwa kipindi cha kukua ni muhimu ili kiumbe kifikie ukomavu.

Kama neno ‘siku’ la sura ya kwanza ya kitabu cha Mwanzo halimaanishi masaa ishirini na nne yaliyozoeleka, hivyo maneno ‘’jioni’’ na ‘’asubuhi’’ hayawezi kutafsiriwa katika ufahamu wa kawaida. Na tuangalie aya hii ya sura ya kwanza ya kitabu cha Mwanzo 1 : ‘Na ikawa jioni na pakawa asubuhi, siku moja’ (Mwa 1 :5). Baada ya hatua moja ya kazi za uumbaji za Mungu idumuyo na kupitia jioni na usiku, kuja kwa asubuhi kulifikiriwa na Mungu kama sehemu ya siku ya kwanza. Ukiendelea na Mwanzo, sura ya kwanza, Mungu alisema, ‘’Na ikawa jioni na ikawa asubuhi, siku ya pili……….siku ya tatu……………siku ya nne…………siku ya tano…………..siku ya sita.’’

‘’Asubuhi’’ humaanisha muda wa kipindi ambacho adili la uumbaji lilitimia. ‘’Jioni’’ humaanisha kipindi ambacho Mungu alimaliza kuumba. Kwa kuijumuisha asubuhi ambayo ilikuwapo baada ya jioni na usiku, Mungu alihesabu vyote hivi kama siku moja. Mungu huonyesha muda unaohitajika kwa ajili ya adili la uumbaji kutimia. Kipindi kuanzia pale Mungu anapoanza kuumba hadi wakati ambapo uhalisi wa Ulimwengu unapodhihirika ni kipindi cha kukua cha viumbe vyote na huwakilishwa na usiku, kipindi kati ya jioni na asubuhi.

Kuanguka kwa mwanadamu kunaonyesha kuwa kuna kipindi cha ukuaji, kwani mtu angekuwa ameumbwa mkamilifu, basi kusingekuwa na uwezekano wowote wa kuanguka kwake. Kama mkamilifu wa wema, anaye fanana na Mungu alikuwa aanguke, kwa hiyo tungehitimisha kuwa wema wenyewe haukukamilika na hivyo kujiuliza kwamba kweli Mungu ni mkamilifu.

Kabla ya anguko, mtu alikuwa hajajikamilisha mwenyewe ; alikuwa akikua kuelekea ukamilifu, na angeweza kuchagua ama njia ya uhai au njia ya mauti (Mwanzo 2 :17). Adili la Mungu juu ya viumbe ni ukamilifu ; hivyo asingeweza kumuumba mtu kuwa wa kutoweza kamilika/mdhaifu. Bado, mtu alianguka ; hivyo ni lazima itakuwa hakuwa amekamilika .Twaweza basi kuhitimisha kuwa alipoanguka, mtu alikuwa kwenye hatua changa/kutokukamilika, katika kipindi alipokuwa akikua kuulekea ukamilifu.




**<u>Mwanzo 2 : 17</u>**

**B. Hatua Tatu za Kipindi cha Kukua**

Kazi nzima ya Mungu ya uumbaji ilifanyika kupitia hatua tatu : jioni, usiku na asubuhi. Msingi wa Nafasi Nne ulijengwa katika hatua tatu za asili, mgawanyiko, na muungano. Vivyo hivyo, kipindi cha kukua kuna hatua tatu : *mwanzo kukua na ukomavu*. Hivyo viumbe vyote huupata ukamilifu kwa kupitia mwanzo kukua na hatua ya ukomavu ambayo inaunda kipindi cha kukua.




Mifano ya tarakimu 'tatu' ambayo inatokea katika Ulimwengu wa asili : makundi matatu ya utawala - wanyama, mimea na madini ; hali tatu za mada - yabisi, majimaji na hewa/gesi ; sehemu tatu za miili ya wanyama wengi - kichwa, kiwiliwili na miguu ; sehemu tatu za mimea – mizizi, shina na majani ; sehemu/safu tatu za udongo - sehemu ngumu ya juu, manto na kiini.

Katika kuanguka kwake, mwanadamu alishindwa kupitia hatua tatu za kipindi cha ukuaji. Kwa vile Biblia ni neno la Mungu la kuwakombolea wanadamu, inajumuisha mifano mingi ya tarakimu 'tatu' : Utatu- Baba, Mwana na Roho Mtakatifu ; hatua tatu za mbingu ; malaika wakuu watatu - Lusiferi, Gabriel, Mikaeli ; watoto wa kiume watatu wa Adam - Kaini, Abeli na Seti ; Watoto wa kiume watatu wa Nuhu - Sham, Ham na Jafeti ; ngazi tatu za Safina ya Nuhu ; aina tatu za sadaka zilizotolewa na Ibrahimu ; siku tatu katika giza nchini Misri katika kipindi cha Musa ; siku tatu za utengano na Shetani katika wakati wa Kutoka ; miaka arobaini mara tatu ya ukombozi wa Kanani ; miaka thelathini ya maisha binafsi ya Yesu na miaka yake mitatu ya huduma kwa umma ; mamajusi watatu na zawadi zao tatu kwa Yesu ; wanafunzi wakuu watatu wa Yesu ; majaribu matatu kwa Yesu ; sala tatu katika Getisemani ; na siku tatu za Yesu kuwa kaburini.

**C. Utawala wa Mungu moja kwa moja.**

Baada ya kupitia kipindi cha ukuaji, mtu hufikia ukamilifu na hapo hapo huishi kwenye *ufalme wa utawala wa Mungu wa moja kwa moja*. Mtu aliumbwa kuwa mtendewa wa Moyo wa Mungu. Ni katika ufalme wa utawala wa moja kwa moja wa Mungu ambamo mtu anakuwa mmoja na Moyo wa Mungu (anakuwawa mtendewa wa Moyo wa Mungu) na Mungu humtawala mtu kwa upendo. Ufalme wa utawala wa moja kwa moja wa Mungu, ni miliki ya ukamilifu, ufalme ambao mtu huufikia baada ya kuji kamilisha mwenyewe ; ni sehemu ambamo mtu yuko chini ya utawala wa kudhibitiwa na Mungu moja kwa moja.



Mtu huingia utawala wa Mungu moja kwa moja anapohitimisha binafsi Msingi wa Nafasi Nne kwa kudhihirisha muungano wa mwili na akili chini ya utawala wa Mungu. Ni katika ufalme wa Mungu wa moja kwa moja ambamo  mme na mke hufanya familia katika Msingi wa Nafasi Nne chini ya Mungu. Hivyo hivyo, ufalme wa utawala wa Mungu wa moja kwa moja ni ufalme ambamo kusudi la kumuumba mwanadamu hutimia.

Mungu aliviumba vitu vyote kwa ajili ya mwanadamu, kuwa chini ya utawala wa mwanadamu. Mtu mkamilifu ambaye yuko chini ya utawala wa Mungu, hutawala vitu vyote vinapokuwa vimepevuka. Huu ni utawala wa moja kwa moja wa mwanadamu kwa vitu vyote. Mungu huvitawala vitu vyote isivyo moja kwa moja kupitia mwanadamu.

**D. Utawala wa Mungu usio wa moja kwa moja.**

Mungu anatawalaje watu na vitu vyote wakati vikiwa katika kipindi cha ukuaji,katika  hali ya uchanga ? Mungu, akiwa mkamilifu, anatawala tu vitu vilivyo kamilika.  Kwa hiyo, watu ambao wako kwenye hali hisiyo kamilifu hawawezi kuwa watendewa wa Mungu. Mungu aweza kutawala sio moja kwa moja, kupitia *Kanuni**. Kwa hiyo, kulingana na hali ya utawala, kipindi cha ukuaji ni *ufalme wa utawala usio wa moja kwa moja.* Mungu kama chanzo cha *Kanuni*, uhusiana na watu na vitu vingine kinyume na moja kwa moja wakati vikiwa vichanga,  (Ɨ) akishughulika moja kwa moja tu na matokeo ya ukuaji kulingana na *Kanuni*, au utawala usio moja kwa moja wa Mungu.

Viumbe vyote mbali na mwanadamu hupitia kipindi cha ukuaji chini ya udhibiti huru  wa *Kanuni*. Mtu, hata hivyo, hawi mkamilifu kupitia tendo la kujitawala la *Kanuni* peke yake, bali pia kwa kutimiliza wajibu wake kwa kufuata amri za Mungu.  Katika kitabu cha Mwanzo 2 :17, Mungu alisema, " '…………….ya mti wa maarifa ya kujua mema na mabaya msile, siku mtakapokula mtakufa.'"  Hii inaonyesha kuwa ni juu ya mwanadamu kutokula matunda na kujikamilisha mwenyewe.  Kutotii kwa mwanadamu kwa neno la Mungu na kuanguka kwa mwanadamu vinafanywa  kwa uhakika na mtu mwenyewe na sio Mungu.




Kwa hiyo, ukamilifu wa mtu hauwezi kukamilishwa kwa wajibu wa Mungu peke yake, hii ni kuwa, kupitia utawala binafsi wa *Kanuni* (u udhibiti wa Mungu katika kipindi cha ukuaji).  Mtu hawezi kufikiria kuwa Mungu atachukua jukumu kwa ajili ya ukamilifu wa mtu yeyote ; mtu atadhihirisha utimilifu wake pale tu atakapotimiza wajibu wake, japo huo wajibu ni mdogo saana unapolinganishwa na ule wa Mungu.  Mtu alianguka kwa sababu alishindwa kutii amri za Mungu.

*Wakati inaindikwa na kuchapishwa katika italiki, 'Kanuni' inarejea sheria ya msingi ya ulimwengu ambayo inatokea kwa Mungu na kukaribia Uumbaji. Neno 'kutokua ndani ya Kanuni' inarejea ukiukwaji ya Kanuni.
(†) Wakati mtu anafikia ukamilifu, Mungu anakaa kati ya huyo mtu (1 Wakorinto : 3:16); hivyo inaweza semewa ya kwamba Mungu kweli huhusiana moja kwa moja na vitu vya ulimwengu.




Baada ya kuona matokeo ya mwanadamu ya kutotimiza wajibu wake - ambao ni, anguko - twaweza kujiuliza barabara kwa nini Mungu alimpa mwanadamu sehemu yake ya kuwajibika. Kwa ufupi, ilikuwa juu mwanadamu afaulu kama bwana wa ulimwengu. Haki ya kweli ya utawala wa moja kwa moja ni ya muumba tu. Zaidi ya hayo, Mungu alimtaka mtu, kiumbe, kuwa na utawala wa moja kwa moja kwa vitu vyote. Ili mtu aweze kuwa na haki ya utawala huu, Mungu alitaka kuwa na mtu, ambaye ni kiumbe, kurithi asili ya muumba. Hii ni kuwa Mungu angepata mtu wa kurithi asili uumbaji wake. Mtu alitakiwa kufanya hivyo kwa hiari akijihusisha kwenye uumbaji wake mwenyewe. Kwa ufupi, mtu hakamilishwi na *Kanuni* ya Mungu na uweza wake pekee. Wajibu wa mtu mwenyewe ni kiasili muhimu, ingawa ni mdogo unapolinganishwa na ule wa Mungu.

Mungu alimpa mtu wajibu ili aufikie ukamilifu. Hivyo, Mungu hawezi kuingilia kati wajibu wa mwanadamu. Mungu alimfanya mwanadamu ashiriki na ashirikiano naye katika kazi zake za uumbaji kwa sababu kwa kufanya hivyo mtu atakuwa mrithi wa haki wa Mungu. Hivyo, wajibu wa mtu ni neema ya thamani anayopewa na Mungu. Bado ni kwa sababu ya kushindwa kukamilisha wajibu wao mababu wahenga wa kwanza wa wanadamu walianguka. Kwa hivyo, wajibu wa mwanadamu ni kiasili muhimu katika nyakati za wokovu, ambapo kupitia wajibu huo Mungu hukomboa mtu aliyeanguka kurudia hali yake ya asili.

Mpango wa Mungu wa kuokoa umekuwa ukirefushwa kwa muda mrefu kwa sababu watu wateule wa vipindi vya Ukombozi wamekuwa wakishindwa kutimilisha majukumu yao, ambayo hata Mungu hawezi kuingilia. Kati kama ilivyoelezwa katika kitabu cha Yohana 3 :18, haijalishi ni kiasi gani cha baraka na upendo Mungu aweza kutoa, wokovu hauwezi kuja kwa wale wasiokuwa na imani. Mathayo 7 : 21 yasema, "'sio kila aniambiaye Bwana, Bwana,' ataingia kwenye ufalme wa mbinguni, bali kila atendaye mapenzi ya Baba yangu aliyeko Mbinguni. Hii yatuambia kuwa mtu atendaye ambayo Baba yake wa Mbinguni anayatamani ni jukumu lake mwenyewe. Kwa nini Mungu mwenye haki asiwape ambao hawaombi ? Kwa nini Mungu asiwezeshe ambao hawatafuti wapate na ambao wasiobisha hodi waingie ? Ni kwa sababu ni jukumu la mtu mwenyewe kutafuta na kubisha hodi, na Mungu hawezi kuingilia kati.

## V. ULIMWENGU HALISI USIOONEKANA NA ULIMWENGU HALISI UNAOONEKANA, CHINI YA UTAWALA WA MWANADAMU.

### A. Ulimwengu halisi usiionekana na ulimwengu halisi unaoonekana.

Ni muhimu mno kwa maisha yetu ya imani kwamba tuelewe kwa usahihi zaidi mambo yahusuyo maisha baada ya mtu kufariki na nafsi ya kiroho ya mtu. Na tuangalie kwa undani maswali haya : Mtu ana nafsi ya kiroho ? Ni nini uhusiano wa Ulimwengu wa kiroho na Ulimwengu wa kimwili ? Kama mtu ana nafsi ya kiroho inafananaje ? Ulimwengu wa kiroho ukoje ? Kuna uhusiano gani kati ya Ulimwengu wa kiroho na Ulimwengu wa kimwili ? Ni kanuni zipi zinatawala Ulimwengu wa kiroho ?

Taarifa nyingi zinakusanywa siku hizi katika uhusiano na Ulimwengu wa kiroho. Hata hivyo, haionekani kuwa rahisi kuelezea kwa ufasaha ama kuelewa vizuri hali ngumu na zisizofafanulika kwa wazi. Na matokeo yake, maswali muhimu yaliyotajwa hapo juu yamewachanganya na hata kuwaogofya watu wengi, na hii imeathiri maisha yao ya kidini. Maelezo ya mantiki ni muhimu kwa ajili ya ufafanuzi wa Ulimwengu wa kiroho unaoonekana ndani ya Biblia, Kama vile hatua tatu za kiroho zilizotajwa katika 2Wakorintho 12 :2, kuonekana kwa Musa na Eliya, pamoja na Yesu kwenye mlima alipobadilika sura, na mifano mingi inayohusu mbingu iliyoandikwa kwenye Kitabu cha Ufunuo.

Ulimwengu hauhusishi tu Ulimwengu unaoonekana unaoweza kulinganishwa na mwili wa mwanadamu ; bali pia unajumuisha Ulimwengu halisi usioonekana, unaoweza kulinganishwa na akili za binadamu. Ulimwengu halisi usioonekana ni Sung Sang ya Ulimwengu mkamilifu, na unaitwa Ulimwengu wa kiroho ; na Ulimwengu halisi usioonekana ni Hyung Sang ya Ulimwengu mkamilifu, na unaitwa Ulimwengu wa kimwili. Twaweza kuuelewa uhusiano uliopo kati ya Dunia hizi mbili kwa kufikiria uhusiano kati ya akili na mwili. Miili yetu ina muda wake wa kuwapo, haiwezi kuzidi wakati wa sasa. Miili yetu ipo tu kwa nyakati, mwishowe huzeeka na kurudi udongoni. Akili zetu hazidhibitiwi na muda ; hakuna kizuizi cha muda chaweza kuzisimamisha akili. Akili zaweza kuakisi mambo yaliyopita na kuwapo kwa ajili ya wakati ujao, kama zinaona umuhimu huo, ni za milele.

Mwili wa kimaumbile huchukua nafasi inayopimika. Huchukua sehemu inayopimika kila wakati na hauwezi kuwa sehemu nyingine muda huo huo. Akili hata hivyo haiwi kwenye sehemu inayopimika. Akili haiachi alama zozote zinazo-onekana kwenye Dunia ya eneo na yaweza kuwa sehemu yoyote, kama inapenda kufanya hivyo. Akili haina mipaka kuwa yaweza kutanda Ulimwenguni kote ; kama itajitanua kwa mapana na marefu yake.

Hivyo, mwanadamu anajumuisha mwili, ambao una mipaka na unakuwapo kwa muda mfupi tu, na akili, ambayo haina mipaka ni ya milele. Kikomo cha matendo cha mwili wenye mipaka, ni Ulimwengu unaoonekana na kikomo cha matendo kwa ajili ya akili isiyo na mipaka na iwayo milele ni Ulimwengu usioonekana. Kama ambavyo akili ya mwanadamu ni mtenda na mhamasishaji wa mwili, Ulimwengu halisi usioonekana ni mhamasishaji wa Ulimwengu halisi unaoonekana (Waebrania 8 :5).

**B. Nafasi ya Mtu kwenye Ulimwengu Mkamilifu.**

Sasa nini uhusiano wa mtu na Dunia hizi mbili ? Mwanzo 2 :7 inasema "…………Bwana Mungu alimfanya mtu kutokana na mavumbi ya ardhi,……….." ambayo humaanisha kuwa Mungu aliuumba mwili wa mwanadamu kutokana na viasili vya msingi vya Ulimwengu halisi unao-onekana. Kuwa Mungu "…….akampulizia puani pumzi ya uhai" (Mwanzo 2 :7), humaanisha kuwa aliifanya roho ya mwanadamu kutokana na viasili muhimu vya Dunia ya kiroho kuunda kile ambacho katika Kanuni kinaitwa nafsi ya kiroho.

Nafasi ya mtu katika Ulimwengu mkamilifu, ni kama ifuatavyo. Kwanza kabisa Mungu alipanga kumfanya mtu kama mwakilishi mdogo kabisa wa Ulimwengu mkamilifu. Mungu aliu-umba Ulimwengu wote kwanza, lakini aliumba kwa kuzingatia mfano bora zaidi wa Sung Sang na Hyung Sang ya mtu halisi, ambaye alipanga kumuumba baadaye. Nafsi ya kiroho ya mwanadamu inajumuisha Ulimwengu halisi usioonekana, na mwili wake wa kimaumbile unajumuisha Ulimwengu halisi unaoonekana. Hivyo Mungu alimfanya mtu mwakilishi mdogo kabisa wa Ulimwengu wa Dunia zote halisi, inayoonekana na isiyoonekana. Hivyo mtu huitwa Dunia mbili kamilifu ndogo.

Pili, Mungu alimuumba mtu awe mtawala wa falme zote za Ulimwengu mkamilifu (Mwanzo 1:28, 1Wakorintho 6 :3). Kulielezea kwa namna nyingine, Mungu aliumba mwili wa mtu kutokana na viasili vinavyoufanya Ulimwengu wa kiumbo, na alimpa mtu utawala juu ya Ulimwengu wa kimwili kupitia milango yake mitano ya fahamu ya kimwili. Vivyo hivyo, Mungu aliumba nafsi ya kiroho kutokana na viasili viufanyavyo Ulimwengu wa kiroho kupitia milango yake mitano ya fahamu. Mtu kwa asili aliumbwa na jozi mbili za milango ya fahamu, moja kwa ajili ya nafsi ya kimwili na nyingine kwa ajili ya nafsi ya kiroho. Kama matokeo ya anguko, milango hiyo ya fahamu ya kiroho ya mtu vilitiwa giza na mtu hakuweza kuwa na ufahamu wa Dunia ya kiroho, ambayo yaweza kueleweka tu kwa akili ya kiroho na mwili wa kiroho. Wale ambao milango yao ya fahamu ya kiroho imekombolewa tayari kwa neema ya Mungu na maisha ya dini wanaweza kuwa na uzoefu na Ulimwengu huu, ama kidogo tu au kwa jumla (Kitabu cha Ufunuo, 2Wakorintho 12 :2, Kujibadili Sura (Math. 17 :2)

Tatu, Mungu alimuumba mtu kuwa kiungo cha maingiliano na kitovu cha uhusiano mwema cha uumbaji. Dunia ya kiroho na Dunia ya kimwili haviwezi kuwasiliana moja kwa mmoja kati yao. Mwili wa mtu na roho yake vinapokuwa kitu kimoja kupitia Tendo la Kutoa na Kupokea, dunia ya kimwili na ya kiroho vitawasiliana kupitia mwanadamu.

Dunia ya Kimwili /Hyung Sang Sang

Dunia ya Kiroho / Sung Sang




1. Ulimwengu mdogo
2. Mtawala
3. Mpatanishi wa maelewano / kitovu cha uhusiano mwema

Kutokana na yaliyokwisha semwa hapo juu, twaweza kutoa muhtasari juu ya nafasi ya mtu katika uumbaji kama ifuatavyo : mtu ni mwakilishi mkamilifu wa Dunia ya kiroho na ya kimwili ; aliumbwa kuwa mtawala wa Dunia hizi mbili ; na kitovu cha uhusiano mwema wa Dunia hizi mbili. Hata hivyo kwa sababu ya anguko la mwanadamu, Uumbaji ulimpoteza mtawala wake na kitovu cha uhusiano mwema. Hivyo ,

…….uumbji unangojea kwa hamu kubwa kudhihirishwa kwa wana wa Mungu; …….kwa maana viumbe vyote pia vinatazamia kwa shauku nyingi kufunuliwa kwa wana wa Mungu. Kwa maana viumbe vyote viliitishwa chini ya ubatilisho kwa hiari yake ,ila kwa sababu yake yeye….. Aliyekiitisha katika tumaini ;Kwa kuwa viumbe vyenyewe vitawekwa huru na kutolewa katika utumwa wa uharibifu,hataviingie katika uhuru wa utukufu wa watoto wa Mungu. Kwa maana twajua ya kuwa viumbe vyote pia vinaugua pamoja hadi sasa……. (Warumi, 8 : 19-23)

**C. Uhusiano kati ya nafsi ya kiroho na nafsi ya kimwili.**

*1. Muundo na ufanyaji kazi wa mwanadamu.*

(a) Nafsi ya kimwili

Nafsi ya kimwili hujumuisha akili ya kimwili na mwili wa umbo. Akili ya kimwili ni mtenda katika nafsi ya kimwili, ikiziongoza kazi za viungo vya mwili katika kuishi, kuzaliana na kutenda. Hivyo, akili ya kimwili hufananishwa na msukumo wa tabia ya asili yamnyama, ikidhihirisha matamanio ya namna hiyo kama matamanio ya kustawisha na matamanio ya kuzaliana. Mwili wa kimaumbile hujumuisha viungo mbalimbali, misuli, na mifupa. Ili nafsi ya kimwili ya mtu ikue katika afya nzuri, ni lazima ipate hewa na mwanga wa jua ; ambavyo ni viini lishe chanya (yang) vya asili na pia hula vyakula

mbalimbali na maji ambavyo ni viini lishe hasi vya asili. Nafsi ya kimwili hurejesha viasili bora kwa nafsi ya kiroho.

(b) Nafsi ya kiroho

Nafsi ya kiroho iliumbwa ili iwe mtenda wa nafsi ya kimwili ; na hii yaweza kueleweka vizuri kupitia hisia za kiroho. Hata kama mtu atakuwa na imani ya kuwapo kwa nafsi ya kiroho kama matokeo ya maisha yake ya imani, kwa vile watu wa anguko wamekuwa na ukuaji mdogo sana hisia za kiroho, bado ana maswali mengi kuhusu kinachotokea kwa nafsi ya kiroho baada ya utengano wake na nafsi ya kimwili baada ya kifo. Inapotenganishwa na nafsi ya kimwili, roho hupotea kama moshi ? Ni roho peke yake inayoacha nafsi ya kimwili ? Inaenda kwenye Ulimwengu wa kiroho na muundo wake halisi ? Kama inaenda kwenye Ulimwengu wa kiroho inapotelea ndani ya Mungu au inachukua sehemu yake katika Ulimwengu wa kiroho ? Kama ndivyo, roho inafananaje ?

Kufuatana na Kanuni, kama ilivyo kwa kila mtu ana nafsi yake ya kimwili , pia ana ya roho yake kamili ; hivyo hiyo roho kamili inaitwa nafsi ya kiroho. Nafsi ya kiroho inafanana katika mwonekano na nafsi ya kimwili, na yaweza kuwasiliana na Mungu moja kwa moja baada ya kuwa timilifu. Baada ya kuuacha mwili wakati wa kufa, nafsi ya kiroho huishi milele katika dunia ya kiroho. Mtu anatamani kuishi milele kwa sababu ana nafsi ya kiroho ambayo ina asili ya umilele. Nafsi ya kiroho inajumuisha akili ya kiroho na mwili wa kiroho. Akili ya kiroho ni kitovu cha nafsi ya kiroho, ikiongoza maisha, upendo, na mawazo bora ya milele ya mtu. Akili ya kiroho hufanya kazi ili mtu aishi maisha ya thamani, akitafuta ukweli, uzuri na upendo. Akili ya kiroho ni kiini cha nafsi ya kiroho,ni mtenda wa mwili wa kiroho, na sehemu ambapo Mungu aweza kukaa. Mwili wa kiroho ni mwili wa nafsi ya kiroho, kama ilivyo kwa mwili wa maumbile ni mwili wa nafsi ya kimwili.




Nafsi ya kiroho huhitaji viini lishe kwa ajili ya ukuaji na ukamilifu. Viini lishe chanya (yang) kwa ajili ya kiroho ni viasili vya uhai kutoka kwa Mungu. Kiasili cha uhai kutoka kwa Mungu ni kiasili cha msingi kinachokuza moyo ndani ya mwanadamu na humwendeleza kuwa kiumbe wa kweli. Kwa

upande mwingine, viini lishe hasi (um) kwa ajili ya ukuaji wa nafsi ya kiroho ni kiasili cha thamani kinachotoka kwenye nafsi ya kimwili. Nafsi ya kimwili inapofanya kazi (inapotenda) kulingana na Neno la Mungu, hutoa kiasili cha thamani cha ukuaji kwa ajili ya nafsi ya kiroho. Nafsi ya kiroho haipokei tu viasili vya thamani kutoka kwa nafsi ya kimwili bali pia hutoa kiasili cha aina fulani kinachoitwa kiasili cha kiroho. Kiasili cha kiroho ni kiasili kinachotoa raha na nguvu kwa nafsi ya kimwili.

(c) Uhusiano kati ya nafsi ya kiroho na nafsi ya kimwili.

Kama ilivyokwisha elezwa hapo juu uhusiano kati ya nafsi ya kiroho na nafsi ya kimwili ni ule wa mtenda na mtendewa, ambapo nafsi ya kiroho inakua na kujikamilisha yenyewe katika msingi wa uhusiano wake na nafsi ya kimwili. Ubora wa maisha ya kimwili ya mtu hubadilishwa kuwa kiasili cha thamani na kuhamishwa katika  nafsi ya kiroho. Hivyo, ubora wa nafsi ya kiroho unategemea ubora wa maisha ya kimwili. Vivyo hivyo nafsi inayopokea jumla ya viasili bora kutoka kwa nafsi ya kimwili huwa kiumbe cha wema, ambapo nafsi ya kiroho inayopokea viasili viovu kutoka kwa nafsi ya kimwili itakuwa ya uovu. Ili nafsi ya kiroho ya uovu iwe ya wema, mtu huyo inambidi atubu akiwa angali hai, roho ya uovu ya mtu inafanywa ya wema kwa kupokea viasili vya thamani kupitia toba yake na imani yake katika neno la Mungu.

Hali ya muhimu zaidi ya nafsi ya kiroho ambayo inahitaji kukamilishwa (kupata ukamilifu)kupitia nafsi ya kimwili ni mwitiko wa mtu mwenyewe kwa upendo wa Mungu. Imekwisha elezwa kuwa kusudi la Mungu la uumbaji linatimizwa kupitia familia (Msingi wa Nafasi Nne, msingi muhimu ambamo uhalisi wake wa upendo waweza kukaa). Kwa hiyo, ni mtu wa kiroho pekee, ambaye akiwa angali Duniani ametimiza mwitiko wake kwa ukamilifu kabisa kupenda kama mtoto, kama mume au mke, na kama mzazi, vyote chini ya utawala wa Mungu aweza kwenda (kuingia) kwenye ufalme wa Mbinguni katika Uimwengu wa kiroho. Ufalme wa Mbinguni unatawaliwa na kuhusiana vema katika upendo wa Mungu ; ni sehemu ambamo kila kiumbe kinaridhika kupitia upendo wa Mungu.

Viumbe vyote hufikia ukamilifu kupitia hatua tatu za ukuaji. Kwa kuzingatia nafsi ya kimwili, nafsi ya kiroho ya mtu pia hupitia hatua tatu za ukuaji. Nafsi ya kiroho katika hatua yake ya mwanzo inaitwa roho ya muundo ; katika hatua ya kukua inaitwa roho ya uhai, na katika hatua ya ukamilisho inaitwa (roho ya utakatifu).

Uhusiano kati ya nafsi ya kimwili na nafsi ya kiroho ni kama ule kati ya mti na tunda lake. Tunda lilivyoiva huvunwa na vishina vyake hurudi ardhini. Vivyo hivyo, kwa nafsi ya kiroho, iliumbwa kuishi kwa milele, baada ya kutengana na nafsi ya kimwili, hubaki na kuishi milele katika Ulimwengu wa kiroho, ambapo mwili hurudi udongoni. Wengi huamini mtu hufa kwa sababu alianguka (alitenda dhambi) lakini hii sio sahihi. Mungu alionya katika kitabu cha Mwanzo 2 :17 kuwa '………..siku utakayokula utakufa' 'Adam na Hawa walikufa kama matokeo ya kula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya. Hata hivyo baada ya Adam na Hawa walipoanguka, waliishi kwa miaka mia nyingi hapa Duniani na wakazaa watoto. Hii ina maana kuwa kifo kilichosababishwa na anguko sio kifo ambacho miili ya kiumbo hurudi udongoni. Mara tu baada ya Babu wa kwanza kutenda dhambi (alipoanguka) kwa kutotii neno la Mungu, roho ambazo zingeweza kuwasiliana na Mungu, hazikufanya hivyo tena ; Mhubiri 12 :7 anasema, '……nayo mavumbi huirudia nchi kama yalivyokuwa, nayo roho humrudia

Mungu aliyetoa’. Hii inaonyesha kuwa kurudi kwa nafsi ya kimwili inaendana sawa na mpango wa uumbaji. Ufafanuzi zaidi juu ya mada hii utatolewa baadaye katika sura ya 'Ufufuo'.

Mtu anapoishi katika nafsi yake ya kimwili kulingana na mpango wa Mungu wa uumbaji, atakuwa akiishi katika ufalme wa Mbinguni Duniani, na Ulimwengu ambamo nafsi yake ya kiroho iliyokamilika itakwenda baada ya maisha yake Duniani itakuwa katika ufalme wa Mbinguni kwenye Dunia ya kiroho.

Hata hivyo, kwa vile Kusudi la Mungu la Uumbaji, ni lazima lidhihirishwe hapa Duniani, dhumuni lake la kwanza katika kazi zake za wokovu, lazima itakuwa ni mtu hapa Duniani. Hivyo, Mungu amekuwa mara kwa mara akituma manabii wake kwenye Ulimwengu huu usio na imani na hata ali mtuma Masihi mwenyewe Duniani. Matumizi ya kutatanisha ya maisha ya kimwili (na nafsi) ndiyo maana Biblia hufundisha kuwa ‘’………Utakacho funga Duniani kitafungwa Mbinguni’ na ‘utakachofungulia Duniani na Mbinguni kimefunguliwa’‘ (Ufasaha uliongezwa) (Math. 18 :18) ; na kwa nini inatufundisha kuomba mapenzi ya Mungu kwa viumbe yatimizwe Duniani (Math. 6 :10).

Sio Mungu anayeamua mtu wa kiroho aende kwenye Ufalme wa Mbinguni ama Jehanamu. Ni mtu mwenyewe ambaye hudhihirisha hili kupitia maisha yake ya kila siku akiwa katika mwili wa kiumbo Duniani. Kila mtu huenda Dunia ya kiroho katika nafasi ambayo nafsi yake ya kiroho ilikuwa imefikia wakati akiwa Duniani. Mungu, Masihi na dini waweza tu kutufundisha njia ya kuiepuka Jehanamu na kutuonyesha njia ya kwenda kwenye ufalme wa Mbinguni. Iwe ama isiwe amepokea mafundisho ya Mungu, na ya kanisa, ni jukumu la mtu binafsi.

Kwenye Ulimwengu ambamo kusudi la uumbaji linatimizwa, shetani, dhambi na jehanamu haviwezi kuwapo. Katika uhalisi wa Mungu, wa uumbaji ni Mbingu tu zilitakiwa kuwapo. Lakini kwa sababu ya dhambi, mtu alipoteza thamani yake ya asili na akawa kama takataka. Sehemu ambayo hizi taka taka zinapotupwa ndipo huitwa jehanamu.

*2. Akili ya Binadamu katika uhusiano kati ya akili ya kiroho na akili ya kimwili.*

Uhusiano kati ya akili ya kiroho ni wa Sung Sang (tabia za ndani) na Hyung Sang (muundo wa nje). Akili ya kiroho, ambayo ni mtenda, na mwili wa kiroho, ambao ni mtendewa, vinapokuwa kitu kimoja kupitia tendo la kutoa na kupokea, akili ya kibinadamu huundwa. Ndani ya mtu mkamilifu tendo kamilifu la kutoa na kupokea chini ya utawala wa Mungu hufanyika na huungana, na kuunda kitu ambacho huitwa akili ya awali (ya asili). Akili ya asili ya mtu muda wote humwongoza kuelekea mapenzi ya kusudi la Mungu. Mwili unaporudi udongoni, akili ya kimwili hukoma (hufikia tamati) bali akili ambayo huundwa kutokana na mwingilio wa akili ya kiroho na akili ya kimwili hubakia ndani ya nafsi ya kiroho.




Akili ya kiroho na akili ya kimwili huwa na mahusiano katika tendo la kutoa na kupokea na huungana chini ya utawala ambao mwanadamu anafikiria ni wa kweli.

Tunauita huu muungano ; dhamira ya mtu. Mtu mkamilifu mara nyingi husimamia ukweli mtimilifu. Kwa hiyo, akili ya asili na dhamira visielekezwe katika mielekeo miwili tofauti, bali viunganishwe. Hii ni kwamba akili ya asili na dhamira inabidi viwe na uhusiano kama hali ya ndani na ya nje na mara zote humwelekeza mtu katika kusudi la Mungu na nia ya Mungu ya wema. Mtu wa anguko bado anayo akili ya asili ndani yake ambayo humwongoza kwenye wema. Hata hivyo, mtu wa anguko amepoteza kiwango halisi cha wema, na kwa hiyo viwango vyao vya dhamira vimekuwa tofauti kati yao kulingana na maoni yao juu ya upi ndiyo ukweli. Kila ambapo wazo tofauti au elimu ya dini inapotolewa, mwelekeo tofauti wa dhamira utakuwapo.




**Akili ya Mtu wa anguko**

Pia kwa sababu mtu amekuwa chini ya utawala wa shetani kama matokeo ya anguko, akili yake ya kiroho haiwezi kwa usahihi kupokea kiasili cha uhai kutoka kwa Mungu na hivyo amebakia mchanga. Akili ya kiroho ya namna hiyo haiwezi kuwa katika nafasi ya mtenda kwa akili ya kumwili na badala yake imetawaliwa na akili ya kimwili. Na wakati ambapo hii akili ya kiroho iliyo changa huwa na tendo la kutoa na kupokea na akili ya kimwili ambayo iko chini utawala ya shetani, akili nyingine huzaliwa, ambayo huelekeza kwenye uovu. Tunaita akili hii akili ya uovu, Akili ya asili na dhamira ya mwanadamu hupigana dhidi ya akili ya uovu, ambayo ni kinyume na mapenzi ya Mungu na mwelekeo na humwelekeza mtu kwenye wema.

## CHAPTER II THE FALL

## SURA YA PILI ANGUKO.

Kila mtu ana akili ya asili, ambayo ina asili ya kufuata wema na kupinga uovu. Lakini watu walio anguka wanaendeshwa bila kujitambua na msukumo wa kutenda ovu, kinyume na matamanio ya akili yao ya asili. Katika Ukristo, yule ambaye huongoza huu msukumo wa kutenda uovu anajulikana kama Shetani (Ibilisi). Sura hii, "Anguko", linaweka wazi utambulisho wa Shetani na asili ya uovu.




### I. MZIZI WA DHAMBI.

### A. Mti wa uzima na Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya.

Kwa kuzingatia kitabu cha Mwanzo katika Biblia, Wakristu wamekuwa na utamaduni ambao umekuwa na imani inayochanganya kwamba dhambi ya asiili na mzizi wa dhambi na uovu vilitokana na mababu wa kwanza wa mwanadamu kula kipande cha tunda – tunda la mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya (kwa kifupi hapa linatokana na kula tunda la wema na ubaya). Hata hivyo tunda la wema na uovu ni tunda halisi au mfano, kama ilivyo kwa maneno mengi kwenye Biblia ? Kulingana na Kanuni ni mfano.

Ingewezekanaje Mungu wa upendo, mzazi wa wanadamu, atengeneze tunda la kuvutia namna ile na kuliacha sehemu ambayo lingeweza kuliwa na watoto wake na kuwasababishia anguko (Mwanzo 3 :6) ? Yesu alisema katika Mathayo 15 :11, " '.........siyo kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi ; ...'" kwa jinsi gani basi chakula kimsababishe mtu kuanguka? Pia haingii akilini kuwa Mungu wa upendo aliumba tunda la wema na uovu kumjaribu – bila huruma na kusababisha mwishowe kifo chake – ili tu kuona kama mtu angetii neno Lake. Ukweli kwamba walikula tunda japokuwa walikuwa wameambiwa wangekufa, inaonyesha

kuwa tunda linawakilisha kitu kingine kinachosisimua kwamba matamanio yao kwa hilo yali kuwa makubwa zaidi ya matamanio yao ya uzima.

**<u>Tunda ni Mfano</u>**

**1. Mungu wa Pendo**

**2. Maneno ya Yesu (Mat 15:11)**

**3. Haikuwa Jaribio**

**4. Tunda hallithaminiwi kuliko maisha**

Kabla ya kuzingatia tunda la wema na uovu linawakilisha nini, yatupasa kujuwa mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya ulikuwa nini. Lakini mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya umetajwa mara chache sana katika Biblia. Hivyo, ili kujua ni nini mti wa Mema na Mabaya unawakilisha kwanza tujifunze mti wa Uzima, ambao kulingana na Biblia, ulisimama kandokando na mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya ndani ya Bustani ya Eden (Mwanzo 2 :9, 2 :17, 3 :3) na umetajwa mara nyingi ndani ya Biblia.

*1. Mti wa Uzima.*

Mithali 13 :12 inasema, "kilichotarajiwa kikikawia huufanya moyo kuugua . Bali haja ya mtu ikipatikana ni mti wa uzima." Mti wa Uzima ndilo tarajio kuu la mwanadamu. Kama Ufunuo 22 :14 inavyosema "Heri wazifuao nguo zao (za dhambi na uovu), wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa malango yake." Vifungu hivi vinaonyesha kuwa kuufikia mti wa Uzima utasababisha furaha kwa mwanadamu aliyeanguka. Sasa, ni mti gani huu wa Uzima, hata kuwa tumaini la Wana Israeli wa Agano la Kale na tumaini la Wakristu wa Agano Jipya ?




Kama watu wa anguko wakiulizwa kiini cha furaha na tumaini kila mtu atatoa jibu tofauti. Mtu mmoja anaweza kujibu kuwa ni nguvu, na mwingine kuwa ni utajiri, au maarifa. Sasa nini kimekuwa tarajio kwa watu wenye imani katika historia ya mwanadamu ? Kitu kimoja

kipo wazi. Kama tumaini la ndani  la mtu aliyeanguka ni mti wa Uzima, basi tumaini la Adam kabla ya Anguko ni lazima lilikuwa Mti wa Uzima.  Sababu ni kuwa kila mtu amesalia na asili ya awali ndani mwake, na hivyo hutafuta asili hiyo ambayo aliitumaini kuwa nayo kabla ya Anguko, lakini ilipotea. Mwanzo 3 :22-24, huonyesha kuwa Adam pia alitumaini kufikia Mti wa Uzima, lakini sababu ya dhambi zake hakuruhusiwa.  Hivyo, mti wa uzima umebakia kama tumaini la pekee la mtu aliyeanguka.

Sasa huu ulikuwa mti gani wa Uzima tumaini la mtu akuaye, Adam ambaye haja kamilika ? Je umiliki wa mali ungeweza kuwa tumaini la msingi kwa Adam ndani ya Bustani ya Eden, au nguvu, au wasiwasi wowote wa kiinje ? Kwa kuwa ilikuwa awe bwana wa Ulimwengu, na kuvitawala viumbe vyote, hakukuwa na sababu kwa Adamu kutumaini umiliki wa vitu zaidi au nguvu.  Kama Adamu alikuwa na tumaini lolote kabla hajakamilika, ingekuwa tu kufikia ukamilifu wake mwenyewe.  Kwa maneno mengine, matamanio yake yangekuwa kuwa mtu mwenye tabia timilifu -mtu ambaye ametimiza Kusudi la Uumbaji.




Hivyo, mti wa uzima ni huwa kilisha  mtu ambaye ametimiza Kusudi la Uumbaji. Kama Adam asingekuwa ameanguka na kukamilisha Wazo la Uumbaji, hapo angekuwa mti wa Uzima na angekuwa ameujenga Ufalme wa Mbinguni hapa duniani ambayo ndiyo Bustani ya mti wa Uzima. Hata hivyo, Adam alianguka, na Mungu aliizuia njia ya kuelekea kwenye mti wa Uzima kwa upanga wa moto (Mwanzo 3 :24).

Kwa kuwa Adam aliliacha Kusudi la Uumbaji, alikuwa mti batili wa uzima na alianza kuzaa watoto ambao walikuwa miti batili ya uzima, na hivyo kuifanya Bustani ya ubatili ya miti ya uzima, badala ya bustani ya miti ya uzima.  Kwa hiyo, ili kuujenga Ufalme wa Mbinguni hapa duniani, ambao ndiyo bustani ya Mti wa Uzima, mti wa Kweli wa Uzima, lazima uonekane katika Ulimwengu wa Anguko na kuwapandikiza wanadamu wote kwake.  Kwa kujua kuwa Mti wa Uzima unamwakilisha Adam, twaweza sasa kufahamu ya kwamba mti wa Uzima

katika Agano la Kale (Mithali 13 :12) humwakilisha Yesu (1 Wakorintho 15 :45), na mti wa Uzima katika Agano Jipya kwenye kitabu cha Ufunuo (Ufunuo 22 :14) huwakilisha Masihi atakaerudi.  Kwa nyongeza zaidi, tunaweza kujua kusudi la kazi ya wokovu ni kuukomboa Mti wa Uzima ambao ulipotea Bustani ya Eden (Mwanzo 2 :9) katika Mti wa Uzima ambao unatajwa katika kitabu cha Ufunuo (Ufunuo 22 :14).



*2. Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya.*

Katika Bustani ya Eden, Mungu alimuumba Adam, na Hawa kuwa mwenza wake.   Kama katikati ya Bustani kulikuwa na mti kumwakilisha mwanaume, si vinginevyo kuwa kungekuwa pia na mti unaomwakilisha mwanamke ?  Ndiyo na mti wa Ujuzi Mema na Mabaya, ambao umesimama pamoja na Mti wa Uzima (Mwanzo 2 :9, 2 :17, 3 :3) ndiyo huu mti.




Katika Biblia, Yesu wakati mwingine alijilinganisha na mzabibu (Yoh 15 :5) au mzeituni (War. 11 :17). Katika mtazamo sawa, Adam na Hawa wamewakilishwa na miti miwili nao kutoa tamko kuwa kulikuwa na Mti wa Uzima na Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya katikati ya Bustani ya Eden haimaanishi kuwa kulikuwa na miti ya kawaida katika kitovu cha kijiografia cha bustani ya kawaida, bali inamaanisha kuwa watu wawili, Adam na Hawa ndiyo kitovu cha Nia ya Mungu ya Uumbaji.  Nia yote ya Mungu ya Uumbaji ni lazima itimizwe kupitia mwanadamu. Tunavyoangalia vitu katika mtazamo huo, twaweza kuona kuwa Mti wa Maarifa ya Kujua Mema na Mabaya humwakilisha mwanamke, Hawa. Ni lazima tuhitimishe kuwa tunda la mti huu lina uhusiano na Hawa. Hata hivyo, ili kujua kwa ufasaha tunda linawakilisha nini, yatubidi tuelewe nyoka Ibilisi ni nani.

**B. Utambulisho wa Nyoka.**

Katika Mwanzo sura ya 3, Biblia inaonyesha kuwa nyoka ndiye aliyemtia Hawa majaribuni na kumsababisha atende dhambi. Hata hivyo, nyoka anayeelezewa hapo haiwezekani akawa nyoka wa kawaida tunayemjua ni ishara.

Mwanzo sura ya tatu pia tunaona kuwa 'nyoka' aliongea na mwanamke na kwamba alijua kuwa Mungu alimwambia Adam na Hawa wasile tunda la Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Ili 'nyoka' aweze kuongea na mwanadamu na ajue ambacho Mungu alikuwa ameamuru, 'nyoka' ni lazima alikuwa kiumbe wa kiroho. Ufunuo 12 :9 unasema 'na joka kubwa lilitupwa, nyoka wa zamani aitwaye Ibilisi na Shetani, audanganyaye Ulimwengu wote – alitupwa chini duniani, na malaika zake walitupwa pamoja naye inaonyesha kuwa 'nyoka' wa zamani ni Ibilisi. Huyu 'nyoka wa zamani' ni yule 'nyoka' ambaye alimtia majaribuni Hawa. Kama tunavyosoma Ufunuo 12 :9 kuwa 'nyoka' alitupwa chini toka Mbinguni, twajua kuwa 'nyoka' alikuwa Mbinguni kabla ya kutupwa chini na hivyo ni lazima alikuwa katika kiumbe wa kiroho.

Kwa kuwa twajua kuwa 'nyoka' ni shetani (Ufunuo 12 :9), twaweza kujifunza nyoka alikuwa nani ; kwa kujua shetani ni nani. Ili tujue shetani ni nani, yatubidi tujue kwanza kiumbe wa kiroho ambaye alikuwa Mbinguni kabla ya kutenda dhambi. Yaweza kukubalika kuwa kwa vile 'Nyoka' awali alikuwa ndani ya Bustani ya Eden kabla ya kutupwa chini kutoka Mbinguni, 'Nyoka' ni lazima hapo awali alikuwa ni kiumbe ambacho Mungu aliumba kikiwa na asili ya wema na kwamba kilikuwa bado hakijakamilika, (1)hapakuwa na kiumbe chochote katika Bustani ya Eden ambacho hakikuumbwa na Mungu, (2) Mungu anaumba wema tu na, (3) hakuna kilicho chema kingeweza kutenda dhambi baada ya kuwa kikamilifu.

Wengine hufikiria kwamba hiki kiumbe cha kiroho ambacho chafananishwa na nyoka kilikuwa kiumbe ambacho kilikuwepo hata kabla ya Uumbaji na kilikuwa kiumbe ambacho kusudi lake lilikuwa ni uovu, kinyume na lile la Mungu. Hata hivyo, mbali ya mtu wa anguko, kila kitu ndani ya Ulimwengu huwapo kulingana na mpango mmoja uliokamilika. Kwa hiyo haiwezekani kuwa kulikuwapo toka mwanzo na chanzo cha dhambi ambacho kilikuwa kinyume na Mungu. Kama toka mwanzo kungekuwepo misukumo miwili inayopingana katika Ulimwengu, kusudi la misukumo hiyo linalopingana, lingesababisha kuharibika kwa Ulimwengu. Inaweza kuhitimishwa tu kuwa kiumbe hiki cha kiroho toka mwanzo kiliumbwa kwa kusudi la wema, lakini baadaye, kikiwa katika hatua za ukuaji kilianguka na kuwa Shetani. Hiki kiumbe kilikuwa na uwezo wa kuongea na mwanadamu, kilijua matakwa ya Mungu, kiliishi mbinguni hapo mwanzo, kilikuwa na uwezo wa kumshawishi mwanadamu, na kiumbe hiki baada ya kuanguka na kuwa Shetani, bado alikuwa mbele ya wakati na nafasi, kushawishi akili na roho ya mwanadamu, na kumsababisha mwanadamu

**NYOKA Mwanzo 3:1-4**

---

1. **Aliweza kuongea na mtu**
2. **Alijua amri za Mungu**
3. **Ufunuo 12:9 „nyoka wa zamani = Ibilisi, Shetani**
4. **Kiasili alikua anaishi Mbinguni**
5. **Alikua na uwezo wa kumjaribu mtu**
6. **Alitawala roho ya mwnanadamu tangu Anguko**

aendeshe maisha ya uovu. Kiumbe gani kimejazwa na uwezo wa namna hiyo ? hakuna kiumbe zaidi ya Malaika kilicho jaliwa na uwezo wa namna hiyo. Mtu aweza kuuliza kama Malaika waweza kutenda dhambi, lakini ushahidi kutoka kwenye Biblia unaelezeka wazi. Kwa hakika tunaposoma waraka wa pili wa Petro 2 :4 unaosema '……kwa maana ikiwa Mungu hakuwaachilia Malaika waliokosa, bali aliwatupa……' twaweza kwa wazi zaidi kuona kwamba Malaika waweza na wanafanya dhambi, kwa kuangalia kwa ufasaha kuwa ufunuo 12 :7-9, katika kusema 'Malaika zake' inaonyesha kuwa 'nyoka' alikuwa kiongozi wa Malaika, twaweza kujua kuwa 'nyoka' alikuwa ni Malaika.

**C. Dhambi ya malaika na dhambi ya mwanaume na mwanamke wa kwanza.**

Dhambi ya malaika huyu ilikuwa nini ? Yuda 6-7 inasema, " Na malaika wasioilinda enzi yao wenyewe, lakini wakayaacha makao yao yaliyowahusu, amewaweka katika vifungo vya milele chini ya giza kwa hukumu ya siku ile kuu. Kama vile Sodoma na Gomora na miji yote iliyokuwa kando kando, ambao kama malaika walifuata uasherati, wakaenda kufuata mambo ya mwili yasiyo ya asili, imewekwa kuwa mfano, wakiadhibiwa katika moto wa milele." Dhambi ya malaika (Bustanini) ilikuwa dhambi ya zinzi. Kwa kuwa uzinzi haufanywi na mtu mmoja peke yake, ni lazima kulikuwa na mwenza. Sasa nani alikuwa huyu mwenza wa malaika ? Biblia inatueleza kuhusu viumbe watatu tu wali vyotenda dhambi katika Bustani ya Eden ; nyoka, Adam na Hawa. Na tuangalie nini dhambi ya mtu wa kwanza na mwanamke ilivyokuwa.

Katika Mwanzo 3 :7, tunasoma ya kwamba baada ya kujaribiwa na nyoka na kutenda dhambi, mababu wetu wa kwanza wakaona haya kuwa uchi wakaficha sehemu zao za siri. Lakini kabla ya anguko walikuwa uchi lakini hawakuona haya (Mwanzo 2 :25). Halafu tunaposoma ya kwamba walifunika sehemu zao za chini, au viungo vyao vya uzazi katika miili yao kwa majani ya tini baada ya kutenda dhambi, lazima tujiulize kama mwanaume naye pia alitenda dhambi ya zinaa.

Ni katika asili ya binadamu aliyeanguka ya kujaribu kuficha ubaya na makosa ; hivyo kama tunda la wema na ubaya lilikuwa tunda katika maana ya kawaida ya tunda, Adam na Hawa wangeficha mikono yao au midomo kama wangekuwa wamechukua tunda kwa mikono yao ama wangekuwa wamekula tunda kwa midomo yao. Lakini tunaona kuwa walifunika viungo vyao vya uzazi na sio mikono na midomo yao. Hii inaonyesha kuwa kosa la Adam na Hawa lilihusisha viungo vyao vya uzazi. Ayubu 31:33 inasema, *"…….nimeyafunika makosa yangu ... kama Adam* kwa kuuficha uovu wangu kifuani mwangu" (ufafanuzi ulioongezwa). Maneno ya Ayubu yanaonyesha kuwa Adam aliyaficha makosa yake, na kwa vile twajua kuwa Adam na Hawa walizifunika sehemu zao za viungo vya uzazi, twaweza kuhitimisha kuwa dhambi yao ilivihusisha viungo vya uzazi.

Katika Bustani ya Eden, dhambi pekee ambayo mwanadamu angeitenda na kuhatarisha maisha yake ni dhambi inayohusisha upendo. Adam na Hawa walipaswa wakue kama kaka na dada, na baada ya kufikia ukamilifu, wangeujenga Ufalme wa Mbingu hapa duniani na wangekuwa mke na mume wa kwanza na kuifanya familia ya Mungu, iliyotimiza Kusudi la Uumbaji. Hata hivyo, Yesu anaposema katika Yoh. 8:44 'Ninyi ni wa baba yenu shetani…..', kwa uwazi anatuonyesha kuwa watu wenye dhambi ni uzao wa Shetani. Adam na Hawa walimsalia Mungu, baba yao wa kweli na wakawa kitu kimoja na baba batili, Shetani, ndiyo sababu Warumi 8:23 inasema, ".... sisi wenyewe ambao tuna matunda ya kwanza ya roho tunalia kimoyomoyo tukisubiri kufanywa wana, na kukombolewa miili yetu" (hili limesisitizwa). Ukweli kwamba tunasubiri kufanywa wana katika kizazi kiake Mungu inatwambia sisi si wa kizazi cha Mungu. Katika Math. 3:7 na Math. 23:33, Yohana Mbatizaji na Yesu na waliwaita watu 'wana wa nyoka'- kwa maneno mengine, wabini/watoto wa manyoka- hili kwa uwazi zaidi linaonyesha sisi watu wa anguko tumo katika uzao wa Shetani. Kwa hivyo, tuaweza kuelewa wazi kabisa kwamba mtu wa anguko ni wa kwa Shetani, sio wa Mungu. Haya ni matokeo ya Hawa kujamiiana na malaika. Matokeo ya uhalifu huu, watu wote wamekuwa wakizaliwa kama 'watoto' wa Shetani.*

______________________

* Ingawa Hawa na malaika mkuu waliungana katika tendo kweli la zinaa kwa njia ya mwili wa kiroho wa Hawa na mwili wa malaika mkuu (mwili wa kiroho), hakuna watoto wanaweza kuzaliwa kweli kwa uhusiano kati ya mwanadamu na malaika. lakini, Hawa alirithi "upendo" wa kishetani, na wakati Hawa na Adam waliingia katika uhusiano, ambao ungezaa watoto, mahusiana yao yalikuwa na msukumo wa upendo" wa aina ya kishetani, na watoto wao walizalikwa kwa upendo" huu. Kwa hivyo, watu wote ni watoto wa Shetani.

**D. Tunda la mema na mabaya na mzizi wa dhambi.**

Kwa kuwa mti hujizalisha kwa tunda lake (ambalo hutoa mbegu) na mtu huzaa kwa njia ya mahusiano ya kujamiiana , kwa hiyo Tunda la Mti wa Mema na Mabaya linaashiria uhusiano wa upendo wa Hawa. Ukweli kwamba Hawa alikula tunda alichochewa na Shetani kwa kula inamaanisha kwamba alitenda tendo la zinaa na Shetani. Kwa kuwa kula kitu humaanisha

kulifanya sehemu ya mwili na damu yetu, Hawa kumpa Adam tunda la mema na mabaya na yeye kulila humaanisha Hawa alisababisha Adam kuanguka kupitia njia ileile ya upendo batili.




Kwa hiyo mzizi wa dhambi si kwa wahenga wetu wa kwanza kula tunda la kawaida, lakini wao kuanzisha uhusiano wa damu kupitia uzinzi na malaika mkuu ambaye ni ishara ya nyoka. Uhusiano huu wa damu ni chanzo cha dhambi ya asili inayopitia kizazi hadi kizazi. Kila dini inayojitahidi kuondoa dhambi wameainisha wazi kuwa uzinzi kama dhambi kubwa kuliko dhambi zote. Kutokana na  mtazamo huu juu ya Dhambi ya Asili, tunaweza kuelewa kwa nini waisraeli iliwapasa kutahiri ili waonekane wateule wa Mungu. Ilikuwa ina hitajika ili kulipa kutokana na matumizi mabaya ya viungo vya uzazi ambavyo kwao binadamu amekuwa na uzao wa kishetani.  Tunaweza kusisitiza kuzuia dhambi nyingine kupitia mikakati ya jamii, elimu, au maendeleo ya kiuchumi, lakini pamoja na ustaarabu na hali ya maendeleo ya jamii na uchumi mpaka kiwango ambacho tunaweza kufurahia maisha imara Kuongezeka kwa ngono na ufuska na kumomonyoka kwa maadili ya binadamu hakuwezi kukazuiwa na yeyote yule.

**Dini** : zinaa, uasherati katika dhambi kubwa zaidi

**Wanaisraeli** : Kutahiri

**Ustarabu ulio endelea** : Haiwezi  kudhibiti ngono, ufuska na kumomonyoka kwa maadili

Sababu kwamba shetani anaweza kuvunja taratibu nzuri za mapenzi ya mtu katika siku hizi za mwisho ni kwa sababu wazazi wa kwanza walikwa mume na mke bila ruhusa au baraka ya Mungu na ku ungana shetani kama baba yao batili.Watoto wao walizaliwa kama watoto wa dhambi na sio wa Mungu na wali anzisha dunia  isiyo na imani uovu na vita. Matokeo yake, shetani ame mtawala mtu kama inavyo onekana  (Jn 8:44).

Mbali na ukweli kuwa Mungu aliumba mtu na Ulimwengu, kamwe bado hajawahi kuwa kiini cha matukio ya hapa duniani, - kutawala kutokana na matakwa yake. Binadamu amemweka shetani kama mhusika mkuu, na shetani kwa ubatili amekuwa akichukua nafasi ya ubwana. Ni kwa sababu hiyo shetani anaitwa mtawala wa dunia hii' (Jn 12:31) na 'mungu wa dunia hii' (2Wakor 4:4 ).

## II. MSUKUMO NA MCHAKATO WA ANGUKO.

### A. Kuumbwa kwa malaika.

Ni kwa msukumo gani na mchakato upi Adam na Hawa na malaika walianguka katika bustani ya Eden? Mungu kwanza aliwaumba malaika ili kusaidia vyote atakavyoumba na kutawala dunia. (Heb. 1:44). Hata hivyo, kwa kuwa mtu aliumbwa kama mtoto wa Mungu na alikuwa awe na mamlaka juu ya malaika. Sababu ambayo malaika siku hizi hufikiriwa kuwa juu ya binadamu ni kwa sababu ya




anguko, mtu alitokea kuwa mpotoshaji sana (Yer 17:9) kwamba yupo nafasi ya chini kabisa kuliko vitu vyote vya uumbaji,wakiwemo malaika.



Wakorinto wa kwanza 6;3 kwa uwazi kabisa inasema mtu ata kuwa na mlaka ya kutawala na ku hukumu malaika, na watu wengi wa kiroho wanaona malaika waki wanazunguka na kuwalinda wenye imani kuelekea paradiso.Mtu ata hukumu malaika na malaika ata mlinda mtu kwa sababu kiasilia mtu ana thamani kubwa kuliko malaika.

**B. Anguko Kiroho na Anguko Kimwili.**

*1. Anguko – Kiroho*

Lusiferi (Is 14:12) alikuwa katika nafasi ya *malaika mkuu* na alikuwa njia ya upendo wa Mungu katika dunia ya malaika. Inaonekana kuwa yeye tu alikuwa katika nafasi ya kupokea upendo wa Mungu. Hata hivyo kwa kuwa Adam na Hawa waliumbwa kama watoto wa Mungu, Mungu aliwapenda zaidi kuliko alivyompenda Lusiferi, ambae aliumbwa kama mtumishi. Bado, Lusiferi aliendelea kupokea upendo wake bila kupungua na hata baada ya kuwaumba Adam na Hawa. Hata hivyo kwa Mungu kuwapa Adam na Hawa upendo zaidi, Lusiferi alihisi kulikuwepo upungufu wa upendo ambao alikuwa akipokea kutoka kwa Mungu. Kwa sababu hiyo Lusiferi ali jaribu kutafuta nyongeza ya upendo alioupokea kwa kuwa karibu zaidi na Adam na Hawa.

Kwa kuwa upendo wa Mungu ni chanzo cha uhai na uzuri, Hawa aliyepokea upendo mwingi kutoka kwa Mungu, alikuwa mrembo sana katika macho ya Lusiferi. Lusiferi alikuwa mara nyingi karibu na Hawa na alikuwa amesisimkwa na shinikizo la upendo kuelekea (Hawa). Hawa, akiwa bado yupo katika hali




ya kutokamilika, alishawishika na ushawishi wa Lusiferi, na wakatenda dhambi ya uzinzi. Hili ndilo lilikuwa *anguko la kiroho*.

Mtu ataweza kuuliza ili wezekana vipi kujamiiana kati ya malaika na mtu. Hili swali linatokea tu kwa sababu ya mtazamo wa kiroho wa mtu aliyeanguka katika hali hiyo ya chini kabisa kwa sababu ya Anguko. Hata hivyo, katika kitabu cha Mwanzo 32:25, Biblia inaonyesha kuwa muungano wa mtu na malaika unawezekana pale ambapo imeandikwa kuwa malaika alipigana mieleka na Yakobo na kumtengua nyonga yake.

*2. Anguko la Mwili.*

Pale Hawa alipounganika na malaika mkuu (kupitia roho zao), alijihisi hofu, ambayo ilitokana na dhamira ya hatia na alipata kung'amua kuwa mwenza wake dhahiri alikuwa Adam na wala si malaika.

Hawa alitaka kukomboa uhusiano wake na Mungu na alitaka kuondokana na hofu iliyotokana na Anguko. Adam alikuwa tegemeo lake pekee la kumrudia Mungu, na Hawa alifikiri ataweza kufanikisha hili angalau kwa kuwa pamoja na Adam, ambaye alikusudiwa kuwa mwenza wake, na hivyo ali mshawishi Adam. Na huu ukawa msukumo wa *anguko la mwili*.




Kama ilivyoelezwa katika 'Kanuni za Uumbaji' Adam na Hawa walikuwa watimize Baraka Tatu. Kwa kufanya haya walipaswa kuwa mume na mke. Kwa maneno mengine Lengo la Uumbaji lilikuwa ni kwa Adam na Hawa kujikamilisha wenyewe binafsi na baadaye wawe mume na mke wa upendo wa milele, chini ya matakwa ya Mungu. Kwa kuwa walijifanya mume na mke kabla ya wakati wao chini ya matakwa ya shetani, uhusiano wao uka sababisha anguko na si kwa kufuata maadili ya Mungu. Kwa kuunganika na Hawa, Adam akarithi viasili vya uovu ambavyo Hawa alivipokea kutoka kwa Lusiferi. Chembechembe hizi baadaye zilienezwa kwa wabini wao kutoka kizazi hata kizazi.




Kama wahenga wa kwanza 'wasingekula tunda la mema na mabaya' wangejikamilisha wenyewe kama mwana na binti wa Mungu, na baadaye wangebarikiwa na Mungu, wangekuwa mume na mkewe chini ya mapenzi ya Mungu na kuzaa watoto wenye uasili wa wema na hivyo kukamilisha Ukamilifu wa Uumbaji. Kisha, baada ya Hawa kutimiza adili la Uumbaji, upendo wake ungekuwa tunda la wema, na angefananishwa na mti wa mema.

Hata hivyo, kabla ya kukamilika, Hawa alitenda dhambi ya uzinzi na malaika mkuu na kuwa mtu aliyeanguka. Zaidi ya hapo alisababisha Adam kuanguka na hivyo wakajenga familia za kwanza za anguko, ambazo hakuna hata moja Mungu anaweza kufanya nazo kazi. Kwa hiyo, Hawa aliye anguka alifananishwa na mti wa ujuzi wa mabaya, na upendo wake ukawa kama tunda la mti huo.



Katika mtazamo huo huo, tunaweza kuona kabla tu ya anguko, Hawa alikuwa katika nafasi ya kuwa ama mti wa wema kwa kukamilisha kusudi la Uumbaji au mti wa uovu kwa kuanguka, ili ashiriwa kama Mti wa Ujuzi wa Mema na Mabaya. Tangu kabla ya anguko, upendo wa Hawa ulikuwa na uwezo ama kuzaa tunda la wema na hivyo kukamilisha kusudi la Uumbaji, au tunda la uovu likisababisha Anguko, upendo wake uli fananishwa na tunda la mema na mabaya.




Kutokana na 'Kanuni za Uumbaji', Mungu alikuwa atimize lengo la kumuumba mtu kwa njia ya upendo. Hivyo, upendo ni kiini cha raha ya mtu, uhai na furaha. Hata hivyo, kwa sababu wahenga wetu wa kwanza hawakutii sheria za mbinguni na wakaanguka, upendo nao ulichafuliwa na shetani amekuwa aki mtawala mwanadamu na kumfanya ateseke. Hivyo shetani, alichafua upendo wa binadamu, ni kiongozi wa kuangamiza familia adilifu.

## III. ILIWEZEKANA VIPI KWA MTU KUANGUKA.

### A. Nguvu ya Upendo na Nguvu ya Kanuni.

Mtu aliumbwa na akue na afikie ukamilifu, akiwa akisukumwa ndani katika kipindi cha kukua, au kipindi cha utawala usio moja kwa moja, kwa *nguvu ya Kanuni* kuishi kutokana na *Kanuni**. Kwa hiyo, nguvu ya *Kanuni* haiwezi yenyewe kumuengua mtu kutoka kwenye mwelekeo wa *Kanuni* na kumfanya aanguke. Lakini kabla ya ukamilifu, mtu anaweza kuenguliwa kutoka kwenye njia kama atapigwa na nguvu nzito zaidi ya ile ya *Kanuni*, ambayo inaelekeza kukua kwa mtu. Nguvu pekee ambayo ina nguvu zaidi ya ile ya *Kanuni* ni nguvu ya upendo. Pale binadamu anapokuwa hajakamilika kabla ya uzoefu wa upendo mkamilifu wa Mungu katika utawala wa moja kwa moja, kuna uwezekano wa kuanguka kwa sababu ya upendo usiyo wa kanuni, upendo ambao una elekea kinyume na upendo wa Mungu.




Kwa nini Mungu alifanya nguvu ya pendo iwe imara zaidi ya nguvu ya *Kanuni* ? Upendo ni msukumo na chanzo cha Mungu kuumba vitu vyote, na kwa hiyo, upendo ni kitu cha thamani sana zaidi ya vitu vyote. Kwa uumbaji ndicho chanzo cha uhai, furaha na raha. Ingawa Mungu aliumba vitu vyote, kulingana na *Kanuni,* au sheria, kwa kuwa alihitaji hatimae utawala wa upendo, aliifanya upendo kuwa nguvu kuu.

**B. Madhumuni ya Amri na kipindi chake umuhumu wake**

Kwa kuwa nguvu ya pendo ni kubwa zaidi ya nguvu ya *Kanuni*, kuna uwezekano wa mara kwa mara kwa wakati wa kukua kwake mtu anaweza kuanguka kwa sababu ya upendo usiyo wa Kanuni'. Ni kitu gani kinachoweza kuzuia hili ? mara nguvu ya upendo usiyo wa Kanuni hutokea katika kipindi ambacho mtu haja fikia ukamilifu na utawala wa moja kwa moja na upendo wa Mungu, anaweza kuanguka. Ili kuzuia hili, Mungu alimpa mtu amri 'asile tunda la kujua mema na mabaya'. Kama wahenga wa kwanza wa binadamu wange tii amri hii kwa uaminifu, wasingeweza kujenga msingi wa uhusiano na malaika mkuu. Hata hivyo, nguvu isiyo ya kanuni isinge kuwepo. Hata hivyo kwa kuwa hawa kuweza kudumisha imani na kutii amri badala yake waka anzisha msingi wa uhusiano wa kutoa na kupokea na malaika mkuu, nguvu ya upendo ovu ili sababisha kuacha na kutoka kwenye njia ya *Kanuni*.




Je, ni kipindi cha muda gani ambacho Mungu ange hitaji hao wahenga wetu wa kwanza kuishika amri ya 'kutokula' ambalo ni sharti la imani ambalo Mungu aliwapa? Pale Adam na Hawa wangejikamilisha na kuazisha upenndo *mlalo* kama mme na mke chini ya matakwa ya Mungu, pasingekuwepo nguvu ambayo ingevunja upendo huo, kwa sababu upendo ambao ungeumbwa miongoni mwao ungekuwa ni upendo yakinifu (usio badilika). Na baada ya kujikamilisha wenyewe, wasinge anguka kamwe. Nguvu ya kiwango cha chini ya upendo wa malaika mkuu isinge weza kuvuruga upendo kati ya mume mkamilifu na mke mkamilifu. Kulingana na amri ya Mungu 'usile' ilihitajika tu pale Adam na Hawa walipokuwa katika kipindi cha kuelekea ukamilifu wao.

**IV. MATOKEO YA ANGUKO**

**A. Shetani na mtu aliyeanguka**

Ni matokeo gani yaliletwa katika uumbaji kwa anguko la kiroho na kimwili la Adam na Hawa na Malaika Mkuu? Ebu tutafakari hili kwa kulinganisha matokeo ya anguko na kile ambacho kingetokea kama Adam na Hawa wasingeanguka, lakini waka timiza Baraka Tatu.

Kama Adam na Hawa wasingeanguka, lakini badala yake wakafikia ukamilifu wa tabia zao binafsi kwa kuwa mfano halisi wa upendo wima la Mungu, wangekuwa mme na mke, waki anzisha upendo mlalo wa Mungu, na wangezaa watoto wakiwa na uhalisia wa wema. Kisha, nafasi nne za Msingi ambazo wangeweza kupata uzoefu wa upendo wa utawala wa moja kwa moja wa Mungu unge timizwa. Lakini kwa sababu Adam na Hawa walianguka na wakawa mwilisho wa dhambi, kama matokeo ya upendo usiyo wa kanuni ulio nzishwa na malaika mkuu, Mungu, ambaye ni Bwana wa *Kanuni*, alitengwa na *Msingi wa Nafasi Nne za uongo*, uli anzishwa chini ya upendo batili wa Shetani, na Shetani ambaye kiubatili akajifanya kama bwana. Hii ndiyo sababu Biblia inasema, watu wa anguko ni watoto wa Shetani (Yoh. 8:44) na kwamba ni Mungu wa Dunia hii (II Wakor 4:4) na ni mtawala wa Dunia hii (Yoh. 12:31).

Kwa asili mtu ilikuwa atawale juu ya malaika, na juu ya uumbaji wote. Hata hivyo, Shetani ali jeuza hili na kuja kutawala  watu na Ulimwengu wote.




Kwa hiyo, kama ilivyo katika Warumi 8:19 anasema, '…….. uumbaji unasubiri kwa shauku kwa kufunuliwa watoto wa Mungu……'. Kwa sababu ya anguko la mtu, vitu vyote vinalia ili vikombolewe kutoka katika utawala wa shetani na kupata uzoefu wa utawala wa watu wa kweli.

**B. Matendo ya Shetani katika Dunia ya Anguko**

Je, Shetani anadhibiti vipi dunia ya anguko? Hata Shetani ambaye ndiye 'mtawala wa Dunia hii' anaweza kufanya vitendo vya ushetani pale anapokuwa na mlengwa ambaye ana msingi wa ushirika naye.




Walengwa wa shetani ni watu wenye roho ya uovu (wale wanaoishi katika dunia ya kiroho), walengwa ni nafsi za roho za watu waishio Duniani, na bila shaka, walengwa ni wanaohusiana na nafsi za roho ni miili yao wenyewe. Kwa hiyo, nguvu ya Shetani, ujionyesha hapa duniani, kupitia kwa watu kwa msukumo wa roho za uovu kutoka dunia ya kiroho. Zaidi ya hapo kwa kuwa shetani ni kiumbe wa kiroho, anaweza kujidhihirisha mwenyewe kupita wakati na mahali, ilimradi tu awe na msingi wa mshirika. Pale Luka 22:3 anaposema Shetani alimwingia Yuda Iskarioti ina maana kwa kuweka msingi wa ushirika na kuwa na uhusiano wa kutoa na kupokeana na shetani, Yuda akawa chombo cha Shetani. Kukomboa Ufalme wa Mbinguni Duniani maana yake ni kutimiza Dunia ambayo Shetani hawezi kutenda kabisa. Ili kufanikisha hili, kila mtu lazima kwa utimilifu akate uhusiano wake na Shetani na akomboe uhusiano wake na Mbingu, awe na uhusiano wa kutoa na kupokea na Mungu pekee.

**C. Wema na Uovu katika Mtazamo wa Dhumuni**

Kama Adam na Hawa wangekuwa mfano halisi wa wema na kuunda nafasi nne za Msingi kwa upendo chini ya matakwa ya Mungu, wangelitimiza Dunia ya wema. Bado, kwa sababu wali husiana kwa njia ya upendo ambao ulienda katka mwelekeo tofauti kusudi na la Mungu, wakawa mfano halisi wa uovu, na ku anzisha nafasi nne za Msingi za uongo (chini ya shetani), na walianzisha Dunia ya uovu.

Ingawa katika hatua za awali za maendeleo ya wema na uovu kimatendo uonekana kushabiana, wakiwa wanajongea mbele kutimiza malengo yao ya ukinzano wanajikuta wametengana na wako tofauti. Wema na uovu hautambuliwi kiasili na kitendo maalum au aina ya kitendo na matokeo yake yenyewe lakini utambulika pale ambapo msukumo, mwelekeo na lengo vinaelekea, matakwa ya Mungu au matakwa ya shetani.




**D. Dhambi**

Dhambi ni kitendo au wazo ambalo huvuruga *sheria za kimbingu**, hujenga sharti ambalo mhusika huwa na uhusiano wa msingi na shetani na huingia katika uhusiano wa tendo la kutoa na kupokea pamoja naye moja kwa moja au isiyo moja kwa moja. Katika dunia adilifu ambapo Mungu alidhamiria, dhambi haipo, pasingekuwepo tendo la dhambi katika ukanda wa mapenzi ya Mungu, sababu shetani asingekuwepo pale. Matokeo yake ile hali ya Adam na Hawa kujenga uhusiano wa tendo la kutoa na kupokea na shetani na kutenda dhambi, mtu huishi katika dunia iliyo kinyume – cha – kanuni na hutenda dhambi kwa kuwa mshirika wa shetani, moja kwa moja au isiyo moja kwa moja




---

*Sheria za Kimbingu ni *Kanuni* zinazo husika katika mwenendo halisi wa mtu.

Dhambi inaweza kuwekwa katika kundi  kama Dhambi ya Asili. Dhambi ya kurithi, Dhambi ya pamoja na Dhambi mtu binafsi. Dhambi ya Asili ni dhambi inayotokana na kuanguka kiroho na kimwili kwa mme na mke wa kwanza. Ni mzizi wa kila dhambi. Dhambi ya kurithi ni dhambi inayorithiwa kutoka kwa

wahenga wa mhusika kupitia nasaba za damu kama inavyotajwa katika amri kumi (Kutoka 20:5). Dhambi hii ni kama shina la mti.  Dhambi ya pamoja si dhambi ya mtu husika au ya urithi, lakini ni dhambi ambayo kila mmoja anawajibika kwa sehemu fulani kama mwachama wa familia. Ukosefu wa imani wa Yohana Mbatizaji, makuhani wakuu, wanasheria dhidi ya Yesu, wali husika katika kusulubishwa kwake (Yesu) Ingawa watu wachache walihusika moja kwa moja katika kumsulubisha, wakristu, hasa, na watu wote kwa ujumla, wamebebeshwa wajibu juu ya dhambi hiyo na matokeo yake wengi wameteseka sana. Dhambi ya pamoja ni kama matawi ya mti. Dhambi  ya mtu binafsi ni dhambi itendwayo na mtu mwenyewe. Na dhambi kama hiyo hufananishwa na majani ya mti. Dhambi zote hutokana na dhambi ya asili, ambayo ni mzizi wa dhambi zote. Hivyo mtu hawezi kusafishwa dhambi nyingine bila kwanza kusafishwa dhambi ya asili.

**E. Hulka ya Anguko (chembechembe za anguko)**

Malaika na mwanaume na mwanamke wa kwanza waliumbwa na lengo la kuwa wema na walitakiwa kuwa na *hulka asili* pekee ambayo walijaliwa ndani mwao wakati walipoumbwa. Kabla ya Anguko, sehemu linganifu ya malaika mkuu katika utaratibu mzima wa Uumbaji haikuwa waziwazi. Mwanaume na mwanamke wa kwanza walikuwa katika hatua ya kukua, kwa maneno mengine walikuwa bado hawaja kamilika  kulingana na uasili wao.  Malaika mkuu na Hawa, na baadaye Hawa na Adam wa anguko, walifanya mapenzi batili, kabla

hawajakamilika. Wakati wa anguko, ile asili njema ghafla uligeuzwa katika uelekeo haramu, na uelekeo huu haramu wa “uasili“ ukawa *Hulka ya anguko* la mtu (chembechembe za anguko). Hii Hulka ya anguko (chembechembe za anguko) ilipitishwa toka malaika mkuu kwa Hawa, toka Hawa alieanguka kwa Adam, na toka Adam na Hawa hadi katika ukoo wao wote. Asili ya hulka ya anguko ni hii “asili“ ya mwelekeo mbaya. Mwisho wake, ile “asili“ ya mwelekeo mbaya ndio asili ya msingi ambayo inatoa hulka ya anguko yote kwa mtu alieanguka. Katika *Kanuni* inaitwa *Hulka ya anguko asilia.*

Chanzo cha hulka ya anguko (chembecbembe za anguko) kili ibuka kutoka katika fikra za malaika mkuu kwa kuhisi upungufu wa upendo kutoka kwa Mungu baada ya Mungu kuumba mtu. Hali hii ya kujihisi kupewa upendo – pungufu ilikuwa ni matokeo yasiyoepukika kwa malaika kwa sababu ndani yake ali jaliwa matamanio na busara katika hulka asilia. Hata hivyo, isingezuilika vilevile kwamba malaika mkuu alianguka kwa sababu ya matamanio ambayo aliumbwa nayo. Pale ambapo binadamu angejikamilisha yeye mwenyewe na kumpenda malaika mkuu kama Bwana wa (malaika mkuu) hisia ya upendo pungufu ingetoweka. Hata katika kipindi mtu akiwa haja komaa, pale upungufu wa upendo wa Mungu ulihisiwa na malaika mkuu kama malaika mkuu ange dumisha uelekeo wake wa asili, akisubiri upendo wa mungu na katika msimamo kwa Mungu pekee, malaika mkuu asingeanguka. Hata hivyo, hisia za kukatiliwa za malaika mkuu zili msababisha kubadili uelekeo wake na kujitegemea yeye mwenyewe, alijijengea hisia ya wivu mkubwa kwa Adam. Wakati Hawa aliporidhia hisia za malaika mkuu, aliweka msingi – mshirika na malaika mkuu ambao uli sababisha uhusiano batili na anguko.

Tunaweza kutenganisha asili ya hulka ya anguko (chembechembe za anguko) katika hali nne kuu.

Kwanza, msukumo wa kuanguka kwa malaika mkuu uliegemea katika kushindwa kwake kumuona Adam kwa mtazamo wa Mungu, kushindwa kwake kumpenda Adam kama jinsi Mungu alivyompenda. badala yake alichukua uelekeo wake na kuwa na wivu dhidi ya Adam. Hali hii huonekana wazi pale mwanafunzi wanapo muonea wivu mwalimu badala ya kumpenda kama mwalimu ampendavyo. Matokeo haya yana asili yake katika asili ya hulka ya anguko (chembechembe za anguko).




Jambo lingine la pili kuu la hulka ya anguko ni asili ya kuacha nafasi aliyopewa mhusika. Tamaa nyingi ya malaika mkuu kutaka kupokea upendo zaidi kutoka kwa Mungu na kufaidi nafasi sawa ya upendo katika jamii ya watu kama alivyofanya katika ukanda wa malaika uli sababisha kuacha nafasi yake na kuanguka. Vitendo ambavyo mtu aliyeanguka huvifanya zaidi ya ukomo wa nafasi zao na mamlaka ili kutimiza tamaa haramu ni vielelezo vya asili hii ya hulka ya anguko, (chembechembe za anguko)




Jambo lingine la tatu la hulka ya anguko ni hali ya kugeuza uataratibu wa utawala. Malaika hatimae alikuwa awe chini ya utawala wa mtu, lakini alimtawala Hawa, na kugeuza utaratibu fasaha. Hawa alipaswa awe chini ya utawala wa Adam, lakini akamtawala. Mageuzi haya ya

utawala yali sababishwa na anguko. Utaratibu mbalimbali usio wa kawaida katika dunia ya anguko una asili yake katika  hulka ya anguko, (chembechembe za anguko)




Jambo la nne ni asili ya kuzidisha matamanio yasiyo na haki  na matendo ya dhambi. Kama Hawa asinge zidisha uhalifu wake kwa kumshawishi Adam baada ya anguko lake, Adam asingeanguka. Kumkomboa Hawa peke yake kungekuwa rahisi kiulinganifu.  Hawa alichukua tamaa haramu ile ya malaika mkuu 'kula tunda la mema na mabaya' na tendo lake la dhambi la kutomtii Mungu na kufanya matakwa yake na uelekeo, na hivyo kuzidisha matakwa na matendo ya malaika mkuu. Nia isiyo ya haki na kuto kutii  viliongezeka kwa Adam,  na hivyo anguko likatokea.  Ukweli kwamba katika Dunia ya anguko,  uovu hupokelewa na kuzidishwa zaidi ya wema ni udhihirisho wa asili hii ya  hulka ya anguko, chembechembe za nguko.


Mungu
Malaika Mkuu
Neno
Neno
Adam
HAWA
Ukoo
Kuzidisha dhambi

## CHAPTER THREE   THE PURPOSE OF THE MESSIAH

## SURA YA TATU

## KUSUDI LA MASIHI

### I. KUSUDI LA MUNGU KATIKA MPANGO KWA AJILI YA WOKOVU .

Kila mtu huumbwa kama mtoto wa Mungu. Pale anapojikamilisha mwenyewe na kuwa kama chombo cha wema, huishi katika ufalme wa Mungu hapa duniani na katika dunia ya kiroho. Sababu ya Mungu kuumba ni kujisikia raha kwa kuwahisi wanae wakiishi katika Ufalme wa Mbingu, ambao ni Dunia ya upendo wa Mungu na moyo wake. Ni ule wenye kujengwa kupitia na chini ya msingi wa kukamilika kwa baraka tatu. Hata hivyo, kwa sababu ya Anguko la Wahenga wa kwanza wa watu, mtu akawa mwilisho wa dhambi na uovu, na tangu hapo amekuwa akiishi katika mateso pande zote za hapa duniani na katika dunia ya kiroho,  na dhumuni la kuumba bado halijakamilika. Je, Mungu aache lengo lake la msingi kuumba na kulitelekeza bila kulikamilisha? Hapana hatoweza.

Kama anavyosema katika Isaya 46:11, “Nimenena nami nitatekeleza, .nimekusudia nita fanya“ Mungu kwa uhakika atatimiza kusudio lake. Mungu wa upendo hawezi kumwacha mwanae katika hali hiyo ya




anguko, sababu mtu aliumbwa kama mtoto wake. Badala yake, Mungu amekuwa akifanya juhudi kwa ajili ya wokovu wa mtu.

Je wokovu ni nini? Wokovu ni ukombozi: kumwokoa mtu anayekufa ni kumkomboa au kumwopoa na kurudia hali yake ya kawaida; kumwokoa mtu anayekufa maji ni kumwopoa na kumrudishia hali yake ya kabla kuanza kuzama. Wokovu wa Mungu kwa mtu ni ukombozi wa Mungu wa mtu aliyeanguka na mwenye dhambi katika hali yake ya asili ya wema kurudi katika nafasi ambayo anaweza kutimiza lengo la uumbaji.

Hivyo, lengo la Mungu la wokovu ni kukomboa mtu kurudi hali ya kutokuwa na dhambi, ile hali aliyoiumba Mungu na kumfanya awe binafsi mwadilifu, na kuanzisha familia adilifu chini ya msingi wa mtu huyo, na kuanzisha jamii adilifu, taifa, na dunia, katika msingi wa familia hiyo adilifu.

## II. KUKAMILIKA KWA MPANGO WA WOKOVU NI KUKAMILIKA KWA DHUMUNI LA UUMBAJI.

Kama mtu angetokea kuwa wa thamani hiyo ya uadilifu, tuseme mtu aliyekombolewa amedhihirisha baraka ya kwanza, huyu atakuwaje? Mtu huyu mkamilifu atakuwa na uhusiano

sawa kwa Mungu kama mwili wa huyo mtu ulivyo kwa akili yake. Akili hukaa mwilini, mwili hutenda kadiri akili inavyouelekeza. Vilevile, mtu mkamilifu ni hekalu la Mungu, na Mungu anakaa akilini mwake. Mungu huwa kiini cha mawazo na matendo yake, kiini cha maisha yake. Mtu wa namna hiyo mwenye ukamilifu wa Tabia hupata uadilifu wa umoja na Mungu, kama vile miili yetu huafikiana na akili zetu. Hili limeelezwa katika waraka wa I kwa Wakorintho 3:16, ambao unasema 'je, hamjui kwamba ninyi ni hekalu la Mungu na kwamba roho ya Mungu inaishi ndani yenu?' na Yohana 14:20 anasema 'katika siku hiyo mtatambua ya kuwa nimo ndani ya Baba na Ninyi ndani mwangu, na mimi ndani yenu?

Kama Adam na Hawa wangejikamilisha wakati huo katika maisha yao Bustani ya Eden je, wangehitaji sala, maisha ya dini, au mwokozi? Kwa nini sala ingekuwa ya lazima kwa waliokuwa wakiendelea kuishi kuwasiliana moja kwa moja na Mungu? Kama maisha ya dini ni maisha ya imani ambayo mtu aliyeanguka huwa nayo katika giza akimtafuta Mungu aliyempoteza, na hivyo kwa nini mtu mkamilifu anayeishi kila siku kama hekalu la Mungu angehitaji namna yeyote ya kuabudu? Hivyo kama mtu asingeanguka katika Bustani ya Eden, pasingekuwepo makanisa au biblia, hakuna mihadhara, hakuna mikesha ya maombi, hakuna mikutano ya mwamsho, hakuna mambo ya namna hiyo. Watu wote watataka kuishi kama walio mwilishwa na wema, akimtumikia Mungu kila siku maisha yake yote. Ni kama wale ambao hawaja zama katika maji hawahitaji mwokozi, watu wakamilifu, wasio na dhambi, hawahitaji mwokozi.




Kama mtu angeanzisha familia adilifu, akatimiza Baraka ya Pili ya Mungu, familia kama hiyo ingekuwaje? Kama Adam na Hawa wangekuwa mume na mke wakimwilishwa katika wema, wakizaa watoto walio mwilishwa na wema, familia hii ingekuwa kiini cha kabila lisilo na

dhambi, jamii, taifa, na dunia. Kupitia familia hii, Ufalme wa Mbingu ungeanzishwa, na kutokea katika familia hiyo jamii adilifu ya familia moja ya Dunia inge endelea, kwa nasaba moja ya 'wazazi wa kweli' (mume na mke wa kwanza) na vizazi visivyo na dhambi vinavyonyumbulika na kustawi kwa siha njema. Mpango kwa ajili ya wokovu wa Mungu ni kuendeleza watu wa Mbingu wa namna hiyo, watu waliotimiza Baraka tatu za Mungu na hivyo kujenga Ufalme wa Mbinguni.




Ni kwa sababu hii, Mungu alimtuma mwanae, Yesu Kristu, kama Mwokozi wa dunia hii. Hivyo, Masihi lazima asimame mbele za Mungu kama chanzo cha waadilifu wote na lazima aanzishe familia adilifu, ambayo ina timiza kusudi la uumbaji na mahali ambapo upendo wa Mungu unaweza kudumu. Lazima aanzishe taifa na dunia adilifu, na hapo ata timiza lengo asilia la Ufalme wa Mungu duniani, na hili ndilo kusudi la Masihi kuja.

### III. MPANGO WA WOKOVU KUPITIA MSALABA.

#### A. Kusulubishwa kwa Yesu.

Mungu kweli aliwapenda watu wateule wake, Waisraeli, ambao walikuwa wawe msingi wa kuja kwake Masihi. Mara nyingi Mungu alitabiri kuja kwa Masihi na hata ali waonya watu

wawe na tahadhari na kumsubiri. Mungu tena alimtayarisha shuhuda mkuu Yohana Mbatizaji, ili kumshuhudia Masihi. Kwa hakika Taifa la Israel lilikuwa na shauku kusubiri ujio wa Masihi.

Kwa masikitiko makubwa, hata hivyo, wateule walio andaliwa walishindwa kumtambua Masihi alipokuja. Mwana wa Mungu ali lalama kuwa yeye ndiye Mwana wa Mungu, lakini maneno yake yaliangukia katika masikio ya viziwi. Hakuna aliye muelewa kamwe ; alidhihakiwa na kuitwa mtu wa kufuru na hatimae akasulubiwa. Kinyume chake, viongozi wa wapagani wa wakati huo walijua usafi wa Yesu (Lk 23:14-16 ; Yoh 18:38 ; Mt 27 :19,23 ; Marko 15:10-14), na wakati huo waliomtia hatiani walikuwa ni watu wake na viongozi wa Uyahudi, ambao Mungu aliowalea na kuwatayarisha kwa muda mrefu. Hata hivyo walikuwa na shauku ya kumpeleka Yesu msalabani. Kwa nini?

Wakristu wamekuwa wakiamini kuwa kifo cha Yesu msalabani kili andikiwa na Mungu kama mpango wa asili . Hapana, haikuwa hivyo ! Lilikuwa ni kosa kubwa sana kumsulubisha Yesu Kristo. Usulubisho wa Yesu ulikuwa ni matokeo ya ujinga mkubwa wa watu wa Israel kuhusu mpango wa Mungu. Niya ya Mungu ili kuwa wazi kwa watu wateule kumkubali na kumwamini Yesu (Yoh. 6:29, 10:37, 38) na kupokea wokovu. Watu wa Israel hawakujua Yesu Mnazarethi alikuwa nani, na hata alivyokuwa anakufa msalabani, walimdhihaki, wakipiga kelele kwamba wangemwamini kama mwokozi pale tu angejinasua msalabani. Biblia inasema kuwa alikuja nyumbani kwake, na watu wake hawakumpokea, (Yoh. 1:11); na Mtume Paulo, anashuhudia kuwa, ‘’hakuna hata mtawala wa zama zile aliyejua hili; na kama wangejua, wasingemsulubisha Bwana wa Utukufu’ (I Wakor. 2:8).

Wakristo wa leo hawana uelewa mzuri wa ukweli ulio nyuma ya matukio kihistoria yaliyojiri wakati wa Yesu. Kama niya ya Mungu kwa ajili ya wokovu wa mtu ingelitimia kwa Kusulubishwa tu, kwa nini ilimchukua muda mwingi kutayarisha watu wateule? Je haikuwa kwa sababu hakutaka kumtoa mwanae kwa watu wasiokuwa na imani?

Katika bustani ya Getsemane, Yesu alisali “‘………Roho yangu ina huzuni nyingi, kiasi cha kufa ; kaeni hapa,mkeshe pamoja nami ….Baba yangu ikiwezekana, kikombe hiki kiniepuke…..’“ (Math26.38-39). Yesu alitamka sala hii si mara moja, ila mara tatu. Wakristo wengi wanaoamini kwamba jukumu la Yesu lilikuwa ni kuleta wokovu kwa kufa msalani, huelezea kuwa Yesu alitamka sala hili kutokana udhaifu wa kibinadamu. Lakini ilikuwaje kwa Yesu Kristu mwokozi wa watu atamke sala kutokana na udhaifu wa kibinadamu?

Mkristu shahidi, Mfia dini wa kwanza, Stephano, na mashahidi waliofuata, kamwe hawakusali katika hali hiyo ya udhaifu. Kwani waliwahi kuomba hata mara moja kusema ‘’naomba kikombe hiki kiniepuke’’, wakati wakifa? Tunaweza je kusema Yesu alikuwa dhaifu zaidi ya hawa mashahidi? Na hasa kama kuja kwake kulikuwa kuja kuwaokoa wote kwa kufa msalabani, je pange wezekana kuwepo sababu yeyote ya kuomba kuepuka msalaba?

Sala ya Yesu haikuwa ya ubinafsi au wasiwasi, aliyotamka kwa woga wa kufa. Kama kusulubishwa kulikuwa njia pekee ya Yesu kuwaokoa watu, angependelea kufa msalabani mara nyingi zaidi ya maelfu. Yesu alikuwa anasikitikia nafasi yake kama Masihi, ambaye

alikuwa atimize Lengo la Uumbaji Duniani. Moyo wake ulihangaika na kutafakari juu ya Mungu atakavyo huzunika kama mpango wake kwa ajili ya wokovu ungecheleweshwa. Yesu alionyeshwa tena mateso na kutokwa damu kwa wanafunzi na wafuasi wake, Wakristu, ambao wangefuata njia yake ya mateso na msalaba. Tena, alifadhaishwa na mtafaruku wa baadae ambao ungewapata watu wa Israel kama wangemkataa. Akiwa anazingatia haya katika akili yake, katika bustani ya Gestemania,




Yesu alitamka sala ya mwisho ya kukata tamaa kwa Mungu, akirudia kumuomba Mungu aendelee kumuacha awepo duniani, hata katika mazingira yasiyo na matumaini kama yale, ili aweze kuendelea na kazi yake ya kubadili mioyo ya watu mpaka ambapo wangemkubali.

Kama kifo cha Yesu msalabani kingekuwa kime pangwa na Mungu, na kwa nini Yesu akasema kwamba Yuda Iskariote, msaliti wake, '' '….ole wake mtu yule ambaye anamsaliti Mwana wa Mungu! Ingekuwa heri kama mtu huyo asingelizaliwa' '' (Math. 26:24); na tunaweza kuelezea vipi kilio cha Yesu msalabani '' '…….Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?' '' (Math. 27:46). Kama kusulubishwa ndilo kusudio asili la Mungu kwa Yesu, na hapo Yesu angejisikia safi mwenye raha pale msalabani kukamilisha kwa mafanikio jukumu lake.

**B. Kiasi cha wokovu unaopatikana kwa njia ya Msalaba na dhumuni la ujio wa kristu mara ya pili**

Kifo msalabani hakikuwa jukumu ambalo kwa asili Mungu alimpangia Yesu, Mwanae. Badala yake lilikuwa toleo la pili la adha kwa Mungu ambalo lililazimishwa na kukosekana kwa imani kwa watu wa Israel. Kitu gani kingetokea kama watu wa Israel wangemwamini Yesu na kumpokea, kumpenda na kuunganika naye? Kwa uhakika kabisa, wokovu kamili ungekuwa umepatikana. Kwa maneno mengine, Yesu angekuwa amejenga Ufalme wa Mbinguni hapa

duniani, mahali ambapo dhumuni la uumbaji lingekuwa limehitimishwa. Dunia ya Mungu ingekuwa imejengwa – dunia ambamo watu wote humwaamini na kumfuata Mwana wa Mungu. Watu wa Israel wangekuwa kiini cha utukufu wa Mbingu. Dunia ya Wayahudi na Wakristo wasingekuwa wamegawanyika, na wala Wakristo wa kwanza wasingeteseka na masumbuko ya kutisha. Zaidi ya hapo, kwa sababu ya Masihi kwamba angekuwa ametimiza jukumu lake, pasingekuwepo haja ya Ujio wa Pili.

Kwa kufahamu suala la wokovu kwa mwangaza huu, tunaweza kuona kuwa kusulubishwa kwa Yesu ilikuwa mpango wa pili wa wokovu na hivyo kutoa *'wokovu wa kiroho'* tu. Pale watu walipotokea kutomwamini Yesu na kumuacha, Mungu ilibidi alipe gharama ya ukosefu wa imani wa Waisrael na watu kwa kutoa maisha ya Mwanae wa pekee kwa Shetani kama fidia. Matokeo yake, Shetani aliharibu mwili wa Yesu kwa kumwangika msalabani, na damu ya Yesu msalabani ikawa malipo kwa ukombozi wa watu.

Kwa kufufua Yesu aliyesulubiwa, Mungu alifungua njia ya wokovu kiroho, njia ambayo ni ukanda huru dhidi ya shambulio la Shetani. Ushindi wa Mungu haukuwa usulubisho, lakini kwa ufufuko wa Yesu. Kama matokeo ya usulubisho, miili ya watu bado inashambuliwa na Shetani, hata hivyo ingawa walikusudiwa kuokolewa kwa mtu kumwamini Yesu na kupandikzwa kwake (War. 11:17). Ni roho tu ya mwanadamu inaweza kupata wokovu kwa sharti la kushiriki ufufuko kwa imani ya mtu katika Kristo Mshindi. Miili yetu bado inahitaji ukombozi (War. 8:23).

**Kama Watu wa Israeli wangelimfwata Yesu**

**1** Ufalme wa Mbinguni ungejengwa hapa duniani

**2** Hakuna kugawanywa kwa Uyahudi na Ukristo

**3** Hakuna mateso kwa Wakristo

**4** Hakuna Ujio wa Pili




Hivyo, hata baada ya kutokea Yesu duniani, dunia inaendelea kufadhaishwa na nguvu za Shetani, na dhambi inadumu katika miili ya binadamu kila mahali. Mtume Paulo alilia, ''…Ole wangu, maskini mimi ! Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti ? …mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu naitumikia sheria ya dhambi. (War. 7:24-25). Yeye kama mtawa, alikuwa mcha Mungu na katika rehema ya Bwana, lakini mwili wake uliendelea kukandamizwa na dhambi. Toba hii haishii kwa Paulo peke yake, lakini kwa kila mtu aliye hai. Hii ndiyo sababu, Biblia inatuambia ''tusali kila mara'' (1Wathes. 5:17)- juu ya kutulinda dhidi ya shambulio la shetani. Vile vile 1Yoh. 1:10 inasema ''kama tukisema hatujatenda dhambi, tunamfanya yeye mwongo…'', akitwambia bado tuko chini ya pingu za dhambi ya asili. Hakuna hata mmoja ambaye amesafishwa dhambi ya asili. Ni kwa sababu hii Masihi atatokea tena duniani, kuondoa dhambi zetu kabisa kabisa na kujenga Ufalme wa Mbingu duniani, akihitimisha Dhumuni la Uumbaji.

**C. Utabiri wa aina mbili juu ya Masihi.**

Kama kifo cha Yesu msalabani hakikuwa muhimu ili kutimiza kusudi la kimasihi, ni kwa nini Isaya 53 anabashiri mateso na kifo cha Masihi? Hapa lazima tukumbuke kuna aya nyingine katika Biblia zinatabiri kuwa Masihi atakuja kama mwana wa Mungu mfalme wa wafalme na atakayeleta ufalme wa Mbingu duniani. Tabiri hizi zinatokea katika Isaya 9:11 na 60, katika aya nyingine katika Agano la Kale, na katika Luka 1:31-33.

Pale Mungu alipomuumba mtu wa kwanza, alimuumba akue afikie ukamilifu kwa njia tu ya mtu kutimiza wajibu wake. Mtu anaweza kutimiza wajibu wake kama Mungu anavyomtaka, au kinyume anaweza kushindwa kutimiza. Kitaratibu, ilikuwa lazima kwa Mungu atoe aina mbili za utabiri kukamilisha Kusudio Lake.

Ni wajibu wa Mungu kumtuma Masihi, lakini ni wajibu wa mtu kumwamini. Bahati mbaya, kwa kutomkubali Yesu, Waisrael walishindwa kutimiza wajibu wao; hawakutimiza utabiri wa awali wa ujio wa Masihi, ambao umo katika Isaya 9,11 na 60 na Luka 1:31-33, lakini kinyume wakachukulia utabiri wa pili wa matokeo ya mateso kwa Masihi, katika Isaya 53.




## IV. YOHANA MBATIZAJI NA KURUDI KWA ELIA.

### A. Masihi na Eliya.

Katika suala hili, kuna jambo moja ambalo lazima tulidadisi hilo linalohusu mpango wa Mungu kuwa Yesu kupitia njia ya msalaba. Mungu amerudia akitabiri mara kwa mara kwa watu wateule juu ya kuja kwa Masihi, na wateule wenyewe walikuwa wakimsubiri kwa shauku na kufurahia ujio wake. Je, Mungu aliwezaje kumtuma Masihi katika hali ambayo watu wateule hawakuweza kumtambua? Je, yalikuwa mapenzi ya Mungu wasimtambue na kumpokea Masihi? Au, je, wateule walishindwa kumtambua mbali na ufunuo wa jinsi ambavyo angekuja?

Ili kupata majibu ya maswali haya, hebu tuchunguze ujio wa pili wa Eliya. KatIka kitabu cha Malaki ambacho ni kitabu cha mwisho cha unabii katika Agano la Kale, ilisemewa, " 'Angalieni, nitawapelekea Eliya nabii, kabla haijaja siku ile ya Bwana, iliyo kuu na kuongofya .........'" (Malaki 4:5,6). "Siku kuu na ya kutisha" inayosemewa ni ya wakati wa kuja kwa Masihi, na hivyo unabii huu unaonyesha kwamba kabla ya kuja kwake Masihi, Eliya lazima kwanza arudi.

Eliya alikuwa nabii mkuu wa Israel aliyekuwepo miaka mia tisa kabla ya Yesu. Kuna maandishi ya juu ya kupaa kwake Mbinguni juu na gari la moto (2Wafalme 2:11). Waisrael waliokuwa wakimsubiri Masihi walikuwa hasa awali wakizingatia hasa ujio wa nabii wa kihistoria, Eliya. Hii ni kwa sababu Agano la Kale halikutabiri kwa dhati ni lini Masihi atakuja, lakini kwa uwazi lilionyesha kuwa Eliya atamtangulia.

Ilikuwa ni katika mazingira kama haya kwamba Yesu alitokea, akijitangaza kuwa Masihi. Aliwaambia Wayahudi kuwa yeye alikuwa Mwana wa Mungu -hili kwa watu hawa walimwona tu kama mvulana kutokea Nazareti. Walikuwa bado kusikia habari zozote juu ya kuja kwa Eliya, hivyo waliuliza "Inawezekanaje Yesu Mnazareti kuwa Mwana wa Mungu?"

Na pale wanafunzi wake walipotoka kwenda katikati ya watu wa Israeli, kushudia juu ya Yesu, watu walikuwa na mashaka kwamba Yesu alikuwa Masihi na kuwapa changa moto kwa kuwauliza wanafunzi juu ya Eliya yuko wapi, kwani Eliya alikuwa amtangulie Masihi. Hivyo wanafunzi wake Yesu walimrudia na kumuuliza Yesu, " '..........eti kwanini waandishi hunena ya kwamba imempasa Eliya kuja kwanza?'" (Mt. 17:10). Yesu akajibu, " '.........Kweli Eliya yuaja kwanza, naye atatengeneza yote, ila nawaambia ya kwamba Eliya amekwisha kuja, wasimtambue, lakini wakamtenda yote waliyotaka.......' Ndipo wale wanafunzi walipofahamu ya kuwa amesema nao habari za Yohana Mbatizaji" (Mt. 17:10-13)

Yesu alijua maana ya swali muhimu la waandishi na kuonyesha kuwa Yohana Mbatizaji alikuwa ujio wa pili wa Eliya. Wanafunzi wa Yesu waliweza kuamini kirahisi juu ya jambo hili, lakini Waisrael wangeweza kuamini jambo hili? Yohana Mbatizaji, hakuja kutoka Mbinguni, na yeye binafsi alikana kuwa yu Eliya (Jn 1:21). Yesu mwenyewe alijua watu wasingekubali hili kirahisi, akisema




"'……….Na ikiwa mnataka kukubali, yeye ndiye Eliya atakayekuja,' " (Mt. 11:14).

Yesu alisema Yohana Mbatizaji alikuwa Eliya ambaye watu walimsubiri kwa muda mrefu, lakini kwa kuwa yeye mwenyewe Yohana Mbatizaji binafsi aljikana ni yupi watu wangemwamini? Kwa kawaida, ingetegemea na jinsi gani watu wa wakati ule walivyo mtazama Yesu na Yohana Mbatizaji.

Kwanza, Yesu alionekanaje mbele ya Waisraeli kwa wakati huo? Yesu alikuwa ni kijana asiye eleweka vizuri katika nyumba nyenyekevu ya fundi seremala na hakujulikana kuwa na uzoefu wa taaluma za kiroho. Bado Yesu alijitangaza kuwa Bwana wa sabato (Mt. 12:8), alijulikana kama mpiga marufuku sheria (Mt 5:17), alikuwa rafiki wa watoza ushuru na watenda dhambi, na alijulikana kama mlafi na mlevi (Math. 11:19). Alijiweka kuwa hatua sawa na Mungu (Yoh. 14:9-11) na akawaambia watu kuwa wampende zaidi ya mtu mwingine yeyote (Math. 10.37). Sababu hii, viongozi wa Wayahudi walifika kiwango kia kusema Yesu alikuwa akifanya kazi zake kwa nguvu ya Beelzebul, mkuu wa mapepo (Math. 12:24).

Na upande mwingine, Waisraeli wa nyakati hizo walimuonaje Yohana Mbatizaji? Alikuwa mwana wa familia mashuhuri, na miujiza tangu atungwe mimba na kuzaliwa kwake ilijulikana inchi nzima (Lk 1:5-66). Alipokuwa mtu mzima aliishi kwa kula nzige na asali huko jangwani, na hivyo kwao, aliishi maisha ya mfano kama mtu wa imani. Kwa kweli, Yohana alionekana mtu wa kiwango cha juu kiroho kwa makuhani wakuu na watu wa kawaida, nao waliuliza kama yeye hakuwa yule Masihi (Lk 3:15, Yoh 1:20)




Katika mazingira ya aina hii, watu wa Israel walijifanya kumwamini zaidi Yohana Mbatizaji, ambaye aligoma hakuwa Eliya, kuliko kwa Yesu, ambaye aliwaambia kuwa Yohana Mbatizaji ndiye Eliya. Watu wakaamua kuwa hoja ya Yesu kuwa Yohana Mbatizaji alikuwa Eliya ilikuwa si ya kusadikika, na walifikiri alisema hivyo ili aaminike kwa madai yake juu yake mwenyewe.

**B. Jukumu la Yohana Mbatizaji.**

Je, ni kwanini basi Yesu alisema Yohana Mbatizaji ni Eliya? Kama ilivyo katika Lk. 1:17 inaonyesha Yohana Mbatizaji alikuwa na jukumu kama la Eliya. Watu wa Israel walikuwa wakiamini maneno ya Agano la Kale kama yalivyo, walichukulia kuwa Eliya mwenyewe kabisa atashuka chini kutoka Mbinguni. Lakini Mungu alimchagua Yohana na akamtuma na jukumu kama la Eliya.

Yohana Mbatizaji alitangaza kuwa alitumwa kabla ya Masihi (Yoh. 3:28):, 'kunyoosha njia ya Bwana' (Yoh. 1:23). Akiwa mtu wa namna ya pekee muhimu, Yohana, kwa busara zake, ali paswa kujua yeye mwenyewe kuwa ni  Eliya.

Wengi wa makuhani wakuu na watu wa Israel waliomheshimu Yohana Mbatizaji walifikiri labda yeye ni Masihi. Kwa hiyo, kama Yohana Mbatizaji angejitangaza kuwa Eliya na kushuhudia kuwa Yesu ndiye Masihi, wa yahudi wa wakati huo wangeweza kumtambua na kumpokea Yesu, na hapo kupata wokovu.  Kisha familia ya Yesu ambapo historia yake ilionyesha kutokuwa na uzoefu kiroho lisingekuwa tabu.  Hata hivyo, kwa sababu ya kuto kujua

mpangp wa Mungu, Yohana Mbatizaji alisisitiza kwamba yeye hakuwa Eliya. Hii ilikuwa sababu kuu iliyowazuia watu wa Israel wasije kwa Yesu.

Tunasoma katika Mathayo 3:11, Yohana Mbatizaji alisema kuwa alibatiza kwa maji, lakini yule anayekuja nyuma zake (Masihi) atabatiza kwa Roho Mtakatifu na moto ; alisema alikuwa hastahili kufungua gidamu ya kiatu chake (Yoh. 1:27). Vile vile katika Yoh. 1 :33, Yohana akasema , ‘’ ‘mimi binafsi sikumjui ; lakini yeye (Mungu ) aliyenituma kubatiza kwa maji aliniambia kuwa, ‘’yule ambaye utaona Roho anashuka na kukaa kwake, huyu ndiye abatizaye kwa Roho Mtakatifu [Kristu]’’. Na nimeona na kushuhudia kwamba huyu ni Mwana wa Mungu.’ ’’ Hivyo Mungu alimpa Yohana Mbatizaji ufunuo wa moja kwa moja kwamba Yesu ni Mwana wa Mungu. Pamoja na kwamba mwanzo Yohana alitimiza jukumu la kumshuhudia Yesu, kwa masikitiko hakumshuhudia kwa maisha yake yote.

Baada ya kukutana na Masihi, kila mtu lazima amwamini na kumtumikia maisha yake yote. Hili ni kweli hasa kwa Yohana Mbatizaji, ambaye alikuja na jukumu la Eliya, ambalo lilikuwa ni kuandaa njia ya Masihi (Lk 1:76). Kwa hiyo, Yohana ilimbidi amtumikie na kukaa na Yesu kama mmoja wa wanafunzi wake. Baba wa Yohana Mbatizaji aliambiwa juu ya jukumu mwanae wakati wa alipozaliwa na akatabiri na kusema, ‘’…………’Na wewe, mtoto, utaitwa nabii wa aliye juu, kwani utaenda mbele zake Bwana kuandaa njia yake, kutoa habari za wokovu kwa watu wake………..’ ‘’ (Lk. 1:76,77). Hata hivyo, hatupati ushahidi katika Biblia ambapo Yohana Mbatizaji alimtumikia Yesu.

Kabla ya Yohana Mbatizaji kufa gerezani, akiwa ameishi bila kutimiza jukumu lake la kumtumikia Yesu, alianza kuwa na mashaka juu ya maisha yake na ya Yesu na akatuma wanafunzi wake kwa Yesu kuuliza, ‘’…..’ Je, wewe ndiye yule ajae au tumsubirie mwingine?’ ‘’ (Math. 11:3). Kifungu hiki kinaonyesha bila mashaka kwamba Yohana hakumwamini Yesu na wala hakumtumikia kabisa.

Yesu ali udhika kwa swali kama hilo na akajibu kwa kuhukumu, ‘’ ‘…….Naye heri awaye asiyechukizwa nami’ ‘’ (Mathayo 11 :6), akionyesha kwamba ingawa wa Israeli walikuwa na heshima kubwa kwa Yohana, lakini Yohana aliishindwa katika jukumu lake

Yesu alisema tena, ‘’ ‘… Amin, nawaambieni, Hajaondokea mtu katika wazao wa wanawake aliye mkuu kuliko Yohana Mbatizaji ; walakini aliye mdogo katika Ufalme wa Mbinguni mkuu kuliko yeye’ ‘’ (Math. 11:11). Mmojawapo alikuwa mkuu sana kuzaliwa na mwanamke, kwa uhakika atakuwa vilevile mkuu katika Ufalme wa Mbinguni. Basi, ingekuwaje Yohana Mbatizaji, ambaye alizaliwa kama mkuu katika historia, awe mdogo zaidi ya mtu mdogo sana Mbinguni?

Mungu alimtuma Yohana Mbatizaji kama mkuu wa manabii, kwa sababu alikuwa amtumikie Masihi na kumtangaza mbele za watu wote. Lakini alihindwa kutimiza jukumu lake. Mathayo 11:12 pia inaeleza hili kwa kusema, ‘’ ‘Tangu siku za Yohana Mbatizaji mpaka sasa Ufalme wa Mbinguni hupatikana kwa nguvu, nao wenye nguvu wauteka.’ ‘’ . Kama Yohana Mbatizaji angemtumikia Yesu vizuri, akitimiza wajibu wake, angekuwa mwanafunzi mkuu ; lakini kwa

vile alishindwa, Petro, ambaye alijitahidi sana miongoni mwa wanafunzi wa Yesu, akawa kiongozi wa wale Kumi na Wawili.

Ili kuandaa watu wa Israel wawe na imani katika Yesu, Mungu alitoa shuhuda nyingi kwa wazazi wa Yohana, Zakaria na Elizabeti, ambao walikuwa wawakilishi wa Uyahudi wa wakati huo. Mungu aliendelea kufanya miujiza kwamba watu wangeweza kukubali yeye ndiye alikua anatumika moja kwa moja kwa kutungwa mimba na kuzalikwa kwa Yohana Mbatizaji. Bila shaka Yohana aliambiwa na wazazi wake juu ya uhusiano wake na Yesu, na kama ilivyoelezwa hapo juu, lazima alipokea ufunuo kwa wingi moja kwa moja toka kwa Mungu.

Bado, mbali na maandalizi yote haya Yohana Mbatizaji alishindwa kwa sababu ya kutokuamini na ujinga wake wa kutokuelewa mambo. Zaidi ya hayo, ujinga wa kutoelewa yeye mwenyewe na kutokuamini kwake hakuku sababisha kupoteza binafsi tu, lakini pia kwa kuwafanya wengine washindwe kuamini na mwisho kusababisha Yesu kusulubishwa.

## CHAPTER FOUR

## THE CONSUMATION OF HUMAN HISTORY

## SURA YA NNE

## UKAMILISHO WA HISTORIA YA BINADAMU

Ebu tujadili dhana ya kibiblia ya *Siku za Mwisho*. Biblia inatuambia kuwa katika Siku za Mwisho mbingu zitapita na vitu vingine vitateketezwa kwa moto (2Petro 3:10), na inatuambia kuwa jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka kutoka mbinguni (Math 24:29). Inaendelea kutabiri kuwa kwa mlio wa tarumbeta (parapanda, baragumu) la Mungu, Kristo atarudi, na waumini wa Kristo waliokufa watafufuka na kukutana naye hewani, wakifuatiwa na waumini wale walio hai Kristo arudipo (1Wathes 4:16,17).

Je, bashiri hizi zitatokea kama zilivyoandikwa (fasihi), au zichukuliwe kama ishara , kama vipengele vingine katika Biblia? Ebu tujibu haya maswali kwa kuelewa historia ya binadamu. Je, historia yake ilianzaje? Inaelekea wapi? Hatima ya lengo lake ni lipi?

### I. MAANA YA SIKU ZA MWISHO.

Ni dunia ya namna gani kama Adam na Hawa wangetii amri ambayo Mungu aliwapa katika bustani ya Eden? Adam na Hawa wangekuwa wakamilifu na katika msingi huo wangeanzisha familia adilifu na kuzaa wana na mabinti wakiwa na hulka ya wema. Mawazo yao na matendo yao yangekuwa chini ya uongozo wa Mungu, na hivyo wangejenga familia, jamii, na taifa na dunia ambamo Mungu peke yake ndiye mtawala. Dunia ya namna hiyo ingekuwa Ufalme wa Mbinguni hapa duniani. Kama hili lingepita, maisha yao yangekuwa maisha ya wema, na historia ya familia zao na dunia zingekuwa historia za wema. Historia ambayo Mungu aliidhamiria awali ni historia ya wema tu.

Hata hivyo, kwa vile mume na mke wa kwanza walianguka hawakutokea kuwa watu wa kweli ambao wameghubikwa na hulka ya Mungu, lakini wakawa watu walio na ghubiko la hulka ya uovu. Adam na Hawa walioanguka walizaa watoto wenye dhambi ya asili na hivyo kueneza familia za uovu, na jamii na dunia ya uovu. Mawazo na vitendo vya mtu aliyeanguka vimekuwa vikitawaliwa na Shetani, na dunia hii ikawa Jehanamu duniani, iliyojaa dhambi na mateso. Historia ya mtu binafsi, familia yake, taifa na dunia, bila kuwacha moja, zimekuwa ni historia linajumuisha kimsingi mitafaruku, dhambi na uovu, kwa kiwango kikubwa.




Kulingana na mpango awali wa Mungu, muktadha wa historia ya binadamu ni kuwa na mambo mema tu nyakati zote, lakini kwa sababu ya anguko, historia ya mwanadamu ilianza kwa uovu. Je, Mungu angejiengua na kuwaacha watu katika hali hiyo? Hapana. Kupitia katika kazi ya wokovu Mungu lazima atimize kile alichokidhamiria awali (Isaya 46:11). Pamoja na kwamba historia ya mtu ilianza kwa dhambi na uovu, kwa sababu ya toleo la mpango wa Mungu kutekeleza Dhumuni la Uumbaji, historia ya binadamu imekuwa historia ya toleo la mpango wa Mungu wa kukomboa Dhumuni la Uumbaji lililopotea. Lengo kuu la historia ya binadamu lilikuwa ni kuibadili kwa kuipandikiza, historia ya uovu na historia njema, ambayo Mungu alikuwa ameipanga. Siku za Mwisho ni kipindi ambacho dunia ya mabaya ya utawala wa Shetani hatimaye unageuzwa kuwa dunia adilifu la utawala wa Mungu. Siku za Mwisho ni wakati ambapo dunia ya dhambi au Jehanamu duniani, itageuzwa kuwa Ufalme wa Mbinguni hapa duniani, mahali ambapo Dhumuni la Uumbaji la Mungu litakuwa limehitimishwa.

Watu wengi wameishi kwa uoga wakiogopa Siku za Mwisho kwa sababu walifikiri utakuwa muda wa (majanga ya miujiza) maafa yasiyo ya kawaida. Hata hivyo, kinyume na yale waliyoamini, hautakuwa wasaa wa majanga. Badala, itakuwa ni wakati wa raha, kwa sababu ni wakati ambao dunia adilifu ambayo tabia asilia ya binadamu imekuwa ikisubiri itaanzishwa. Siku za Mwisho ni wakati ambao historia ya uovu itakoma, lakini pia ni wakati wa tumaini kwa sababu zinaashiria mwanzo wa zama za wema. Hata hivyo, Mungu hawezi kujenga Ufalme wa Mbingu bila kuangamiza dhambi na jehanamu. Hukumu hii itatolewa na Neno la Mungu (ni kama ilivyoelezwa katika kifungu IIB). Kwa hiyo wale wanaoishi maisha ya uovu watazamie Siku za Mwisho kwa kiharo (hofu) bali wale wanaotii matakwa ya Mungu watazamie Siku za Mwisho kwa matumaini na matarajio yenye raha.

Akiwekeza roho na pendo zake zote,( Katika hali isiyo na ukomo,) Mungu amekuwa akitumika wakati wote ili kuhitimisha dunia adilifu; hivyo ameendelea bila kituo akitafuta kurejesha Siku za Mwisho. Lakini kwa bahati mbaya, kila anapojaribu kuleta Siku za Mwisho, binadamu hakutimiza wajibu wake kikamilifu, na mapenzi ya Mungu yamebaki bila kutimizwa. Kulingana na 'Kanuni ya Uumbaji', lengo la Mungu haliwezi kutimizwa na Mungu peke yake; ushirikiano na binadamu ni wa dhati na lazima kabisa. Na hivyo katika msingi wa kanuni hii, toleo la Siku za Mwisho, ambalo ni kutimiza Lengo la Uumbaji, nalo pia haliwezi kutimizwa na Mungu peke yake.






Ni kwa sababu hii kwamba Biblia inaonyesha kumekuwapo majaribio kadha wa kadha ya kuleta siku za mwisho. Kwa mfano wakati wa Nuhu, Mungu alisema, 'nimepania kufanya mwisho wa miili kwa kuwa dunia imejaa mitafaruku juu yabo; chunga, nitawaangamiza pamoja na dunia (Mwa 6:13), hii inaonyesha siku za Nuhu zilikuwa ni Sza Mwisho. Mungu alitaka kuweka mwisho wakati wa miaka elfu moja na mia sita (kulingana na hesabu ya biblia) ya historia ya dhambi na uovu kwa njia ya *Hukumu ya Gharika*. Mungu alilenga kuteketeza uovu na baadaye kujenga dunia adilifu ya mamlaka yake na kuanza historia mpya ya wema katika msingi wa familia ya Nuhu. Nyakati hizo za Nuhu zilikuwa ziwe Siku za Mwisho, lakini kwa sababu ya kushindwa kwake Ham, familia ya Nuhu haikuweza kutimiza wajibu wake (rejea Familia ya Nuhu Katika "Toleo la Ukombozi"), na nia ya Mungu ya kuleta Siku za Mwisho haikuweza kutimizwa wakati huo. Ingawa familia ya Nuhu haikuweza kutimiza mapenzi ya Mungu, na kwa kuwa kusudio lake ni la dhati, lisilobadilika, Mungu aliendeleza toleo lake. Akiegemea kwa manabii, Mungu ameendeleza toleo lake kwa Siku za Mwisho – hii ndiyo kusema, kuelekea hukumu ya dhambi na uovu na matayarisho ya kujenga dunia adilifu.

Kwa msingi huu, Yesu alikuja kumaliza historia ya uovu na kuhitimisha Kusudi la Uuumbaji. Hivyo kuja kwake kulitoa kigezo kingine cha kuleta Siku za Mwisho. Hii ndiyo sababu Yesu alijitambulisha kama aliyekuja kuhukumu (Yoh 5:22) na kwa nini Malaki alitabiri, "na angalia siku inakuja, inayochoma kama tanuru, pale wote wenye kiburi na waovu wote watakapokuwa kuni. Siku inayokuja itawachoma moto…….ili isiwaache na mzizi wala tawi" (Malaki 4:1).

Lakini kwa kutomwamini Yesu, watu wa Israel walishindwa kutimiza wajibu wao. Hii ilicheleweshwa kutimizwa kwa makusudio ya Mungu mpaka Ujio wa Pili. Hivyo Siku za Mwisho zitakuwepo nyakati za Ujio wa Pili. Ndiyo maana Yesu alisema, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, na hivyo itakuwa siku za Mwana wa Mtu (Lk 17:26). Ni hii pia ndiyo maana katika Mathayo 24:29 anabashiri kuwa katika Ujio wa Pili maono na mabadiliko katika mbingu sawa

na yale yalibashiriwa wakati wa Nuhu na Yesu vitatokea, (Mwa. 6:6, 7, 13 na Isa. 24:19 kwa mpangilio).

## II. MATUKIO YALIYOTABIRIWA KWA AJILI YA SIKU ZA MWISHO.

Ili kuelewa vifungu vya Biblia vinavyoelezea juu ya matukio yaliyobashiriwa katika siku za mwisho, ni lazima tuelewe hulka na makusudio ya Mungu kwa lengo la uumbaji, ambalo linapelekea kuwepo kwa toleo la siku za mwisho. Kwa kuwa Mungu hawezi kukamilisha lengo la uumbaji mpaka akomeshe dunia ya uovu, katika siku za mwisho, uovu utaangamizwa. La muhimu zaidi, hata hivyo, siku za mwisho ni wakati wa kukamilisha Lengo la Uumbaji, ni rahisi kuona kuwa vifungu vya Biblia ambavyo vitatia hofu kwa kutokea majanga katika Siku za Mwisho, kama vile kuteketeza mbingu na dunia,

| Utabiri za Biblia kuhusu Siku za Mwisho | |
|---|---|
| **Mbingu na Dunia Kuteketezwa**<br>**Mbingu na Dunia Mpya** | 2 Pet 3 :12,<br>Mw 6 :13,<br>Isa 66 :22,<br>Ufunuo 22 :1 |
| **Hukumu kwa Moto** | 2 Pet 3 :12 |
| **Kukutana na Bwana Hewani** | 1 Wa Thes 4 :17 |
| **Juan a Mwezi kuwekwa Giza**<br>**Nyota kuporomoka toka Mbinguni** | Math 24:29 |

hakuwezi kuchukuliwa kifasihi (kama yalivyo). Kama maandishi haya hayawezi kuchukuliwa kifasihi yanaashiria nini?

### A. Mbingu na Dunia vitateketezwa na Mbingu na Dunia Mpya Vitajengwa

(2 Petro 3:12, Mwa. 6:13, Isaya 66:12, Ufunuo 21:1).

Ingawa mwanzo 6:13 inasema Mungu alilenga kuangamiza dunia nyakati za Nuhu, Mungu hakufanya hivyo kikweli kweli. Penginepo, Biblia inatuhakikishia dunia ni ya milele, kizazi hupita na kizazi huja, lakini dunia hudumu milele (Mhu. 1:4) na “alijenga madhabahu yake kama mbingu za juu, kama dunia ambayo ameiweka milele” (Zab. 78:68). Mungu asingepanga ili mipango ili mipango yeyote kamwe juu ya Bustani ya Eden, Ufalme wa Mbinguni wa milele

hapa duniani, kama isingehitimishwa. Kwa kuwa Ufalme wa Mungu ni wa milele, na dunia ndiyo mahali atakapojenga Ufalme wake, basi nayo lazima iwe ya milele.

Na nini maana ya aya mistari za Biblia za II Petro 3:12 na Isaya 24:19 ambazo hutaja kuangamiza mbingu na dunia? Kuangamizwa mbingu na dunia ambako kumeelezwa katika biblia kunamaanisha kuangamiza utawala wa Shetani ambao ulidhibiti mbingu na dunia tangu anguko la mtu. Kutokea kwa mbingu na dunia mpya kunamaanisha kuanzishwa kwa Ufalme wa Mbingu, ukiwa chini ya Masihi, chini ya utawala wa Mungu.

**B: Mbingu na dunia kuhukumiwa kwa moto**

(2 Petro 3:12)

2 Petro 3:12 anatuambia, "……..Mbingu zitawashwa moto na kuteketezwa, na vitu vyote vitayeyuka kwa moto!" Kama haya yangetokea kifasihi, basi Lengo la Mungu la Uumbaji lisingetimizwa. Malaki 4:1 anatabiri kwamba nyakati za Yesu zitakuwa za maangamizo kwa moto, na Yohana 5:22 na Yohana 9:39, Yesu ni Bwana wa Hukumu; na katika Luka 12:49, Yesu alisema alikuja kuwasha moto duniani. Lakini kamwe Yesu hakuleta hukumu kwa moto fasaha (kama tujuavyo moto).

Hivyo nini basi maana ya aya hizi? Lazima zina maana ishara. Katika maandishi ya Yeremia 23:29, Mungu anasema kuwa neno lake linaweza kufananishwa na moto. Hukumu kwa moto ni hukumu kwa Neno, au Ukweli. Katika Yohana 12:48, Yesu anasema, "Yule anaye nikana na akataaye kupokea maneno yangu yu na hakimu, maneno niliyoyasema yatakuwa hukumu yake siku ya mwisho " ………..II Wathes 2:8 inasema kuwa ……..asiye na sheria atafunuliwa, na Bwana Yesu atamhukumu kwa pulizo la mdomo wake, ambalo kwa uhakika humaanisha Neno. Vile vile, Isaya 11:4 anasema, "..... na ataipiga dunia kwa fito la mdomo wake, na pulizo la mdomo wake (Neno) atawahukumu waovu, (weka msisitizo). Yohana 5:24 anasema, " '..... Yule asikiaye neno langu na kumwamini yeye aliyenituma, ana uzima wa milele; hatahukumiwa, bali amepita katika kifo kuelekea uzima. Kutokana na aya hizi, ni wazi kuwa hukumu kwa moto humaanisha hukumu kwa Neno.

**C. Kukutana na Bwana Hewani**

(1 Wathes 4:17)

Waraka wa kwanza wa Mtume Paulo kwa Wathesalonike 4:17 unasema "na sisi tulio hai, ambao tumebaki, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu ili kukutana na Bwana hewani, na hivyo tutaendelea kuwa na Bwana. Siku za mwisho ni wasaa wa kukamilisha Dhumuni la Uumbaji. Kwa hiyo kwamba waumini watakutana na Bwana hewani siku za mwisho hakuwezi kuwa kwa kifasihi, sababu hewani si mahala ambapo Dhumuni la Uumbaji litatimizwa.

Katika Biblia kwa kawaida 'mbingu' humaanisha utakatifu, uchaji na ukanda usio na dhambi ambao upo chini ya utawala wa wema, na 'dunia', kinyume chake, humaanisha isiyo takatifu,

ya kudharaulika na ukanda wa dhambi chini ya utawala wa uovu. Kwa mfano, tunaposema, …Baba yetu uliye mbinguni… (Math. 6:9) hatumaanishi Mungu yumo mbinguni kidete, lakini tunarejea kwa utakatifu na ukanda wa uchaji wa uwepo wa Mungu. Hivyo "kukutana na Mungu hewani" hakumaanishi kuinua viwili wili vya Wakristo hewani kukutana na Kristo mbinguni, lakini inarejea katika maendeleo ya kukuwa kwao ndani – kiroho na kuwa na thamani ya kumtumikia Kristo katika dunia ya wema atakaporudi na kujenga Ufalme wa Mbingu duniani.

**D. Jua na Mwezi vitatiwa giza: Nyota zitadondoka kutoka mbinguni.**

(Math. 24:29).

Math 24:9 anasema, " 'Papo hapo baada ya mateso ya siku hizo jua litatiwa giza, na mwezi hautatoa mwanga wake, na nyota zitaanguka kutoka mbinguni….' ". Kama majanga haya yata dhihirika , Dhumuni la Uumbaji halitatimizwa. Na hapo, nini maana ya utabiri huu? Katika kitabu cha Mwanzo 37:9;10 zinatupa mwanga. Pale tunakuta tafsiri ya moja ya ndoto za Yusufu, ambamo jua huashiria baba, mwezi huashiria mama, na nyota huashiria watoto wao. Yesu na Roho Mtakatifu waliwapa uhai watu wa anguko na hivyo wanasimama katika nafasi ya baba na mama (rejea "Ukristologia"). Hivyo katika Agano Jipya, (Math. 24:29), jua na mwezi huwakilisha Yesu na Roho Mtakatifu, ambao ni chanzo cha mwanga wa ukweli ambao huangazia roho na moyo wa binadamu, na nyota huwakilisha waumini (Wakristo), ambao ni "watoto" wa Yesu na Roho Mtakatifu.

Katika mtazamo huu, mwanga wa jua huashiria mwanga wa ukweli wa maneno ya Yesu, na mwanga wa mwezi huashiria mwanga wa Roho Mtakatifu. Kwa kusema kuwa jua na mwezi vitatiwa giza ni kusema kuwa maelezo mapya ya ukweli yatafunika yale ya Yesu na Roho Mtakatifu (hii ndiyo kusema, Agano Jipya). Je, hili linawezekanaje? Kama Agano la Kale lilivyozibwa na Yesu na Roho Mtakatifu alikuja na maneno mapya ambayo yalikuwa ni kukamilisha Agano la Kale, pale Kristu anapokuja tena na maelezo mapya ya ukweli, maneno ya Yesu na Roho Mtakatifu yataghubikwa. Kwa ukweli kupoteza mwanga wake inamaanisha kipindi cha utume wake kimekwisha kwa ujio wa kizazi cha maelezo ya ukweli mpya. "Nyota" kuanguka katika siku za mwisho ni wakristu watakaokataa kukubali ukweli kutoka kwa Bwana na hivyo kupoteza nafasi yao kama watoto wa Mungu.

Katika Luka 18:8 Yesu aliuliza " ' …..je, pale ajapo Mwana wa Mtu atakuta imani duniani? ' " Katika wakati mwingine alisema kuwa wakati wa Ujio wa Pili atawaambia waumini wengi, " '…….sikuwajua ninyi, ondokeni, enyi watenda dhambi…' " (Math. 7:23). Ingawa viongozi wa Israel walikuwa wakimsubiri sana Masihi, wote "walianguka" kwa kukataa mafundisho mapya ambayo Yesu aliyaleta. Yesu aliona uwezekano wa viongozi wa dini wa wakati wa siku za mwisho kufanya jambo lilelile, na hivyo alisema mambo haya kama onyo.

**III. SIKU HIZI NI SIKU ZA MWISHO .**

Yesu aliahidi angerudi punde tu (Ufunuo 22 :20, Math 10 :23, 16 :28, Yohana 21 :22). Matokeo yake, Wakristo wa kila wakati wamekuwa wakiamini kuwa wakati wao ndio siku za mwisho na wakati wa kurudi kwa Kristo. Katika msingi wa mtazamo mzima wa Toleo la Ukombozi, tunaweza kujua kuwa sasa tunaishi katika wakati wa Ujio wa Pili.  Hili litaelezewa kwa uwazi zaidi katika somo la 'Ujio wa Pili'. Hata hivyo, tunaweza kujua kuwa wakati wetu ni wa Siku za Mwisho kwa kuchunguza matukio katika dunia inayotuzunguka. Kama Yesu alivyosema,

> Kwa mzeituni jifunzeni somo lake, mara tu matawi yake yanapochipukia na kutoa majani, mnajua kuwa kiangazi kinakaribia. Hivyo hivyo, unapoona mambo haya yote, mjue kwamba amekaribia kwenye malango. (Math 24 :32, 33).

Ni ishara gani zinatuonyesha kuwa tumo katika Siku za Mwisho ? Lengo na hatima ya historia ya binadamu ni kujenga uadilifu wa Mungu duniani, ambamo ni dunia iliyohitimisha Baraka Tatu. Siku za mwisho ni pale dunia ovu inapoangamizwa. Lakini ni muda ambao unaelekea katika uanzishaji wa dunia – adilifu. Kwa hiyo, kama kipindi chetu ni siku za mwisho, lazima tuwe makini kujua ishara zitokazo duniani kwamba Baraka Tatu zinatimizwa. Chini ya msingi wa ujuzi, huu lazima tuonyeshe kwamba sasa tunaishi katika siku za mwisho. Hebu tuangalie kipindi chetu katika mwanga wa Baraka Tatu.




Baraka ya kwanza ni kwamba kila mtu anaweza kukamilisha tabia yake na kuwa mmoja katika roho na Mungu. Katika kusudi alilolitaka Mungu, mtu huyu atapata raha ya uhuru wa mawazo na matendo yake na atajighubika upendo asilia na atakuwa wa tabia na thamani ya mtoto wa Mungu na Bwana wa uumbaji. Hivyo ataishi maisha yaliyomo katika ufalme wa mbingu. Hata hivyo kwa sababu ya anguko binadamu hakuweza kuhitimisha Baraka ya kwanza. Siku za mwisho ni hatua za mwisho ambamo toleo la Mungu la kukomboa kila mtu aliyeanguka kuwa mtu wa tabia kamilifu.

Katika nyakati hizi, mtu wa anguko anapanua kiu yake ya kuukomboa muktadha wa Baraka ya kwanza kama ukweli katika maisha yake. Mwelekeo huu ni dhahiri katika matukio ya hivi karibuni duniani kote kuelekea upendo kwa wote, ukombozi, usawa, haki za binadamu na

heshima. Dhumuni halisi si kukomboa uhuru wa mambo ya kimwili tu au uhuru bandia na maadili. Haya ni kwa binadamu kukomboa upendo wa asili, maadili ya asili, na uhuru wa asili ambao aliumbwa nao, lakini ukapotezwa. Hatima ya Toleo la Mungu katika Siku za Mwisho itakuwa ni kuhitimisha Baraka ya kwanza.

Tunaweza tena kujua siku hizi ni Siku za Mwisho tunaposhuhudia ukombozi wa Baraka ya Kwanza kwa kukomboa hali ya kiroho ya mwanadamu.  Tayari tumeelezea kwamba kila mtu ameumbwa ili awe mmoja katika roho na Mungu na kuwa na uwezo wa kuwasiliana na dunia ya kiroho kikamilifu atakapokuwa amejikamilisha. Hata hivyo, kabla ya anguko, Adam na Hawa walikuwa na uwezo wa kuwasiliana na Mungu na dunia ya kiroho, ingawa uwezo wao haukuwa umekomaa kwa utimilifu. Kwa sababu ya anguko, Adam na Hawa na wazaliwa wao wote, ambao ni watu wote, walitumbukia katika hali ambamo hawawezi walipo kuhisi uwepo wa Mungu.  Lakini kama Biblia inavyoonyesha, mawasiliano na dunia ya kiroho yatakombolewa Siku za Mwisho : " , "…katika siku za mwisho…nitamwaga Roho yangu katika miili ya wote, na wana na mabinti zenu watatabiri, na vijana wenu wataona maono,  na wazee wenu wataota ndoto; ……kwa watumishi na wahudumu wangu katika siku hizo nitamwaga Roho yangu na watatabiri" ' " (Mate. 2 :17,18).  Matukio ya hivi karibuni ya maajabu ya kiroho na matukio ya kihekima duniani kote yanalenga kuonyesha kukombolewa kwa roho na hulka ya mtu kufikia kile kiwango cha Adam na Hawa walichokuwa nacho kabla ya Anguko na kuashiria kuwa mwanadamu yuko katika upeo wa kukomboa Baraka ya Kwanza.

Baraka ya pili ya Mungu kwa mtu ilikuwa ni uwezo wa Adam na Hawa kujikamilisha wenyewe kama wazazi wa kweli na kuunda familia adilifu, na baadaye jumuiya moja, dunia moja inayotokana na familia hiyo kwa maneno mengine, uwezo wa kuumba familia ya mfano na kufanya dunia ya familia moja. Kituo cha kwanza cha dunia hiyo ni familia adilifu. Kupitia kwayo himaya ya upendo wa Mungu itabadilisha dunia na kuwa dunia ya utamaduni mmoja chini ya upendo wa kweli.



Hata hivyo, Adam na Hawa walianguka na kuwa wazazi walio na dhambi ya asili, na hivyo watu wote wakawa na hulka ya uovu na kuhitimisha dunia iliyotokana na mamlaka ya uovu, kwa hiyo Mungu amekuwa akifanya kazi zake kupitia dini na kuendeleza mambo ya ustaarabu na kumwopoa mtu kuelekea kujenga utamaduni unganiko na dunia ya familia moja.

Kihistoria, tamaduni mbalimbali zimekuwepo kupitia nyakati, hata hivyo, tamaduni za juu zimejitokeza chini ya dini mpya zinazochipua. Njia ya kumeza tamaduni mbalimbali ndogondogo kwa zile ambazo ni za hali ya juu na za kilimwengu, unganisho la tamaduni limekuwepo. Matokeo yake, kuna tamaduni kuu nne zilizobaki, Ukristu, Uislamu, Mashariki ya mbali (chini ya Ubuddha, Ukonfusia na Utao), na Uhindu. Upatanisho huu wa kihistoria unaashiria mwelekeo wa kwenda dunia ya utamaduni mmoja- na kuwa Baraka ya Pili ya Mungu inakombolewa.

Dunia ya utamaduni mmoja itokanayo na upendo wa kweli wa Mungu itakamilishwa pale watu wote wanapokuwa makaka na madada pamoja na Mungu kama mzazi wao. Katika mtazamo huu, Ukristo ni dini kuu katika kutimiza ahadi ya Mungu ya ukombozi kwa sababu Ukristu ulimtambulisha Mungu kama mzazi wa watu wote, sababu wanamsubiri Masihi, ambaye anakuja kujenga utamaduni mmoja, sababu amejitahidi kuunganisha dunia kuwa familia moja.

Matokeo ya kazi ya toleo la mpango wa Mungu wa ukombozi mtu, tangu Vita vya Pili vya dunia, katika kiwango kisichotarajiwa, ameng'amua umuhimu wa ushirikiano wa kimataifa na serikali ya dunia. Ung'amuzi huu umepelekea kuundwa kwa umoja wa mataifa na tume mbalimbali za kimataifa na zote zikiwa na dhima za viwango vya kimataifa na udhibiti wa ndani wa kila kitu kama vile lishe na amana za vyakula vinavyotawika na raslimali – bahati, nishati ya atomiki na uhusiano wa viumbe hai – hadi sheria za kimataifa, katika masuala ya maslahi ya watoto (e.g. taasisi na wakati wa kulea na kupata watoto wa kimataifa na UNICEF) na misaada ya maafa (kwa mfano, shirika la Msalaba Mwekundu) afya ya dunia (mfano, shirika la Afya duniani WHO) na yale ya uchumi wa dunia (mfano, shirika la fedha duniani IMF na Benki ya dunia), na nyinginezo nyingi. Uhuru wa kiuchumi na ushirikiano umekua kufikia kiwango cha kuwa nchi zilizostawi kwa kiasi kikubwa zimekuwa soko kuu la watu wa dunia tunajikuta hatimae, tukiishi katika jumuiya ya dunia, ambamo rangi, uraia lugha, mila, utamaduni na mazao ya dunia huchanganyika na kuafikiwa kinyume cha hapo awali.

Kwa sababu ya maendeleo makubwa katika nyanja za usafirishaji na mawasiliano dunia ' imesinyaa' kiasi kwamba tunaweza kusafiri karibu kila sehemu ya dunia kwa masaa machache. (Ni kama miaka hamsini au sitini iliyopita katika kiwango cha masaa hayo machache, dunia yetu ilikuwa na (radius) nusu ya kipenyo cha mamia ya maili). Kwa urahisi huu wa kusafiri kiwango cha wingi wa safari kimeongezeka kwa kasi katika nchi hizi na kuelekea kukutana sana kwa watu ambako kumeleta muingiliano wa vitendo na maelewano mema na furaha baina ya watu mbalimbali na tamaduni, ukituleta kwenye mshikamano wa dunia yenye umoja.

Katika karne hii kumekuwepo maendeleo yasiyotarajiwa miongoni mwa watu wengi duniani kwa kiwango cha kuvumiliana na kuelewana na watu wengine na kwa moyo wa upendo. Ni toleo la Mungu la kukomboa Baraka ya pili ambayo imepelekea kuibuka kwa mitazamo hiyo.

Vile vile imepelekea kuzijali nchi zilizoshindwa na washindi wa kidemokrasi baada aya Vita ya Pili ya Dunia na kutoa uhuru kwa makoloni na maeneo – rehani; imepelekea mikakati ya misaada ya nchi za kigeni, kuongezeka kwa sala na maombi ya pamoja na ushirikiano wa kitamaduni kuwa na umoja, ushirikiano katika ndoa za kimataifa, na upatikanaji na utunzaji watoto (urasibisho). Haya yote yanaashiria mwelekeo kuelekea ukombozi wa Baraka ya Pili ya Mungu kwa binadamu - baraka ya upendo wa kweli miongoni mwa watu na kuanzishwa kwa familia moja ya dunia.




Mambo haya yote, na matumaini ytazaa matunda pale zawadi hitimisho za historia zitakapowadia, Bwana wa ujio wa pili na itikadi kuu ya ulimwengu anayoileta, kwa maneno mengine zawadi za Roho ya Mungu na itikadi itikanayo na Mungu. Hakuna nyumbani pa kweli bila ya wazazi, kwa hiyo, matamanio ya mtu kwa ajili ya furaha na upendo yatahitimishwa pale Mungu na Masihi watakapoweza kusimama katika nafasi ya kuwa wazazi wa mtu.

Baraka ya Tatu ya Mungu kwa mtu ni haki na uwezo wa mtu mkamilifu kuwa na mamlaka ya mwili na roho kwa viumbe vilivyoumbwa, ndiyo kusema, mamlaka yote kwa nje na ndani. Mamlaka ya ndani ya uumbaji humaanisha mamlaka ya upendo. Mamlaka ya nje ni matumizi ya uumbaji kwa maendeleo ya maisha y ake kupitia njia ya sayansi na teknolojia.

Ushahidi kwamba wakati huu ni wakati wa Siku za Mwisho na kwa hiyo hatua kabla ya ukombozi wa baraka ya tatu ya Mungu, unaweza kuonekana katika jitihada za kimaendeleo na kuyapenda maumbile na vile vile katika harakati za maendeleo ya sayansi na teknolojia ya hali ya juu.




Kwa asili, husudisho na upendo wa mtu kwa uumbaji ni sawa na ukuaji wa roho yake. Ushahidi wa ukombozi wa upendo wa mtu kwa ajili ya viumbe unaweza kudhihirika katika uwiano wa viumbe hai na harakati za kuyajali mazingira, katika jumuiya za kuzuia ukatili kwa wanyama, kukataza uchafuzi wa hewa wa makazi, katika mashirika na vilabu (vyama) ambavyo vimeundwa kwa ajili ya kuyajali na kuyapenda mazingira ya asili.

Kwa njia ya sayansi na teknolojia, mtu anayakomboa mamlaka - nje juu ya viumbe. Maendeleo lukuki ya sayansi yamefikiwa katika karne hii. Kupitia maendeleo haya binadamu amekuwa akipata mafanikio ya kudhibiti maradhi na mambo ya bahari, ardhi, hewa na hata zaidi ya anga za juu. Binadamu yuko katika ukingo wa kuweza kuweka kiwango cha juu cha hali ya maisha kwa watu wote kupitia mambo haya kwa kuzalisha zaidi, kupata mavuno ya mazao zaidi, kugeuza majangwa kuwa mashamba ya kulima, na kudhibiti mazingira. Matumizi ya sakafu – bahari na hata ukanda wa barafu kaskazini na kusini pia ni mifano ya uwezo wa mtu kugeuza

uumbaji uwe nyumba adilifu. Hapa tunaweza kuona kuwa Baraka Tatu zipo njiani kukombolewa na kurudishiwa binadamu. Hivyo tunaweza kugundua kuwa kujengwa kwa dunia ya uthamini wa Mungu upo miongoni mwetu - kwamba tumo katika Siku za Mwisho.



## CHAPTER FIVE RESURRECTION

## SURA YA TANO UFUFUO

Kama tungechukulia kila kitu kilivyo katika Biblia kifasaha, basi hapo ingetubidi tuamini kuwa wakati wa Ujio wa Pili waliozikwa na kuoza mwili wa nyama ya wa amini wote tangu kale wata kombolewa na kuwa wa hali ya asili ya maisha katika mwili wa nyama (II Wathes. 4 :16, Math. 27 :52). Lakini twaweza amini hili ? Ili kutanzua suala hili ebu kwanza tuchunguze maana ya ufufuo.

### I. MAANA YA UFUFUO .

Neno ‘ufufuo’ humaanisha kupita kifo kwenda uzima. Ili kuelewa maana ya ‘kupita au kutoka kifo kwenda uzima’ ebu tufikirie maana ya maneno uzima na kifo.

Katika Luka 9 :60 tunasoma kuwa kwa mwanafunzi aliyetaka kwenda nyumbani kwenye msiba au kifo cha baba yake, Yesu alisema,… waache wafu wazike wafu wao…. (msisitizo upo). Katika maneno haya ya Yesu tunapata mitazamo ya aina mbili tofauti ya uzima na kifo. Mtazamo mmoja unahusishwa na kazi ya viungo vya mwili wa nyama. Mwingine unahusishwa na watu wanaohudhuria mazishi ya baba wa mwanafunzi. Je, ni kwa nini Yesu alionyesha watu watakaozika nao pia ni wafu ambapo kwa kweli wapo hai ? Ilikuwa kwa sababu wapo chini ya mamlaka ya Shetani, walikuwa hawajui dhumuni la maisha na hawakumjua Mungu, ambaye ni kiini cha maisha. Ufunuo 3 :1 unasema,… mna jina la kuwa wazima lakini umekufa, ‘kutokana na aya hii tunaweza kugundua kuwa hata kama mtu anaishi kimwili, kama yuko chini ya mamlaka ya Shetani, hapo kulingana na msimamo wa Yesu (mtu huyo) amekufa, kwa mtazamo huu wa kifo, uzima utamaanisha kuwa katikati ya utawala wa Mungu kutimiza madhumuni pewa ya Mungu ya maisha. Katika Yoh. 11 : 25-26, Yesu anasema ….. yule aniaminiye, hata kama akifa, lakini ataendelea kuishi, na yule aishiye na kuendelea kuamini hatokufa kamwe. Hii inatuonyesha kuwa yeyote aliye na uhusiano na mamlaka ya Mungu ya kupitia kwa Kristo ana uzima (yu hai), hata kama mwili wake wa nyama umekufa au yupo hai bila kujali yuko duniani au katika dunia ya roho.




**A. Kifo kilichosababishwa na Anguko.**

Kuhitaji Ufufuo ni matokeo ya kifo kilichosababishwa na Anguko. Ebu tuchunguze ni kifo gani kati ya vile viwili vilivyotajwa hapo juu kimesababishwa na anguko la wahenga wa kwanza wa binadamu. mwili wa maungo wa binadamu unaelekezwa kurudi ardhini baada ya kuzeeka na kufa. Kama Mungu angedhamiria watu waishi milele duniani katika miili yao nyama, pasingekuwepo haja ya kuumba dunia ya roho kwa ajili ya roho, Mungu aliiumba dunia ya kiroho hata kabla ya mtu kuanguka. Hakuumba baada ya anguko ili tu roho za wenye dhambi zikaishi huko. Ili kuwa ni mpango wa Mungu Kwamba mwili wa mtu urudi ardhini na kuwa roho yake pekee iishi milele na Mungu katika dunia ya roho (Mhu. 12 : 7). Kifo cha mwili wa nyama siyo kifo kilichosababishwa na anguko.

Pale Mungu alipomwambia Adam na Hawa hakika wangekufa siku hiyo wakila Tunda la Ujuzi wa Mema na Maovu (Mwa. 2 : 17), kifo kinachoelezwa hapa siyo kifo cha mwili. Tunaona katika Mwanzo kwamba Adam na Hawa waliendelea kuwa watendaji na hai na kuzaa, watoto kwa zaidi ya miaka mia tisa baada ya kula Tunda la Ujuzi wa Mema na Maovu. Bado, kama tunaamini Neno la Mungu, kwa mantiki hiyo, lazima wangekufa hapo hapo baada ya kuvunja Amri ya Mungu.

Upendo wa Mungu ni kiini cha maisha. Kwa hiyo kwa kuacha miliki ya upendo wa Mungu na kuingia miliki ya shetani, ambamo hakuna upendo wa kweli, ni kifo. Katika waraka wa I Yoh. 3 : 14 tunajifunza kuwa 'yule asiyependa anajitosa katika kifo'. Vile vile, Warumi 8 : 6 na Warumi 6 : 23 kwa mpangilio, tunasoma 'kuweka akili kwenye mwili wa nyama (kufikiria mwili peke yake) ni kifo, lakini kuweka akili katika roho ni uzima na amani 'na' … mshahara wa dhambi ni kifo, lakini zawadi ya bure ya Mungu ni uzima wa milele katika Kristo Yesu…..kwa hiyo kulingana na mtazamo wa Biblia, kifo kilichosababishwa na anguko ni hali itokanayo na dhambi-hali ya kujitenga mbali na upendo wa Mungu.

**B. Maana ya kweli ya Ufufuo.**

Ebu tuhitimishe maana ya Ufufuo. Kama  mwili wa nyama una rudi Duniani siyo kifo kilichosababishwa na anguko, basi ni wazi maana ya 'kutoka kifo kwenda uzima' -ndiyo kusema ufufuo- hauwezi kuwa uamsho wa miili uliooza.  Kulingana na 'Kanuni ya Uumbaji', ilikuwa ni mpango asili  wa Mungu kwamba mwili wa nyama ufe na kurudi ardhini pale unapozeeka (Mhu. 12 : 7). Kwa hiyo mara  mwili wa nyama unapo oza hau wezi kurudi  katika hali yake ya awali.




Kwa kuwa ufufuo hauelezei uhai na kifo cha kimwili, lazima utakuwa una elezea uhai na kifo cha kiroho. Hivyo kufufuka ni mchakato wa mtu kukombolewa kutoka utawala wa shetani na kwenda utawala wa Mungu wa moja kwa moja kwa njia ya mpago wa  Ukombozi. Kama mtu atatubu dhambi zake na kuwa mwema leo zaidi ya alivyokuwa jana, huyo amefufuka kwa kiwango ambacho. Yesu alisema, " '…….yule asikiaye maneno yangu na kumwamini aliye nituma, ana uzima wa milele, haji kuhukumiwa lakini amepita katika kifo na kuelekea uzima.' " (Yoh. 5 : 24). Hii inaonyesha kuwa ufufuo au kupita kifo kwenda uzima, huanza kwa kusikia maneno ya Yesu na kumwamini Mungu.  Biblia inasema "…kama ilivyo katika Adam wote hufa, hivyo vilevile katika Kristo wote watafanywa wazima " (I wak 15 : 22). Kwa sababu ya anguko la Adam, kizazi chake chote kimekuwa cha shetani na hivyo kimekufa. Hivyo, kufufuliwa kuna maana kuwa katika kizazi cha Mungu, kupitia kwa Kristo.

Katika msingi huu wa uelewa wa ufufuo, tusitegemee mabadiliko makubwa ya nje kutokana na ufufuo. Ingawa Adam na Hawa walikuwa tofauti baada ya anguko na kutokana na hilo walikufa kiroho, hakuna mabadiliko ya kimwili yaliyotokea. Hivyo hakuna tofauti ya nje kati ya mtu ambaye ana maisha ya milele kwa sababu ya kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Mtakatifu, na mwizi ambaye yupo chini ya utawala wa kifo.

Hata hivyo, Math. 27 : 52 huelekea kuunga mkono imani katika ufufuo wa mwili wa nyama. Ebu tuchunguze kifungu hiki, kinasema "….makaburi yalifunguliwa na miili ya waliolala

iliinuliwa, na ilipotoka nje baada ya kufufuka kwake [Yesu] walikwenda katika mji mtakatifu na kuwatokea wengi." Hata hivyo, kama hili lingetokea kihalisia, hapo historia ya kuwatesa wakristo isingekuwepo. Hata hivyo Waisrael walishakosa imani na kumsulibisha Yesu, kwa kuendelea kuamini kuwa hakuwa Bwana. Hata hivyo, kama wangeshuhudia manabii wakifufuka kutoka makaburini mwao na kuwasikia wakishuhudia kwamba Yesu alikuwa Masihi, je wasingemwamini Yesu ? Je, kwa nini walithubutu kuwa tesa wanafunzi wa Yesu ?

Pia kwa kuwa ufufuo unasemekana kurudisha uzima wa milele, je tusingeweza kuwaona wale manabii waliofufuliwa katika agano la Kale wakiishi pamoja nasi hii leo ? Na je, isingekuwa wale waliofufuliwa na kurejeshewa uzima kupitia heri ya ufufuo wangeshuhudia mengi juu ya Mungu na Yesu ? Na hapo kwa uhakika katika maandiko ya matendo ya mitume tungepata habari zao. Pamoja na hayo kuna sehemu moja tu katika Biblia inayowaelezea hayo –ni ile katika Mathayo inasemea kuinuka kwao kutoka makaburini na kuwatokea wengi (Math. 27 : 52).

Uelewa wa maana ya kweli ya ufufuo utatatua kirahisi tatizo hili. Kwa kuwa ufufuo haumaanishi kurejesha maiti katika uhai, isingekuwepo miili ya nyama iliyonuka toka kaburini" na "kurudia uhai. Kwa neema ya Mungu, roho zao au nafsi zao, za watakatifu waliokufa zilikuwa karibu na ukamilifu. Mathayo na wanafunzi wengine wakiwa wamemulikwa na Roho Mtakatifu, walipata uono wa roho wa muda mfupi, na waliweza kuona watu wale wa kiroho. Wale waliobaki bila kuguswa na Roho Mtakatifu walibaki na uonaji wa kimwili wa kawaida, na hivyo hawakuweza kuona miili ya kiroho ya manabii wa Agano la Kale.

**II. KANUNI ZA UFUFUO.**

Kwa kuwa ufufuo humaanisha tukio litokalo katika mlolongo wa kukomboa uasili wa mtu aliyeanguka kuelekea katika kile kilichoumbwa na Mungu, Mpango wa Mungu wa ufufuo kwa hakika ni Mpago wa Ukombozi. Vilevile Mpango wa Mungu wa Ukombozi ni Mpango wa kuumba upya pia. Mwisho Mpango wa Mungu wa ufufuo hufanyika kwa kuzingatia yale yalioelezewa katika "Kanuni za Uumbaji".

Kwanza kabisa, kulingaana na "Kanuni za Uumbaji", kusudii la Uumbaji huhitimishwa wakati mtu anapotimiza wajibu wake, kwa kuamini na kuishi kama neno la Mungu linenavyo. Kwa hiyo katika ufufuo ambako ndiko kuumbwa upya, Mungu humpa mtu neno Lake –ali lotoa Agano la Kale na Agano Jipya, na kaahidi kutoa Agano Kamilifu mara Kristo atakaporudi. Ili kufufuliwa mtu lazima atimize jukumu lake -kuamini katika na kuishi kama neno linenavyo. Kwa jinsi hii, ufufuo unakamilika kwa Mungu kutoa Neno Lake (kweli) kwa mtu pamoja na mtu kutimiza jukumu lake la kuamini na kuishi katika ukweli.

Pili kulingana na "Kanuni za uumbaji", kila roho pekee ya mtu imeumbwa ikue na ikamilike kwa msingi tu wa uhusiano na upekee wa mwili. Kutokana na kanuni hii, ufufuo (utakaso, ukuaji




na ukamilifu) wa roho ya mtu binafsi lazima udhihiriswe kwenye msingi na upekee wa mwili wake, na hivyo wakati bado anaishi hapa Duniani. Kwa hakika mpaka leo hii, ufufuaji umekuwa ukieleweka kuwa kufufua mwili wa nyama uliokufa wakati wa kurudi Kristo. Lakini hii siyo sahihi ; mpango wa Mungu kwa ajili ya ufufuo ni mchakato unaoendelea ambao umekuwa ukilenga watu ambao ni hai Duniani. Ni kwao kwamba amewatuma manabii wakiwa na Ukweli.

Tatu, kwa kuzingatia 'Kanuni za Uumbaji', mtu ameumbwa ili awe mkamilifu kwa kukua kupitia hatua tatu za kipindi cha ukuaji. Kwa hiyo mpango wa Mungu wa ufufuo kwa mtu wa anguko utatimizwa kupitia hatua tatu za mpango olio kwisha tolewa.

Nne, ingawa wateule wa Mungu mbalimbali katika mpango wake wa ukombozi hawakuweza kutekeleza majukumu yao kwa utimilifu, walifanya kila walivyoweza kwa unyenyekevu mkubwa kwa Mungu. Unyenyekevu wao na ucha Mungu wao, umelimbikizwa kwa manufaa Duniani, kwa msingi huu wa moyo uliowekwa na watu waaminifu wa nyakati za mwanzo, watu wa vizazi vya baadaye wameweza kupokea faida za ziada kiasi kwa kila zama fulani cha nyakati katika mpango wa Mungu wa ufufuo. Mpago wa Mungu wa ufufuo hufanyika kwa kuzingatia manufaa ya nyakati. Kwa maneno mengine kiasi cha uwezekano wa ufufuo katika wakati fulani hutegemea msingii historia ya moyo wa Mungu uliokwishawekwa na waaminifu wa nyakati za kale.

## III : MPANGO KWA AJILI YA UFUFUO WA WATU DUNIANI .

### A. Mpango wa Mungu wa ufufuo unatokana na watu waliomo Duniani.

Mpaka hivi leo, Wakristo walipofikiria juu ya ufufuo, wamekuwa wakifikiri juu ya watu walio kufa kimwili wakipokea uhai mpya pale Kristo anarudi. Lakini pale tunapo elewa maana ya kweli ya ufufuo na kanuni za Mpango wa Mungu wa Ufufuo tumeelewa kuwa Mungu huweka Mpango wake wa Ufufuo akiegemea kwa watu waliopo Duniani. Kwa mtazamo wa binadamu, inaweza kuonekana kama tu marudio kutoka kizazi hadi kizazi. Kwa mtazamo wa Mungu, ambaye hutekeleza mpango wake, kurithisha vizazi hakuna uhakika. Kwa mtazamo wa Mungu historia yote si kingine bali kazi ya kumfufua mtu mmoja aliyekufa, Adam. Kama muhenga wa kwanza wa wanadamu Adam asinge anguka na kwamba angekua kupitia hatua tatu za kipindi cha kukuaji, roho yake ingekua kupitia hatua ya roho changa (mwanzo) – hai ya (pili} mpaka kuwa roho takatifu, (tatu) roho ya yule atimizaye makusudi ya uumbaji.

Hata hivyo,kutokana matokeo ya Anguko, roho ya mtu ili poromoka kutoka kiwango cha ukamilifu katika kipindi cha kukua, mpaka kiwango cha chini kabisa – hii ndiyo kusema alianguka chini ya kiwango ambacho alicho umbiwa ki asilia. Adam na Hawa walianguka nje katika ukanda usio wa Kanuni na kurithi Hulka ya (chembechembe} za anguko kutoka kwa malaika mkuu aliyeanguka.

### B. Hatua tatu katika Mpago wa Mungu wa Ufufuo.

Mungu alianza mpango wa ufufuo kwenye familia ya Adam, ambayo ilianguka nje ya miliki ya Kanuni. Hata hivyo kwa kuwa watu katika familia za Adam na Nuhu zilishindwa kutekeleza wajibu wao, ufufuo wenyewe haukuanza mpaka katika familia ya Abraham. Kwa hiyo kwa kutazama yaliyopita kipindi cha miaka elfu mbili kutoka kwa Adam hadi Abraham kiliisha katika kipindi ambacho ni msingi tu wa mpango wa Mungu wa ufufuo ulianzishwa. Hivyo, kipindi hiki kinaitwa *zama za Mpango wa Mungu kwa ajili ya Msingi wa Ufufuo.*

Kwa msingi huu, Mungu alitekeleza hatua ya mwanzo ya mpango wa ufufuo, ambao tena kwa sababu




ya mtu kurudia kushindwa, uliishia kuchukua miaka elfu mbili, kutoka kwa Abraham mpaka Yesu. Watu waliopata manufa ya zama za hatua za mwanzo wa ufufuo walikuwa watimize wajibu wao kwa kuishi na kushika sheria ya Agano la kale, hatua ya mwanzo wa neno uumbaji upya. Kwa kuwa watu walikuwa wathibitishwe kwa wao kutekeleza sheria (Neno),hizi zama zinaitwa *zama za kuthibishwa kutokana na kutekeza sheria'*. Kama mtu alitimiza wajibu huo, akiegemea mwili wake, roho yake ingekua kupitia hatua ya mwanzo ya ufufuo na kuwa *'roho changa (hatua ya awali) mtu ambaye amefikia hatua ya awali hapa Duniani aki achana na mwili wake wa nyama roho yake huenda kuishi katika hatua ya awali Dunia ya kiroho.*

Ufufuo mkamilifu ulikuwa upatikane kupitia kwa Yesu, Masihi ; hata hivyo kwa sababu ya kushindwa kwa binadamu kumkubali Yesu, kipindi baada ya kifo chake kimekuwa ni kipindi cha ufufuo kwa hatua ya kukua tu. Kwa sababu ya Waisrael kukosa imani kwa Yesu, alisulibiwa na utimilifu wa mpango wa ufufuo ulicheleweshwa mpaka Ujio wa Pili. Kwa kuangalia yaliopita, tunaweza kuona kutoka kipindi cha Yesu mpaka wakati wa Ujio wa Pili kimekuwa ni zama *za hatua ya kukua ya ufufuo.* Wakati wa zama hizi, watu Duniani waliweza kupokea manufaa ya zama katika hatua ya kukua ya ufufuo na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ku amini kuishi agano jipya. *katika hatua ya kukua tu.* Katika nyakati hizo, watu duniani walikuwa wakipokea mafao ya kipindi cha kukua kwa hatua ya ufufuo kwa kutekeleza wajibu wao kwa kuamini na kulishi Agano Jipya, neno la Mungu katika hatua ya kukua ya kuumba upya. Kwa hiyo zamai hizi zinaitwa *zama za kuthibitishwa kwa njia ya imani'*. Watu wa zama hizo waliweza kupitia hatua ya kukua kupitia ufufuo na kufikia kupata roho – hai kwa kuamini na kuishi neno la agano Jipya. Wakati mtu aliyefikia kiwango cha roho hai anapouacha mwili wake, huenda kuishi Paradiso, ambapo ndipo *kiwango cha roho hai {kukua} cha Dunia ya kiroho*.

Mpango wa *zama za* hatua kamilifu ya ufufuo utakamilika sehemu mbili roho na mwili* (nafsi ya roho na mwili) na Masihi wakati wa Ujio wa Pili. Masihi ataleta Agano Kamilifu ambalo

litaleta hitimisho la Agano la Kale na Agano Jipya. Watu duniani wanaweza kupokea manufaa ya zama za hatua ya ufufuo kamili kwa kutekeleza wajibu wao katika kuamini na kulishika neno jipya na moja kwa moja kumtumikia Masihi kwa utii wa moyo wote. Kwa hiyo, wakati huo unaitwa zama za *kuthibitishwa*

---

**ingawa Yesu alileta wokovu kwa mtu, kama inavyo weza kuoneka katika warumi 7 :14-25,dhambi ya asili bado imesalia kwa mtu. Wakati sahihi wa kondoa dhamdi ya asili ni wakati wa ujio wa pili.*

*kwa kuhudumia.* Wakati mtu anamuamini na kumhudumia Masihi wakati wa Ujio wa Pili, roho yake hufikia kiwango cha hatua ya ufufuo kamili na kuwa roho takatifu. Sehemu Duniani ambapo watu wa hatua hii ya roho takatifu huishi panaitwa Ufalme wa Mbingu Duniani. Pale mtu mkamilifu anayeishi katika Ufalme wa Mbingu duniani anapouacha mwili wake, huenda kuishi katika Ufalme wa Mbingu katika Dunia ya roho, ambapo ni mkoa wa Dunia ya kiroho mahali pa roho takatifu.

**C. Mbingu na Paradiso.**

Kiutamaduni, Wakristo wamefahamu kuwa Mbingu na Paradiso ni kitu kimoja. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa hapo juu, Ufalme wa Mbingu ni Dunia ya kiroho ambamo watu wa kiroho walofikia kiwango cha roho takatifu wakiwa na mwlili wa nyama hapa duniani huishi. Ingawa Yesu, Masihi alikuja kuhitimisha wokovu wa binadamu, kwa sababu ya kifo chake msalabani lengo la Uumbaji ambalo linakamilishwa katika Ufalme wa Mbingu katika dunia ya kiroho na hapa duniani, halikuhitimishwa wakati huo. Hakuwepo mtu aliyefanikiwa kufika kiwango cha roho takatifu wakati akiwepo duniani na kwa hiyo, Ufalme wa Mbingu katika dunia ya kiroho umebaki tupu – hakuna hata mmoja aliyeingia, kwa kuwa ni kiwango cha roho takatifu cha dunia ya kiroho. Kwa nini basi Yesu alisema kuwa yeyote aniaminiye ataingia Ufalme wa Mbingu ? Alisema hivyo kwa sababu lengo lake la asili lilikuwa kuleta Ufalme wa Mbingu. Hata hivyo, kwa sababu ya ukosefu wa imani ya watu wa Israel, alikufa msalabani bila kudhihirisha Ufalme wa Mbingu.

Wakati Yesu anasulibishwa msalabani, wezi wawili walisulibishwa pamoja naye, mmoja kulia kwake na mwingine kushoto kwake. Pale mwizi wa kulia alipoonyesha kuwa anamwamini Yesu, Yesu alimwambia kuwa atakuwa naye katika Paradiso (Luka 23 : 43). Paradiso ni kiwango cha roho hai cha Dunia ya kiroho sehemu ambayo watu wanaomwamini Yesu hufikia baada ya kuachana na miili yao. Wale walipo paradiso lazima waombe ili kufikia lengo la ukamilifu na wasubiri kufunguliwa malango ya Ufalme wa Mbinguni.

**D. Matukio ya kiroho yatakayotokea Siku za Mwisho.**

Mtu alianguka kutoka hatua ya kiwango cha kukamilika cha hatua ya kukua. Jinsi mtu anapoingia katika Siku za Mwisho, huingia katika zama ambazo anaweza kujikomboa yeye mwenyewe katika hatua ya ukamilifu hatua ya kukua. Kwa kuamini na kulishika neno la Agano

Jipya, nafsi roho ya mtu huweza kufikia kiwango cha ukamilifu katka hatua ya kukua, nafasi ya mtu mara kabla ya anguko.

Siku za Mwisho ni pale mtu anapokomboa katika kiwango cha Duniani kote, kiwango alichokuwa amekifikia kabla ya anguko -kiwango cha roho hai, kiwango ambacho Adam aliweza kukifikia uwezo wake wa kuwasiliana na Mungu kwa ufanisi mkubwa. Kwa sababu hii, katika Siku za Mwisho, katika kilele cha kiwango cha kukua kinasogelewa, kutakuwa na watu wengi watakaokuwa na uwezo wa kuwasiliana na dunia ya kiroho. Kwa kuona mambo katika mtazamo huu tunaweza kuelewa ahadi ya Mungu ya kushusha roho yake kwa miili yote Siku za Mwisho. (Matendo. 2 : 17).

Katika Siku za Mwisho, watakuwepo watu wengi watakaopokea ufunuo, ''Wewe ni Bwana''. Hii

haimaanishi kuwa wao ni Bwana wa Ujio wa Pili, lakini ina maana kuwa wanafanywa upya katika nafasi hii ya bwana wa uumbaji, nafasi ambayo ilizopotezwa kwa sababu ya anguko la Adam. Kwa maneno mengine, wanakomboa kiwango cha maendeleo ya kiroho ambao Adam alikuwa amefikia punde kabla ya anguko.

Kama vile Yohana Mbatizaji alivyokuwa aandae njia ya Yesu,kutakuwepo watu wengi ambao wata takiwa kuandaa njia ya Bwana wa Ujio wa Pili,kwa kuwa kila mtu ana jukumu fulani ana mwakilisha bwana wa ujio wa pili katika kila mmoja atapata ufunuo ''Wewe ni Bwana'', ingawa inaweza kuwa wakifanya kazi katika zama au katika mazingira tofauti na yale ya Bwana. Kama katika muda huo mtu atakuwa anapokea mawasiliano ya kiroho asielewe kanuni ambayo imepelekea hali hiyo na kwa makosa kufikiria kuwa yeye ni Bwana wa Ujio wa Pili na hujifanya kana kwamba yeye ni Bwana wa Ujio wa Pili na kutenda sawa kama yeye ndie Bwana, ana kuwa mpinga Kristo. Ndiyo maana Biblia imetabiri kwamba wapinga Kristo wengi watatokea katika Siku za Mwisho.

Pia, ingawa watu wenye uwezo wa kuwasiliana kiroho huwa siliana na Dunia ile ile ya kiroho, kwa kuwa kiwango wa roho, mazingira, na tabia binafsi ni tofauti kwa watu walio wazi kiroho, kiwango cha dunia ya roho ambamo wanawasiliana na yaliyomo katika ufunuo wanaoupokea hutofautiana moja baada ya mwingine (IWakor 15 : 41, 12 : 8 – 10). Kwa sababu hiyo kumekuwepo na kuto kukubaliana na migogoro miongoni mwa watu wakiroho. Hasa kwa kuwa wana uhusiano wima na Mungu, na hivyo huwajibika kwa sehemu moja tu ya Mpango wa Mungu wa Ukombozi, mara nyingi hawajui uhusiano wao mlalo na wenzao wenye mawasiliano na dunia ya kiroho uwe vipi. Kwa kuwa kila mmoja wao ni bora katika eneo lake la jukumu, Mungu humpatia kila mmoja ufunuo ya kuwa ''Wewe ni bora'' kumpongeza afanye vizuri zaidi. Bado kwa vile hawajui picha kamili ya kile akifanyacho Mungu, mara nyingi hugombana miongoni mwao. Mtafaruku uliopo utatoweka kati ya wanaowasiliana na dunia ya kiroho wakati wa maelezo ya ukweli mpya, utakaoelezea madhumuni yote ya Mpango wa Mungu wa Ukombozi. Kutokana na msingi wa hitimisho la ufahamu huu, watu wa kiroho watafikia muafaka ki mlalo, ushirikiano kiwima na Mungu. Uwezo wao unapaswa kufaa katika madhumuni ya jambo la wote.

**IV. MPANGO KWA AJILI YA UFUFUO WA NAFSI ZA ROHO .**

**A. Ufufuo Marejeo wa nafsi za roho.**

Watu wasiohesabika wamekufa na kwenda dunia ya kiroho, hakuna hata mmoja alie jikamilisha yeye mwenyewe akiwa Duniani katika mwili wake wa nyama. Inawezekanaje nafsi hizi za roho zikafufuliwa ? Nafsi ya roho haiwezi kukua hata kufufuliwa nje ya mwili wenyewe wa nyama. Kwa hiyo wale walio katika dunia ya roho ili kufufuliwa lazima warudi duniani kukamilisha wajibu ambayo waliacha bila kutimiza wakati wanaishi katika mwili Duniani. Hutimiza hili kwa kushirikiana na watu waliopo duniani na hufanya kazi kupitia miili ya wengine ili wasaidiwe kutimiza wajibu wao katika utumishi wao. Hii ndiyo maana Yuda 1 : 14 anasema kwamba "Katika Siku za Mwisho….Bwana alikuja na watakatifu wake, maelfu maelfu…". Ni kwa namna gani nafsi za kiroho zinashirikiana na watu waliopo duniani ili kukamilisha Kusudio la Mungu ? Wakati mtu duniani, kupitia sala au matendo ya kiroho hutokea kujenga msingi unaokubalika kufanya mawasiliano na roho, kwa ushirikiano, basi mtu wa nafsi roho atarudi na kuanza kushirikiana na mtu huyo hapa duniani kwa njia ya tendo la Kutoa na Kupokea kupitia nafsi roho yake.




Nafsi roho ya mtu humsaidia mtu hapa duniani kupokea ufunuo au kupata uzoefu mzito wa ukweli, na wakati mwingine humsaidia kupata uzoefu mwingine wa kiroho kama vile uponyajii wa maradhi mbalimbali, uwezo wa kutabiri, au moto wa kiroho.

**B. Ufufuo-marejeo wa Nafsi Roho za Watu Waliomuamini Mungu.**

Zama za Yesu miaka elfu mbili iliyopita na pale Kristu anaporudi katika Siku za Mwisho zama zote mbili ni wakati maalum ambapo waumini wote duniani wanaweza kuinuliwa kiroho

(kulingana na Mpango wa Mungu kwa Ukombozi). Hasa kwa kuwa hizi ni nyakati ambazo Neno la Mungu la uumbaji upya hutokea upya, (kama Injili na maneno mapya kimpangilio), hivyo kulingana na kanuni za ufufuo nyakati hizi ni muhimu sana – ni wakati ambao nafsi roho ya mtu inaweza kufufuliwa kwa kasi iliyoongezwa. Kwa hiyo, katika wakati wa Yesu, roho changa za Agano la Kale ambazo zilipambana na Sheria tu, zote zimedhamiria kurudi na kutimiza sharti la kushirikiana na waumini duniani.

Kwa kuwa Eliya alitokea kama roho kwa Yesu na wanafunzi katika mlima wa Kubadilika–sura (Math. 17 : 3) ni wazi kuwa Eliya yuko katika dunia ya roho. Lakini bado, Yesu alionyesha kuwa Yohana Mbatizaji, aliyekuwa duniani ndiye alikuwa Eliya (Math. 17 : 12, 13; 11 : 14). Katika mtazamo wa kanuni za ufufuo marudio tunaweza kuelewa kuwa Eliya alirudi ili kukamilisha jukumu lake ambalo aliliacha bila kulikamilisha alipokuwa hai hapa duniani kwa kushirikiana na Yohana Mbatizaji. Kutokana na kanuni ziendeshazo ufufuo – marudio, mwili wenyewe wa Yohana Mbatizaji ni mwili badala ya ule wa Eliya.

Math. 27 : 52 anasema kuwa Yesu alipokufa msalabani watakatifu wengi waliibuka kutoka makaburini. Hili pia ni tukio la ufufuo wa nafsi roho za watu, ufufuo wa wale ambao wamefikia kiwango cha roho changa wakiwa hapa duniani. Kwa kushirikiana na waliopo duniani wamuaminiye na kumtumikia Bwana wa Ujio wa Pili kwa kuwasaidia wawe roho takatifu, nafsi roho za watu wenye kiwango cha roho hai (Paradiso) – wanaweza kupokea manufaa yaleyale na wao wenyewe kuwa roho takatifu.



Waebrania 11 : 39-41 anasema ”Na wale wote hawa (Watakatifu wa Agano la Kale), pamoja na kuonyesha imani yao, hawakupokea ahadi iliyotolewa [kuruhusiwa kuingia katika Ufalme wa Mbingu] kwa kuwa Mungu aliona mbele yao kilicho bora zaidi [Ufalme wa Mbinguni] kwetu sisi [watu duniani] ya kwamba mbali na sisi, wao [nafsi roho] wasikamilishwe.” Maneno haya yanaonyesha kanuni ya ufufuo wa nafsi roho zinazorudi hapa duniani ili zipate ufufuo.

**C. Ufufuo-Marejeo kwa Nafsi Roho Zote Nyinginezo.**

Nafsi roho zilizoamini katika dini tofauti na Uyahudi na Ukristo wakati zinatoweka (kufa)lazima pia zirudi na kushirikiana na watu duniani (ardhini) na wale ambao ni dini moja na wao. Ni kwa kuwa na hao kwamba waweza kujenga kiurahisi msingi wa kushirikiana baina yao.

Watu wema wa nafsi roho walioishi kidhamiri wakati wapo hapa Duniani, ingawa si kwa kumcha Mungu, hurudi na kushirikiana na watu wema duniani wenye kiwango cha kiroho sawa na wao na mazingira yanayoruhusu ushirikiano huo.

Mathayo 25 : 41 humtaja shetani na malaika wake. Katika kifungu hiki, malaika wake (shetani) ni pamoja na nafsi roho ovu. Na hata kwa nafsi roho pia, hakuna njia nyingine ya kufufuliwa isipokuwa kwa njia ya ufufuo marejeo wa nafsi roho, ambayo yawezekana tu kwa nyakati maalum. Lakini nafsi roho ovu haziwezi kushuka ardhini kirahisi zipendavyo, na hata kama zitashuka haziwezi kupokea manufaa ya nyakati za ufufuo marejeo. Kabla nafsi roho ovu hazijapokea manufaa ya nyakati za ufufuo marejeo kupitia Ujio wa Pili, kazi ya kwanza lazima itimize sharti la malipizi* kama sharti la kuhitimiza _______________________

**Kuona “Mtazamo wa Kanuni za mpango kwa ajili ya ufufuo’’.*

mapenzi ya Mungu kuondoa dhambi zao kwa kuwaadhibu.

**D. Ufufuo-Marejeo na Nadharia ya Umwilisho.**

Kazi ya Mungu inalenga katika mpango kamili wa ukombozi kwa kuita watu binafsi wengi na kumpa sehemu ya kazi ambayo inamstahili yeye (mhusika). Kwa jinsi mpango wa Mungu wa ukombozi unavyoendelea mbele, kiongozi mpya huteuliwa kwa ajili ya utume huo, Mungu hatua kwa hatua hupanua kipimo cha mpango wa Mungu, hupanuka kutoka kwa mtu mmoja binafsi hadi upeo wa




**Ufufuo Marejeo na Nadharia ya Umwilisho**




**Ufufuo Marejeo na Nadharia ya Umwilisho**

familia, taifa na dunia. Mtu anayekufa bila kutimiza jukume lake lazima arudi na kushirikiana na mtu aliepo duniani ambaye ana jukumu sawa na hali sawa kiroho. Kutokana na mtazamo huu wa jukumu mwili wa mtu duniani huwa mwili wa nafsi roho inayokuja (rudi) vilevile. Kwa mantiki hii mtu aliyepo duniani huwa 'ujio wa pili' wa nafsi roho ya mtu arudiye. Ukiangalia kwa macho ya kiroho, mtu aliyeko duniani huonekana kana kwamba anamwilishwa nafsi roho ambayo inayoshirikiana (unganika naye).

Kwa sababu hii Siku za Mwisho watu wengi watatokea wakijiita Eliya, Buddha, Konfusia, au Mzeituni. Itaonekana kama kwamba nadharia ya kubadilika sura au umwilisho, ni matokeo ya kutafsiri kile kinachotokea kwa msingi wa muonekano, bila kufahamu kanuni za ufufuo marejeo.

**E. Muungano wa Dini kwa Kwa njia ya Ufufuo Marejeo.**

Katika msingi wa kilichoelezwa katika sehemu ya ufufuo – marejeo wa nafsi roho tunaweza kuona ya kuwa nafsi roho ya kiwango cha roho hai ambazo ziko Paradiso, lazima bila kipingamizi zirudi ardhini na kushirikiana na waumini wakati wa ujio wa pili. Muda au wakati na aina ya msaada ambao mtu duniani anapokea kutoka kwa nafsi roho inategemeana na tabia ya mtu, imani na nafasi ya manufaa ya




nyakati za mababu zake. Bado wale wenye imani thabiti mwisho wataongozwa na Roho Mtakatifu kumtambua Bwana wa Ujio wa Pili ambako wanaweza kujizatiti wenyewe kwa kazi ya mapenzi ya Mungu. Kwa kuwa waumini wengi watamzunguka Bwana kupitia ushawishi nafsi roho muungano wa wakristu utatokea wakati wa Ujio wa Pili.

Kama tutakavyojadili katika sehemu ya historia – kiini na pembezoni katika (''Ujio wa Pili'') Ukristo si dini ya Wakristo peke yao; ni dini kuu ikiwa na jukumu lakukamilisha lengo la dini zote ambazo zinaenda katika wema. Kutokana na hali hiyo, waumini wa dini mbalimbali ambao wako dunia ya roho watarudi kwa wale wenye imani moja ambao wapo duniani na kuwaongoza kwa Bwana wa Ujio wa Pili. Lakini hata hivyo muda ambao kila nafsi roho itaunganishwa na dini kiongozi, itatofautiana kulingana na upeo wa kiwango cha nafsi roho na cha imani ya mhusika duniani. Hata kama waumini wa dini mbalimbali hawajaweza kuwa na

mawasiliano na wenzao mpaka sasa, kwa chagizo la watu wa nafsi roho, waumini wote wa dini mbalimbali wataelekea kuungana chini ya Bwana wa Ujio wa Pili.

# SURA YA SITA.

## (PREDESTINATION)

## KUANDIKIWA.

Upungufu wa mafundisho ya kiutamaduni kuhusu ya kuandikiwa umekuwa ndiyo chanzo cha mtafaruku miongoni mwa wanatheolojia na miongoni mwa wanadini na miongoni mwa wacha Mungu. Kuandikiwa katika maana yake kubwa zaidi, ni mafundisho ambayo husema vitu vyote na matukio vimetabiriwa (kuandikiwa) kihatima na Mungu katika kuelekea ukamilisho wa lengo lake milele. Katika maana ndogo, funzo la kuandikiwa hufundisha kuwa wokovu wa binadamu au kulaaniwa inaelekezwa kwa upekee na Mungu na haitokani na jitihada zake binadamu.

Nadharia mbalimbali za kuandikiwa zinapata msingi wake mkubwa kutoka Agano Jipya, na hasa sura ya 8,9 na ya 11 ya barua ya Mtakatifu Paulo akiwaandikia Warumi. Katika sura hizo, Paulo anaweka msisitizo katika rehema kama msingi pekee wa wokovu na kuteuliwa na Mungu. Vifungu vingine katika biblia, vinaweza kutafsiriwa vikionyesha hali zote za maisha ya binadamu kwamba hutabiriwa (hupangwa) na Mungu, kwamba furaha na mikasa ya binadamu na bahati na mikosi, pamoja na kuinukia na kuangamia kwa mataifa vyote hupangwa na Mungu.

**Vipengele vya Biblia vinavyo onekana kusisitiza kuandikiwa kamili**

| | |
|---|---|
| Warumi 8 : 29-30 | Warumi 9: 15-16 |
| Warumi 9 : 10-13 | Warumi 9: 21 |

**Vipengele vya Biblia vinayo pinga kuandikiwa kamili**

| | |
|---|---|
| Mwanzo 2: 17 | Ezekieli 33: 11 |
| Yoh. 3: 16 | Yonah 3: 10 |
| Mathayo 7: 7-8 | Marko 5: 34 |
| Mwanzo 6: 5-7 | Yakobo 5: 14-15 |
| 1 Samueli 15: 11 | |

Kwa namna nyingine, kuna vipengele vingi ambavyo hupinga hoja hii. Kwa mfano, pale tuonapo ona kwamba Mungu alimkataza mwanamume na mwanamke wa kwanza wasile tunda la mti wa ujuzi wa mema na uovu (Mwanzo 2 :17) inakuwa dhahiri kuwa anguko la mtu halikupangwa na Mungu, lakini yalikuwa matokeo ya mtu kukosa utiifu. Yesu alisema "…….kwa jinsi hiyo Mungu aliipenda Dunia na akamtoa Mwanae wa Pekee, yakuwa yoyote amwaminiye hatoangamia bali awe na uzima

wa milele“ (Yoh. 3 :16). Kwa kutumia neno ‘yeyote’ Yesu alionyesha kuwa wokovu upo wazi kwa kila awaye yote, na hivyo hakuna anayepangiwa laana.

Katika Mathayo 7 :7 Yesu alisema, ‘ombeni mtapewa, tafuteni mtapata, bisheni mtafunguliwa. Kwani kila aombaye hupewa, na atafutaye hupata, na yule abishaye atafunguliwa’ (sisitizo limewekwa), kwa uwazi inadhihirishwa kuwa jitihada za binadamu zinachangia sana kubadili matukio, kwamba maisha hayaelekezwi tu na utabirisho mtakatifu.

Kama tungekubaliana bila sharti mafundisho ya kiutamaduni ya kuandikiwa yakinifu, hapo sala, mahubiri, wema, na jitihada za binadamu zisingekuwa na thamani katika Toleo la Mungu la Ukombozi. Hata hivyo, kama kila kitu kingepangwa  kabisa na Mungu basi harakati za binadamu zisingetengua mwelekeo wa maisha uliowekwa sawa kabisa. Sasa hebu tujibu maswali yanayohusu kuandikiwa katika msingi wa Kanuni.

**I : KUA NDIKIWA KWA NIYA YA  MUNGU.**

Kusudi la Mungu ni kuhitimisha adili lake juu ya Uumbaji. Kama matokeo ya anguko la mtu, kusudi la Mungu limebaki bila kutimizwa, na Mungu ilimbidi kufanya kazi ya kukamilisha kusudio hili kwa njia nyingine, Toleo la Ukombozi. Kwa kuwa Mungu ni mwema, lengo lake la asili la kuumba ni jema. Mungu asingeweza kuandikia jambo ambalo lingekwenda kinyume cha kusudi lake mwenyewe. Katika mwanga huu,tuna weza kuona ya kuwa Mungu asingeweza kumuandikia binadamu vitu kama anguko la mtu, dhambi na hukumu na kuadhibiwa kwa mtu.

**Mungu : Mwema**

**Lengo la Mungu la kuumba : Jema**

**Kusudi la mpango wa Ukombozi : Jema**

**kuandikiwa : kwema**

Kama Mungu alipanga anguko la mtu, basi kwa nini amtazame mtu mwenye dhambi na kusema, ya kuwa anasikitika kumuumba mtu (Mwanzo 6 :5-6) ?  Kama matendo yote ya mtu yamepangwa na Mungu, basi kila anapotenda dhambi mtu, au kutokuwa mtii kwa Mungu, matendo haya pia lazima yawe ni matokeo yaliyopangwa na Mungu. Na kama dhambi zote ni matendo ya utovu wa nidhamu kwa Mungu ni mpango wa Mungu, basi kwa nini Mungu alichukizwa na matendo ya mfalme Sauli ya kutotii, na kwa nini ajutie kumfanya Sauli mfalme? (I Sam 15 :11)

Si anguko la mtu, wala ukosefu wa imani wa mfalme Sauli vilipangwa na Mungu, yalikuwa ni matokeo ya kushindwa kwao kutimiza wajibu. Na si kweli kwamba Mungu alipanga hukumu na adhabu ya mtu aliyeanguka. Mungu hatamani kuona mtu anateseka, kama ushahidi kutoka aya zifuatazo, ‘waambie watu, kama ninavyoishi Bwana Mungu, sina furaha kwa kufa mtu mdhalimu, lakini kwamba mdhalimu anabadili njia yake na kuishi, rudi, achana na njia zako za uovu, na kwa nini uje kufa, ee nyumba ya Israeli ? (Ezek 33 :11). Hivyo wakati ule, watu wa Ninive walipoacha njia

yao ya uovu na walipotubu dhambi zao, Mungu hakutimiza utabiri wake kwamba jiji lao lingetekwa (Yoh 3 :10) ni kama vile Mungu alivyosema katika Ezekieli 33 :14 – 15…… Ingawa nasema kwa waovu, 'hakika mtakufa' lakini kama ata achana na dhambi zake na atafuata sheria na kutenda haki, kama mwovu atadumisha ahadi, na kurudisha vile alivyochukua kwa wizi na kuenenda katika haki maishani, asitende uovu ; hakika ataishi, hatakufa.




Mungu : Wa milele, Asiyebadilika, ya kinifu

Kusudi la Mungu : Milele, lisiobadilika, yakinifu

Lengo la Mungu : Kutimiza Kusudi la Uumbaji na Kusudi la

Mpango wa Ukombozi

∴**Lengo la Mungu : la milele, lisilo badilika, ya kinifu**

Ni kwa kiwango gani Mungu ali andikia niya yake, ambayo ndiyo lengo lake la Uumbaji na Kusudi la mpango wake wa Ukombozi ? Mungu ni ya kinifu, wa milele, na asiye badilika ; Kwa hiyo niya yake ambayo ni kutimiza Kusudi Lake la Uumbaji na mpango wake wa Ukombozi lazima pia unakuwa yamilifu, wa milele na usiobadilika (Is 46: 11). Kwa kuwa niya ya Mungu ni yakinifu na lisiobadilika, mtu alieteuliwa na Mungu akishindwa kutimiza jukumu lake, Mungu ataendelea kutafuta kutimiza Lengo lake kwa kuchaguwa mtu mwingine katika nafasi yake.

**II : MPANGO WA MUNGU WA KUTIMIZA KUSUDI LAKE.**

Kama ilivyoelezwa katika ''Kanuni ya Uumbaji'', Madhumuni ya uumbaji hutimizwa pale tu mtu anapotimiza wajibu wake, ambao ni kuishi kwa kufuata amri za Mungu. Kusudi la Mungu kwa ajili ya mpango wa Ukombozi, ambao ni kutimiza Dhumuni la Kuumba, ni yakinifu, na kwa hiyo liko zaidi ya chagizo la binadamu. Pamoja na hayo, kutimia kwa kusudi lake kunategemea kutimizwa kwa jukumu la mtu. Basi, kwa kiwango gani Mungu hupanga kutimizwa kwa kusudi lake ? Kusudi lake Mungu ni yakinifu, lakini kutimizwa kwa kusudi lake hutegemea kutimizwa kwa jukumu la mtu. Mungu huandikia kuwa kusudi lake litimizwe – lakini ni kwa kupitia tu katika kukamilisha kwa

pamoja jukumu la Mungu na lile la mteule wake. Tunaweza kusema kuwa jukumu la binadamu ni la asilimia tano (5%), na lile la Mungu ni la asilimia tisini na tano (95%), kama njia ya kuelezea kuwa jukumu la binadamu kwa kutimiza kusudi la Mungu ni dogo ukilinganisha na lile la Mungu. Hata hivyo, ili kukamilisha asilimia tano, binadamu lazima aweke juhudi za asilimia mia moja (100%).

**Kutimizwa kwa kusudi la Mungu**

↑

**Kutimizwa kwa jukumu la mtu**

+

**Kutimizwa kwa Jukumu la Mungu**

**Kiwango cha jukumu la mtu kwa kutimiza kusudi la Mungu**

**Jukumu la Mungu : 95 %**

**Jukumu la mtu : 5 %**

Hivyo Mungu ali andikia kwamba kusudi lake likuwa litimie wakati ambapo Adam na Hawa watakapotimiza jukumu lao la kutokula tunda la mti wa ujuzi wa mema na mabaya (Mwanzo 2 :17). Katika mpango wa wokovu kupitia kwa Yesu, Mungu ali andikia kwamba mtu alie anguka angetimiza wajibu wake kwa kumuamini Yesu kama Masihi na kumfuata (Yoh 3 :16, Mt 19 :21). Bado mtu hajaweza kutekeleza wajibu wake wa sehemu ya jukumu lake, na hii imesababisha kutimizwa kwa toleo la Mungu kwa ajili Ukombozi kuchelewa tena na tena.

Kama vipengele vifuatavyo vya biblia vinavyoonyesha, hata katika maisha yetu ya kila siku, tunapokea rehema za wokovu kutoka kwa Mungu pale tu tunapotimiza wajibu wetu : ''………sala ya imani itamwokoa mgonjwa…….'' (waraka wa yak 5 :15); ''…….imani yako imekuponya...'' (Marko 5 :34); "... Kwa kila aombaye atapokea, na kwa yeyote atafutaye hupata, na kwa yule abishaye hufunguliwa" (Math 7 :8). Kwa uwazi, Mungu hu andikia ya kuwa rehema yake huweza kupokewa pale tu mtu anapotimiza wajibu wake.

**III : KUANDIKIWA NA MUNGU KUHUSU MTU MTEULE.**

Ili mapenzi ya Mungu yatimie, Mungu lazima amteue mtu mmoja atakayetimiza jukumu la kibinadamu (kama itakavyoelezwa katika "Uchambuzi wa Kanuni za toleo la Ukombozi"). Hata hivyo, mtu aliyeteuliwa na Mungu anaweza akatimiza wajibu wake au akashindwa kutimiza wajibu wake. Hivyo Mungu hapangi kwamba mtu aweze kutimiza kazi yake ambayo anatamani yeye kuwa. Basi je Mungu hupanga matukio ya mtu, na kama ndivyo ni kwa kiwango gani ?

Ndiyo Mungu hu andikia mtu. Mungu anpo mwandikia mtu kwa kazi fulani, humwandikia mtu huyo kwa "asilimia 95 (95 %)". Kwa maneno mengine ni kwamba hummwandikia mtu kwa kiwango cha kwamba iwapo atawajibika kwa kiwango cha "asilimia 5 (5 %)" ya sehemu ya jukumu lake, atakuwa

na uwezo wa kutimiza kazi aliyotumwa. Iwapo mtu atashindwa kutimiza wajibu wake, hawezi kuwa mtu wa aina ambayo Mungu alimtaka awe ; wala mapenzi ya Mungu kupitia kwake hayawezi kuhitimishwa.

Kwa mfano, katika msingi wa asilimia 95“ za kuandikiwa kwa Mungu, Mungu ali andikia Adam na Hawa wawe wahenga wa kwanza wa kweli kwa sharti kwamba watimize wajibu wao. Hata hivyo kwa sababu ya matokeo ya kushindwa kwao kutimiza hayo, mapenzi ya Mungu hayakutimizwa. Kama matokeo ya kushindwa huku, ikawa ni lazima kwa Mungu kumtuma Masihi ili aje awe Baba wa kweli wa wanadamu. Mungu pia ali andikia Yuda Iskariote awe mfuasi wa Yesu mwaminifu kama sharti lake la kutimiza wajibi wake. Hata hivyo, wakati Yuda alipomsaliti Yesu, mapenzi ya Mungu yakawa yamebaki bila kutimizwa, na Mungu akamweka Mathias badala ya Yuda (Matendo 1 :15 – 26)

Lingine hebu tuchunguze mambo yanayompa sifa mtu ya kuwa mteule wa Mungu katika mpamgo wa Ukombozi. Kwanza mtu huyo awe amezaliwa katika Taifa teule,Taifa lililoteuliwa kutekeleza mpango wa Ukombozi. Hii ni kwa sababu watu wateule wako karibu zaidi na Mungu katika roho. Pili, mtu huyo lazima atoke kwa wahenga ambao wana historia ya haki. Ni kawaida kwamba ili kutimiza mpango kwa ajili ya Ukombozi, Mungu angewachagua wale wenye mlolongo wa wahenga maarufu ambao kuna malimbikizo ya manufaa yatokanayo na wao kujitoa mhanga na kuhudumia kwa ajili ya wema kwa wengine.
Tatu, mtu huyo lazima awe amejaliwa tabia ya kiasili inayofaa kutimiza kazi anayopangiwa.
Nne, mtu huyo lazima awe amepata elimu ya kutosha, mafunzo na uzoefu muhimu kwa ajili ya kutimiza jukumu maalum
Tano, mtu huyo lazima azaliwe katika wakati muafaka na sehemu ili kutekeleza mapenzi ya Mungu.

**Sifa za kuwa mtu mteule kwa ajili ya Mpango wa Mungu wa Ukombozi**

| |
|---|
| **1. Taifa Teule** |
| **2. Mababu wazuri** |
| **3. Tabia ya kiasili ifaayo** |
| **4. Elimu na Uzoefu muhimu** |
| **5. Wakati na Mahali muafaka** |

Hata hivyo, pamoja na kwamba mtu anaweza kuwa na sifa zote hizo, na kuandikiwa na Mungu kwa ajili ya kazi fulani, awe atafaulu au kushindwa katika kazi hiyo, hatakuwa ame andikiwa na Mungu. kwa matokeo hayo. Kupata na kuendeleza kazi yake kunawezekana tu pale anapotimiza jukumu lake.

**IV : MAELEZO BAYANA AMBAYO HUONEKANA KUUNGA MKONO MAFUNDISHO YA KUANDIKIWA YAKINIFU.**

Tunawezaje kufafanua vipengele vile vinavyoelekea kuonyesha kuwa kuteuliwa na wokovu wa mtu vinakuwa moja kwa moja vime andikiwa ? Kwa mfano, tunaelewaje Warumi 8 :29 – 30. “Kwa wale

ambao aliwajua hivyo aliwachagua…….na wale aliowachagua aliwaita pia……..na wale aliowaita ali wahesabia haki, na wale alio wahesabia haki aliwatukuza ?

→ kuuwajua kuwachagua ⤵ ⤴kuwa hesabia haki → kuuwatukuza

**Kutimizwa kwa**

**jukumu la mtu**

**Warumi 8 : 29-30**

Kwa kuwa Mungu ni mjuaji wa yote, anajua nani mwenyesifa ya kuteuliwa kama mtu – kiongozi katika mpango wa toleo la Ukombozi. Kwa kutimiza mpango kwa ajili ya Ukombozi, Mungu hu andikia na kumwita mtu. Hata hivyo mtu anae itwa ha andikiwi kuhesabiwa haki na kutukuzwa moja kwa moja. Ili aweze kuhesabiwa haki, ni lazima atimize majukumu yake. Ni pale tu atakapotimiza wajibu wake kwa kuhesabiwa haki, ndipo anaweza kufurahia utukufu kutoka kwa Mungu. Hiki kipengele kutoka katika Warumi huonekana kutetea kuunga mkono mafundisho ya kuandikiwa yakinifu kwa sababu tu kwa hiki kiwango Biblia haitaji kuhusu jukumu la mtu.

Warumi 9 :15 – 16 inasema, " 'Nita mrehemu yeye ani mrehemuye, nitamhurumia yeye ni mruhumiaye'. Hivyo haitegemei mapenzi au jitihada na utashi wa mtu, ila tu kwa huruma ya Mungu". Kipengele hiki kinaonekana kuonyesha kuwa tamanio la mtu, matumaini yake, sala zake, na juhudi zake hazifai kitu na kwamba mtu lazima amtegemee Mungu tu kwa rehema zake. Hata hivyo, hebu tulichunguze suala hili kwa undani zaidi.

Kutokana na msingi wake wa kujua kitu kabla hakija tokea, Mungu peke yake huchagua mtu anayekidhi haja ya kutimiza mpango wa Ukombozi, na niya ya mtu au juhudi zake haziwezi kuzuia au kuathiri maamuzi ya Mungu. Kwa mfano, hakuna anayeweza kuchagua azaliwe nchi fulani, au wa uzao wa familia fulani (maalum), hakuna yeyote anayeweza kuamua ni wapi au lini atazaliwa, hakuna anayeweza kuamua kwamba atazaliwa akiwa na vipaji fulani (maalum) na hakuna anayeweza kuamua juu ya maumbile ya namna hii. Hata hivyo mtu anapochaguliwa, mtu huyo, tamaa yake, matumaini yake, sala zake, na juhudi zake hupelekea iwapo Mungu atamtumia. Madhumuni ya vipengele hivi vya Biblia ni kusisitiza nguvu na rehema za Mungu, kusisitiza vigezo ambavyo Mungu hutumia kuteua na kile anachoamua kufanya na mtu si kazi ya mtu kujua. Madhumuni yake si kukana sehemu ya jukumu la mtu. Warumi sura 9 :21 inasema, 'Je, mfinyanzi hana haki juu ya udongo, kutengeneza sura ya chombo cha urembo na kingine cha matumizi ya kawaida.' Mtu kama kiumbe cha Mungu hapaswi kukataa utashi wa Muumbaji wake katika hali yoyote. Kwa hiyo, mtu aliyeanguka, ambaye hana thamani, hastahili kulalamikia utendaji wowote wa Mungu, ambaye ni kiini cha wokovu wake.

Katika Warumi 9 :10 – 13, tunasoma kuwa Mungu alimpenda Yakobo na kumchukia Esau, hata walipokuwa bado ndani ya tumbo la mama yao, na kuwa Esau mkubwa kati yao, alikuwa amtumikie mdogo wake, yaani Yakobo. Kama itakavyofafanuliwa kwa mapana zaidi katika somo juu ya Familia

ya Ibrahim katika mpango wa toleo la Ukombozi. ' Mungu alikuwa anafanya kusudio maalum kupitia kwa kaka hawa. Ukweli kuwa Yakobo alikuwa 'anapendwa' na Mungu haimaanishi angepokea neema za Mungu bila sharti. Ili kupokea upendo wa Mungu, ilimbidi atimize jukumu lake. Pamoja na kwamba Esau alikuwa 'anachukiwa' na Mungu (kwa sababu ya mpango maaum ambao utafafanuliwa baadae), kama angetimiza jukumu lake, naye pia angepokea baraka ya upendo wa Mungu.

Kuamini katika kuandikiwa kiya kinifu kunatokana na kukosekana uelewa juu ya uhusiano kati ya jukumu la binadamu na jukumu la Mungu katika kutimiza kusudio la Mungu katika mpango wa Ukombozi. Kutoelewa hili kumesababisha kuamini kuwa niya ya Mungu hutimizwa kwa tendo la Mungu pekee na kushindwa kung'amua umuhimu mkubwa wa majukumu ya binadamu.

# CHAPTER SEVEN

# SURA YA SABA

# UKRISTOLOJIA (UKRISTO )

# CHRISTOLOGY

Yesu ni mtu wa namna gani ? Kuna uhusiano gani kati ya Yesu na Mungu ? Kuna uhusiano upi kati ya Yesu na Roho Mtakatifu ? Kuna uhusiano upi kati ya Yesu na mtu wa anguko ? Utatu na kuzaliwa tena (upya) humaanisha nini?

Kristolojia hukabili maswali haya. Ili kuyajibu lazima tuanze kuelewa thamani ya mtu asili na wa kweli. Sababu yake ni kuwa kama Adam na Hawa wangejikamilisha na wangekuwa watu wa kweli, mume na mke wa kweli, na wazazi wa kweli, wakizaa wazawa waliomwilishwashwa (ghubikwa) na wema, pasingekuwepo haja ya majadiliano ya Masihi (na hivyo basi hakuna haja ya majadiliano juu ya Kristolojia).

## I : THAMANI YA MTU AKAMILISHAYE DHUMUNI LA UUMBAJI

Kutokana na dhana zifuatazo, hebu tujadili thamani ya mtu anayekamilisha dhumuni la uumbaji, hii ina maana kuwa, ni yule afuzuye thamani ya Adam mkamilifu.

Awali ya yote nini thamani ya mtu huyu mkamilifu kwa kumhusisha na Mungu ? Kutokana na "Kanuni ya Uumbaji", mtu ameumbwa kama mtoto wa Mungu, kama mtendewa ambaye kimwili hufananishwa na Mungu asiyeonekana. Pale mtu akamilishapo dhumuni la uumbaji, huwa mwili wa Mungu, kiumbe ambacho Roho wa Mungu huishi ndani yake. (1Wakor 3 : 16). Kimaumbile ana asili ya kimungu na ni mmoja na Mungu kihulka. Ni mtu wa kweli, amekamilika kama Baba yake wa Mbinguni alivyokamilika, kama Yesu alivyosema (Math 5 : 48). Hivyo mtu wa kweli ni yule ambaye anaonekana aliyemwilishwa (ghubikwa) na Mungu, ni mwana au binti wa kweli wa Mungu, ana hulka ya Mungu, na anakamilisha Dhumuni la Uumbaji.

Pili, nini thamani ya mtu mkamilifu katika uhusiano na watu wengine ? Kutokana na « Kanuni ya Uumbaji », dhumuni la Mungu la kuumba mtu ni Mungu kufaidi raha ya furaha kupitia kwake mtu huyo. Hivyo kila mtu ni mtendewa kimwili akifananishwa kimaumbo na tabia ndani ya Mungu, ambaye ndiye mtenda. Kwa kuwa watu hufanana mambo yote ya ulimwengu ya Mungu, watu wote wana asili moja. Hata hivyo kila awaye yote hufanana na tabia pekee ndani ya Mungu. Hivyo hakuna watu wawili ambao ni wale wale sawia. Kama Mungu aliumba, popote katika Uumbaji wake, watu wawili au zaidi ambao tabia zao ni sawia, basi Uumbaji wake Mungu ungekuwa ni kazi bure. Kwa kuwa mtu ameumbwa ili awe

ni wa milele, tamanio la Mungu la kupata raha kupitia mtu awaye yote inatimizwa tosha kupitia mtu huyo mmoja.

Kwa hiyo mtu anayekamilisha lengo la uumbaji huwa mtu asiye na mfano, ni wa pekee katika ulimwengu wote, hata awe wa namna gani. Kwa maneno mengine mtu wa kweli, mtu akamilishaye dhumuni la uumbaji, ni mtu namna ya pekee ambaye hatafananishwa milele daima, hivyo ana thamani aliyozaliwa nayo pekee, ambayo haiwezi kukataliwa.

Tatu, nini thamani ya mtu mkamilifu katika uhusiano wake na uumbaji wote ? Kufuatana na kanuni ya uumbaji, mtu aliumbwa atawale dunia ya kiroho kwa uwezo wa roho yake na dunia ya umbo kwa uwezo wa mwili wake. Mtu, kwa hali hiyo huwa muunganishi wa dunia hizi mbili katika uhusiano wao. Mtu anayekamilisha dhumuni la uumbaji anapaswa kuutawala ulimwengu wote (Mwa 1 : 28).




**Thamani ya mtu akamilishaye dhumuni la uumbaji :**

1. Thamani ya takaifu
2. Thamani ya kipekee
3. Thamani ya kiulimwengu

Roho ya mtu ni kuwa maikrokosimu (ulimwengu-mdogo) wa dunia ya roho na mwili wake uwe maikrokosimu wa dunia ya kimwili. Mtu wa kweli, yule anayekamilisha dhumuni la uumbaji, ni ulimwengu- mdogo (ana ana thamani ya ulimwengu wote. Ukweli kwamba mtu kiasili ana thamani ya ulimwengu ni hoja ya maoni ya Yesu, kwa kusema " 'na itamfaidia nini kama mtu atapata dunia yote na kuangamiza maisha yake ? (Math 16 : 26).

**II : YESU NA MTU AKAMILISHAYE DHUMUNI LA UUMBAJI.**

**A : Yesu na mtu mkamilifu.**

Kama ilivyoelezwa katika 'anguko', kama Adam angekuwa mtu wa kwanza kukamilisha uthamani wa uumbaji, angekuwa hasa Mti wa Uzima ambao unatajwa katika kitabu cha mwanzo 2 : 9, na hivyo , wabini wake wote wangekuwa ni miti ya uzima. Hata hivyo kwa kuwa Adam alianguka, hakuweza kufikia thamani ya mti wa uzima (Mwa 3 : 24) na kuanzia

hapo, watu wa anguko wamekuwa wakitumainia ukombozi wao na kuwa miti ya uzima (Mithali 13 : 12, Ufunuo 22 : 14).

Mwanzo 2 : 9 Mti wa Uzima Ufunuo 22 : 1



Mtu adilifu…..Adam mkamilifu ……… ……………Yesu ……Mtu adilifu

Ingawa mtu wa anguko ana jina la kuwa 'hai' kwa kweli yeye ni mti wa uzima batili na uliokufa (Ufunuo 3 : 1). Kwa kuwa watu wa anguko hawawezi kujikomboa kama miti ya uzima kwa nguvu zao wenyewe, Mti wa Uzima – kwa maneno mengine mtu ambaye amekamilisha uthamani wa uumbaji – lazima aje, ampandikize mtu wa anguko kwake. Mtu ajaye kama Mti wa Uzima ni Kristu (Ufunuo 22 : 14). Hivyo Adam mkamilifu aliyeashiriwa kama Mti wa Uzima katika Bustani ya Eden, na Yesu, anayefananishwa na Mti wa Uzima katika Ufunuo 22 :14, wanafanana katika mtazamo kwamba wote ni watu ambao wametimiza adili la uumbaji.

Na hapo basi, Yesu ni mwanadmu ? Ndiyo ni mwanadamu. Ni mfano wa mtu aliyekamilisha adili la uumbaji ; ni mtu wa kweli, mfano wa mtu yule ambaye alipaswa kuwa tangu awali, kwa jinsi hiyo thamani yake haiwezi kulinganishwa na mtu wa anguko.

Kama ilivyokwisha tajwa, mtu wa kweli ni yule atimizaye kusudi la uumbaji, ni mwilisho wa Mungu, na ni mkamilifu kama Mungu alivyo mkamilifu, akiwa na thamani takatifu. Mtu mkamilifu pia ni wa pekee, asiyeshabihiana (rudufu) na mtu mwingine na ni Bwana wa ulimwengu wote na ni mwenye thamani ya ulimwengu wote. Yesu ni mtu wa kweli, na hivyo ni mtu wa thamani hiyo.




**Thamani ya Yesu :**

1. Thamani takatifu
2. Thamani ya kipekee
3. Thamani ya kiulimwengu

Kanuni haikatai moja kwa moja imani ya pamoja ambayo imechukuliwa na wakristo wengi kwamba Yesu ni Mungu, kwa sababu mtu mkamilifu, wa kweli ni mmoja na Mungu. Zaidi ya hayo, pale Kanuni inapoweka msimamo wa kuwa Yesu ni mtu wa kweli, hii haipunguzi hata kidogo thamani yake. Hii ni rahisi kwamba pale mtu anapochunguza thamani ya mtu mkamilifu, tunagundua ni sawa na thamani ya Yesu. Kwa kweli, kama mwanaume na mwanamke wa kwanza wasingeanguka nao wangekuwa mwanaume na mwanamke wa thamani hiyo, hapo kuja kwa Yesu kusingekuwa kwa lazima. Lingekuwa kosa kubwa kusema ukweli, kuchukulia kuwa thamani ya mtu wa anguko inaweza kulinganishwa na Yesu, sababu Yesu alikuwa ni mtu. Alikuwa ni mtu wa kweli. Hebu tudodose mingi ya kibiblia ya kusema hili.

> Kwa kuwa kuna Mungu mmoja, kuna mwakilishi/mpatanishi kati ya Mungu na watu, *mtu huyu* Kristu Yesu (I Tim 2 :5)
>
> Kwa kutotii mtu mmoja wengi walifanywa wenye dhambi, na hivyo kwa utiifu wa mtu mmoja wengi watafanywa wenye haki (Warumi 5 :19).
>
> Kwa jinsi kifo kilikuja kupitia kwa Adam, kwa mtu (Yesu) kumekuja ufufuko wa wafu. (I Wakor 15 :21)
>
> ………kwa sababu amepanga siku ambayo atahukumu dunia kwa haki ya mtu ambaye amemchagua, na kwa hili ametoa uhakika kwa watu wote kwa kumfufua katika wafu. (Maten 17 :31)

Vipengele hii vinaonyesha kuwa Yesu alikuwa mtu. Yesu mwenyewe alijitambulisha kama Mwana wa mtu katika shemu nyingi za biblia (mfano Lk 17 :26, 18 :8).

**B : Je, Yesu ni Mungu ?**

Mpaka sasa hivi, wakristo wengi wameamini kwamba Yesu ni Mungu, muumbaji, wakiwa wameegemea kimsingi vifungu vifuatavyo kutoka katika Biblia :-

Wakati Filipo alipomwomba Yesu amwonyeshe Mungu, Yesu alijibu, « yule aliyeniona amemwona Baba', inawezekanaje mkasema, 'tuonyeshe Baba' ? Je hamuamini kuwa nipo ndani ya Baba naye ndani yangu ? » (Yoh 14 :9, 10) hata hivyo hii haimaanishi kuwa Yesu ni Mungu. Kama ilivyokwisha fafanuliwa hapo juu , Yesu alikuwa udhihirisho wa Mungu asiyeonekana na ni mmoja na Mungu katika Roho ; na bado hii haimaanishi kuwa alikuwa ni Mungu. Filipo alimwambia Yesu kumwonyesha Mungu. Lakini Mungu anaweza kung'amuliwa kwa dhati na mtu ambaye ni mkamilifu. Filipo alikuwa bado hajafikia ukamilifu, na kwa hiyo Yesu hakuwa na uchaguzi mwingine zaidi ya kujionyesha mwenyewe.

Vile vile Biblia inasema, 'Alikuwa Yesu duniani, na dunia iliumbwa kupitia kwake, bado ulimwengu haukumtambua' (Yoh 1 :10). Katika msingi wa kifungu hiki, wakristu wanaamini kuwa Yesu ni muumbaji.

Mengwa mkuu wa thamani ya Mungu ya uumbaji ni mtu, na mbingu zimepangwa na kuumbwa ili ziwe eneo ambalo kila mtu mwadilifu atalitawala. Hivyo Mungu akafanya ya kuwa mtu atakayekamilisha dhumuni la uumbaji kuwa wa thamani ya hali ya juu kabisa. Kutoka kiumbe cha chini hadi cha juu, Mungu aliviumba vyote na baadaye alimuumba Adam kama bwana wa vitu vyote. Halafu yote kama mtu aliyekuwa anatimiza dhumuni la uumbaji, akawa mtu wa thamani ambayo Mungu aliiona mapema kabla ya uumbaji kuumbwa. Katika hali hii, Yesu alikuwepo tangu mwanzo. Wengine hujaribu kumfananisha Yesu na Mungu katika msingi wa kunukuu katika Yoh 5 :58, ambamo Yesu alisema 'kabla ya Ibrahim kuwepo, mimi nipo'. Lakini Yesu hakumaanisha kuwa alikuwa Mungu. Kwa namna nyingine Yesu aliweza kusema hivi kwa sababu, pamoja na kwamba ubini wake ulitokana na Ibrahim, kiukweli yeye ni mkongwe wa Ibrahim kwa sababu alikuja kutoa kuzaliwa upya, kwa watu wote katika mingi wa Adam mkamilifu, hii ndiyo kusema, kutoka katika nafasi ya mzazi wa kweli, babu wa kweli wa watu wote.

Kama Yesu alikuwa Mungu na hapo katika dunia ya roho, baada ya kufufuka kwake angeweza kuwa mmoja na yule yule Mungu, kuliko kuwa katika nafasi ambayo ni 'karibu na Mungu'. Hata hivyo, katika dunia ya roho, Yesu anasemekana kuwa mkono wa kulia wa Mungu akituunganisha sisi kwake (War 8 :34). Yesu alizaliwa duniani kama mwana wa mtu na alikuwa na mwonekano wa umbo kama la mtu mwingine yeyote. Katika dunia ya kiroho anaishi kama nafsi roho kama vile wanafunzi wake waishivyo, tofauti pekee iliyopo ni kwamba nafsi roho yake haina asili ya dhambi hivyo hung'ara sana.

Kama Yesu angekuwa Mungu, iweje atuunganishe kwake mwenyewe ? wakati alipoomba alionyesha wazi ya kuwa hakuwa Mungu kwa kumwita Mungu Baba (Yoh 17 :1) kama Yesu angekuwa Mungu ingewezekana vipi atiwe majaribuni ? (Math 4 :1) na kuteswa na kupelekwa kusulubiwa msalabani na shetani ? ni dhahiri kwa ushahidi maalum kwamba Yesu siye Mungu wakati akiwa msalabani, akalia kwa sauti, Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha ? (Math 27 :46)

**C : Yesu na mtu aliyeanguka.**

Mtu aliyeanguka halinganishwi na Yesu. Mtu wa anguko hakamilishi dhumuni la uumbaji, na yuko mbali na roho ya Mungu. Nini zaidi, kwa sababu ana dhambi ya asili, yumo katika hali ya chini mno kiasi kwamba hata huwaonea wivu malaika, ambao waliumbwa wawe watumishi wa mtu, na hawezi kujinasua na shutuma za shetani kwake. Hivyo mtu wa anguko ni tofauti sana na Yesu ambaye alikuwa mkamilifu, mtu wa kweli, hata hivyo pamoja na kwamba mtu wa anguko hana thamani , kwa kuzaliwa upya kiroho kupitia kwa Yesu, ambaye alipaswa kuwa baba wa kweli, mtu wa anguko atakombolewa kama mwanaye wa kiroho na baadae kufanana na Yesu. Halafu Yesu huwa mkuu wa kanisa (Waef 1 : 22) na watu wa anguko ndiyo mwili wake na waumini (I Wakor 12 :27). Yesu ndiye Hekalu kuu nasi tu matawi

ya hekalu hilo ; (Yoh 15 : 5). Ili tuwe miti ya mizeituni ya kweli, sisi kama miche ya mizeituni pori, tunapaswa kupandikizwa kwake Yesu, ambaye ndiye mti wa mzeituni wa kweli (Warumi 11 : 17). Hivyo Yesu alituita sisi rafiki zake, na Yohana akasema kuwa atapotokea Yesu, tutakuwa kama yeye (I Yoh 3 : 2). Biblia inasema pia ya kuwa Yesu ndiye 'matunda ya kwanza' nasi tutafuata nyuma yake (I Wakor 15 : 23).

## III. KUZALIWA MARA YA PILI NA UTATU .

### A : Maana ya kuzaliwa mara ya pili, (kuzaliwa upya).

Yesu alimwambia Nikodemo mtawala wa wayahudi kwamba, bila mtu kuzaliwa upya, hawezi kuuona ufalme wa Mungu (Yoh 3 :3). Na halafu kwa nini mtu azaliwe upya ?

Kama Adam na Hawa wangekamilisha uthamani wa uumbaji na wangekuwa watu wa kweli, wazazi wa kweli, wa kuzaa watoto wa kweli (bila dhambi), ufalme wa mbingu duniani ungekamilishwa. Hata hivyo, kwa sababu ya anguko lao, walitokea kuwa wazazi batili, na wazawa wao wamekuwa na dhambi ya asili na kudhihirisha ufalme wa jehanam duniani. Kwa hiyo watu wa anguko hawawezi kuuona ufalme wa Mungu isipokuwa tu wazaliwe upya kama watoto wa mbingu wasio na dhambi ya asili.

Hatuwezi kuzaliwa bila wazazi. Watu wa anguko kwa dhati wanahitaji wazazi wa wema ambao watawapa uzao mpya na kuwa watoto wasio na dhambi ya asili ; ukimwezesha kila mmoja kuingia katika ufalme wa Mungu. Yesu alikuwa baba wa kweli ambaye alikuja kutupa kuzaliwa upya kama watoto wa wema. Kwa hiyo, (I Petro 1 : 3 ) anasema, 'abarikiwe Mungu na baba wa bwana wetu Yesu Kristu ! kwa huruma yake kuu tumezaliwa upya katika tumainI – hai kwa ufufuko wa Yesu Kristo kutoka kwa wafu'. Hii inaonyesha kuwa Yesu ni kiini cha kuzaliwa upya. Yeye anaitwa vilevile 'Adam wa mwisho' (I Wakor 15 : 45) na 'Baba wa milele' (Isaya 9 : 6) kwa sababu alikuwa awe Baba wa kweli, ambapo Adam alishindwa kuwa hivyo.




Hata hivyo, kuwapa watu wa anguko uzawa mpya kama watoto wa wema, lazima awepo si Baba wa Kweli tu ila na Mama wa Kweli. Roho Mtakatifu ndiye yupo katika nafasi ya Mama wa Kweli akiwa na Yesu mfufuka. Hii ndiyo maana Yesu alimwambia Nikodemo kwamba lazima azaliwe upya – azaliwe na Roho Mtakatifu (Yoh 3 :3 – 5). Kwa kuwa Roho Mtakatifu alikuja kama Mama wa Kweli, au Hawa wa pili, wapo wengi ambao hupata ufunuo ukionyesha kuwa Roho Mtakatifu ni Roho – jike. Roho Mtakatifu huliwaza na kuvutia roho za watu (I Wakor 12 :3 – 10). Yesu amekuwa akifanya kazi katika dunia ya kiroho, na wakati huo huo Roho Mtakatifu akifanya kazi duniani ya kusafisha dhambi za watu. Tunapomwamini Yesu, tunaingia katika upendo utokanao na uhusiano kiushirika kati ya Yesu mfufuka na Roho Mtakatifu ambao ni Baba wa Kweli wa roho na Mama wa Kweli wa roho. Kwa kuzaliwa upya kutokana na kumwamini Yesu na kumpokea Roho Mtakatifu humaanisha roho ya mtu huwa mpya na mhusika hupokea uzima mpya kupitia upendo wa Wazazi wa Kweli wa kiroho. Huku ndiko kuzaliwa upya kiroho. Hata hivyo kwa kuwa mtu alianguka kiroho na kimwili, kila mtu awaye yote lazima azaliwe kiroho na kimwili. Hii ndiyo sababu kuwepo kwa haja ya ujio wa pili.

**B : Maana ya utatu.**

Mpaka hivi sasa, kutokana na taaluma ya dini ya Ukristo, Wakristo wameelewa ya kuwa Mungu ambaye anafanya kazi ya wokovu wa mtu kuwa ni mtatu mmoja (Mungumwoja mwenye nafsi tatu) na wameamini kuwa ajidhihirishapo hutokea mmoja katika nafsi tatu, Baba, Mwana na Roho Mtakatifu. Anapojifunua kama muumbaji, huwa katika nafsi ya Baba yetu wa mbinguni. Anapojifunua kama mwokozi yupo katika nafsi ya mwana, na anapojidhirisha yeye mwenyewe kama mleta amani anakuwa katika nafsi ya Roho Mtakatifu.

Nadharia ya Utatu imechangia mjadala mrefu katika historia. Hebu tuchunguze hili katika ufahamu wa Kanuni. Kama anguko la mtu lisingetokea Mungu asingekuwa na haja na Roho Mtakatifu na Yesu wafanye kazi ya kumkomboa mtu. Kama Adam na Hawa wangejikamilisha wao wenyewe kama mwana na binti wa Mungu, kila mmoja akighubikwa na umungu wa Mungu, na hapo wangekuwa wakamilifu kama Baba yao wa mbingu alivyo mkamilifu (Math 5 : 48), na wangepata umoja wa thamani pamoja na Mungu (Yoh 14 : 20), na hapo Adam angekuwa mwana mtakatifu wa Mungu, na Hawa bintiye mtakatifu. Wangekuwa mume wa kweli na mke wa kweli, chini ya utawala wa Mungu. Kama Adam na Hawa wangekuwa kitu kimoja kama wazazi wa kweli, chini ya Mungu wao pamoja na Mungu ndio wangekuwa *utatu asilia*. Utatu uliotokana na roho na thamani ya Mungu.




Utatu wa Kishetatni

*Ulikamilishwa*




Utatu Asilia wa Mungu

*Haukukamilishwa*

Hili ni sharti la muhimu kwa kudhihirisha Baraka Tatu na Msingi wa Nafasi Nne ambazo hukamilisha Dhumuni la Mungu la Uumbaji. Na bado kwa sababu ya Anguko, Adam na Hawa wakatokea kuwa wazazi batili wa mtu, na kushindwa kutimiza Dhumuni la Uumbaji, walijenga utatu wenye msingi kwa Shetani. Kwa hiyo, ili kukamilisha Dhumuni la Uumbaji, Mungu akawa na Yesu na Roho Mtakatifu wachukue nafasi ya Adam na Hawa, wakawa kama Adam wa pili na Hawa wa pili na kama Wazazi wa Kweli. Hata hivyo, katika kuwapo utatu wa kiroho chini ya Mungu, Yesu na Roho Mtakatifu walihitimisha kazi ya kuwa Wazazi wa Kweli wa kiroho tu. Kwa hiyo, Bwana wa Ujio wa Pili anakuja kuwa Baba wa Kweli atakayeujenga utatu katika roho na mwili.







Adamu wa Pili Hawa wa Pili

Utatu wa Kiroho

Adamu wa Tatu Hawa wa Tatu

Utatu wa Kiroho na Kimwili

## CHAPTER EIGHT

## OVERVIEW OF THE PRINCIPLES OF RESTORATION

## SURA YA NANE

## MWANDANI MWA KANUNI ZA UKOMBOZI

### I. HISTORIA KUTOKANA NA MTAZAMO WA MPANGO KWA AJILI YA UKOMBOZI .

Kama ilivyofafanuliwa katika ‘Kanuni za Uumbaji’, Mungu alimuumba mtu aishi katika upendo wake milele- kwanza, katika Ufalme wa Mbinguni hapa duniani, na baadaye kama mwili wa kiroho, katika Ufalme wa Mbinguni katika dunia ya roho. Hata hivyo kwa kuwa mwanaume na mwanamke wa kwanza walianguka (katika kipindi cha kukua) wali mwilishwa dhambi na kutawaliwa na Shetani. Lakini Mungu asingeweza kuacha Kusudi lake la awali kwa ajili ya Uumbaji bila kutimizwa. Katika Isaya 46 :11 Mungu anasema “ ‘Nimesema, na Nitalipitisha; Nimedhamiria na Nitalifanya, ‘ “ akionyesha dhahiri atatimiza mpango wake asilia. Amepania kumkomboa mtu. Mpango wake wa kumuokoa mtu wa anguko linahusika na kumkomboa mtu na kumweka katika hali yake ya asili. Ebu tuangalie jinsi Mungu alivyokuwa akifanya kazi kumuokoa mtu katika muda wote wa historia.

Historia haihusiki tu na nani alifanya nini, wakati walipofanya hivyo, na wapi ilipofanyika. Ni uzoefu wa binadamu kwamba ni vigumu aweze kuunda mlolongo wa historia yake binafsi. Kutokana na mtazamo wa Mungu, historia ya mtu ni kumbukumbu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu –ambao




Ndiyo mpango kwa ajili ya ukombozi wa mtu wa anguko, ambaye yupo chini ya utawala ya Shetani. Historia ya mtu ni uthibitisho wa kazi ya Mungu katika kukamilisha dhumuni la ukombozi. Hivyo, ni historia ya Toleo la Mungu la Ukombozi.

Lengo la  Mungu kwa ajili ya mpango wa Ukombozi ni ukombozi wa mtu wa anguko katika nafasi ambayo anatimiza Dhumuni la Uumbaji na ukombozi wa ulimwuengu kama ulivyo umbwa kiasili.  Kwa hiyo, historia ya binadamu inaweza kutafsiriwa kama historia ya mpango wa Mungu kujenga upya dhumuni la uumbaji katika maisha ya mtu.

**A.  Mtu aliye anguka ni Tumbo la .wema na uovu.**

Mtu anayetimiza dhumuni la Mungu la uumbaji huwa Hekalu la Mungu, ambamo Roho ya Mungu hukaa (I Wakor 3 :16). Mtu wa namna hiyo atakuwa na tabia takatifu tena " '..... atakuwa mkamilifu kama Baba [yake] wa mbingu alivyo mkamilifu' " (Math 5 :48).  Na Mungu atakuwa daima kiini cha mawazo, matendo na maisha ya mtu wa namna hiyo. Historia binafsi ya mtu huyo itakuwa nzuri ; na historia za familia za watu wa namna hiyo zitakuwa nzuri, na mataifa na dunia yenye watu wa aina hiyo, watakuwa si kitu kingine zaidi ya wema. Kwa hiyo uadilifu wa historia ya watu kama ilivyobuniwa katika akili ya Mungu waweza kutamka kwa neno moja : wema.




Hata hivyo, kwa sababu ya Anguko, mtu hakuweza kuwa Hekalu la Mungu. Kinyume chake akawa makao ya Shetani, na kwa kuwa kitu kimoja na Shetani, mtu akawa na tabia ya uovu badala ya asili takatifu. Matokeo yake, Shetani ndiye" '...mtawala wa dunia hii"'… (Yoh 12 :31) na "....Mungu wa dunia hii……."(II Wakor 4 :4) na hudhibiti mawazo ya mtu wa anguko, matendo yake, na maisha yake.  Matokeo yake, Historia ya binadamu imekuwa ni ya

uovu,historia ya watu hao familia za watu hao, na taifa lenye watu wa namna hiyo, isingeweza kuwa nyingine isipokuwa ya uovu. Historia ya binadamu ilianza kama historia ya dhambi na uovu na imeendelea vivyo hivyo.




Kama ilivyokuwa imefafanuliwa awali katika 'Anguko', mtu alianguka wakati akikua kuelekea ukamilifu. Ukamilifu wa namna hiyo humaanisha kumwilisha Uthamani wa Uumbaji. Hata hivyo, matokeo ya anguko, mtu wa anguko amemwilishwa na kuwa tumbo la mema na mabaya. Adam na Hawa walikua kufikia hatua fulani chini ya Mungu. Hivyo kwa kiasi fulani walikuwa na msingi mema ndani mwao, uliofanana na Mungu, pamoja na kwamba ulikuwa bado mchanga. Kwa nyongeza walijenga msingi wa uovu ndani mwao wenyewe kwa kupokea chembechembe za uovu kutoka kwa malaika mkuu. Chembechembe za anguko zilizopokelewa kutoka kwa malaika mkuu ni Dhambi ya Asili. Hata hivyo, kiwango cha wema na ubaya kilichomo ndani ya mtu wa anguko hakijakua kwa nafasi sawa. Msingi wa uovu umefikia kiwango cha juu kabisa kiasi kwamba umezaa tunda na hivyo inakuwa rahisi kuufanya na kuonekana. Kwa upande mwingine, msingi wa mtu wa wema ni mchanga tu, na kwa hivyo ni pale tu juhudi za ufahamu wa kiroho utakapofanywa kuupa moyo, vinginevyo ni vigumu kwa wema huo kuzaa tunda.




**B : Mapambano kati ya wema na uovu – Mwelekeo Uliofichika katika historia.**

Ili kudhihirisha dhumuni la uumbaji miongoni mwa dunia ya anguko, ambayo shetani hutawala, Mungu kwa ufanisi makini ametekeleza mpango kwa ajili ya Ukombozi kwa kutenganisha mema na maovu. Matokeo yake, Historia yote ya binadamu imejengeka kupambana kati ya wema na uovu. Mtu wa anguko huunganika na shetani katika akili yake na kutenda dhambi kwa njia ya mwili wake. Lakini bado binadamu ana akili ya asili ndani yake ambayo imeumbwa na Mungu, na daima mwelekeo wake huelekea kwa Mungu.

Katika mpango kwa ajili ya Ukombozi, kuna mapambano yasiyo onekana kati ya Mungu na shetani. Na mtu akiwa amemwilishwa wema na uovu, hujikuta kanasa katikati ya mapambano– kati ya Mungu, anayejitahidi kumleta mtu kwake kwa kupitia njia ya msingi wa wema (Akili Asili) ndani ya mtu, na shetani, akifanya chini juu kumweka mtu upande wake kwa njia ya msingi wa uovu (Akili Ovu) ndani ya mtu. Bila kuelewa sababisho lisiloonekana la Mungu na shetani, historia ya binadamu haiwezi kueleweka vizuri. Haiwezi kueleweka kirahisi kwa kuangalia juu-juu shughuli za binadamu Duniani.

Kuna mgongano unaoendelea kati ya utawala wa shetani mwovu, ambao anajaribu kumshikilia mtu, na utawala mwema wa Mungu, anayejaribu kumrudisha na kumkomboa mtu.




Hili linaonekana katika mapambano kati ya wema na uovu katika dunia hii. Katika mapambano kati ya Mungu na shetani ndipo kuna sababu ya umwagaji damu wa kwanza uliowekwa katika kumbukumbu za Biblia, pale Kaini alipomuua Abeli ; na katika mapambano haya haya kuna sababu ambayo historia ya binadamu imetiwa alama na mitafaruku na vita, bila kujali iwapo mtu anaangalia Mashariki au Magharibi. Bila kujali kama nafasi za uongozi katika mapambano haya zinashikwa na mtu binafsi mmoja, familia mbalimbali, makabila, mataifa au kambi za mataifa, haya mapambano, yote hujumuisha mapambano kati ya Mungu, anayeshughulikia upande wa wema, na Shetani anayeshughulikia upande wa uovu. Kwa mpango huo, ni kazi ya Mungu na ni kazi ya Shetani kwamba wanahusika katika kila pambano la kibinadamu, iwe ni pambano kati ya mtu binafsi na






mwingine, familia moja na nyingine, kabila moja na lingine, taifa moja na lingine au kambi moja ya mataifa na mengine.

Kwa wakati mwingine, mapambano yamekuwa juu ya mal , ardhi au watu na wakati mwingine, juu ya itikadi na imani tofautitofauti. Lakini haya yote ni marejeo ya harakati kati ya Mungu na Shetani. Mungu anajaribu kumkomboa mtu kuelekea dhumuni la wema, na Shetani anajaribu kudumisha nafasi yake ya uovu na mamlaka. Mapambano haya baadae hujidhihirisha katika dunia kama mitafaruku iliyowekwa katika kumbukumbu ya historia ya binadamu.

**C : Chanzo cha maendeleo na hatua za historia.**

Basi, ni nguvu gani inayoendesha historia ? Pale tunaposema kuwa historia yote ni kielelezo cha mpango wa kazi ya Mungu, je, inamaanisha kuwa historia huendelea tu kwa mpango wa kazi ya Mungu ? Hata hivyo lengo la historia ni kukomboa Dhumuni la Uumbaji, je mgongano kati ya wema na uovu huendelea moja kwa moja kwa kawaida kuelekea Dhumuni hilo ? Kama ni hivyo, ni namna gani basi tunaweza kufafanua uovu mwingi na maafa katika historia, kama vile kuenea na kuendelea kuwepo uovu au mateso kwa watu wema, vitu ambavyo visingefikirika kama kazi ya Mungu mwenye – enzi Mungu wa wema ?.

Hapo mwanzo, Mungu alimpa mwanaume na mwanamke wa kwanza amri ambayo walipaswa kuitii mpaka wajikamilishe. Kutimizwa kwa Dhumuni la Uumbaji kunawezekana tu pale mwanaume na mwanamke wanapotimiza wajibu wao, kwa kutii amri. Dhumuni la Uumbaji si kutimizwa kwa kuangalia tu kuhusika, na matendo ya upande wa Mungu tu. Ingawa jukumu la mtu linaweza kuonekana kuwa dogo ni kanuni ya Uumbaji kwamba jukumu la mtu ni jambo la lazima. Hivyo, ili kukomboa Dhumuni la Uumbaji lililopotezwa, sehemu ya jukumu la mtu ni muhimu kabisa – hili halifanywi na nguvu za Mungu na mpango pakee.




Lakini inawezekana kwa mtu kutimiza wajibu wake au kuto kutimiza. Pale mtu anapotimiza wajibu wake, kusudi la Mungu hudhihirishwa katika historia kupitia kwa mtu huyo ; na mpango wa Mungu unakamilishwa kwa dhati na ukombozi unaendelea. Lakini mtu ashindwapo kukamilisha wajibu wake, mpango wa Mungu kupitia mtu huyo unavurugika na badala yake matakwa ya shetani hutokea kuonekana katika historia. Hivyo, mtu anaweza kumfurahisha Mungu kwa kutimiza wajibu wake, au kumhuzunisha Mungu kwa kushindwa wajibu wake. Sababu ambayo hufanya historia ya mtu kuwa si chochote zaidi ya kuwa marejeo ya mara kwa mara ya historia ya dhambi, kwa matarajio ya dunia adilifu ionekana kuwa mbali sana, si kwa sababu Mungu hana uwezo, au kwa sababu si yakinifu, ila ni kwa sababu, mtu hajatimiza wajibu wake katika kutekeleza matakwa ya Mungu. Mungu ni yakinifu, wa milele, na mwenye uwezo usio zuilika. Kwa hiyo ukamilishaji wake wa dhumuni la uumbaji na dhumuni lake la ukombozi vyote ni yakinifu. Kusudi la Mungu la ukombozi litatimizwa bila shaka (Isaya 46 :11). Kwa hiyo, iwapo mtu anaetekeleza mapenzi ya Mungu asipo timiza jukumu lake→ Mungu baada ya muda hukomboa msingi sawia na masharti kama ya awali na




huchagua mtu mwingine kuchukua jukumu hilohilo. Hii ndiyo sababu tunashuhudia matukio yanayofanana yakitokea miaka mingi katika historia ya toleo la Mungu, hata baada ya vipindi vya miaka elfu mbili hadi nne. Tunaita vipindi hivi vya matukio marejea, uanisho

(utambulisho) wa muda wa toleo. (kwa ufafanuzi mrefu rejea somo la uanisho wa muda wa toleo)

**II : KANUNI ZA UKOMBOZI.**

**A : Mpango kwa ajili ya ukombozi na Masihi .**

Ni kanuni zipi maalum za mpango wa Mungu kwa ajili ya ukombozi wa mtu wa anguko ? Katika kiwango cha utimilifu wa hatua ya kukua , mtu alianguka na hivyo akawa chini ya utawala wa Shetani. Ili Mungu awakomboe watu wa anguko, Mungu lazima kwanza awatenganishe mbali na Shetani. Hii ni kwa sababu pale mtu anapoendelea kuwa mtendewa wa Shetani, au kukaa chini ya chagizo lake Dhumuni la Uumbaji haliwezi kukamilishwa. Ili kutenganishwa kabisa na Shetani, bila kuacha msingi wowote ambao Shetani anaweza kushambulia tena, mhusika lazima asafishwe (atakaswe) dhidi ya Dhambi ya Asili. Kwa sababu ndiyo mzizi wa yote ambayo Shetani hushitakia na kumshambulia mtu wa anguko. Hata hivyo Dhambi ya Asili haiwezi kuondolewa bila mtu kuzaliwa upya kupitia kwa Masihi ambaye anakuja kama Mzazi wa Kweli. Ni Masihi tu anayeweza kuondoa dhambi ya asili.

Masihi ambaye ni mtu kiongozi ni muhimu kupindukia katika Toleo la Ukombozi,mtu wa kati kwa ajili ya toleo la ukombozi na mfano wa mtu wa kweli, ni kupitia yeye Mungu hu umba watu binafsi wa kweli, familia, makabila, mataifa na Dunia ambayo hutimiza thamani asili ya Uumbaji. Kwa hiyo, Mungu hawezi kumtuma Masihi Duniani bila maandalizi ya kutosha. Maandalizi ni lazima kwa sababu tangu siku za anguko la mtu, binadamu wamekuwa wakimtumikia bwana batili, Shetani, na kama Masihi angetumwa katika mazingira ambayo hayajaandaliwa, kuna hatari ya kwamba dunia ya kishetani itajaribu kumuangamiza. Kwa hiyo, kutoka miongoni mwa watu ambao wanamtumikia bwana batili, Mungu kwanza huchagua mtu mmoja ambaye atamheshimu na kumtii. Katika msingi wa mtu huyu mmoja, Mungu huumba familia na mataifa ambayo yanakuwa yamejitenga mbali na upande wa familia za Shetani na mataifa ambayo baadae yanaweza kutumika kama msingi wa imani ambao Masihi anaweza kuja kupitia msingi huo.

Kwa kuwa tangu mwanzo wa toleo la Mungu kwa ajili ya ukombozi Masihi bado hajaja, mtu wa anguko lazima afuate sharti la kujikomboa yeye mwenyewe kiishara kufikia kwenye kiwango ambacho mwanaume na mwanamke wa kwanza waliangukia. Hii ina maana kuwa, mtu lazima ajitahidi kufanya sharti la kuashiria (kiishara) kujikomboa mwenyewe mpaka kwenye kiwango cha utimilifu wa hatua ya kukua. Kwa hiyo mtu huweka msingi wa kumpokea Masihi. Ili kuanza mchakato huu, mtu lazima aenende katika mlolongo wa kujinasua kutoka kwa Shetani. Na kama matokeo ya mchakato huu, mtu wa anguko humpokea Masihi, ambaye huja kama Mzazi wa Kweli, na huwa amezaliwa mara ya pili. Kwa njia ya kuzaliwa upya, mtu anakombolewa kurudi katika nafasi ya Adam au Hawa kabla ya Anguko. Kwa kuwa kiwango ambacho mwanaume na mwanamke wa kwanza waliangukia

ulikuwa ni kiwango cha utimilifu wa hatua ya kukua, vilevile unakuwa ni kiwango wa mtu kuzaliwa upya katika mlolongo wa Ukombozi.

Kwa hiyo, hatua ya ukamilifu hubaki ili ipitiwe. Mtu hukua kupitia hatua hii kwa kumfuata Masihi, na hatimae kufikia nafasi ambapo hukamilisha Dhumuni la Uumbaji. Kwa uasili, jukumu la mtu katika kipindi cha kukua ni kufuata tu *'Njia ya Kanuni'*. Hata hivyo, mtu wa anguko anahitajika kupita milolongo 'miwili'kuelekea ukamilifu – (1) hatua ya kwanza ni *Njia ya Ukombozi*, ambayo yahusu njia ya kufuata mpaka ajapo Masihi na kuzaliwa kwa mhusika mara ya pili kupitia kwa Masihi. (2) mlolongo wa pili ni *Njia Asili ya Kanuni*, ambayo ni njia anayopaswa kuifuata mpaka hatua inayobaki ya kipindi cha kukua, ambacho ni hatua ya ukaimilifu. Mtu wa anguko hutekeleza hili kwa kumfuata Masihi.




Kama Adam na Hawa wangejikamilisha wenyewe, na hivyo wakawa Wazazi wa Kweli na Mababu wa Kweli wa uzawa wa watu, watoto wao wangefuata njia ya kanuni chini ya uongozi wa ulinzi wa wazazi wao. Baada ya kuzaliwa upya kupitia kwa Masihi, njia ya kanuni humtaka mtu kuwa mtiifu kabisa – kwa Masihi na kumtegemea wakati ananakua kuelekea ukamilifu, kwa kuwa anasimama kama Mzazi wa Kweli.

**B : Ukombozi kupitia malipizi.**

Basi ni Njia ipi ya Ukombozi, ambayo ni lazima ifuatwe mpaka Masihi ajapo ? Kwa maneno mengine, ni kanuni zipi za mpango wa  Mungu mpaka atakapomtuma Masihi ? Maswali haya yanaweza kujibiwa kwa kuelewa yaliyomo katika maandalizi ya kumpokea Masihi. Kwa kuwa Masihi anakuja katika nafasi ya Adam (I Wakor 15 :45), hawezi akatokea wakati wowote, anaweza kutokea pale mwanadamu atakapokuwa amekombolewa mpaka kwenye kiwango

cha nafasi ya Adam aliyokuwa amefikia kabla ya anguko, nafasi hiyo ambayo itakuwa ni utimilisho wa hatua ya kukua. Ndiyo kusema, Masihi anaweza kutokea tu pale ambapo kuna msingi unaomwezesha asimame katika nafasi ya Adam asiye na dhambi. Hata hivyo, mtu wa anguko hawezi kufikia hali hiyo yeye kwa njia zake kwa sababu ana Dhambi ya Asili. Kwa hiyo, Mungu anahitaji mtu huyo wa anguko apitie masharti fulani, masharti ambayo yanaweza kumfanya mtu kiishara ahusike kama aliyekombolewa katika kiwango hicho – kwa maneno mengine kwamba mtu huyo amekomboa kiwango cha ukombozi katika hatua ya kukua katika ishara. Kwa hiyo toleo la Mungu kabla ya kuja kwa Masihi linaweza kufafanuliwa kwa kifupi kuwa ni harakati za mtu kukomboa msingi ambao Masihi anaweza kutokea. Matokeo yake, katika njia ya ukombozi, jukumu la mtu ni kukomboa msingi wa kumpokea Masihi.

Je, 'Ukombozi kwa njia ya malipizi' humaanisha nini ? Ili kitu kikombolewe katika nafasi au hali yake iliyokuwa imepotezwa, masharti kadhaa lazima yatekelezwe. Kutekeleza masharti hayo ndiko *kulipia* hasara ya kile cha awali asili na hivyo, *kukomboa kupitia malipizi*.
Mtu alipoteza hali yake ya asili na nafasi kwa sababu ya Anguko. Ili huyo mhusika kukomboa nafasi hiyo asili na hali yake, lazima atimize masharti fulani. Kwa kuwa kutekeleza masharti haya hulipa hasara, kurudia hali ya awali kwa kufanya masharti kunaitwa Ukombozi kwa njia ya malipizi. Masharti ambayo yanahitajika kwa mchakato huu wa ukombozi kupitia malipizi huitwa masharti ya malipizi. toleo la kukomboa tabia ya awali ya mtu wa anguko kwa kutekeleza masharti ya malipizi huitwa toleo la Ukombozi kupitia Malipizi.
Kifuatacho sasa tunataka kujua aina mbalimbali za masharti ya malipizi. Aina ya kwanza ni *'sharti la malipizi la kiwango sawa'*, ni kama tunavyonukuu (Kutoka 21 :23-25). 'Kama kuna madhara yoyote yanayofuatia, hapo mtatoa maisha kwa maisha, jicho kwa jicho, jino kwa jino, mkono kwa mkono, mguu kwa mguu, moto kwa moto, kidonda kwa kidonda, kiboko kwa kiboko'. Hii inamaanisha kuwa hali ya awali inakombolewa kwa kulipa malipizi yenye thamani ambayo ni sawia na hasara au madhara.
Aina ya pili ya sharti la malipizi ni *malipizi katika kiwango cha chini*. Katika hali hii, hali ya asili inakombolewa kwa kulipa malipizi ya thamani ambayo ni ndogo zaidi ya ile iliyopotezwa. Kwa mfano, tunapata manufaa makubwa kwa ufufuko wa Yesu kutoka wafu kwa kutimiza sharti dogo la kuwa na imani ya ukombozi kwa njia ya msalaba. Mifano mingine ya masharti ya malipizi ya kiwango cha chini ni kubatizwa na komunio takatifu. Kwa njia ya kubatiza tunatimiza sharti la kusafishwa dhambi, na katika komunio takatifu tunatimiza sharti la kiwango cha kuwa kitu kimoja katika roho na mwili na Kristo.
Aina ya tatu ya sharti ya malipizi ni *'sharti la malipizi la kiwango kikubwa'*. Pale mtu anaposhindwa kutimiza wajibu wake katika sharti la malipizi katika kiwango kidogo, hapo lazima akomboe hali ya asili kwa kufanya sharti la malipizi la kiwango cha juu. Kwa mfano wakati Waisraeli walipopewa siku arobaini kupeleleza katika Kanaan (wakati wa Musa) walishindwa kupata kibali cha Mungu, muda wa sharti la malipizi uliongezwa mpaka mwaka mmoja kwa kila siku za asili. Badala ya kutaabika siku arobaini katika jangwa, ikawalazimu kutaabika miaka arobaini (Hes 14 :34). Kingine, ni njia gani itumikayo katika kutimiza sharti la malipizi ? Sharti la malipizi ni hali ambayo lazima itimizwe ili

kukomboa kitu fulani kurejea nafasi yake ya asili au hali. Sharti la malipizi hupatikana kwa kuenda kinyume na mchakato uliopelekea kupoteza hali au nafasi ya awali (asili). Kwa sababu mwanaume na mwanamke wa kwanza walishindwa kutimiza wajibu wao na wakaanguka mbali kutoka kwa Mungu, wazawa wao wametakiwa kutimiza masharti ya malipizi yanayo hitajika i katika njia ya Ukombozi.

**C. Msingi kwa ajili ya Masihi .**

Kama ilivyofafanuliwa awali, pamoja na kwamba Mungu hutuma Masihi kutokana na neema zake, ili kumpokea Masihi, mtu lazima akamilishe wajibu wake, kwa kutimiza sharti la malipizi. Ni masharti gani ya malipizi ambayo yanahitajika ili kujenga *Msingi kwa ajili ya Masihi ?* Kwa kuwa masharti ya malipizi lazima yageuze mchakato ambao Adam alipoteza nafasi yake ya asili na hali, ili kujibu swali hili lazima tujuwe mchakato gani aliopitia wakati wa anguko la Adam –




Ni kitu gani alichofanya nai kitu gani iambacho hakufanya kilicho acha Dhumuni la Uumbaji bila kutimizwa.
Kwa kuwa Adam na Hawa hawakuamini neno la Mungu, hawakuweza kujenga '*Msingi wa Imani'* na walianguka. Ili kumpokea Masihi mtu wa anguko lazima kwanza akomboe *Msingi wa Imani* kwa kulipia kushindwa kwake kuamini katika neno la Mungu.
Baada ya kuanzisha Msingi wa Imani, mtu wa anguko lazima, kwa ajili ya malipizi, aweke *'Msingi wa Matendo'*. Hebu tuchunguze sababu ambazo zinaashiria lazima wa kujengwa msingi huu. Kama Adam na Hawa wangejenga Msingi wa Imani, wangekuwa mwili mkamilifu wa Neno la Mungu. Kwa maneno mengine, wangeendeleza tabia za watu wakamilifu. Ukamilifu huu wa mwili ndio dhumuni lengwa la kuumba mtu. Imani katika amri ya Mungu 'usile' ilikuwa lazima kwa Adam na Hawa mpaka pale tu ambapo wangekuwa wamefikia ukamilifu (ukomavu). Matakwa ya Mungu yalikuwa wao wawe watu

waliomwilishwa na tabia zake na kufanana naye.  Wakati hili lilipotokea wangeweza kuwa wenye haki kutawala vitu vyote Ulimwenguni, wakiwemo malaika mkuu. Lakini kwa sababu Adam na Hawa hawakuwekeza maisha yao katika hulka ya imani, walipoteza msingi ambao kwao wangeweza kujimwilisha na tabia ya Mungu na kufanana naye ; na badala  yake wakaja kutawaliwa na Malaika Mkuu, ambaye  alikuwa awe mtumishi wa Mungu na mtu. Hivyo, msingi kwa ajili ya Masihi ambapo mtu wa anguko lazima aujenge huhitaji kuwekwa kupitia njia ya malipizi kwa ajili ya Msingi wa Imani na Msingi wa Matendo.




*1.  Msingi wa Imani*

Kwanza, masharti gani ya malipizi ambayo lazima yatimizwe ili kujenga msingi wa imani ? Ili kuyajua, lazima tujuwe Adam na Hawa walishindwa kufanya nini ? Adam na Hawa walishindwa kuanzisha msingi huu kama matokeo ya wao kutokuwa na imani katika amri ya Mungu wakati wa kukua kwao. Ili kulipa kushindwa huku, , kwanza lazima awepo mtu – kiongozo atakae simama katka nafasi ya Adam na kukomboa msingi wa imani. Pili,kulipia na kukomboa kushindwa kwa Adam na Hawa kutii amri ya Mungu ,kiongozi huyo anatakiwa afanye sadaka inayo takiwa kwa imani yakinifu.Tatu, Adam na Hawa hawakauenenda katika kipindi kizima cha kukua katika msingi wa kusudio la Mungu, hivyo wakashindwa kutimiza sharti linaloonyesha imani. Kwa maneno mengine, hawakuweza kisawasawa kupitia kipindi cha kukua ambamo walikuwa wabebe wajibu wao – kwa kuishi kulingana na kusudio la Mungu.




Matokeo yake, mkakati wa kimahesabu kwa kuangalia muda wa kufanya malipizi kufidia kipindi cha kukua kilichotumika vibaya ukawa wa lazima. Kinaitwa 'kipindi cha hisabati cha malipizi'. Msingi wa imani ni uhusiano wima wa dhati ambao mtu analazimika kuujenga kwake na Mungu. Kwa kuwa uhusiano wima na Mungu ulipotezwa na mwanaume na mwanamke wa kwanza kwa sababu ya kutokuwa na imani kwa Mungu, sharti linalohitajika kulipia na kukomboa hali hii inaitwa msingi wa imani. Sababu ambayo kwamba katika historia, watu mashuhuri wa Mungu kama vile Abeli, Nuhu, Abraham na Isaka walitakiwa waonyeshe imani kubwa kwa sababu wao walikuwa watu binafsi waliokuwa na jukumu la kukomboa kwa njia ya malipizi Msingi wa Imani.

2. *Msingi wa Matendo*

Hebu tufikirie masharti ya malipizi yanayohitajika kuweka Msingi wa Matendo. Kama katika Misingi yao ya Imani, Adam na Hawa wangejikamilisha kama watoto wa kweli wa Mungu, wangekuwa mwili kamili katika Neno la Mungu, na wangekuwa na tabia kamili ya Mungu asiyeonekana. Kama hili lingetokea, mtu angekuwa na milki ya vitu vyote vilivyoumbwa, akiwemo malaika mkuu, mpaka hapo wangekuwa wamehitimisha Baraka ya Tatu ya Mungu. Uhusiano wa Kikanuni ungekuwa umewekwa kati ya watu na vitu vyote ikiwa ni pamoja na malaika. Hata hivyo Adam na Hawa hawakuweka kamwe Msingi wa Imani, na matokeo yake hawakuweka Msingi wa Matendo. Badala yake, Adam na Hawa walinajisiwa na Hulka ya anguko na wakaishia wakiwa wanatawaliwa na malaika mkuu.




Ukamilifu wa tabia ya mtu & Utaratibu
Unaofaa katika Dunia iliyoumbwa

Ili kuweka Msingi wa Matendo, mtu wa anguko lazima atimize *Sharti la Malipizi la Kuondoa chembechembe za nguko* na kukomboa utaratibu wa uhusiano mlalo ambao ulivurugwa. Hili linafanyika kwa kugeuza mchakato ambao mtu alipitia kupata chembe chembe za nguko. Ni kitu gani hasa cha kufanya ili kuondoa chembe chembe za anguko ? Kigezo cha kwanza katika mchakato uli sababisha anguko la Malaika Mkuu ulikuwa katika Malaika Mkuu kushindwa kumpenda Adam, ambaye alikuwa akipokea upendo mwingi kutoka kwa Mungu. Mtu wa anguko alirithi hali hii ya anguko kwa 'kutochukua mtazamo kwa Mungu'. Ili kuondoa chembembe hii ya anguko, mtu katika nafasi ya Malaika Mkuu lazima ampende mtu katika nafasi ya Adam, mpaka hapo atakuwa amechukuwa mtazamo sawa kama wa Mungu.

Kigezo kingine cha pili katika mchakato wa anguko la Malaika Mkuu kilikuwa katika sababu ya kukataa kwake kupokea upendo wa Mungu kupitia kwa Adam ambaye alikuwa karibu na Mungu. Badala yake, Malaika Mkuu alijaribu kuchukua nafasi ya Adam, akaanguka na akachochea mfumuko wa chembe chembe za anguko, mtu kuacha nafasi yake. Ili kuondoa chembe chembe hii ya anguko mtu katika nafasi ya Malaika Mkuu lazima apokee upendo wa Mungu kupitia kwa mtu katika nafasi ya Adam, hivyo kukaa katika nafasi yake sahihi.

Kigezo cha tatu katika mchakato wa anguko kilikuwa katika malaika mkuu kumtawala Adam na Hawa badala ya yeye kuruhusu ili wamtawale. Kutokana na hali hii kukazuka tabia ya anguko ya kugeuza utaratibu wa kutawala. Ili kuondoa chembechembe hii ya anguko, mtu katika nafasi ya malaika mkuu anapaswa kuwa mnyenyekevu na kujisalimisha kwa mtu aliye katika nafasi ya Adam, kwa hiyo kuanziisha utaratibu sahihi wa utawala.




| Chembechembe za anguko | Sharti ya Malipizi |
|---|---|
| 1.kutochukua mtazamo kwa Mungu’ | Upendo |
| 2.Kuacha nafasi yake | Kupokea upendo kupitia |
| 3.kugeuza utaratibu | Kuwa chini ya utawala wa |
| 4.kuzidisha dhambi | Kujifunze njia ya Mungu kutoka |

Utashi wa wema wa kutokula tunda la mti wa mema na maovu uli paswa upokelewe kutoka kwa Mungu na Adam, na kutoka kwa Adam upokelewe na Hawa, na kutoka kwa Hawa upokelewe na Malaika Mkuu, kwa hivyo kuzidisha wema. Hata hivyo badala ya kuzalisha mema, Hawa akakubaliana na Malaika Mkuu kula tunda la mti wa ujuzi wa mema na uovu, na Adam akapokea mwongozo huo kutoka kwa Hawa, kwa hivyo waka zidisha nia kwa ajili ya uovu na kuwa sababisha waanguke. Kwa jinsi hii mtazamo wa mwisho wa chembechembe ya anguko uliumbwa – asili ya kuzidisha dhambi ! ili kuondoa chembechembe hii ya anguko ya kuzidisha dhambi, mtu katika nafasi ya Malaika Mkuu lazima apokee nia njema kutoka kwa mtu aliye katika nafasi ya Adam, kukomboa asili izidishayo nia ya wema.
Pale masharti haya yanapotimizwa, Masharti ya Malipizi ya Kuondoa chembechembe ya nguko yanakuwa yametimizwa, na hili linahusisha pia Msingi wa Matendo. Msingi kwa ajili ya Masihi unafanyika kwa kukomboa kwa njia ya malipizi Msingi wa Imani na Msingi wa Matendo. Ni kwa msingi huu tu kwamba mtu wa anguko anaweza kumpokea Masihi.
Kutokana na yaliyo tangulia, tunaweza kuelewa kuwa historia ya binadamu ni historia ya mpango ambao Mungu humwongoza mtu kujiandaa mwenyewe kumpokea Masihi kwa kumchagiza mtu kutimiza wajibu wake. Pale mtu atimizapo maandalizi haya, Mungu atamtuma Masihi na kuhitimisha mpango kwa ajili ya ukombozi.
Tafsiri hii ya historia kutokana na kanuni ya mpango wa Mungu kwa ajili ya Ukombozi ina iitwa mtazamo wa Ukombozi juu ya Historia au Mtazamo wa historia ya umoja. Na sasa hebu tuchunguze historia ya kiini katika mpango wa Mungu wa Ukombozi.

**D. Historia kuu na zile za pembezoni katika mpango wa Mungu kwa ajili ya Ukombozi.**

Kwa njia ya mpango kwa ajili ya Ukombozi, Mungu hutafuta kuokoa watu wote. Njia zake za kutimiza mpango wake zimetofautiana kutokana na historia mbalimbali, desturi, asili ya kiutamaduni, hali za maisha ya watu ambao aliwashirikisha katika shughuli zake. Hata hivyo,

Mungu anafanya kazi ya mpango wa mfano kupitia nchi moja teule. Hufanya mpango wake katika nchi nyingine kama 'historia za pembezoni', katika hatua fulani historia ya pembezoni hupandikizwa kwenye historia kuu ili watu wote waweze kupokea faida za wokovu.
Kama jinsi inavyoweza kuonekana katika Agano la Kale, Mungu ilimpasa kuenenda katika matatizo mengi katika mchakato wa ukombozi kabla ya kupata taifa moja kuui. Kutokana na yaliyoandikwa kwenye Biblia, inaonekana kuwa pale Mungu alipo anzisha Israel kama taifa teule. Alifanya kazi kupitia taifa hilo tu. Na ni kweli kwamba mafunzo ya waisrael waliyopokea kutoka kwa Mungu yalikuwa makini sana na maalum na kuwa walipokea baraka maalum ambazo haziwezi kupatikana miongoni mwa watu wengine.
Hata hivyo, Yesu hakumtambulisha Mungu kama tu Mungu wa wayahudi, lakini kama Mungu wa mataifa yote. Hili linaonekana katika Yoh. 3 :16, pale Yesu aliposema 'kwa jinsi hii Mungu aliipenda Dunia kwamba ali mtoa mwanae wa pekee, kwamba 'yeyote' amuaminie hato angamia bali awe na uzima wa milele '(ufafanuzi ume ongezwa). Hii ina maana mtu yeyote anaweza kuunganishwa kwenye mpango mkuu wa Mungu- hata wale katika historia za pembezoni.

Tunapoendelea kujifunza Biblia inakuwa wazi kwamba Mungu amelenga katika kuelimisha kiongozi mkuui, familia, kabila, na Taifa ambalo litachukuwa jukumu la mpango mfano,.Vilevile ameongoza bado,pia ameongoza mpango wa pembezoni kuelekea siku ambayo ataunganisha watu hao maalum, familia, makabila, na mataifa kwa Masihi.

Yohana Mbatizaji pia alionyesha kuwa wokovu ulikuwa miongoni mwa wote wakati alipo watia adabu waisrael ambao hawakuwa na imani thabiti na kwa kiburi walijisifu wenyewe kwa kuwa wateule pekee wa Mungu, akiwaambia….., Msije mkadhania,kwa kujisemea wenyewe, tunaye Abraham kama baba yetu, sababu nawaambia Mungu anaweza katika mawe haya akamwinulia watoto Abraham (Math 3 :9)
Mpango mkuu wa Mungu wa maandalizi kwa ajili ya Masihi unaonekana wazi katika agano la Kale. Tangu mwanzo mpango wa Mungu katika familia ya Adam lilivurugwa na Kaini kumuua Abeli. Baada ya vizazi kumi, niya ya Mungu ilii hamishwa katika familia ya Nuhu. Hata hivyo, kwa sababu ya kutoamini na kushindwa mwana wa pili wa Nuhu, Ham, msingi wa familia kwa ajili ya Masihi haukujengwa. Haikuwa mpaka wakati wa familia za Abraham na Yakobo kwamba msingi wa Masihi uli anzishwa (rejea sura ya 11). Kutokana na msingi wa familia ya Yakobo, Mungu aliweza kuunda waisrael kama watu wateule. Mpango wa Mungu kwa ajili ya waisrael ulikuwa ni kutayarisha eneo la imani la Masihi kwa kuwa na wana wa Israel wakiandaa msingi wa taifa kwa ajili ya Masihi. Kama ilivyo fafanuliwa vyema katika kusudi la masihi, Waizrael walishindwa kuanzisha msingi wa Taifa kwa ajili ya masihi. Wakaishia kufanya kosa la kihistoria la kuto muamini Masihi.
Yesu aliahidi Ujio wa Pili. Lazima kuwepo maandalizi Duniani kwa ajili ya Ujio wa Pili sawa na ule uliofanywa kwa ajili ya Ujio wa Kwanza. Miaka elfu mbili ya historia ya Ukristo iliyopita – historia imekuwa na lengo kuu moja – ambalo ni kuweka msingi duniani kote kwa ajili ya ujio wa pili wa Masihi. Kwa hiyo, historia ya Israel kabla ya kuja Yesu na historia ya ukristo baada ya siku zake,ni kiini muuhimu cha historia katika mpango kwa ajili ya Ukombozi.

Kwa kuangalia historia katika njia hii, tunaanza kuelewa maana na umuhimu wa matukio katika historia ya wayahudi kama yalivyonukuliwa katika agano la Kale. Si historia ya nchi moja maalum, lakini ni historia ya mfano ambao Mungu amefanya kazi ya mpango wake kwa ajili ya wokovu. Historia ya wayahudi katika msingi wa Uyahudi , na historia ya magharibi katika msingi wa Ukristo, zote pamoja ni kumbukumbu wazi za mpango wa Mungu, na kwa mshangao, tunaweza kuona kanuni makini ambayo ilitumika katika kipindi chote cha historia hizi mbili.

Kwa kuwa dini huongoza akili na roho ya mtu kuelekea kutimiza ukombozi wa watu katika mtazamo wa mpango, historia ya dini ni historia kuu ya mpango wa Ukombozi wa Mungu. Historia nyingine, kama vile historia za maendeleo ya siasa, uchumi, sayansi na utamaduni zinaweza kuchukuliwa kama historia za pembezoni.




Dhumuni la Mungu la Uumbaji ni kukamilika kwa Baraka tatu. Kwanza kila mmoja lazima ajikamilishe mwenyewe.Inayofuata, aanzishe familia adilifu, na dunia adilifu, na kuishi katika hali adilifu. Matokeo yake jukumu la kwanza katika mpango wa Mungu wa Ukombozi si kukomboa taasisi za jamii, au hali ya maisha, ni kwa ajili ya kukomboa watu. Vilevile, kwa msimamo wa mpango, historia ya kidini ni histori kuu, na Historia nyingine ni za pembezoni (ndogondogo).

**III. NJIA YA MPANGO WA MUNGU KWA AJILI YA UKOMBOZI.**

Hebu tufupishe historia ya mtu kutoka kwa Adam hadi leo katika mwanga wa yale tuliyojadili. Njia yote ya mpango inaweza kugawanywa takriban katika zama tatu katika vifungu vya miaka elfu mbili kila moja (ya zama).

1. Zama kutoka Adam hadi Ibrahim

2. Zama kutoka kwa Ibrahim hadi Yesu

3. Zama za Yesu hadi ujio wa pili

Kipindi baada ya ujio wa pili ni zama mpya ambamo uadilifu wa Mungu unakamilishwa katika mapana yake duniani na katika dunia ya roho. Sasa hebu tuangalie yaliyomo katik mpango kwa ajili ya kila zama kutoka misimamo mbalimbali. Awali ya yote, zama hizi zinaweza kuchunguzwa kutegemea uelekeo wa neno la Mungu la Uumbaji Upya.

Sehemu I :

1. Wakati wa zama kutoka Adam hadi Abraham haikuwezekana bado kwa mtu kupokea neno la Mungu, ambamo mpango kwa ajili ya Ukombozi unafanyika. Kwa njia ya matoleo ya sadaka ambayo Mungu ali elekeza mtu afanye, mtu alikuwa anajenga msingi wa kupokea neno la Mungu. Hivyo kipindi hiki kinaitwa zama za mpango wa Msingi kwa ajili ya neno.

2. Zama kutoka kwa Abraham hadi kwa Yesu zinaitwa zama za agano la Kale na hatua ya kuanza katika historia ya ukombozi.

3. Zama kutoka Yesu hadi ujio wa pili zinaitwa zama za agano Jipya na hatua ya kipindi cha kukua katika historia ya ukombozi.

4. Muda baada ya Ujio wa Pili unaitwa zama za agano Kamilifu na hatua kamilifu katika historia ya ukombozi.




Sehemu II :

Pili, zama hizi zinaweza kugawanywa katika msimamo wa mpango kwa ajili ya ufufuo. Kama ilivyofafanuliwa katika 'Ufufuo' mpango wa kihistoria unaweza kugawanywa kama ifuatavyo :-

1. Zama kutoka wakati wa Adam mpaka Abraham ni zama za mpago wa msingi wa ufufuo.

2. Zama kutoka wakati wa Abraham mpaka kwa Yesu ni zama za mpango wa hatua ya mwanzo wa ufufuo.

3. Zama kutokea kwa Yesu hadi Ujio wa Pili ni zama za mpango wa hatua ya kukua ya ufufuo

4. Muda baada ya Ujio wa Pili unaitwa zama za mpango kwa ajili ya hatua ya utimilifu wa ufufuo




Sehemu III :

Tatu, zama za imani zinaweza kugawanywa kutokana na msimamo wa ukombozi kupitia malipizi kama ifuatavyo :

1. kipindi cha miaka elfu mbili kutoka kwa Adam hadi Abraham kilishambuliwa na shetani, lakini kika kamilishwa na ushindi wa familia ya Abraham. Kipindi hiki kilijenga msingi kuanza kipindi cha ukombozi kupitia malipizi ya kile kilichopotelea kwa shetani. Kwa hiyo kipindi hiki kinaitwa zama za mpango wa msingi kwa ya ukombozi kupitia malipizi.

2. Zama toka Abraham hadi Yesu ni zama za mpango wa ukombozi kupitia malipizi.

3. Zama kutoka kwa Yesu hadi ujio wa pili ilitokea kwa sababu mpango ambao ilibidi likamilishwe wakati wa ujio wa kwanza lilirefushwa mpaka ujio wa pili kwa sababu ya kukosa imani kwa wateule. Kipindi hiki kinaitwa zama za mpango wa kurefushwa ukombozi kupitia malipizi.

4. Muda baada ya ujio wa pili ni zama za mpango kwa ajili ya ukamilifu wa ukombozi.



Adam Miaka 2000

Nne, zama hizi zinaweza kugawanywa kutokana na msimamo wa kiwango cha msingi kwa ajili ya Masihi:-

1. Katika zama toka Adam hadi Abraham mpango wa Mungu kuandaa msingi kwa ajili ya Masihi uliwekwa katika msingi wa familia. Kwa hiyo kipindi hiki kinaitwa zama za mpango wa msingi wa familia kwa ajili ya Masihi.

2. Zama toka Abraham hadi Yesu zinaitwa zama za mpango wa msingi wa taifa kwa ajili ya Masihi

3. Zama toka Yesu hadi ujio wa pili, ni zama za mpango wa msingi wa Dunia nzima kwa ajili ya Masihi.

4. Muda kuanzia mwanzo wa ujio wa pili ni zama za mpango kwa ajili ya Ulimwengu (Dunia ya kimwili na Dunia ya kiroho) msingi kwa ajili ya Masihi.




Hatimaye, zama zinaweza gawanywa kufuatana na utambuzi wa nyakati katika mpango kama ifuatavyo:-

1. Wakati wa zama toka Adam hadi Abraham, mtu ali anzisha imani yake mbele za Mungu kupitia matoleo – ishara, na hivyo kipindi hiki kinaitwa zama za utambuzi wa nyakati katika ishara.

2. Katika zama toka Abraham hadi Yesu, mtu alionyesha imani yake kwa Mungu kwa kutoa vitu sadaka katika hali ya taswira – hii ni, kwa kutoa vitu sadaka kama kisanduku (maskani) na hekalu, ambavyo vilionyesha taswira ya mtu wa kweli, ambaye alipotezwa wakati wa anguko. Hivyo, kipindi hiki kinaitwa zama za utambuzi wa nyakati katika taswira (mfano).

3. Toka wakati wa Yesu hadi ujio wa pili, mtu alionyesha imani yake kupitia Yesu, hekalu halisi. Kipindi hiki kinaitwa zama za utambuzi wa nyakati katika mwili (matendo).


B.U.P. Miaka 2000
Yesu Miaka 2000 utambuzi wa nyakati halisi (matendo
Ibrahim Miaka 2000 utambuzi wa nyakati katika taswira (mfano).
utambuzi wa nyakati katika ishara
Adam Miaka 2000

## Chapter 9 ADAM'S FAMILY IN THE DISPENSATION FOR RESTORATION

## SURA YA 9FAMILIA YA ADAM KATIKA MPANGO WA MUNGU WA UKOMBOZI

Mpango wa Mungu wa kukomboa na kuokoa mtu kwa kumtuma Masihi ulikuwepo tangu muda anguko lilipotokea. Hivyo toleo lake la kuanzisha Msingi kwa ajili ya Masihi ulianza katika familia ya Adam.

### I. MSINGI WA IMANI.

Kwa kuwa alikuwa ni Adam ambaye hasa alitenda Dhambi ya Asili, na si Kaini au Abeli, Adam angekuwa mtu wa kuwajibika kukomboa Msingi wa Imani kwa kufanya Sadaka Inayohitajika kwa Mungu. Kuhitimishwa au kutokuhitimishwa kwa Msingi wa Imani kungeamuliwa kufuatia iwapo Adam angefanya matoleo ya sadaka yake inayostahili.

### A. Utenganisho kwa ajili ya Sadaka

Hata hivyo katika Biblia hakuna kumbukumbu za Adam kutoa sadaka. Sadaka zilitolewa na Kaini na Abeli. Kwa nini ?

Kufuatana na 'Kanuni ya Uumbaji' mtu aliumbwa ahusiane na Bwana mmoja. Hivyo, Mungu hawezi kufanya kazi ya toleo la kanuni pamoja na mtu aliye na uhusiano na Bwana wawili. Kama ilivyofafanuliwa mapema, katika sura yenye somo 'Mwandani Mwa Kanuni za Toleo la Ukombozi', pamoja na kwamba Adam aliumbwa na Mungu, alitokea baadae kuwa na ubini wa shetani, na hivyo alikuwa katikati, alikuwa na mahusiano pande mbili, kwa Mungu na kwa Shetani.

Kwa kuwa Adam alikuwa mwilisho wa pande mbili za wema na uovu, kama Mungu angejaribu kufanya naye kazi, Adam na sadaka yake, Shetani naye angejaribu kufanya naye kazi na sadaka yake kwa misingi ya kuwa Adam ni wa ubini wake. Kama hili lingetokea, Adam angekuwa katika nafasi ya kufanya kazi na mabwana wawili, na hivyo katika nafasi isiyo ya Kanuni. Hivyo Mungu asingeweka toleo lake kupitia Adam.




Mungu hakuwa na namna nyingine isipokuwa kutenganisha katika vitu viwili vya hulka mbili zinazokinzana  za wema na uovu ambazo zilimwilishwa ndani ya Adam. Mpaka hapo, Mungu alipata mmoja wa wana wa Adam akiwakilisha wema na mwingine uovu*.  Na hapo Mungu aliwaweka katika nafasi ambapo mmoja alifanya kazi na Mungu na mwingine na shetani. Kwa maneno mengine, Mung aliwataka wote sadaka wakiwa katika nafasi zao lakini ambapo kila mmoja alifanya kazi na bwana mmoja.




**B. Mwana wa pili katika toleo la Mungu**

Wote Kaini na Abeli walikuwa wana (wabini) wa Adam. Na ni yupi kati ya hao wawili atakuwa mwakilishi wa mema na hivyo kuhusiana na Mungu na yupi atawakilisha uovu, na hivyo kuhusiana kishughuli na shetani ? Wote Kaini na Abeli walikuwa matokeo ya anguko la Hawa, na swali la nani atawakilisha upande upi uliamuliwa katika msingi wa mchakato wa anguko la Hawa, ambaye aliwajibika kwa anguko.
Hawa alihusika katika namna mbili za vitendo vya mapenzi ya anguko (uasherati). Tendo la kwanza lilikuwa uhusiano wake na malaika mkuu, uliosababisha anguko la kiroho, la pili ni uhusiano wake na Adam, uliosababisha anguko la kimwili.
Matukio haya mawili ya anguko yalikuwa makosa, lakini kama tukifikiri lipi lilikuwa 'karibu sana' na kanuni na hivyo kusamehewa kirahisi katika macho ya Mungu, tungesema ni tukio la pili la anguko ndilo lililokuwa rahisi zaidi kusamehewa, tukio la kwanza la anguko lilichangiwa na tamaa iliyozidi ya Hawa ya kufurahia kitu ambacho hakustahili kuwa nacho kwa wakati huo, ni kwamba lilichangiwa na tamaa yake ya kufunguliwa macho na kuwa kama Mungu (Mwan 3 :7) – kabla ya kukomaa. Pia, katika tendo la kwanza la anguko

uhusiano wa Hawa ulikuwa na malaika mkuu, ambaye kufuatana na kanuni, kamwe hakukusudiwa kuwa mume wa Hawa. Kwa upande mwingine, tendo la pili la anguko lilichangiwa na tamaa ya Hawa kumrudia Mungu baada ya kung'amua uharamu wa asili ya tendo lake

______________________________________________

**Ingawa Abeli na Kaini walisimama kila mmoja pande zote mbili za wema na uovu, nafasi zao zilikuwa za mda tu. Kwa kweli wote walikuwa na Dhambi ya Asili na Hulka Anguko – na kwa hiyo wote walikuwa na hulka za uovu na wema.*

la kwanza. Pamoja na hayo, hata kama tendo lilifanywa katika muda punde tu kabla ya muda




aliokuwa ameupanga Mungu, ulikuwa ni uhusiano kati ya Adam ambaye kufuatana na mpango wa Mungu, ndiye hatimae angepaswa kuwa mchumba wake.

Kwa kuwa Kaini na Abeli walikuwa ni matokeo ya upendo mwovu wa Hawa, Mungu aliwaweka katika nafasi zilizowakilisha uovu na wema katika msingi wa matendo mawili ya ngono. Kaini kama tokeo la kwanza la anguko, aliwakilisha tendo la kwanza la kuanguka kwa Hawa, uhusiano pamoja na malaika mkuu, na hivyo aliwekwa katika nafasi ya kuhusiana na Shetani. Abeli aliashiria tendo la pili, ambalo lilikuwa kati ya Hawa na Adam, na hivyo aliwekwa katika nafasi ya kuhusiana na Mungu. Shetani alipata nguvu ya kudhibiti viumbe vya Mungu kabla ya Mungu hajatawala, na kwa kuwa Shetani ni kiumbe kinyume na Kanuni, alipelekea kuwepo Kanuni – bandia ya dunia kabla Mungu hajadhihirisha dunia ya Kanuni. Kwa hiyo, Mungu alianza toleo lake kwa kuweka mwana wa kwanza ambaye aliashiria tendo la kwanza, katika upande wa shetani na mwana wa pili ambaye aliashiria tendo la anguko, kwenye upande wake. Mungu alimwambia Kaini 'kwa nini una hasira', na kwa nini unaghafirika ? Kama ulifanya vizuri, je hautakubaliwa ? na kama hufanyi vizuri dhambi inabisha mlangoni ; tamaa yake yakutafuta wewe, lakini yakubidi kuidhibiti' (Mwanzo 4 :6-7). Hii inaonyesha kuwa Kainialikuwa katika nafasi ya kushughulika na Shetani. Pale waisrael walipokimbilia Misri, Mungu alishambulia vifungua mimba wote wa Misri, na pia ng'ombe zao (Kutoka 12 :29). Tena, Biblia inasema kuwa Mungu 'alimpenda' mwana wa pili, Yakobo, na 'alimchukia' mwana wa kwanza Esau, wakiwa tumboni mwa mama yao (War 9 :13). Na katika suala la Yakobo kwa wana wajukuu zake Efraimu na Manase, Yakobo aliwabariki kwa kukatiza mikono yake ili mkono wa kulia uwekwe kwenye kichwa cha Efraimu mwana wa pili (Mwan 48 :14). Katika kila tukio la jinsi hii ni mfano wa jinsi Mungu alivyomweka mwana –mzawa wa pili katika nafasi ya kupendelewa.

Katika msingi wa kanuni hii, Mungu alimweka Kaini na Abeli katika nafasi ambazo kila mmoja alikuwa ashughulike na bwana mmoja, na baadae akawaacha kila mmoja atoe sadaka. Mungu alikubali sadaka ya

Abeli (Mwan 4 :4) kwa sababu alikuwa katika nafasi ya kumwakilisha Mungu na alifanya sadaka katika hali inayokubalika (Waheb 11 :4). Kwa njia ya sadaka inayokubaliwa, msingi wa imani ulijengwa katika familia ya Adam na mwana wa pili, Abeli, akiwa katika nafasi ya Adam. Mungu hakukataa sadaka ya Kaini kwa sababu alimchukia Kaini, na wala halikuwa lengo la Mungu kumlaani milele. Hata hivyo kwa kuwa Kaini alikuwa katika nafasi ya kufanya kazi na shetani tu, Mungu hakuweza kufanya kazi naye isipokuwa tu akamilishapo sharti la malipizi ambalo lingemwondoa yeye mwenyewe kutoka kwenye nafasi ya kuhusiana na shetani. Sharti la malipizi ambalo lilikuwa litimizwe na Kaini linaitwa ‘sharti la malipizi la kuondoa Hulka Anguko’.

**II. MSINGI WA MATENDO.**

Ili familia ya Adam iweke Msingi wa Matendo Kaini ilimbidi atimize sharti la malipizi la kuondoa Hulka – Anguko. Kama angefanya hivyo, Mungu angeweza kukubali sadaka yake (Kaini) kwa furaha.

Kwa kuwa Kaini alikuwa katika upande wa Shetani, asingekuwa mtendewa wa Mungu, ambaye ni mtenda wa wema. Kwa njia ya Kaini kutimiza sharti lililotakiwa ili kuondoa Hulka – Anguko, angerudi katika nafasi ambayo Mungu angeshughulika naye. Je, sharti hili la malipizi la kuondoa Hulka – Anguko lingefanyika vipi ?

Mwanaume na mwanamke wa kwanza walirithi hulka anguko kwa njia ya mahusiano yao na malaika mkuu. Sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko lazima lianzishwe kwa ishara ya kugeuza mchakato (hatua) wa anguko.

Malaika mkuu, aliyeumbwa katika nafasi ya mbali zaidi toka kwa Mungu kuliko Adam, ilimbidi ampende Adam sawa kama Mungu alivyofanya, kwa jinsi hiyo angekuwa na mtazamo sawa kama wa Mungu. Ilimbidi ahusiane na Mungu na Adam akiwa muunganishaji wake, na ingembidi ajikamilishe yeye mwenyewe kwa kufuatia njia ya

kimbingu ya kujinyenyekeza mbele za Adam na kumtii.  Lakini malaika mkuu hakufanya hivyo. Sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko linatimizwa kwa kufanya kinyume chake.

Baada ya Abeli kutoa sadaka yake, Kaini aliwekwa katika nafasi ya malaika mkuu, na Abeli katika ile ya Adam. Kutokana na nafasi hizi sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko lingeweza kutimizwa kwa Kaini kumpenda Abeli, kwa kumtii Abeli, na kujinyenyekeza mbele yake Abeli. Kufanya hivyo, kungemleta karibu na Mungu. Lakini, badala yake Kaini alimuua Abeli, alirudia mchakato kama ule wa anguko la malaika mkuu. Hili halikuwa kosa tu la kaka mkubwa kumuua mdogo wake, ilimaanisha upande wa shetani ulishambulia upande wa Mungu, harakati za Mungu kutenganisha wema dhidi ya uovu katika familia ya Adam zilivurugwa, na upande wa wema ulipotezwa.




Lile ambalo Kaini alitakiwa kutimiza lilikuwa sharti la msingi la malipizi ambalo linahitajika  kwa kila mtu aliye mbali kutoka mahali alipo Mungu kuja karibu sana naye.  Ndani ya kila mtu akili iliyoelekezwa kwenye wema (War 7 :22) imo katika nafasi ya Abeli.  Na mwili ambao huelekeza kutumikia ‘sheria ya dhambi’ (War 7 :25) umo katika nafasi ya Kaini. Ni pale tu mwili utakapojisalimisha chini ya uongozi wa akili na kuitii ndipo watu, kila mmoja ataweza kuwa mwema. Hata hivyo, katika maisha ya mtu wa anguko, mwili mara kwa mara huasi dhidi ya mwongozo wa akili, ukifanya kama alivyofanya Kaini kwa kumuua Abeli, kwa jinsi hii, kulea uovu ndani ya kila mtu.




Sisi kama watu wa anguko, tupo katika nafasi ya Kaini – kwa Masihi. Kwa hiyo, kwa kujinyenyekeza sisi wenywe mbele zake, na kumtumikia, kumtii na kumpenda, tunapata wokovu kupitia uunganishaji wake (Yoh 14 :6, I Tim 2 :5). Kama Yeremia 17 :9 anavyotuambia, mtu alikuwa 'mdanganyifu juu ya vitu vyote….' Kwa hiyo, ili kuja kwa Mungu mtu alikuwa aenende kupitia vitu vya uumbaji, ambavyo vilikuwa katika nafasi ya Abeli kwake. Hii ni kanuni aliyoweka Mungu kufuatia ukweli huo mtu kutumia sadaka katika Toleo.

Kama ilivyofafanuliwa awali msingi ambao Masihi anaweza kuja ni Msingi wa Imani na Msingi wa Matendo uliokombolewa. Katika familia ya Adam Msingi wa Imani ulifanikiwa kujengwa na Abeli kwa kutoa sadaka ambayo Mungu aliikubali. Kwa njia hii Abeli alijithamanisha yeye mwenyewe kuwa kiongozi kwa ajili ya Msingi wa Matendo. Hata hivyo, kwa kuwa Kaini alimuua Abeli, Sharti la Malipizi la kuondoa Hulka Anguko halikuanzishwa. Hivyo, Msingi wa Matendo na kama

matokeo yake, Msingi wa Masihi, havikuwekwa, na Toleo la Mungu halikutimizwa katika familia ya Adam.

### III. MSINGI KWA AJILI YA MASIHI

Kama Kaini angetimiza sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko kwa kujinyenyekeza mbele za Abeli na kumtii, msingi wa matendo ungekuwa umejengwa katika familia ya Adam. Msingi huu pamoja na msingi wa imani, ingeweka msingi kwa ajili ya Masihi. Kwa maneno mengine kwa Abeli kutimiza sharti la malipizi ili kukomboa uhusiano wa wima na Mungu, angeweza kusimama katika msingi wa imani. Kama Kaini angerudisha utaratibu wa kawaida katika uhusiano wa mlalo na Abeli, msingi wa matendo ungekuwa umejengwa. Misingi hii yote miwili ingejumuisha msingi kwa ajili ya Masihi.

Katika msingi huu, Masihi angeweza kuja. Katika hatua hiyo ya historia ya binadamu, toleo la Mungu lilikuwa katika kiwango cha upeo wa familia, hivyo, iwapo Abeli na Kaini wangeanzisha mssingi kwa ajili ya Masihi, ingekuwa katika kiwango cha upeo wa familia. Kama familia ya Adam ingefanya msingi wa aina hiyo, wangempokea Masihi na wangezaliwa upya kupitia kwake. Katika njia hii, wangekuwa




wamekombolewa na kuwa familia adilifu ambayo Mungu awali alikuwa ameikusudia, na historia mpya kabisa ingekuwa imeanza.

Badala yake, Kaini akamuua Abeli, na toleo la Mungu kwa ajili ya familia ya Adam halikutimizwa. Hata hivyo, nia ya Mungu kumwokoa binadamu haibadiliki na ni yakinifu ; hivyo, hata kama Mungu hawezi kuendeleza kazi yake kupitia mtu ambaye hawezi kutimiza wajibu wake, humchagua mwingine miongoni mwa wazawa wa huyo anayemuacha kuendeleza Nia yake.

## CHAPTER TEN NOAH'S FAMILY IN THE DISPENSATION FOR RESTAURATION

## SURA YA 10 FAMILIA YA NUHU KATIKA MPANGO WA MUNGU LA UKOMBOZI

Mpango wa Mungu la Ukombozi chini ya uongozo la familia ya Adam aukutimizwe kwa sababu Kaini alimuuwa Abeli. Walakini, Nia ya Mungu la kukamilisha Kusudi la Uumbaji ilipangwa kama isio badilika ; kwa hivio, kwa msingi wa roho na uaminifu wa Abeli kwa Mbingu, Mungu "akmkabithi" Seti kuchukua nafai zake (Mw 4:25). Basi, kwa baina ukoo wake Seti, Mungu humchaguwa Nuhu na familia yake kusimama kwa nafasi za Adam na familia zake, na Mungu huanza Toleo lake la Ukombozi chini ya uongozo wa familia ya Nuhu.

Mw 6:13 inasema kwamba "...Mungu akamwambia Nuhu, Mwisho wa kila mwenye mwili umekuja mbele zangu ; kwa sababu wameijaza dunia dhuluma, basi nitawaharibu pamoja na dunia." Hii inaonyesha wazi wazi kuwa Mungu alikusudia kuzileta Siku za Mwisho wakati ule. Kwa njia ya familia ya Nuhu kuwa msingi, Mungu alikusudia kutimiza Dhumuni la Uumbaji kwa kumtuma Masihi baada ya Hukulu kwa Mafuriku. Kwa sababu hii, Toleo la Mungu la Ukombozi katika familia ya Nuhu ilikuwa toleo la kuqeka sawa Msingi kwa ajili ya Masihi.

### I. MSINGI WA IMANI

#### A. Mtu Kiongozi mwenye Kuiitwa juu ya Kukomba Msingi wa Imani

Katika mango chini ya uongozi ya familia ya Nuhu, Nuhu ndie alikuwa mtu kiongozi alie teuliwa juu ya kukombowa Msingi ya Imani. Mungu akamupata vizazi kumi na miaka elfu moja mia sita bada ya Adam. Mungu akamubariki sawz vile alimubariki Adam mapema, akimuongoza Nuhu kuwa "....Nanyi zaeni, mkaongezeke ... (Mw 9:7). Mbele za Mungu, Nuhu alikuwa mtu wa haki (Mw 6:9), ambaye basi aliehitimu kuwa mtu kiongozi kwa ajili ya Msingi wa Imani.




**B. Sadaka iliyotakiwa juu ya kuikomboa Msingi wa Imani**

Sadaka ambaye Nuhu alipashwa kufanya juu ya kukomboa Msingi wa Imani ilikuwa safina. Maana ya hii safinambele zake Mungu kwa mtazamo wa mpango wa Mungu kwa ukombozi ilikuwa nini ? Nuhu alichaguliwa na Mungu juu ya kukomboa kiishara ulimwengu, ambaye ulikabidhiwa mikononi mwa Shetani kwa njia ya anguko la Adam. Tokeo lake, ilimbidi Nuhu kufanya sadaka ambaye ingeweza kuonyesha kiishara ulimwengu mpya, na kuweza kukubaliwa na Mungu. Safina ilikuwa sadaka kama hiyo. Mungu kisha towa uongozo wake, Nuhu kapitisha miaka mia moja na ishirini katika ujenzi wa safina, akiwa anavumilia aina yote ya kudharauliwa toka kwa watu na dunia waovu kwa sababu ya utiifu kamili wake kwa Mungu.

Ma daraja tatu za safina zilionyesha ulimwengu ambaye uliumbiwa kwa hatua tatu za ukuaji. Wanamemba wanane wa familia ya Nuhu ambaye waliingia ndani ya safina walitakiwa kuikombowa na kuilipiya malipizi kushindwa kwa manamemba wanane wa familia ya Adam. Kwa vile safina iliakilisha ulimwengu wote, Nuhu, kama mkuu wa safina, alimwakilisha Mungu ; wanamemba wa familia zake waliakilisha wanadamu wote; na mnyama ndani ya safina waliakilisha vyumbe vingine vyote ndani ya ulimwengu. Mara tu safina

ilipojengwa, Mungu alihukumu wanadamu na kuharibu uovu kwa njia ya mafuriko ya siku arobaini. Kulingana na “Kanuni za Uumbaji“, mwanadamu aliumbwa ili amtumikie bwana mmoja; kwa hivyo Mungu hawezi kuwasiliana na mtu wa anguko kama bwana na kiwango cha pili, ye ule ambaye anakuwa na Shetani kuwa bwana wake. Ingekuwa hivi, taratibu za toleo zingekuwa inje ya Kanuni. Kwa hivyo, kwa ajli ya ili apate kusimamisha mtendewa mmoja juu toleo lake, ambaye kwa njia yake angeweza kutumika, Mungu alileta hukumu kwa mafuriko juu ya kuharibuwote na vyote zilizobaki chini ya utawala wa Shetani.

Kwatika njia ya Toleo la Ukombozi, maana ya mafuriko ya siku arobaini ilikuwa nini ? Nia ya Uumbaji ya Mungu inakamilishwa juu ya Msingi wa Nafasi Nne. Walakini, Msingi wa nafasi Nne huu ulipotezwa kwa Shetani ; hivyo Mungu alitumika Toleo ake la kukomboa Msingi wa nafasi Nne. Kwa vile nambari *kumi* ni nambari za kurudi katika umoja, ina maanisha kurudi kwa Mungu. Basi, kwa kutumika juu ya kukomboa Msingi wa Nafasi Nne katika kila kizazi ndani ya vizazi kumi toka Adam hadi Nuhu, Mungu aliweza kutimiza sharti la kukomboa Msingi wa Nafasi Nne ngambo zake. Basi, wakati toka Adam hadi Nuhu inaweza kuonekana kuwa wakati wa malipizi juu ya kukomboa Msingi wa Nafasi nne kwa Mungu. Hivyo, nambari arobaini (nafasi 4 x vizazi 10) alikuja kuakilisha kurudi kwa Msingi wa Nafasi Nne kwa Mungu.



Kwa sababu ya tamaa na uasi za watu wa wakati za Nuhu, kipindi cha vizazi kumi za malipizi, ambaye ilikusudia kukomboa Msingi wa Nafasi Nne, ilivamiwa na Shetani. Tokeo lake, kwa msingi wa Safina la Nuhu, Mungu aliiweka kipindi cha mafuriko ya siku arobaini ikuwe wakati wa sharti la malipizi la juu ya kukomboa kipindi cha wakati kutoka Adam hadi Nuhu, ile ilivamiwa. Ni kwa msingi huu ndio nambari 'arobaini' ilihitajiwa katika ma juhudi za siku zitakazo fuata juu yakujitenga na Shetani juu ya

| **Vipindi za nambari 40 za kutengana na Shetani** | |
|---|---|
| Nuhu | Siku 40 za Mafuriko |
| Abraham | Miaka 400 baada ya Nuhu |
| WaIsraeli | Miaka 400 katika Misri<br>Miaka 40 Jangwani |
| Musa | Ma Siku 40 za mafungo |

| **Vipindi za nambari 40 za kutengana na Shetani** | |
|---|---|
| Sauli,<br>Dawidi<br>Solomoni | Miaka 40 ya Ufalme ya kila mmoja |
| Elia | Siku 40 za mafungo |
| Yonah | Siku 40 za Utabiri kuhusu Ninive |
| Yesu | Siku 40 za mafungo<br>Kipindi cha Siku 40 kilifwata Ufufuo |

kukomboa Msingi wa Imani kwa njia ya malipizi.  Katika Biblia, tukonaona  vipindi vingi za sharti za malipizi hizo kwa ajili za kujitenga na Shetani : kipindi cha miaka mia nne toka Nuhu hadi Abraham ; kipindi cha miaka mia nne cha waisraeli kuteswa utumwa katika Misri ; kipindi cha miaka arubaini cha waisraeli kuangamia katika jangwa ; vipindi  viwili vya siku arubaini za Musa kufunga mafungo, na kuomba uongozo wa Mungu.kipindi cha siku arubaini za upelelezi katika Kanani ; vipindi tatu za utawala wa waflme tatu Sauli, Dawidi na Solomoni ; siku arubaini za mafungo za Eliya ; Utabiri wa Yona wa Kwamba Niniva itateketezwabaada ya siku arubaini ; siku arubaini za mafungo na maombi ya Yesu ; na kipindi cha siku arubaini za Yesu baada ya kufufuka kwake.

Kwa kujenga safina kulingana na maagizo ya Mungu na kutii Nia ya Mungu katika imani wakati wote wa mafuriko Nuhu aliitimiza sharti la malipizi na kuikomboa Msingi wa Imani.

## II.  MSINGI  WA  MATENDO

Ilibidi sasa familia ya Nuhu ichukuwe hali wima ya imani ambayo Nuhu aliweka mbele za Mungu na kuitimiza kimlalo katika mauhusiano baina yao, juu ya kitimiza kwa njia hiyo sharti la malipizi la kuweza kujenga Msingi wa Matendo.  Sharti hili la malipizi juu ya kuondoa Tabia Mbaya ya Anguko ilipashwa itimizwe kwa mtoto mwana ume wa pili wa Nuhu, Hamu, na mkubwa wake , Semu.

Katika familia ya Adam, nafai ya Adam, mtoto mwana ume wake wa pili, Abeli, alitoa sadaka ambaye ilikubaliwa na Mungu, kwa hivyo hujenga uhusiano wima na Mungu, ambaye ni Msingi wa Imani.  Kwa hivyo, Abeli kwa kawaida alihitimu kuwa kiongozi kwa Msingi wa Matendo.

Katika familia ya Nuhu, walakini, Nuhu ndie mwenyewe alitimiza sharti la malipizi juu ya kujenga Msingi wa Imani. Kwa hiyo, nafasi ya mtoto wake muana ume wa pili, Hamu, ilikuwa bado kufikia nafasi ya Abelibaada ya sadaka yake. Kwa maneno mengine, Hamu alikuwa bado kujenga uhusiano wima wa imani na ibada kamilifu na kubwa na Mungu. Kwa ajili ya Hamu kuwa nafasi ya mtu kiongozi kwa kujenga Msingi wa Matendo, kia kwanza, ilimbidi kurithi Msingi wa Imani na utiifu wa Nuhu. Kwa sababu hiyo ilikuwa na maana kwa Hamu kujenga uhusiano wa roho usiovunjika na




Nuhu, ambaye kwa ushindi alijenga Msingi wa Imani. Kwa maneno mengine, ilimbidi Hamu kuunga, na katika umoja wa roho na Nuhu, akimtii na kuona nia yake kuwa ya maana na umuhimu sawa uzima yenyewe.

Biblia huesabu ma sharti ambaye Mungu aliweka juu ya kuongoza toleo lake la kuunganisha katika kimoja Nuhu na Hamu (Mw 9:20-25). Lakini, wakati Hamu alimuona Nuhu analala uchi katika hema yake,aliisikiya haya na hakufurahishwa, na akaamsha haya ile ile ndani ya wa ndugu zake, Shemu na Japhet. Wakirejesha wazo la baba yao kuwa uchi, Shemu na Japheti walitembeya kinyumenyume na kumfinika na vazi. Hii ilikuwa uhalifu kubwa mno kiasi kia Nuhu

alimlaini Hamu, akisema, "…'Alainiwe Kanaan; mtumwa wa watumwa wa kaka zake' " (Mw 9:25).

Kwa kutazama mwenendo wa kawaida wa Nuhu, Ucha Mungu wake kubwa, pamoja na hesabu za imani kamilifu zake, haitakubaliwa kwamba alihusika na ulevi hama kujinyesha kusiofaa ambaye humletea jukumu. Ni kawaida kuwaza kama kulala uchi kwa Nuhu ulikuwa kwa kiasi yasiofaa, walakini laana ilimwangukiya sio Nuhu ni Hamu, ambaye aliiwaza tendo la Nuhulilikua la aibu sana na akachochea Shemu na Japhet kuamua kumfinika Nuhu. Sababu inahusiana moja kwa moja na toleo la Mungu.

Kwa sababu gani Hamu alilainiwa ? Swali hili laniwaza kujibiwa kwa kuelewa sababu gani tendo la Hamu lilikuwa zinifu. Tendo linakuwa zinifu pale tu inamkabithi Shetani sharti, au msingi, ya kuvamia, ikiunda mtendewa ambaye Shetani atatenda kazi kwa njia yake. Uwezo wa Shetani kutenda inategemea Tendo la Kutoa na Kupokea na mtendewa kama huu. Shetani hana peke yake na nguvu ya kutenda isipokuwa apate mtendewa ule ambaye huna husika naye katika Tendo la Kutoa na Kupokea.

Basi ni nini Hamu aliifanya ya kuweza kumkabithi Shetani sharti la kuvamia ? Mara tu baada ya Anguko, Adam na Hawa walizifinika sehemu zao za uzazi, wakionyesha kuingia kwao katika uhusiano wa damu na Shetani. Mukuona uchi wa baba yake, Hamu naye akasikia aibu vile vile na akamfinika. Kwa mtazamo wa kazi za toleo, ukweli kwamba Hamu alijiskia aibu kwa uchi wa baba yake na kuongoza ma kaka zake kumfinika ilikuwa uandikishaji wa uhusiano wake wa damu na Shetani, sawa na kile kifanyajo familia ya Adam. Shetani ambaye alikuwa alitengwa kwa njia ya Hukumu la Mafuriko, alirudishwa ndani kwa tendo la Hamu, na Hamu alijikutwa katika hali ya kusimama na nafasi ya kuwa katika umoja naye. Kwa hivyo akalainiwa.

Kwani ni dhambi kuangalia mwili uchi wa mtu kwa kujisikia aibu ? Hapana. Lakini, familia ya Nuhu iliteuliwa na Mungu juu isimame katika nafasi ya familia ya Adam, na kwa hivyo ilikuwa na utumishi wa kuondoa ma sharti zote ambazo kwa njia yazo Shetani alikubaliwa kuvamia watu wote – sharti ambazo familia ya Nuhu iliwekwa katika nafasi ya kuondoa. Ilikuwa kwa kulinganishwa na toleo la Mungu ndio Nuhu mtu wa haki aliruhusiwa kulevika na kulala uchi katika hema zake. Mungu alimwezesha kufanya hivi ili kwa kuonyesha imani, Hamu angeweza kuingia katika umoja wa roho na Nuhu, ule ambaye aliweka tayari Msingi wa Imani. Kila chochote Nuhu alifanya , ilikuwa katika kulingana na toleo la Mungu.

Ingawa kwa mtazamo wa nje kosa la Hamu ilikuwa tu ya kuonesha haya na kukosa furaha juu ya kuona mwili uchi wa baba yake, kwa mtazamo wa toleo la Ukombozi alilainiwa kwa kosa la kujenga msingi wa ushawishi wa Shetani, ambaye alikuwa alisha tengwa kwa njia ya Hukumu la Mafuriko. Kwa hivyo, Hamu hakuweza kusimama kuwa mtoto muana ume wa pili mshindaji na kuwa kiongozi katika Msingi wa Matendo. Basi hakupatikane hesabu katika Biblia, ya sehemu Hamu na Shemu wakitumika pamoja kutimiza ma sharti za kuondoa Hali za Anguko au kujenga Msingi wa Matendo.

Mungu hakuweza kuingilia katika sharti la mailipizi ambaye hamu alipasha kutimiza, juu ni uajibu wa Hamu. Kwa hivyo, Mungu hakumufundisha Hamu moja kwa moja kumtii baba yake na kuungana na kuwa moja na ye bila shaka katika hali zote.




Kwa uzoefu wa Hamu kwa mafuriko na Nuhu kujenga safina, ingeweza kuwa wazi ya baba yake alikuwa muntu mmoja mwakilishi wa Nia ya Mungu. Na kwa hivyo, baada ya mafuriko, ilikuwa jukumu la Hamu kudumisha imani kamilifu kwa Nuhu na kumtii katika hali zote.

## CHAPTER 11   ABRAHAM'S FAMILY IN THE DISPENSATION FOR RESTAURATION

## SURA YA 11   FAMILIA YA ABRAHAM KATIKA MPANGO WA MUNGU LA UKOMBOZI

Matokeo ya kukosa imani kwa Ham, mpango wa Mungu la ukombozi haukutimizwa katika familia ya Nuhu. Hata hivyo, Mungu amejidhatiti kuyakinisha kusudio lake kutimiza Dhumuni la Uumbaji. Kwenye msingi wa uaminifu na moyo wa dhati wa Nuhu, Mungu alimwita Abraham kuendeleza toleo lake. Hivyo, Abraham ilimbidi ajenge msingi kwa ajili ya Masihi, ambao familia ya Nuhu ilishindwa.




## I.  MSINGI WA IMANI .

**A : Mtu kiongozi kwa ajili ya kukomboa msingi wa imani.**

Katika toleo la ukombozi ulioegemea familia ya Abraham mtu kiongozi kwa ajili ya kukomboa msingi wa imani alikuwa Abraham. Baada ya kipindi cha miaka mia nne na vizazi kumi kutoka wakati wa Nuhu, Mungu alimchagua Abraham kuchukua nafasi ya Nuhu. Abraham alikuwa mwana wa Terah, mwabudu sanamu, na hivyo alipendwa na shetani. Mungu alimchukua Abraham kama malipizi ya kumkomboa Ham aliyechukuliwa na shetani, mwana wa pili, ambaye amekuwa katika nafasi ya kupendwa na Mungu. Kwa kuwa Abraham alichukuwa nafasi ya Nuhu, na hivyo nafasi ya Adam, Mungu pia alimbariki Abraham, na kusema kuwa Abraham 'atabarikiwa' na kuwa atafanya uzao wa Abraham kuwa taifa kubwa (Mwa 12 :2). 'na alimtoa nje na kusema 'tazama kuelekea mbinguni na hesabu nyota, kama unaweza kuzihesabu ….'Mimi ni Bwana ambaye alikuleta kutoka nchi ya wakaldayo, ili nikupe ardhi ya kumiliki' (Mwa 15 :5-7). Hii ilikuwa ahadi ya Mungu ya kumbariki Abraham.

**B : Sadaka iliyohitajika kukomboa msingi wa imani.**

*1. Sadaka ya ishara*

Wakati huo Abraham aliuliza ni masharti gani ambayo yangemfanya apate baraka ya Mungu '….Ee Bwana nitajuaje kuwa nitakuwa nayo?' (Mwa 15:8). Hizi aina tatu za matoleo ni sadaka zilizohitajika kukomboa msingi wa imani. Zilionyesha (ishara ) aina zote vitu katika mbingu, ambavyo hujikamilisha vyenyewe kupitia hatua tatu za kukua. Kwa maneno mengine, Mungu alimtaka Abraham atoe sadaka ya ng'ombe (mtamba), kondoo na mbuzi jike, njiwa na ndege mwana kama ishara za

mbinguni kote, ambazo zilipotezwa kwa sababu ya anguko. Hivyo, sadaka hii inaitwa 'sadaka ya ishara'. Kwa kuongezea, sadaka hizi tatu (altareni) madhabahuni zilidhamiriwa kuwakilisha na kukomboa kimlalo masharti yalioingiliwa ya vizazi vitatu vya taleo wima – lile la Adam, Nuhu na Abraham.

Je, Abraham alifanyaje ishara hii muhimu ya sadaka? Tunasoma katika Mwanzo. 15:10-13 Abraham alikata sadaka katika vipande viwili na kulaza nusu moja dhidi ya nyingine, isipokuwa ndege, ambao hakuwakata vipande viwili. Ndege wawindaji (kunguru) walishuka kwenye mizoga, na Abraham aliwafukuza. Jioni ile jua linapozama Mungu alimtokea Abraham na kusema ………..'tambua kwa hakika wazawa wako watakuwa watumwa katika nchi ambayo si yao, na watakuwa watumwa huko, na




watakandamizwa kwa miaka mia nne…….' (Mwa. 15:13). Ndege wawindaji (kunguru) walishuka juu ya mizoga sababu Abraham hakuwakata katika vipande viwili. Hili lilisababisha kwa waisraeli

kuteseka kwa miaka mia nne. Hebu tuchunguze maana ya ndege wawindaji wakitua juu ya sadaka.

Tangu anguko la mwanaume na mwanamke wa kwanza, kila mara Mungu afanyapo kusudio lake, shetani husogea kuziba njia ya Mungu. Wakati Kaini na Abeli wakitoa sadaka, shetani alikuwa 'akibisha mlangoni' (Mwa. 4:7) wakati wa Nuhu ndege mwarabu aliashiria shetani, ambaye alikuwa anatafuta wasaa wa kuingilia familia ya Nuhu mara tu baada ya hukumu ya mafuriko, (Mwa. 8:7). Vilevile wakati wa sadaka ya ishara ya Abraham, ukweli kwamba shetani alishambulia sadaka (matokeo yake masharti yaliyofanywa) kwa ishara inanukuliwa katika Biblia kwa ndege wawindaji wakishuka kwenye sadaka. Halafu ipi ilikuwa dhambi ya Abraham? Ilikuwa ni kushindwa kwake kugawanya ndege mwana na njiwa. Kwa nini sadaka zilikuwa zigawanywe ? Kama matokeo ya anguko, mtu na dunia yake walitokea kumiilishwa (ghubikwa) na vyote, wema na uovu. Dhumuni la toleo la wokovu ni kukamilisha dhumuni la uumbaji. Mungu amefanya kazi kukamilisha dhumuni la uumbaji kwa kutenganisha wema na uovu ndani ya wote binadamu na dunia yake na baadae kuharibu uovu na kupanua wema. Ili Mungu aweze kuhusiana na kitu lazima kwanza kitenganishwe kiishara kutoka kwa shetani. Hivyo, sadaka zilipaswa kugawanywa.

Ilikuwa baada ya mtu mmoja Adam kugawanyika sehemu mbili katika hali ya wanae, Kaini na Abeli, kwamba sadaka ya kafara iliweza ku[illegible]yika. Waka[illegible]a Nuhu, dhumuni la Mungu kutenganisha mabaya






na baadae kuharibu uovu kwa njia ya mafuriko ilikuwa ni kukomboa utawala (himaya) ya wema. Mungu alitazamia toka kwa Abraham kulipa malipizi juu ya kushindwa kwa Adam na Nuhu kwa kutenganisha kiishara wema na uovu kwa kumtaka Abraham akate sadaka katika mafungu mawili.






Umuhimu zaidi wa kutenganisha sadaka ulikuwa kwamba ungeanzisha sharti ambalo lingepelekea utenganishi kiishara wa dunia njema kiutawala na ile ambayo ipo chini ya utawala wa shetani. Pia kutenganisha sadaka na kutiririsha damu hujenga utakaso kwa kuondoa kiishara 'damu ya kifo', ambayo ilirithiwa kwa njia ya uhusiano wa damu na Shetani.

**Umuhimu halisi wa kutenganisha wa mnyama katika vipande viwili**

1. **Mgawanyiko wa Kaini na Abeli**
2. **Kutenganisha wema na uovu kwa njia ya Garika**
3. **Kutenganisha Utawala wa Mungu na huyu wa Shetani**
4. **Kuapishwa kwa kuondoa « damu za ushetani »**

Kwa kutokata sadaka katika pande mbili ilikuwa ni sawa na kutotenga Kaini na Abeli, bila kumuacha mtendewa ambaye angekuwa katika

nafasi ya Abeli ili kuwasiliana na Mungu. Pili, kiliwakilisha (kushindwa) kutotenga wema na uovu baada ya hukumu ya gharika wakati wa Nuhu, matokeo yake yalikuwa kutokuwepo mtendewa wa wema ambaye kupitia kwake Mungu angeweza kuendeleza toleo lake.  La tatu, kunawakilisha (kushindwa) kutimiza matakwa ya Mungu ya kuzitenga (kiishara)dunia ya utawala wema toka dunia iliyomilikiwa na shetani. Kushindwa kutenga dunia ambamo Mungu anaweza kuwa na mamlaka. Mwishoe, kwa kuwa kutogawanywa kwa sadaka kulimaanisha kutoondoa 'damu ya kifo', kuwa sadaka hazikutakaswa na kwa hiyo kwamba Mungu hakuweza kujihusisha na sadaka. Matokeo yake, ingawa kwa nje Abraham alitoa sadaka kwa Mungu, katika mtazamo wa maana ya toleo haikuwa sadaka iliyogawanywa na kwa hiyo haikuwa sadaka inayokubalika kwa Mungu.  Kwa sababu Abraham alitoa vitu ambavyo havikugawanywa, sadaka yake ilikuwa ni sawa na kutoa sadaka kwa shetani, na hivyo ikawa dhambi.

Nini yalikuwa matokeo ya makosa yake katika sadaka – ishara? Baada ya Abraham kushindwa katika sadaka, Mungu alimwambia, 'tambua kwa uhakika kwamba wazao wako watakuwa wahamiaji katika nchi ambayo si yao', na watakuwa watumwa huko na watanyanyaswa kwa miaka mia nne……….(Mwa. 15:13). Hii ilikuwa adhabu kali, kama hii ilikuwa adhabu ya makosa ya Abraham, kwa nini iliwaangukia wazawa wake na siyo Abraham mwenyewe? Na kwa nini ilikuwa kwa miaka mia nne?

Kwa kuwa  Abraham alishindwa katika sadaka ya ishara, kipindi cha miaka mia nne ya malipizi ambayo yalikuwa ya lazima kumpata Abraham kama mtu kiongozi yaliingiliwa na shetani. Kwa hiyo, katika mtazamo wa Mungu, akifanya ili kurejesha miaka mia nne iliyopotea ingehitaji kipindi cha miaka mingine mia nne ya kujitenga kutoka kwa shetani. Miaka hii isingetimizwa katika kizazi cha Abraham peke yake.

Kwa sababu hiyo wazawa wake iliwabidi kukomboa kipindi kilichopotezwa cha malipizi. Hili lilifanyika katika kipindi cha kunyanyaswa Waisrael miaka mia nne nchini Misri. Hivyo, kipindi cha mateso kilikuwa ni kipindi cha namna mbili, kipindi cha adhabu kwa kosa la Abraham katika kutoa sadaka na kipindi cha kuweka msingi wa kutenganisha kutoka kwa shetani kwa ajili ya mpango mpiya.

Kama Abraham angetoa aina tatu za sadaka iliyohitajika kulingana na matakwa ya Mungu, kwa maneno mengine, kama sadaka – ishara zingekubaliwa hapo msingi wa imani ungekuwa umekombolewa. Na hapo kazi ya kuanzisha msingi wa matendo ungefanyika katika familia ya Abraham kwa kuegemea kwa wanae. Hii ingehusisha sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko kati ya Isaka, mwanae wa pili, na Ishmaili, mwanae wa kwanza. Hakuna lisemwalo juu ya hili katika Biblia sababu Abraham alishindwa katika sadaka yake, ambayo ingekomboa msingi wa imani.




*2. Sadaka ya Abraham ya kumtoa Isaka .*

Baada ya kushindwa Abraham katika sadaka - ishara, Mungu alimwamuru kumtoa Isaka kama sadaka ya kuteketeza (Mwa. 22:2) na hivyo kuanza toleo jipya. Mwanzo 22:9-10, anasema 'walipofika mahala ambapo Mungu alimwambia, Abraham alijenga madhabahu pale na akalaza kuni kama alivyoagizwa na akamfunga mikono Isaka mwanaye, na akamlza juu ya madhabahu katika kuni. Ndipo Abraham akanyoosha mkono wake, na kutwaa kisu ili amchinje mwanaye. Akiwa na imani ya dhati, Abraham alijitosa katika sadaka ya kumteketeza mwanaye, Isaka ambaye alimpokea kama baraka. Wakati huu, 'Malaika wa Bwana' alimwamrisha, usiweke mkono wako kwa kijana au kufanya lolote kwake, kwa kuwa sasa ninajua kuwa unamwogopa Mungu, kwa kuona kuwa hukumng'ang'ania mwanao wa pekee, kutoka kwangu (Mwa. 22:12).

Katika macho ya Mungu, kumtoa kafara Isaka kulikuwa na maana kubwa zaidi ya kujaribu imani ya Abraham.Mpango wa Mungu wa kukomboa msingi wa imani ulikuwa umesonga mbele kupitia hatua tatu katika familia ya Adam, Nuhu, na Abraham. Pamoja na kwamba Abraham alishindwa katika sadaka ishara, lilikuwa kusudio la Mungu kwamba msingi wa imani ukombolewe wakati wa Abraham sababu ilikuwa ni jaribio la tatu. Kwa njia ya kumtoa Isaka, Mungu alifungua toleo jipya, katika upeo mpya. Kwa Abraham aliye thamanisha kwa dhati baraka ya Mungu, kuua kwa mikono yake na kumtolea Mungu mwanae ambaye Mungu alimpa kama baraka iliumiza roho yake zaidi ya yeye mwenyewe kujitoa muhanga kikafara. Abraham aliweza kufanya hii kafara ngumu katika tabia inayokubalika (Mwa. 22:12) kwa sababu ya imani yake yakinifu, utii, na kumcha Mungu.

Wakati Mungu alipomwamuru kumtoa Isaka, hali ilikuwa kiasi kwamba uumbaji wote, Isaka akiwemo, ulikuwa katika makucha ya shetani

kutokana na kushindwa kwa Abraham kutoa sadaka – ishara. Ili kumtenganisha Isaka kutoka kwa shetani. Mungu alimuomba Abraham kumtoa Isaka kama kafara. Mpaka ile hatua ambayo Abraham alikuwa tayari kumtoa sadaka, imani yakinifu na utii ndani ya moyo wa Abraham haikuacha nafasi ya shutuma toka kwa shetani kwa namna yoyote. Hivyo shetani alilazimika kumwacha Isaka. Akiwa ametenganishwa kutoka kwa shetani, Isaka alisimama katika nafasi ya mbingu, na Mungu alimwamuru Abraham asimuue Isaka. Mungu kwa wakati huo akawa amemkomboa Isaka, aliyekuwa amepotezwa. Pale Mungu anaposema 'sasa najua' katika (Mwa. 22:12), tunaweza kuelewa kuwa alikuwa anaelezea hali ya ??????? ya kushindwa kwa Abraham katika kutoa sadaka ya ishara na raha vilevile kwa Abraham katika kufanikiwa kumtoa sadaka Isaka. Abraham alifanikiwa pamoja na ukweli kuwa ilikuwa vigumu sana kwake zaidi ya kutoa uhai wake kama kafara ya kuteketezwa.




Kwa kumtoa Isaka, Abraham kiishara alijiua yeye mwenyewe kwa sababu ya kushindwa kwake na aliwezesha Isaka kumweka kama Abraham mfufuka. Kupitia sadaka hii Abraham alitimiza sharti la malipizi la kumruhusu Isaka kuchukua nafasi yake kama mtu kiongozi kwa ajili ya msingi wa imani. Pamoja na kuwa Abraham mfufuka na Isaka walikuwa watu wawili tofauti, kitoleo waliwakilisha mtu mmoja mfufuka.

Matokeo yake, sadaka ya Isaka, iliashiria kuhama kutoka kwa Abraham kwenda kwa Isaka kama mtu kiongozi katika toleo la ukombozi chini ya familia ya Abraham.

**II : MSINGI IMANI ULIOEGEMEA KWA ISAKA.**

**A:Mtu kiongozi kwa ajili ya kukomboa msingi wa imani.**

Isaka aliyemwakilisha Abraham mfufuka, alikuwa mtu kiongozi mpya. Alifufuliwa kutoka kwenye ukiongo wa kuelekea kufa. Onyesho la imani ya Abraham kwa Mungu lilitukuzwa sana. Lakini Isaka, yeye mwenyewe naye pia alionyesha imani isiyotikisika, pale alipokuwa na moyo wa utii, alikubali hatima ya kuteketezwa kama sadaka.  Haiko wazi kuelewa Isaka alikuwa na umri wa miaka mingapi wakati huo wa sadaka, lakini kwamba alibeba kuni za kutumika wakati wa sadaka na kumuuliza baba yake yuko wapi kondoo kwa ajili ya sadaka. (Mwa. 22: 6 – 7), inaelekea kuwa Isaka alikuwa amekua kiasi cha kuelewa nia ya Abraham kwa kiasi fulani.  Kama Isaka angemgomea baba yake kwa kile ambacho kilionekana si cha busara katika mpango wa kumuua kwa ajili ya sadaka za kuteketeza, Mungu asingeweza kukubali sadaka. Kwa namna hii tunaweza kujifunza kuwa Isaka alikuwa mtu kiongozi ambaye utiifu wake haukuwa mdogo ukilinganisha na ucha Mungu wa Abraham.

**B. Sadaka iliyohitajika kwa ajili ya kukomboa msingi wa imani .**

Sadaka iliyohitajika katika kukomboa msingi wa imani ilikamilishwa na kondoo aliyetolewa sadaka na Abraham na Isaka, ‘na Abraham aliinua macho yake na akaangalia tazama, nyuma yake alikuwepo kondoo, na Abraham alikwenda na kumchukua kondoo na kumtoa sadaka ya kuteketezwa badala ya mwanae’ (Mwa. 22 : 13).
Katika nafasi ya Isaka, Abraham alitoa sadaka ya kondoo iliyotayarishwa

na Mungu. Ni rahisi kupata taswira ya Isaka, akiwa ameghubikwa na hisia za raha na shukrani kwa kuwa aliokoka katika kifo, kwa hiari kwa kushirikiana na Abraham katika kutoa sadaka ya kondoo kama sadaka ya kuteketezwa. Hii ilikuwa ni sadaka ya ishara iliyokomboa msingi wa imani ulioegemea kwa Isaka. Pamoja na kwamba Abraham alitoa sadaka ya kondoo, kutokana na msimamo wa toleo, Isaka alikuwa mmoja na Abraham na alirithi jukumu lake (utume) hivyo, alikuwa ni Isaka aliyekomboa msingi wa imani, kupitia malipizi kwa kufanikiwa kutekeleza sadaka ishara, katika nafasi ya baba yake.

**III: MSINGI WA MATENDO.**

Katika msimamo wa msingi wa imani ambao Isaka aliujenga, msingi wa matendo ulikuwa ufanyike wakati huo ili kukamilisha msingi wa Masihi. Kwa sababu hii, wana wawili wa Isaka Esau na Yakobo, iliwabidi watimize sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko. Kama tukichunguza nini kimetajwa katika biblia katika msingi wa matukio ya nje shughuli za familia ya Yakobo zinaleta maswali mengi. Kwa nini mapacha Esau na Yakobo, walipigana hata wakiwa ndani ya tumbo la mama yao? (Mwa. 25:22-23). Kwa nini Mungu alimpenda mwana wa pili Yakobo, wakati akiwa tumboni mwa mama yake? (War. 9:13). Kwa nini Yakobo alizaliwa akiwa mkono mmoja uking’ang’ania kisigino cha Esau? (Mwa. 25:26). Kwa nini Yakobo alimtaka Esau aape katika kuuza haki yake kwa kuzaliwa mwana wa kwanza kwa kubadilishana naye michuzi kadha wa kadha? (Mwa. 25:32-34). Kwa nini Yakobo kwa ujanja alimdanganya baba yake kipofu na kuchukua baraka ya Esau (Mwa. 27:1-36)? Kwa nini Mungu kwa wingi alimpenda, kumlinda na kumbariki Yakobo katika maisha yake yote, bila ya kujali ukweli kwamba alifanya mambo mengi ambayo yanazua maswali mengi? Na katika ukweli wa mambo haya, kwa nini Mungu alimfanya yeye mzizi wa taifa teule?

Kumbukumbu ya mitafaruku kati ya Esau na Yakobo hata wakiwa tumbini mwa mama yao inatuambia kuwa mahusiano yao hayakuwa ya kawaida kati ya ndugu hao wawili. Kutokana na mtazamo wa toleo la Mungu, Esau na Yakobo walirudia toleo lake la kumtenganisha Kaini na Abeli, akiwa na Yakobo na Esau waliwakilisha mema na uovu katika mpangilio huo. Mungu 'alimpenda' Yakobo na 'alimchukia' Esau (War. 9:11-13). Hata walipokuwa tumboni mwa mama yao kwa sababu mmoja aliwakilisha mema na mwingine uovu.




Yakobo alikuwa awe mtu kiongozi wa Msingi wa Matendo. Awali ya yote, alikuwa afanye sharti la malipizi ya kukomboa nafasi ya Abeli. Yakobo alitimiza sharti hili kwa kukomboa haki ya mwana wa kwanza wa familia. Kwa maneno mengine, kwa kuwa Shetani alidanganya na kuchukua viumbe vyote vya uumbaji vya Mungu kupitia nafasi ya mzawa wa kwanza, Yakobo ilimbidi atimize masharti fulani ambayo yangemkomboa mzawa wa kwanza kurudi upande wa Mungu.

Yakobo vilevile ilimbidi atimize masharti ambayo yangekomboa haki ya uzawa wa kwanza kwenye kiwango cha upeo wa mtu binafsi. Kwa busara na ujanja. Yakobo alichukua haki ya uzawa kutoka kwa kaka

yake, Esau, kwa kuinunua kwa mkate na kibakuli cha mboga za majani (Mwa. 25:33-34). Mungu alimbariki Yakobo kwa sababu Yakobo aligundua haki ya uzawa ilikuwa na thamani kubwa na alijitahidi kuikomboa. Hii ndiyo sababu pia iliyomfanya Mungu amruhusu Isaka atoe baraka yake kwa Yakobo. (Mwa. 27:27). Kwa upande mwingine, Mungu hakumbariki Esau kwa sababu Esau hakuweka maanani thamani ya baraka na aliuza kwa bei ya kibakuli cha mboga.

Pili, kwa kupitia kipindi cha miaka ishirini na moja cha mateso huko Haran, kipindi ambacho kiliashiria dunia ya Shetani, Yakobo alikamilisha masharti ya kukomboa familia kutoka dunia ya Shetani kwenda upande wa Mungu.

Jambo la tatu, kupitia miaka ishirini na moja nchini Haran ni ushindi wake katika mieleka na Malaika, Yakobo pia alitimiza masharti ya kukomboa umiliki wa vitu vyote (vikiwakilishwa na vitu na utajiri alioupata kutoka kwa Laban). Wakati Yakobo akirudi kutoka Haran kwenda nchi ya ahadi ya Kanaan, alipigana mieleka na kumshinda Malaika kwenye jabali la Jabbok. Kwa kufanya hivyo, Yakobo alikomboa utawala wa binadamu juu ya Malaika.

**Kukomboa haki ya uzawa wa kwanza**

1. **Mtu binafsi :** Yakobo ananunua haki ya uzawa wa kwanza kwa mkate na kibakuli cha mboga za majani

2 **Familia :** Yakobo anakomboa familia ku Haran

3. **Utawala juu ya Vitu vyote :** kukomboa umiliki wa vitu vyote, na kupigana mieleka na kumshinda Malaika.

Kwa kukomboa utawala juu yake binafsi, juu ya familia, juu ya uumbaji na hasa juu ya Malaika, Yakobo alitimiza masharti ambayo Mungu angemkubali. Lakini kwa namna nyingine Yakobo alitimiza masharti ya lazima ya kurithi msingi wima wa imani ambao Isaka aliuweka na kwa kufanya hivyo, alikomboa kupitia malipizi nafasi ya Abeli na akawa mtu kiongozi wa msingi wa matendo. Kwa jinsi hii, Esau na Yakobo waliziweka nafasi za Kaini na Abeli kama zilivyokuwepo wakati Mungu alipokubali sadaka ya Abeli.




Ili kutimiza sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko, Esau, aliyekuwa katika nafasi ya Kaini, awali ya yote ilimbidi ampende Yakobo, ambaye alikuwa katika nafasi ya Abeli. Pili, Esau ilimbidi amkubali Yakobo kama mpatanishi wake. Tatu, Esau ilimlazimu amtii na kumnyenyekea Yakobo na kuwa chini ya milki ya Yakobo. La nne, Esau alilazimika kuwa katika nafasi ya kupanua (kuzidisha) wema, kwa kurithi wema kutoka kwa Yakobo, ambaye alipokea baraka kutoka kwa Mungu.

**Msingi wa Matendo**

Mungu
↑
Malaika Mkuu → Adam

Esau Yakobo

| Hulka Anguko | Sharti ya Malipizi |
|---|---|
| **1.** Kutokua msimamo moja na Mungu | Kupenda Yakobo |
| **2.** Kuacha nafasi zake | Kupokea upendo wa Mungu kupitia Yakobo |
| **3.** Kupindua uongozi | Kutii, Kunyenyekea na kuwa chini ya Yakobo na |
| **4**. Kuongeza dhambi | Kupanua wema, kurithi wema kutoka kwa Yakobo |

Juhudi za Yakobo kumshawishi Esau amkaribishe nyumbani na kumnyenyekea kwa hiari yake yalikuwa ya kusisimua moyo. Hata wakati Yakobo anarudi kutoka Haran kuelekea Kanaan, Esau bado alikuwa na kinyongo dhidi ya Yakobo sababu awali Yakobo alichukua baraka yake. Hivyo, Esau aliongoza jeshi la askari mia nne na kwenda kukutana na Yakobo. Pale Yakobo alipopata habari hizo aliomba kwa Mungu na kufanya yale aliyoweza. Yakobo alifikiri ‘..........naweza kumbembeleza kwa zawadi itakayotangulia, na baadaye nitaiona sura yake, labda atanipokea’ (Mwa. 32:20).Bila kusitasita alitanguliza zawadi kwa Esau zaidi ya mifugo mia tano ambazo alipata kama tuzo la ufanyaji kazi kwa bidii huko Haran. Vilevile Yakobo alibuni namna nyingine, kwa kugawa watu na mifugo katika makundi mawili, kwamba moja litakimbia iwapo Esau atashambulia jingine (Mwa. 32:7-8). Pale alipokuwa anakaribia kukutana na Esau kwa makusudi alimweka mke wake mpendwa na

mtoto nyuma kabisa ili kujiweka tayari kabisa kutoroka kama ingebidi (Mwa. 32:2). Yeye mwenyewe alitangulia mbele akisujudu mara saba, mpaka alipomkaribia kaka yake (Mwa. 33:3). Kwa kiasi kikubwa alijinyenyekeza, alimwambia Esau '......kwa kweli kuona sura yako ni sawa na kuona sura ya Mungu, kwa upendeleo huo umenipokea' (Mwa. 33:10). Yakobo alijitahidi kutimiza kusudio la Mungu na kubadilisha roho ya Esau kutoka chuki kubwa mpaka upendo ule wa kukumbatiana naye kwa upendo. Esau alishangazwa na juhudi hizo na utii kwa upande wa Yakobo na alimkaribisha. (Mwa. 33:4) anaendelea kusema, '............Esau alimkimbilia kukutana naye, na akamkumbatia, na kuanguka kwenye shingo yake na kumbusu na wote wakalia' kwa kuwa Esau alimpenda Yakobo na kumkaribisha mbali ya kwamba alichukua haki yake ya uzawa wa kwanza kutoka kwa Esau, sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko lilitimizwa.

**A: Kiini cha wateule .**

Ushindi wa Yakobo haukuwa tu ushindi wa mtu binafsi. Alikuwa ni mtu wa kwanza wa anguko aliyeshinda ushindi wa upande wa Mungu. Kwa kumzukia Malaika wakati akitoka Haran kwenda Kanaan, Yakobo alitimiza sharti la malipizi la kuondoa utawala wa mtu juu ya Malaika. Kwa sababu hii aliitwa Israel na aliteuliwa kama msingi kuwapata watu wateule (Mwa. 35:10-11). Katika Kutoka 3:6 Mungu alisema '........mimi ni Mungu wa baba yako, Mungu wa Abraham, Mungu wa Isaka na Mungu wa Yakobo'. Hii ina maana kuwa kusudio la Mungu kwa Abraham lilitimizwa kupitia kwa Isaka na Yakobo na kuwa, kutokana na msimamo wa mpango wa Mungu, vizazi hivi vitatu vinafikiriwa kama kizazi kimoja. Yakobo alifanikisha tabia ya unyenyekevu wa hiari wa

Esau ili Esau akamilishe sharti la malipizi la kuondoa hulka anguko. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwamba upande wa Mungu (Abeli) ulilazimisha upande wa Shetani  (Kaini) kukubali kushindwa.

Yakobo → « Israel »

(Mw 32 : 28)

(Mw 35 : 10 – 11)




Kwa njia hii, Mungu alimweka mtu mmoja mshindi na familia ya ushindi – mtu mmoja binafsi na familia ambayo imetimiza masharti ya malipizi kumtiisha shetani. Na halafu kutoka hatua hii ya mwanzo, Nuhu alilea na kuendeleza watu wateule. Katika mtazamo wa ufahamu huu, Waisrael kuwa wateule wa Mungu ni matokeo ya ushindi wa mtu mmoja Yakobo wa kutiisha upande wa Shetani.

Mlolongo wa njia ya Yakobo ulifanikisha mpangilio wa kumshinda Shetani, na mfumo huu ulikuwa ufuatwe na kila mmoja ajaye baada yake. Musa na manabii wote walilazimika kufuata mlolongo wa mfano huo, na Waisrael wote iliwapasa kufuata njia hiyo. Historia ya Waisrael inatoa taarifa za hakika ambazo zinaonyesha mlolongo wa mfano wa kumshinda shetani katika kiwango cha taifa. Hivyo, historia ya Waisrael mpaka wakati wa ujio wa Yesu ni historia kiongozi ya toleo la ukombozi. Hii ndiyo sababu biblia huelezea historia ya Waisrael kwa mapana yake, ingawa kwa sasa inaweza kuonekana haina la kutufaa zama hizi.

Na sasa, hebu tutafakari maana ya aya katika Warumi 9:13 ambapo tunasoma kuwa Mungu 'alimchukia' Esau hata alipokuwa tumboni. Aya hii humaanisha kuwa Mungu alikuwa akifanya kazi kutimiza toleo la ukombozi kwa ajili ya malipizi kulingana na kanuni za toleo la ukombozi kwa kumuweka Esau katika nafasi ya Kaini. Baada ya Esau kutimilisha wajibu wake kwa kumpokea na kumpenda Yakobo, angekuwa katika nafasi ya Kaini aliyekombolewa na hatimaye angepokea upendo na baraka ya Mungu (Mwa. 36:7).

**B. Msingi wa Masihi.**

Baada ya mlolongo wa ucheleweshaji uliosababishwa na kushindwa kwa watu viongozi katika toleo la ukombozi, msingi wa Masihi ulitafutwa tangu wakati wa Adamu hatimaye kwa mara ya kwanza uliwekwa katika familia ya Isaka. Lakini, kwa sababu Abraham alishindwa katika kutoa sadaka – ishara, wazawa wake walikuwa bado waenende kipindi cha malipizi cha miaka mia nne ya ukandamizwaji. Hivyo, pamoja na kwamba wazawa wa Isaka waliweka msingi wa Masihi, wangeweza kumpokea tu mara baada ya kupitia kipindi hiki cha malipizi. Ndiyo, ilikuwa haiwezekani kwamba familia ya Isakaiwe na watu walewale kwa

miaka mia nne. Wakati wa kipindi hiki familia yake ilikua na kupanuka katika makabila na taifa. Baada ya kipindi chao cha kuteseka wazawa wote wale katika familia walioweka msingi wa Masihi sasa walilazimika kuujenga katika upeo wa taifa.

Kwa hiyo, Msingi kwa ajili ya Masihi uliojengwa katika familia ya Isaka ukawa ndiyo msingi wa kuanzisha mlolongo wa njia ya malipizi ambayo yangepelekea kujenga msingi wa kitaifa kwa ajili ya Masihi. Kwa kujirudia, ushindi binafsi wa Yakobo ulipelekea kujengwa kwa familia ambayo Mungu angeweza kujihusisha nayo. Halafu chini ya familia hii, katika zama zijazo, Mungu akaanza toleo lake la kujenga msingi wa kitaifa kwa ajili ya Masihi. Kiroho (kindani) Mungu Alipanua msingi wa kifamilia kwa ajili ya Masihi kwa kufikia kiwango cha upeo wa kitaifa. Kimwili (kinje), hata hivyo, wazawa wa Isaka bado iliwalazimu kuenenda katika kipindi cha mateso kwa muda wa miaka mia nne kama malipizi kwa ajili ya kushindwa kwa Abraham.



Kwa hivyo, watoto kumi na wawili wa Yakobo na ndugu wa familia yake sabini walikwenda Misri, ambayo iliwakilisha upande wa shetani duniani, na walibaki pale kwa muda wote wa miaka mia nne ya mateso. Kwa kuwatenganisha mbali na shetani kwa mara ingine tena, ambaye awali alikuwa amewavamia, matukio haya yangewalea watu wateule kufikia hatua ambayo Mungu angeshughulika nao kwa upendo. Mungu halafu alipanga kuwaleta watu wateule kurudi Kanaan, ili kuanzisha msingi wa kitaifa kwa ajili ya Masihi. Katika msingi huo, Masihi angeweza kuja na kukamilisha toleo la Mpango wa Ukombozi.

Mungu aliwapenda na kuwalinda Waisrael na aliwatuma manabii wengi kwao ili kuandaa msingi kwa ajili ya Masihi. Baada ya Waisrael kushinda kiishara na Shetani kusalimu amri , Mungu angemtuma Masihi, ambaye ni tunda la mpango wa Mungu na ambaye ni hekalu la kweli. Mfano uliowekwa na Yakobo, katika nafasi ya Abeli, katika kuletwa kutii kwa Esau (katika nafasi ya Kaini) ulipaswa kuzaa matunda katika mahusiano ya mwisho kati ya Masihi (Abeli) na Israel, ikiwakilisha watu wote (Kaini). Hivyo, kuwawakilisha watu wote, taifa teule lilikuwa lihitimishe ujumbe wake kwa upendo, likitii na kumtumikia Masihi, ambaye ni Abeli kwa ajili ya watu wote.

# CHAPTER 12   MOSES IN THE DISPENSATION FOR RESTORATION

# SURA YA 12   MUSA KATIKA MPANGO WA MUNGU WA UKOMBOZI.

**I.  MUNGU HUTUMIA MLOLONGO – MFANO KATIKA MPANGO WAKE.**

**Sababu ya kuweka mlolongo wa mfano**

Dhumuni la toleo la Ukombozi hatimae linakamilishwa pale mtu anapotimiza wajibu wake na hivyo hupata salimisho la hiari la Shetani na kuwa na mamlaka juu yake (Shetani). Hata hivyo, Shetani hakumtii au kujisalimisha kwa Mungu na baadae asingeweza kumtii au kujisalimisha kwa Yesu, ambaye angekuja kama Mkongwe wa Kwanza na Mzazi wa Kweli. Bila shaka asingeweza kujisalimisha kwa mtu yeyote yule. Yeye kama muumbaji wa mtu, Mungu kwa hiyo alichukua wajibu wa kumfanya Shetani ajisalimishe.

Mungu alimweka Yakobo kama mwakilishi ambaye kwake angeonyesha mfano wa mlolongo kwa ajili ya kumtiisha Shetani. Hii hutoa mwanga kwa kile alichokimaanisha Amosi 3:7, ambaye anasema, " 'Hakika BWANA MUNGU hafanyi lolote bila kufunua siri yake kwa watumishi wake manabii' ". Kuna mengi katika upana (uwazi) ambapo Yakobo alimwongoza Esau ajisalimishe na si jitihada za mtu mmoja Yakobo. Huu ni mlolongo mfano uliofanywa na Mungu, kupitia kwa Yakobo, kuonyesha njia ili kupata salimisho la hiari la Shetani, akishughulika kupitia kwa Esau. Mlolongo wa Yakobo wa kumtiisha Shetani ni sehemu ambayo Musa alifuata katika ngazi ya Taifa.  Na Yesu, Masihi alikuja kufundisha watu jinsi ya kumshinikiza Shetani kujisalimisha kwa hiari. Kama Baba wa Kweli wa mtu au Babu wa Kwanza, Masihi lazima azindue njia ambayo itakuwa ni sehemu ya watu wote kufuata kwa dhati kumsalimisha Shetani. Yesu yeye binafsi kwa dhati alimdhibiti Shetani kwa kufuata mlolongo wa mfano ambao Mungu amekwisha onyesha kupitia kwa Yakobo na Musa.

Katika mwelekeo uleule, mtu yeyote anaweza kumdhibiti Shetani kwa kufuata mlolongo wa njia ya Yesu.  Matendo 3:22 anatwambia kuwa Musa alisema "............Bwana Mungu atamwinua Nabii kwa



ajili yenu kutoka miongoni mwa ndugu zenu kama alivyoniinua mimi. Mtamsikiliza yeye kwa kila atakalowaambia. Hili linarejea ujio wa Masihi ajaye (Yesu) ambaye atafuata mlolongo wa njia ya Musa. Katika Yohana 5:19 Yesu alisema kuwa anafuata njia ambayo Mungu alishaonyesha kupitia kwa Musa kwa njia ya mlolongo wa mfano : "Yesu alimwambia amin amin nawaambia, Mwana hawezi kufanya kitu kwa niaba yake, lakini tu kile aonacho Baba akifanya kwa kila afanyalo na mwana hufanya vilevile". Musa alikuwa mfano ambao Yesu alifuata.

Kwa mtazamo wa nje, inaweza kuonekana kama Yakobo alikuwa tu kiongozi wa familia katika zama za kabila, na Musa kwamba alikuwa kiongozi wa taifa la Israel, na Yesu alikuwa Masihi. Na bado hawa watu watatu walifuata mifumo sawia katika milolongo ya maisha yao, kwa kuwa Mungu aliweka mlolongo mfano katika toleo lake.

## II. MLOLONGO WA MUSA NA YESU ULIFUATA MFUMO WA MLOLONGO WA YAKOBO.

Kama ilivyokwishatajwa, mlolongo wa Yakobo ulikuwa wa kumfanya shetani aanguke. Kila mlolongo unaolenga kumtiisha shetani lazima ufuate njia ambayo ni kinyume cha ile aliyoitumia shetani kupata mamlaka batili. Hebu tulinganishe milolongo, waliochukua Musa, na Yesu na ule mlolongo mfano wa Yakobo.

**A**. Pale Adamu na Hawa waliposhindwa kuzingatia Amri ya Mungu na hawakushinda ushawishi kutoka kwa Malaika mkuu, walianguka. Pale kwenye jabali la Jabbok, Yakobo alipambana na Malaika kwa kuatarisha maisha yake na akapata ushindi dhidi yake (Malaika) – na hapo akapata jina la Israel (Mwa 32, 25-28). Mungu alimjaribu Yakobo kwa kumweka Malaika katika nafasi ya Shetani na matokeo yake ushindi, katika kinyang'anyiro hicho kilifidia majaribu ambayo Adam na Hawa walishindwa kuyakabili. Dhumuni la majaribu ilikuwa si kumpeleka Yakobo kwenye mabaya bali kumweka Yakobo kama mtu ambaye angeweza kutekeleza ukombozi katika upeo wa kiwango cha familia kwa kumfanya akomboe utawala dhidi ya Malaika. Ili Musa awe mtu ambaye anaweza kutimiza ukombozi wa kitaifa wa Kanaan, ilimlazimu pia kushinda majaribu ya kuatarisha maisha yake, jaribio ambalo Mungu alitaka auwawe (Kat. 4:24-26). Na ili Yesu kuwa mtu ambaye angetimiza ukombozi wa duniani kote wa Kanaan na kuwaongoza watu wote kuelekea Ufalme wa Mbinguni , tena ilimbidi kushinda mapambano dhidi ya shetani kwa kuatarisha maisha yake. Alifanya hili kwenye kipindi cha siku arobaini nyikani (Math 4:1-11)

| | **A. Jaribio la Imani** |
|---|---|
| Yakobo | Pambano na Malaika<br><br>Mw 32 : 25-28 |
| Musa | Jaribu la Mungu la ku muuwa Musa<br><br>Kutoka, 4 : 24-26 |
| Yesu | Majaribio baada ya kufunga kwa siku arobaini<br><br>Math 4 : 1-11 |

**B.** Hulka Anguko ilifanyika kwa sababu ya anguko la kiroho na la kimwili. Yakobo na Musa iliwalazimu kutimiza masharti fulani fulani ili kuondoa kiishara Hulka Anguko. Kwa kununua haki ya uzawa kutoka kwa Esau, Yakobo alitumia mkate na bakuli la mboga za majani (Mwa 25:34) ili kuzindua mlolongo wa malipizi kwa ajili ya Msingi wa Matendo, mkate na mboga viliashiria mwili na roho. Ili kuzindua

mlolongo kwa ajili ya Msingi wa Matendo katika mlolongo wake Musa aliwapa Waisrael manna na manumanu vilevile akiashiria mwili na roho. Yoh 6:49-53 inaonyesha kuwa Yesu alifuata mfano huu wa mlolongo : “............Mababu zenu walikula manna nyikani na walikufa .............. isipokuwa tu mkila mwili wa mwana wa mtu na kunywa damu yake hamtakuwa na uzima ndani yenu.........”. Katika njia ya mlolongo wa ukombozi wa dunia yote, mtu wa anguko anaweza akatimiza sharti la malipizi la kuondoa Hulka ya Anguko kwa kumwamini Yesu kwa dhati tu na kuishi alivyoagiza (Yoh 3:16, Math 28:19, 20).

**B. Mwili na Roho**

| | |
|---|---|
| Yakobo | Mkate na bakuli la mboga za majani<br>Mw 25 :34 |
| Musa | Mana na kware<br>Kutoka : 16:12-15 |
| Yesu | Mkate na Vino<br>Yoh 6:48-58 |

**C.** Kwa sababu ya Anguko, hata mwili wa binadamu aliyekufa ni mali ya Shetani. Hata hivyo, kwa kuwa Yakobo alikuwa tayari amebarikiwa na kutakaswa pale mwili wake ulipotunzwa (bila kuoza) kwa siku arobaini na walimwomboleza (Mwa 50:2,3), sharti la mwili wake uliokufa kutenganishwa na Shetani, lilitekelezwa kwa kuwa Musa alifuata njia ya mlolongo mfano ya Yakobo. Kwa msingi wa mafao wa wakati wake, aliweza pia kutekeleza sharti la kuutenganisha mwili wake mbali na Shetani. Kwa sababu hiyo, ndiyo maana Malaika Mkuu alipigania mwili wa Musa dhidi ya Shetani (Yuda 1:9). Na vivyo hivyo, baada ya kifo cha Yesu kulikuwepo na matukio yasiyo ya kawaida ambayo yalijiri juu ya mwili wake (Math 28:12,13).

**D.** Kwa sababu ya anguko la wakongwe wa kwanza wa binadamu (katika kipindi chao cha kukua), Shetani alipata mamlaka batili juu ya mtu. Ili kukomboa hili, Mungu alipanga masharti katika msingi wa (namba, tarakimu au hesabu) ambazo ziliashiria urefu wa kipindi cha shambulio. Hivyo, katika hatua (mchakato) za ukombozi kwa njia ya malipizi, Mungu amefanya toleo lake kwa kumtaka binadamu atimize masharti ya hesabu ambazo zinawakilisha kipindi hicho

| | **C. Mwili** |
|---|---|
| Yakobo | ulitunzwa kwa siku arobaini<br>Mw 50 : 3 |
| Musa | Malaika Mikaeli hupigania mwili wa Musa dhidi ya Shetani<br>Yuda 1 :9 |
| Yesu | Mwili ulipotea<br>Math 28 : 12-13 |

## D. Toleo la mpango la ukombozi kwa mtazamo wa namba, tarakimu na mahesabu

| | Viwango 3 | Wazawa 12 | Siku 7 za Uumbaji |
|---|---|---|---|
| **Yakobo** | Kipindi cha siku 3 baada ya kutoka Haran<br>Mw 31 : 22 | Watoto wanaume 12<br>Mw 35 : 22 | Memba za familia 70<br>Mw 46 :27 |
| **Musa** | Ilimbidi kipindi cha siku 3<br>Kutoka 5:3 | Kabila 12<br>Kutoka 24 :4 | Wazee 70<br>Kutoka 24 :1 |
| **Yesu** | Kipindi cha siku 3 baada ya kusulubiwa<br>Luka 18 : 33 | Watume 12<br>Math 10:1 | Wanafunzi 70<br>Luka 10:1 |

Kwa mfano, wakati Yakobo aliporudi kutoka Haran kwenda Kanaan, kulikuwepo siku tatu za kutenganishwa mbali na shetani (Mwa 31:22), kipindi hicho kilikuwa kipindi cha lazima kuzindua toleo jipya. Kulikuwepo kipindi cha siku tatu za namna hiyo pale Musa alipozindua mlolongo wakuongoza Waisrael kutoka Misri kwenda Kanaan (Kutoka 5:3). Pia Yesu alikaa siku tatu kaburini (Lk 18:33) ili kutenganishwa na Shetani kabla ya kuanza mlolongo wake wa duniani kote wa ukombozi wa kiroho wa Kanaan. Yakobo alikuwa na wana kumi na wawili, ili kukomboa (kimlalo) masharti ya wima ya ukombozi wa vizazi kumi na mbili kutoka nyakati za Nuhu hadi nyakati zake, ambayo yalikuwa kunyakuliwa na Shetani. Kwa sababu hiyo, kulikuwepo makabila kumi na mbili chini ya Musa (Kut 24:4), na Yesu alikuwa na mitume kumi na mbili (Math 10:1).

Uthibiti batili wa Shetani wa kipindi cha siku saba za uumbaji ulifidiwa na familia ya Yakobo kuwa na watu sabini (Mwanzo 46, 27) Musa kuwa na wazee sabini (Kut 24:1), na Yesu kuwa na wanafunzi sabini (Lk 10:1), kila kundi likifanya kazi muhimu katika mwelekeo wa mlolongo wa ukombozi.

### E. Mkongojo

| | |
|---|---|
| Yakobo | Kuvuka mtoni Yordani akiegemea mkongojo<br>Mw 32 : 10 |
| Musa | Kuvuka Bahari ya Sham (Nyekundu) na mkongojo<br>Kutoka 14 : 16 |
| Yesu | Fito la chuma (kuvuka bahari chafu ya dunia ya mateso)<br>- |

E: Mkongojo, ambao unaweza kupiga ufisadi, ukiongoza njia, na kuweka nguvu, ni ishara ya Neno la Mungu, na hivyo, ishara ya Masihi ajaye. Yakobo aliingia katika nchi ya Kanaan akiegemea mkongojo wake pale alipokuwa anavuka Yordan (Mwa 32:10) na Musa aliwaongoza Waisrael kuvuka Bahari ya Sham (Nyekundu) akiwa na mkongojo wake (Kut 14:16). Hili linafunika mtu wa anguko akivuka toka dunia ya dhambi na kuingia dunia adilifu, wakiongozwa na Masihi na kumtegemea Masihi, anayechapa ufisadi. Yesu anayechapa ufisadi kama "fito la chuma" (Ufu 2:27, 12:5), alikuwa aongoze watu wote toka dunia ya mateso, kuvuka bahari chafu ya dunia hii, na kuifikia dunia adilifu.

| F | **Ushirika wa Mama na Mvulana wake** |
|---|---|
| Yakobo | Rebeka na Yakobo<br>Mwanzo 27:43 |
| Musa | Mama wa Musa anamponesha na kumkomesha<br>Kutoka 22:8 |
| Yesu | Maria anamponesha Yesu<br>Math 2:13 |

| **G. Dunia batili** | **→ Dunia Adilifu** |
|---|---|
| Yakobo | Haran → Kanaan<br>Mw 31 : 13, 17, 18 |
| Musa | Misri → Kanaan<br>Kutoka 3:8 |
| Yesu | Misri → Palestina<br>Math 2:13 |

**F:** Dhambi ya Hawa ilikuwa dhambi – mzizi, ambayo ilizaa tunda pale Kaini alipomuua Abeli. Hivyo, shetani alimvamia binadamu na kusindika tunda la dhambi kupitia kwa mama na mwana. Katika msingi wa kanuni ya ukombozi kwa njia ya malipizi, mama na mwana lazima wageuze mlolongo huu, kwa kushirikiana kupelekea utenganisho kuondokana na shetani. Hivyo, zilikuwa jitihada za mama na kwa njia ya ushirikiano kwamba Yakobo alipata baraka na alikuwa tayari kutimiza sharti la kumtenganisha na Shetani (Mwa 27:43). Na kwa njia ya kushirikiana na mama yake, Musa alitokea kuwa katika nafasi ya kutimiza kusudio la Mungu (Kut 2:2). Yesu pia alisaidiwa na mama yake katika kukamilisha utume wake (Math 2:13).

**G:** Mtu kiongozi katika toleo la ukombozi lazima afuate mlolongo wa ukombozi ambao huongoza toka dunia ya shetani kuelekea dunia ya kimbingu. Yakobo alitembea katika mlolongo wa ukombozi kutoka Haran kwenda Kanaan (Mwa 31-33), na Musa alitembea katika mlolongo kutoka Misri kwenda Kanaan (Kutoka 3:8). Yesu naye alitoa maisha yake yote kubadilisha dunia ya Shetani kuwa dunia adilifu.

**H:** Hatima ya Toleo la Ukombozi ni kumwangamiza kabisa Shetani. Kwa hiyo, Yakobo alizika sanamu chini ya mkwaju zikimwakilisha Shetani. (Mwa 35:4), Musa aliiteketeza sanamu ya ndama wa dhahabu (Kutoka 32:20), naye Yesu, kupitia maneno yake na nguvu, ilikuwa auwe dunia ya dhambi na kupata ushindi wa shetani kujisalimisha.

**H. Kuuwa dunia ya dhambi**

| | |
|---|---|
| Yakobo | Kuzika sanamu chini ya mkwaju<br>Mw 35:4 |
| Musa | Kuteketeza sanamu ya ndama wa dhahabu<br>Kutoka 32:20 |
| Yesu | Kumsalimisha Shetani |

## III. MPANGO WA MUNGU WA UKOMBOZI CHINI YA MUSA.

A. Maelezo ya Jumla ya Mpango wa Mungu.

Kanuni ya Toleo la Ukombozi lilikuwa sawia wakati wa Musa kama katika toleo la awali, kwamba ilimbidi akomboe msingi wa Imani na msingi wa Matendo ili kuweka msingi wa Masihi. Hata hivyo, katika Toleo la Ukombozi chini ya Musa, tunagundua kuwa kuna tofauti aina mbili kutokana na toleo la nyuma. Kwanza, Musa alisimama katika msingi wa Masihi uliofanikiwa ambao tayari ulishawekwa na familia ya Isaka, na mafao ya kazi hii iliyotimilika ilikuwa kwa Musa kutimiza masharti ya malipizi yake. Pili upeo wa toleo ulikuwa umepanuka kutoka upeo wa familia hadi upeo wa taifa. Mungu alimchagua Musa kuongoza Waisrael kutoka dunia ya Shetani ya Misri hadi Kanaan, ambayo iliwakilisha Ufalme wa Mbingu. Kwa maneno mengine Mungu alifanya toleo lake ili kukomboa Ufalme wa Mbingu (Kanaan) katika upeo wa taifa.




1 Msingi wa Imani.

a- Mtu kiongozi kwa ajili ya kukomboa Msingi wa Imani

Musa alikuwa mtu kiongozi ambaye alikuwa akomboe Msingi wa Imani. Hata hivyo, Mungu alimchagua Musa, katika nafasi ya toleo kwa namna fulani tofauti na wale viongozi waliotangulia, Adam, Nuhu na Ibrahim. Awali ya yote, Musa alisimama katika nafasi akimwakilisha Mungu, na hata "kuwa kama" Mungu (Kut 4:16, 7:1), pili, Musa kama mwakilishi wake ikimaanisha kumweka Musa kama kielelezo cha Yesu. Ndiyo kusema kwa kuwa Roho wa Mungu angekaa ndani ya Yesu, halafu Mungu kumfanya Musa kuwa mwakilishi wake ina maana kumjenga Musa kuwa mfano wa kuigwa na Yesu.

b- Sadaka iliyohitajika kwa ajili ya Msingi wa Imani

kwa sababu ya kuwa katika nafasi ya toleo maalum, Musa hakulazimika kutoa sadaka-ishara ya vitu kama ile ya Abeli, Nuhu na alivyotoa Ibrahim. Aliweza kukomboa Msingi wa Imani kwa kutimiza kipindi cha siku arobaini za msingi za kutenganishwa na shetani. Kuna sababu mbili juu ya hili.

Kwanza Musa alisimama katika msingi wa mafanikio ya sadaka za vitu alizotoa Abeli, Nuhu na Isaka. Pili kwa kuweka msingi wa ushindi kwa ajili ya Masihi uliowekwa na familia ya Isaka, zama zilikuwa zimepita ambazo kafara ilikuwa sadaka iliyohitajika badala ya Neno, na Musa alikuwa ameingia katika zama za toleo la msingi wa ukombozi zilikuwa zimeisha na zama za toleo la ukombozi zilikuwa zimeanza.

Kwa kuwa toleo lilikuwa limecheleweshwa muda mrefu hata tangu nyakati za Adam – sharti la malipizi lilikuwa lazima ili kukomboa kipindi hiki kirefu cha shambulio la shetani. Lilipaswa kuwa sharti lenye msingi wake katika nambari arobaini, ambayo ni namba inayowakilisha kujitenga na shetani. Katika zama za toleo la ukombozi, msingi wa imani ungeweza kukombolewa kupitia malipizi ya mtu kabakia katika umoja wa Neno la Mungu katika kipindi cha kujitenga na shetani, kipindi ambacho kina msingi wa namba arobaini badala ya kutoa sadaka ya mali.

2. Msingi wa Matendo.

Kiongozi mkuu kwa ajili ya toleo la kuweka Msingi wa taifa wa matendo alikuwa Musa mwenyewe. Kama ilivyoelezwa awali, Musa alikuwa kiongozi mkuu akiwajibika kuweka Msingi wa Imani, ambao ni uhusiano wima na Mungu. Kwa kufanya hivyo alikuwa katika nafasi ya Yesu kwa sababu alikuwa anasimama kama Mungu kwa watu (Kut 4:16, 7:1). Kwa sababu hiyo, Musa alikuwa katika nafasi ya mzazi wa taifa la Waisrael. Bado na yeye kama nabii, alikuwa na jukumu la kutayarisha njia kwa ajili ya Yesu, Musa vilevile alikuwa kama mtoto wa Yesu. Hivyo aliweza vilevile kuwa kiongozi mkuu, au kusimama katika nafasi ya Abeli, kwa ajili ya Msingi wa kitaifa wa kimatendo. Hii ni kanuni sawia na aliyoitumia Abeli, katika nafasi ya mzazi, akafanikiwa kutoa sadaka na kuweka Msingi wa Imani ambao awali ungewekwa na Adam.

Kama Waisrael, katika nafasi ya Kaini, wangempenda Musa na kumtii kwa dhati baada ya kuweka nafasi ya Abeli kwa ajili ya Msingi wa Matendo, na hapo sharti la malipizi la kuondoa Hulka Anguko katika upeo wa taifa lingetimizwa, uhusiano wa wima wa Musa na Mungu ungekuwa katika utaratibu mlalo baina ya Musa na watu na Msingi wa kitaifa wa kimatendo ungeanzishwa.

3 Msingi kwa ajili ya Masihi .

Kama Musa angepita moja kwa moja katika kipindi cha arobaini cha kutenganishwa toka kwa shetani chini ya Neno la Mungu, hapo sharti la malipizi Msingi wa Taifa wa Imani ungetimizwa. Kama Waisrael, chini ya Musa mshindi, wangekomboa Msingi wa Matendo basi Msingi wa Taifa wa Masihi ungekuwa

umeanzishwa. Katika msingi huu, waisrael walipaswa kumpokea Masihi na kuzaliwa upya na kutakaswa kutokana na dhambi ya asili. Na hapo wangeitambua hulka Asili na wangekuwa watu wakamilifu. Hata hivyo, waisrael hawakumwamini Musa, na mlolongo wa taifa wa kuikomboa Kanaan uliishia kwa kurefushwa mara mbili.

**B: Mlolongo wa kwanza wa Ukombozi wa kitaifa wa Kanaan.**

Ili Musa awe kiongozi mkuu akiwakilisha waisrael kwa ajili ya mlolongo wa malipizi ambayo yangekomboa Msingi wa kitaifa wa imani, Musa alitumia miaka arobaini katika Ikulu ya Firauni, makao makuu ya dunia ya Shetani. Ingawa kwa dunia alikuwa Mwana – Mfalme kwa sababu alilelewa na binti mfalme (Kut 2:10), kiukweli Musa alilelewa na mama yake, aliyeishi Ikulu kama yaya wake (Musa) na alimmiminia uja uzito wa Mungu wa Israel na juu ya urithi wake kama mmoja wa watu wateule. Hatimae aliiacha Ikulu, akichagua kuteseka na watu wa Mungu kuliko kufaidi Ikulu ya dhambi, na Ulimwengu usiodumu wa Ikulu ya Firauni (Waheb 11:24). Kwa kipindi chote cha miaka arobaini katika Ikulu Musa alitimiza kipindi cha –arobaini cha kujitenganisha na Shetani na kukomboa Msingi wa Imani.

Ili kujenga Msingi wa Imani, Musa wakati huo huo alifaulu kuwa katika nafasi ya Abeli katika Msingi wa Matendo. Waisrael, waliokuwa katika nafasi ya Kaini, iliwabidi kwa imani wamtii na kujisalimisha kwa Musa, aliyekuwa katika nafasi ya Abeli. Wangekuwa kitu kimoja na Musa na wangerithi kusudio la Mungu. Hili lingekomboa Msingi wa kitaifa wa Matendo. Kama hili lingefanyika, Msingi wa Matendo ungewekwa wakati wa kipindi cha waisrael kurudi kwao Kanaan chini ya uongozi wa Musa.




Akiwa na dhumuni hili akilini, Musa alitimiza sharti la kuanza mpango wa Mungu. Musa alihakikisha kupania kwake kwa Mungu na kwa Waisrael alipomuua Mmisri pale alipomuona akimpiga Mhebrania (Kut 2:12)*. Baada ya kuona Musa anafanya hivyo Waisrael wangemwamini na kuungana na Musa. Na hapo kupitia kwa Musa wangeambiwa na Mungu kusafiri kuelekea nchi ya agano ya Kanaan kwa njia ya moja kwa moja kupitia jimbo la Wafilisti, na wasingepita njia ndefu kupitia bahari (Nyekundu) ya Sham kwenda mbuga za Sinai. Kwa kuunganika kwao na Musa wakati wa siku-ishirini na moja za safari ya kuelekea Kanaan, msingiwa matendo ungeweza kwa mafanikio kuwekwa, na mlolongo huu ungefidia miaka ishirini na moja ya mlolongo wa Yakobo nchini Haran. Kutoka 13:17 inasema, pale Firauni alipowaacha watu kwenda, Mungu hakuwaongoza kwenye njia ielekeayo nchi ya Wafilisti, ingawa hiyo ilikuwa karibu ; kwa kuwa Mungu alisema, pengine watu watatubu watakapoona vita, na kurudi Misri.' " Kifungu hiki kinaonyesha kuwa mpango wa awali wa Mungu aliokuwa nao ilikuwa wapite nchi ya Wafilisti, ambayo ilikuwa ya haraka na ya moja kwa moja.

Hata hivyo, badala ya kumwamini Musa, waisrael wakatoa habari ya kuua alikofanya Musa, na Musa akatoroka toka kwa Firauni kama ilivyoandikwa Kutoka 2:15, "pale Firauni aliposikia habari hizo,

---

**Ingawa Musa alimuuwa mtu, alifanya hivi kwa kumteteya mtu mwingine, tena na kujuakabisa ya kwamba diambo hili likijulikane, yeye atapotesha nafasi zake za pekee pamoja na maisha yake. Ka hivyo, lilikuwa tendo la uhaki na ishara ya kuonyesha kupendelea kwake kwa kusimama upande wa wa waisrael.*

alimtafuta Musa amuue” Musa aliendа kujificha katika mbuga za Midiani, na hivyo mlolongo wa kwanza wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan usingeweza hata kuanza bado.

**C: Mlolongo wa Pili wa Ukombozi wa kitaifa wa Kanaan.**

*1.Msingi wa wa Imani na Msingi wa Matendo.*

Kwa kuwa mlolongo wa kwanza wa ukombozi wa taifa wa Kanaan ulikuwa haujaanza bado malipizi ya kipindi cha miaka arobaini ambayo Musa aliweka akiwa Ikulu kwa ajili ya msingi wa Imani yalivamiwa na shetani. Kwa hiyo Musa alilazimika kuweka kipindi cha pili cha miaka arobaini cha kutenganishwa na shetani. Alifanya hivyo kwa ya njia ya kukimbilia uhamishoni katika mbuga za Midiani. Kwa njia hii aliweza kuukomboa msingi wa Imani wa mlolongo wa pili wa kitaifa.

> Mwishoni mwa kipindi hiki, Mungu alimtokea Musa na kusema,
>
> ........nimeona adha ya watu wangu waliopo Misri, na nimesikia kilio chao kwa sababu ya uongozi wao wa kazi, najua mateso yao, na nimekuja kuwakomboa toka mikononi mwa Wamisri, na kuwaopoa na kuwaleta katika nchi nzuri, kubwa, nchi inayotiririka maziwa na asali, katika maeneo ya Wakanaan.........na sasa, tazama, kilio cha watu wa Israel kimenifikia na nimeona ukandamizaji ambao Wamisri wanawafanyia. Njoo, nitakutuma kwa Farao ili uwalete watu wangu wana wa Israel, toka Misri (Kut 3:7-10).

Katika kipindi cha miaka yake arobaini katika mbuga za Midiani, Musa alikomboa msingi wa Imani na wakati huo huo akaanzisha nafasi yake kama kiongozi mkuu wa msingi wa matendo. Toleo la Mungu lilianza na Musa kuanzisha msingi wa kuweka mlolongo wa ukombozi wa kitaifa kwa kuwapiga Wamisri kwa miujiza mitatau na maafa kumi (Kut 4:7-10). Waisrael waliyashuhudia haya na kugundua kuwa Musa alikuwa kiongozi kweli aliyetumwa na Mungu. Katika kianzio hiki mlolongo wa pili wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan hatimae uliweza kuanza. Hata hivyo, ukweli kwamba Waisrael walikuwa mwishowe wakimfuata Musa haikumaanisha kuwa sharti la malipizi la kuondoa Hulka Anguko lilikuwa limeisha (kutimizwa). Shetani aliweza kushambulia wakati wa mlolongo wa toleo hili na kusababisha kipindi hiki kirefu kupewa yeye. Ili kukomboa kipindi hiki kilichopoteza malipizi katika kianzio cha taifa, Waisrael, katika nafasi ya Kaini, walijisalimisha kwa Musa, kumtii na kubaki kuwa kitu kimoja katika kipindi chote, mpaka ujio wao katika nchi ya Kanaan. Matokeo yake, Waisrael walilazimika kuingia Kanaan wakiwa watiifu kwa Musa wakati wote wakiwa katika mlolongo wa mbugani. Na hapo ndipo Msingi wa kitaifa wa Matendo uliweza kujengwa.

Mungu tayari alijua hili, ingawa Waisrael walimwamini Musa vya kutosha kuanza safari kwenda nchini Kanaan, hawakuwa na imani timilifu pamoja naye. Mungu alihofu kwamba kama wangeenda moja kwa moja, kulikuwepo hofu ya kupigana vita (Kut 13:17) kungechangia ukosefu wao wa imani,



na ilikuwa rahisi kurudi Misri na kuacha toleo lake bila kutimizwa. Kwa sababu hiyo, Mungu badala yake aliwaongoza kupitia bahari (Nyekundu) ya Sham na kupitia Sinai, hata kama itachukua muda mrefu, mungu aliendelea kuwaonyesha neema yake kwa kutenda miujiza. aliKuwa anajaribu kuifanya (safari) ngumu kwao ili wakose kuamini na kurudi Misri. Matokeo yake, Musa alianza pamoja na Wanaisrael kile ambacho kingekuwa mlolongo wa miezi ishirini na moja kupitia kwenye pori (mbuga).

*2. Hema katika mpango wa Ukombozi.*

Mwanzoni mwa mwezi wa tatu baada ya Waisrael kutoka Misri, walirejea katika mbuga za Sinai. Pale, Mungu alimpa Musa maagizo maalum. Mungu alimwambia awatakase watu (Kut 19:10) na kuimarisha imani yao. Na hapo Musa alipanda mlima Sinai akiwa na wazee sabini na kukutana na Mungu (Kut 24:9,10). Huko, Mungu alionyesha utukufu kwa watu wake, kama inavyofafanuliwa katika Kutoka 24:15-17,

> na hapo Musa alikwea mlima na .......utukufu wa Bwana ulitua juu ya Mlima Sinai, na wingu liliufunika kwa siku sita, na siku ya saba alimwita Musa kutoka katikati ya mawingu. Wakati huu tokeo la utukufu wa Bwana lilikuwa kama moto uteketezao juu ya mlima na kuonwa na watu wa Israel.

Hii ilikuwa ni kuwaonyesha kuwa Mungu alichukua hatua hizi ili watu wa Israel wawe na imani thabiti kwake.

Mungu alimwita Musa kileleni na kumuomba afunge kwa siku arobaini ili aweze kupokea vipande viwili vya mawe vikiwa na Amri kumi (Kut 24:18). Wakati Musa akiendelea kufunga mlimani, alipokea maagizo juu ya sanduku la agano na Hema (Kut 25-31). Pale, funga ya siku arobaini ilipomalizika, alipokea vipande viwili vya mawe vikiwa vimeandikwa Amri kumi (Kut 31:18). Pale Musa alipotelemka chini ya mlima, alikuta Waisrael wamepoteza imani kwa Mungu na walikuwa wanamwabudu ng'ombe wa dhahabu kama Mungu wao (Kut 32:2-4). Wakati wa siku arobaini ambazo kiongozi wao hakuwa pamoja nao, Waisrael walishapoteza imani na waliasi dhidi ya Mungu mwenyewe ambaye aliwaongoza pamoja na miujiza mingi. Pale Musa alipoona hali hii, alichukizwa sana, akiwa kwenye kitako cha mlima, alitupa vipande hivyo ardhini, akavivunja (Kut 32:19).

Mungu alimtokea Musa tena na kumpa maelekezo kukata mawe mawili kama yale ya kwanza (Kut 34:1). Baada ya Musa kumaliza funga yake ya siku arobaini alipokea tena Amri kumi, zikiwa zimeandikwa kwenye vipande viwili vya mawe. Waisrael walijenga kisanduku cha agano na Hema , vipande vya mawe mawili ndani yake kama kiini :-

a: Umuhimu wa vipande na sanduku la agano

*(i) Umuhimu wa vipande*

Adam na Hawa waliumbwa kwa Neno. Kama wangejikamilisha wenyewe, wangekuwa miili mikamilifu ya neno. Hata hivyo kwa sababu ya Anguko, walipoteza Neno. Vipande vilivyokuwa na Amri za Mungu ambazo Musa alipokea baada ya kipindi cha arobaini cha kutenganisha toka kwa shetani, vilikuwa na maana maalum. Hivi ni viwakilishi hasa vya Neno, kiishara vikiwakilisha kukombolewa kwa Adam na Hawa toka dunia ya Shetani. Hivyo, viapnde viwili kama ishara ya Adam na Hawa, vilevile viliashiria Yesu na Roho Mtakatifu, ambao wangekuja kama umwilisho kamili wa Neno. Hii ndiyo maana Yesu anaonyeshwa kama "jiwe jeupe (Ufunuo 2:17)na "Mwamba" (1Wakor 10:4).

Kupokea vipande kwa Musa vikiwa na maneno ya Mungu pia kunaonyesha kuwa zama za toleo la msingi wa ukombozi zimepita. Kwa maneno mengine, zama ambazo mtu angeweza kujihusisha na Mungu tu kupitia sadaka za vitu imepita, na mtu wa anguko ameingia zama za mpango wa ukombozi, ambamo mtu anaweza kuhusiana na Mungu kupitia Neno.

*(ii) Umuhimu wa Hema*

Yesu alilinganisha hekalu katika Yerusalem na mwili wake (Yoh 2:21), na Paulo alisema Wakristu ni mahekalu ya Mungu (1Wakor 3:16). Hekalu ni taswira-wakilishi ya Yesu. Hata hivyo, wakati wa mlolongo wao jangwani, Waisrael hawakuweza kujenga hekalu na hivyo walijenga Hema badala yake. Hivyo, Hema ambayo ilikuwa kielelezo kidogo cha hekalu, ilikuwa ni kiwakilishi-ishara cha Yesu. Kwa sababu hii pale Mungu alipomwamuru Musa kujenga Hema alisema........hebu wanifanyie mimi madhabahu, ili niishi katikati yao. (Kut 25:8) kutokana na hayo, Hema ni ishara ya Masihi ambaye Waisrael walikuwa wamtumikie kwenye mlolongo wao kule mbugani.




*(iii) Muundo wa Hema*

Tabenako ilikuwa na sehemu Takatifu sana (Kut 26:33,34). Ni makuhani wakuu tu wangeingia sehemu Takatifu sana, na hilo ni mara moja kwa mwaka, kwa ajili ya kutoa kafara. nDani ya sehemu Takatifu sana kulikuwemo sanduku la agano, ndani mwake mlikuwa na vipande viwili vya mawe, hivi viliashiria Yesu na Roho Mtakatifu, na mbingu na dunia. Tunaweza kufikiria sanduku la agano , kwamba katika tafsiri finyu, ni ulimwengu mdogo wa Ulimwengu, na kuwa kiduchumbingu cha tabenako. Sehemu Takatifu sana inaashiria roho-pekee ya Yesu na dunia halisi isiyoonekana, na sehemu Takatifu, ambayo ilikuwa ni sehemu ya kawaida kwa ajili ya sadaka za kafara, inaashiria mwili wa Yesu na dunia halisi ionekanayo.

b: Dhumuni la mpango wa Mungu pamoja na vipande vya mawe na Hema.

Kwa mtazamo wa Mungu, mara tu Waisrael walivyoondoka Misri ilikuwa imeamriwa kwamba waende moja kwa moja Kanaan bila kurudi nyuma, ilikuwa ni lazima kuingia Kanaan kwa gharama zozote.




Mpaka hapo, Mungu alitafuta namna ya kuwatia moyo Waisrael ili kumwamini kwa kuendelea kufanya miujiza, akianza mwanzo kabisa mwa toleo.

Baada ya kuanza safari yao ya kwenda Kanaan, Mungu aliwaongoza na kuwalinda wana wa Israel katika safari yao yote mbugani kwa kuwafanyia miujiza mbalimbali aliwaongoza kwa nguzo wingu lililong'ara kama moto na kwa nguzo ya moto (Kut 13:21) kwa kugawa maji ya Bahari Nyekundu (Kut 14:21); kwa kuwapa manna na nyama (kware) (Kut 16:12, 13,35); alimwamuru Musa kutoa maji kutoka kwenye mwamba kwa ajili ya kuwanywesha watu (Kut 17:6);  na akawashinda kwa Amaleki kwa nguvu zake (Kut 17:10-13). Mbali na haya yote, wana wa Israel wakapoteza imani kwa Musa na Mungu mara nyingi, na mwisho kukawa na hatari ya kwamba hata Musa mwenyewe pengine angetenda isivyostahili kwa kukosa imani.

Kwa sababu hii, Mungu aliona umuhimu wa kuumba mtendewa wa imani ambaye hawezi kubadilika daima, hata kama mtu atabadilika. Kama kutakuwepo hata mtu mmoja miongomi mwa Waisrael ambaye ataamini katika mtendewa huyu wa imani, basi Mungu angeweza kutekeleza nia yake kwa kumfanya mtu huyo imani yake iwe mwakilishi wa Waisrael. Na baadae kuipitisha kwa kila mtu kama vile mchezo wa kupokezana fimbo. Mtendewa huyo wa imani ilikuwa ndiyo tabenako, ambalo lilihifadhi kinara na vipande vya mawe na kuashiria Masihi. Kwa jinsi hii, Waisrael kujenga tabenako ilikuwa na maana kwamba Masihi amekwisha kuja. Vivyo hivyo kama wangeendelea kumfuata Musa mpaka waingiapo nchi  iliyobarikiwa ya Kanaan, na kuitumikia tabenako kwa unyenyekevu unaostahili mbele ya Masihi, basi wangekuwa wamejenga msingi wa matendo wa kitaifa.

c. Msingi wa Hema.

Kwa kuwa ujio wa Masihi lazima utanguliwe na msingi kwa ajili ya Masihi na Hema lilikuwa Masihi mfano, hivyo kulipokea kunatanguliwa kuwepo kwa ajili ya vivyo hivyo msingi wa imani na msingi wa matendo ulikuwa lazima kwa msingi wa Hema.

*(i) Msingi wa kwanza kwa ajili ya Hema*.

Kutokana na funga ya siku arobaini ya Musa pale Mlimani Sinai {Kut.24:18}, Mungu alimtaka aanzishe kipindi cha arobaini cha kujitenga kutoka kwa Shetani na hivyo kuweka Msingi wa Imani wa Hema. Kilichokuwa kifuate, Waisraeli walitakiwa kumtumikia na kumtii Musa wakati wa kipindi cha siku arobaini cha kujitenga toka kwa shetani na mpaka ambapo watakuwa wamejenga tabenako, kwani hii ingeweka Msingi wa Matendo. Hata hivyo Waisraeli walitokomea katika kutoamini na kutengeneza na kuabudu ndama wa dhahabu {Kut.32:2-4}. Kwa kuwa sharti la malipizi la kuondoa Hulka Anguko halikutimizwa, Msingi wa Matendo haukuwekwa. Pale Musa alipowaona Waisraeli bila imani chini ya mlima, alipandisha hasira na kurusha vipande {vya amri} ardhini na kuvivunja {Kut.32:19}.

Kwa kuwa vipande hivyo viliashiria Yesu na Roho Mtakatifu, Musa kwa kuvivunja kama hatua dhidi ya ukosefu wa imani wa watu alifanya uchuro kuwa Yesu ajapo atasulubishwa kama Waisraeli wasingekuwa na imani.




{ii} Msingi wa Pili kwa ajili ya Hema.

Baada ya kumleta Haruna na watu kutubu, Musa alifunga siku arobaini mchana na usiku kwa mara ya pili, hivyo kurudisha kipindi cha arobaini cha kutenganishwa toka kwa shetani. Katika msingi huu, Mungu aliandika jozi nyingine ya vipande na Musa maadili ya Tabenako {Kut.34:28}. Waisraeli sio tu walimtii Musa katika kipindi cha siku arobaini, bali pia walijenga Hema kulingana na maelezo toka kwa Mungu na Musa.

Hii ilikuwa ni siku ya kwanza ya mwezi wa kwanza wa mwaka wa pili tangu Waisraeli waondoke Misri. Hata hivyo, Msingi wa matendo usingeweza kutekelezwa kwa Waisraeli kujenga tabenako tu. Ili

kuujenga, Waisraeli walikuwa wawe kitu kimoja na Musa na kumtii na kuzingatia maadili ya Mungu juu ya tabenako kuwa ni thamani zaidi ya maisha yao.

Ilipofika siku ya ishirini ya mwezi wa pili wa mwaka wa pili tangu kutoka Misri, Waisraeli, wakiwa wamebeba kwa heshima Hema {Hesabu.10:11-12} waliondoka katika mbuga za Sinai kuelekea Kanaan chini ya uongozi wa nguzo ya wingu. Hata hivyo, walitumbukia kwa kukosa imani na kumlalamikia Musa, hivyo Mungu aliunguza sehemu ya kambi {Hesabu.11:1}, katika jitihada ya kuwaamsha. Lakini hawakuamka kutimiza makusudio ya Mungu na waliendelea kumlalamikia Musa na kutamani kurudi Misri {Hesabu.11:4-6}. Kwa kuangalia tena hali hii, tunaweza kuona kuwa Msingi uliofaulu kwa ajili ya Tabenako ulishambuliwa na Shetani.




Kwa hiyo, Mungu kwa mara nyingine aliwaagiza Waisraeli kuweka msingi wa siku arobaini wa kutenganishwa kutoka kwa shetani. Aliwapa kipindi cha siku arobaini cha kupeleleza kama sharti la kutimiza mlolongo wa pili wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan. Mungu alichagua watu kumi na mbili kupeleleza kwa siku arobaini, mtu mmoja kila kabila (Hesabu.13:1-15). Hata hivyo, isipokuwa tu Joshua na Kalebi wote walirudisha taarifa zisizo na imani (Hes 13:28-32). Waisrael waliposikia habari hizi kwa hasira walimlalamikia Musa na kung'ang'ania kumchagua kiongozi mpya mwingine ili warudi Misri. Na hapo Mungu aliwatokea watu wote na kumwambia Musa, "......mpaka lini watu hawa watanipuuza? Na ni mpaka lini wataendelea kutoniamini, pamoja na maono yote niliyowafanyia?" (Hes 14:11). Hapo Mungu akasema, "lakini watoto wenu ambao mlisema watakuwa mawindo nitawaleta ndani wationa nchi mliyoisusa. Lakini kwenu ninyi miili yenu iliyokufa itaanguka mbugani na watoto wenu watakuwa wachungaji kondoo mbugani kwa muda wa miaka arobaini, na watateswa kwa sababu ya kukosa imani kwenu, mpaka mwili wa mwisho uliokufa ulale mbugani. Kulingana na hesabu ya siku mlizotumia kupeleleza nchi, siku arobaini kwa kila siku katika mwaka, mtalipia uovu wenu, kwa miaka arobaini, na mtabaini kisichonipendeza " , " (Hes 14:31-34).

Kwa hiyo taarifa zisizokuwa na imani zilipelekea kushindwa kwa kipindi cha upelelezi cha siku arobaini, na waisrael hawakuwa na uwezo wa kuweka msingi wa matendo pale Kadesh-Barnea. Matokeo yake, mlolongo wa pili wa taifa (mlolongo wa siku – ishirini na moja katika mbuga) ulirefushwa mpaka mlolongo wa tatu, mlolongo wa miaka – arobaini kwa mara ingine tena mbugani (Nyikani).

**D. Mlolongo wa tatu wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan.**

*1. Msingi wa Imani.*

Kwa sababu ya kukosa imani kwa waisrael, mlolongo wa pili wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan uliishia kushindwa. Hivyo, kipindi cha miaka arobaini katika mbuga za Midiani, ambao Musa aliweka msingi wake wa imani wa mlolongo huu wa pili, ulichukuliwa na Shetani. Kwa kushindwa kazi ya kupeleleza siku arobaini nchini Kanaan, ili kukomboa msingi wa imani kwa kipindi cha mlolongo wa tatu. Hivyo aliwaongoza waisrael katika mlolongo wa miaka arobaini ya kutangatanga mbugani ambao uliishia baada ya kurudi Kadesh – Barnea. Kwa kuitunza tabenako kwa imani kuu na utiifu katika kipindi hiki cha miaka arobaini wakitangatanga, Musa, aliweka tena kipindi cha arobaini cha kutenganishwa kutoka kwa Shetani.

2. Msingi wa matendo .

Kama wakati wa kipindi cha miaka arobaini cha kutangatanga (mbugani), nyikani, waisrael wangejisalimisha na kwa utiifu wangeungana na Musa, ambaye aliitunza na kuwa pamoja na Hema bila kubadili imani, na hivyo wakaingia nchi ya Kanaan, msingi wa matendo ungewekwa katika mlolongo wa tatu wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan. Vivyo hivyo hiki kipindi cha miaka arobaini ya kutangatanga mbugani kilikuwa ni kipindi ambacho msingi wa imani ulipaswa kuwekwa kwa ajili ya mlolongo wa tatu ili kupata msingi wa wa kuondoka katika mlolongo wa tatu kuelekea Kanaan. Mlolongo wa tatu kwa ajili ya msingi wa matendo ulianzishwa chini ya Musa, lakini ulihitimishwa chini ya uongozi wa Joshua. Lazima ueleweke katika mtazamo wa awamu hizi mbili.

a. Msingi wa matendo chini ya Musa.

Akiwa na wasiwasi kwamba watu wake wangetumbukia tena katika kukosa imani, Mungu katika rehema zake, aliwapa waisrael sanduku, Hema na vipande vya mawe vikiwa na amri kumi. Kama waisrael wangeshika maadili ya tabenako wakiwa na imani yakinifu baada ya kupokea rehema hii kutoka kwa Mungu katika mlima Sinai, au wakati wa kipindi cha upelelezi, basi pale wangeweza kulipia mwanzo ulioshambuliwa na mlolongo wa pili.

Kwa maneno mengine, wangeweza kukomboa hali yao mpaka ile ambayo walikuwa nayo wakati wanaondoka Misri, kwamba kwa kuunganika na Musa baada ya kupokea rehema ya maajabu matatu, na maafa kumi. Vivyo hivyo kama hawa waisrael ambao walimfuata Musa Kadesh – Barnea baada ya kipindi cha malipizi ya miaka arobaini mbugani wangenyenyekea na kuhudumia vipande, kinara na tabenako, hapo taifa la Israel kwa ushindi lingeelekea nchi ya Kanaan.

Kwa kuwa vipande vilikuwa sehemu ndogo ya mfano wa sanduku, na sanduku lilikuwa mfano mdogo wa Hema basi vilevile vipande vilikuwa sehemu ndogo ya mfano wa Hema. Hivyo Hema au sanduku vinaweza kuwakilishwa na vipande au zaidi , na chanzo cha vipande ambacho ni mwamba ambamo kwayo vilifanyika. Hivyo Biblia huandika kumbukumbu kwamba kuanza kwa mlolongo wa tatu wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan chini ya mwamba kule Kadesh – Barnea (Hes 20:8-11)



Waisrael walikuwa wananong'ona ng'ona kwa chuki dhidi ya Musa kwa sababu hawakuwa na maji. Ili kuwaokoa waisrael, ambao kwa mara nyingine walikuwa wanajitosa katika ukosefu wa imani pamoja na kusota miaka arobaini mbugani (Hes 20:4-10), Mungu alimuamuru Musa awape watu maji (20:8) kwa sababu walikuwa wakilalamika na kumlaumu kwa kutokuwa na maji, Musa alikasirishwa na watu wake na akapiga mwamba mara mbili kwa ufito wake (Hes 20:11), Mungu hakufurahishwa, na alisema, "kwa kuwa hukuniamini, kunitakatisha mbele za macho ya waisrael, kwa hiyo hutalileta kundi hili katika nchi ambayo nimewapa (Hes 20:12)

Kwa kupiga mwamba mara mbili, pale ambapo angepiga mara moja (kama Mungu alivyomtaka afanye mapema pale Refidim (Kut 17:6), Musa alishindwa kuzindua toleo kwa mafanikio na pia alijizuia mwenyewe asiingie katika nchi iliyobarikiwa ya Kanaan, pamoja na kwamba ilikuwa inaonekana (Hes 20:24; 27:12-14; Kumbukumbu la Torati 3:23-37). Kuna tofauti ipi kati ya wakati Musa alipopiga mwamba pale Horeb huko Refidim na muda huu mpaka Mungu akamkemea kumzuia Musa asiende nchini Kanaan, ambamo Musa alitamani kuingia?. Baada ya kufanya kazi kwa udhati kabisa kwa muda wote wa maisha yake, aliongoza watu wake wasio na imani kuelekea hatima maridhawa, nchi iliyobarikiwa, ni kwa kiasi gani Musa alitaka kuingia Kanaan! Alimuomba Mungu, " " "Niruhusu niendelee, naomba, na nione nchi nzuri ng'ambo ya Yordan, nchi nzuri ya milima na Lebanon""" (Kumbukumbu la Torati 3:25). Mungu alimjibu kwa ukakamavu, " " " usiongee zaidi kwangu juu ya hili""" (Kumbukumbu la Torati 3:26). Pamoja na Musa kufika Yordan, kwa sababu ya tatizo la kuleta maji kutoka kwenye mwamba alikufa mlimani Pisgah katika nchi ya Moab bila kukanyaga nchi ya Kanaan (Yoshua 34:1-6).

Lazima tujifunze kutokana na makosa ya Musa. Katika maeneo yote mawili ya Refidim na Kadesh, Musaalileta maji baada ya kupata maagizo toka kwa Mungu. Kuonyesha kwake kwa vitendo nguvu za Mungu kwa watu wasio na imani na matumizi ya fimbo yake ni hali sawia katika matukio hayo mawili. Tofauti pekee ilikuwa ni ile ya Kadesh alipiga mwamba mara mbili. Hebu tuangalie ni kwa nini mwamba ulikuwa upigwe mara moja na kwa nini kuupiga mara mbili ilikuwa dhambi.

Katika Biblia Yesu anaashiriwa kama jiwe jeupe (Ufu 2:17) na kama mwamba (1Wakor 10:4). Kwa kuwa Yesu alikuja kama mti wa uzima (Ufu 22:14; vilevile rejea "Anguko"), mwamba unawakilisha pia mti wa uzima. Mti wa uzima katika bustani ya Eden (Mwa 2:9)uliashiria Adam mkamilifu. Kwa kuwa mti huo wa uzima pia ni mwamba (jiwe), mwamba lazima pia uashirie Adam mkamilifu.

Katika bustani ya Eden, Shetani alimpiga Adam na kusababisha anguko la Adam ambaye alikuwa awe mwamba. Kwa kuwa Adam hakupata kuwa mti wa uzima (Mwa 3:22-24), alishindwa kupata kuwa mwamba ambao milele ungetoa maji ya uzima kwa wazawa wake.

Hivyo, mwamba ambao haukutoa maji kabla ya Musa kuupiga kwa fimbo uliashiria Adam wa Anguko. Mungu kwa kuzingatia kanuni ya ukombozi kwa njia ya malipizi, alitaka kuweka sharti la kumkomboa Adam kama mwamba unaoweza kutoa maji, kwa Musa kuupiga mara moja mwamba huo (tasa) mkavu, ambao ulikuwa ni ishara ya Adam wa Anguko, na kutoa maji kutoka kwa huo mwamba.

Vivyo hivyo, Mungu alimtaka Musa kuupiga mwamba mara moja kama sharti la kumkomboa Adam wa kwanza wa Anguko kupitia malipizi na kuwa Adam mkamilifu wa pili ama Yesu. Kwa hiyo mwamba uliotoa maji baada ya kupigwa mara moja uliashiria Yesu, ambaye alipaswa kuja na kutoa maji ya uzima kwa watu wa anguko "kwa maana waliunywea mwamba wa Roho uliowafuata na mwamba ule ulikuwa ni Kristu" (1Wakor 10:4). Kitendo cha Musa cha kuupiga mwamba mara mbili kiliwakilisha kumpiga Yesu, ambaye alikuwa ndiye mwamba uliokombolewa ambao ungetoa maji ya uzima kwa watu wote. Kwa maneno mengine, Musa kuupiga mwamba mara mbili (kwa kuwakasirikia waisrael

kutokuwa na imani) kulipelekea kuwepo msingi wa Shetani kuweza kumshambulia Yesu moja kwa moja, ambaye alikuwa mwamba wa kweli, kama waisrael wangekosa imani kwa Yesu katika enzi zake. Ndiyo maana kitendo cha Musa kilikuwa kosa kubwa mno.




Hivyo, msingi wa kuanza toleo, msingi ambao ungeanzia kwenye mwamba haukudhihirishwa. Badala ya Musa, alikuwa Yoshua ambaye, bila kubadilika kiimani na utiifu, aliongoza kizazi kipya kuingia Kanaan. Alifanya hivyo katika msimamo wa msingi aliouweka kwenye tabenako kupitia kipindi cha siku arobaini za kupeleleza nchini Kanaan.

b. Msingi wa matendo chini ya Yoshua.

Kwa kuwa Musa alipiga mwamba mara mbili, jukumu lake la kuongoza waisrael alipewa Yoshua.

> Na Bwana akamwambia Musa, “mchukue Yoshua, mwana wa Nun, mtu ambaye kwake mna roho, na mwekee mikono juu yake; mfanye asimame mbele za Elieza kuhani na kundi lote, na utamtuma mbele yao. Umpe madaraka yako yote, ili kundi lote la Israel waweze kumtii.” (Hes 27:18-20).

Yoshua alikuwa mmoja wa waisrael wawili ambao hawakuanguka katika kutoamini katika kipindi cha siku arobaini za upelelezi na alisimama kidete juu ya msingi wa imani ambao Musa aliweka kwa ajili ya Hema. Alikuwa mmoja wa wawili tu ambao waliweka msingi wa tabenako na kulihudumia kwa imani isiyobadilika na utiifu mpaka mwisho. Ingawa imani ya Musa ilitikisika, maadili ya tabenako yalibaki vilevile bila kubadilika katika msingi aliouweka Yoshua.

Kwa hiyo Mungu, alimchagua Yoshua kuchukua nafasi ya Musa na alitekeleza mpango wake kwa namna ambayo ili kuanza mlolongo wa tatu, waisrael walipaswa kutubu na kujiegemeza wenyewe katika Hema (Hes 21:6-8) ilikuwa sasa nia ya Mungu kuanzisha msingi wa matendo kwa ajili ya mlolongo wa tatu akimtumia Yoshua kama kiongozi kwa kuwafanya waisrael waingie Kanaan wakiwa katika utii yakinifu kwa Yoshua.

Kwa hiyo Mungu alimwambia Musa,

> “ .........(Yoshua) atasonga mbele (kuingia Kanaan) mbele ya watu hawa na atawapa ardhi utakayoiona”
>
> (kumbukumbu la Torati 3:28).

> Baadae Mungu alimwambia Yoshua
>
> > “.........Musa mtumishi wangu amefariki dunia, sasa kwa hiyo inuka, songa mbele ng’ambo ya Yordan, wewe na watu hawa, katika nchi ninayowapa, kwa watu wa Israel” (Yoshua 1:2).
> >
> > “.....Kama nilivyokuwa na Musa vivyo hivyo nitakuwa nawe; sitokuangusha au kukutelekeza. Uwe mwenye nguvu na mwenye ari; kwani utawafanya watu hawa kurithi nchi ambayo niliapa kuwapa baba zao. (Yoshua 1:5-6).

Wakati huo huo, kizazi cha pili cha waisrael, ambacho kilizaliwa mbugani, kilipania kumfuata Yoshua kwa kujitoa maisha yao, wakisema

> “...kila lile unalotuamuru tutalifanya, na popote utakapotutuma tutaenda........yule akupingaye amri yako na asiyetii maneno yako, lolote unalomwamuru, atauwawa. Uwe na nguvu tu na mwenye ari njema. (Yoshua 1:16-18).

Pia walitoa taarifa zao za uaminifu baada ya kupeleleza Yeriko na kusema “.....Kweli Bwana ametoa nchi yote mikononi mwetu na zaidi ya yote wenyeji wote wa nchi wana hofu kwa sababu yetu (kuwamiliki) (Yoshua 2:24). Hivyo kizazi cha pili cha Israel kiliunganika kabisa na Yoshua ambaye alisimama katika msingi wa Hema kulingana na maagizo ya Mungu na waliongozwa kuelekea Yordan. Mto ulikuwa umefurika, unatiririka juu ya kingo zake. Lakini makuhani waliobeba kinara wakasonga mbele kama walivyoagizwa, na maji yakasita yakajikusanya kiwimawima na yakatiririka upande wa chini na waisrael wote wakapita kwenye nchi kavu kuelekea Kanaan (Yoshua 3:16-17).

Katika kuitwaa Yeriko kutokana na maagizo ya Mungu, askari elfu arobaini walijongea katika kundi, wakifuatwa na makuhani saba wakitembea na matarumbeta saba, watu walitanguliza sanduku la

agano, ambalo lilibebwa na makuhani wa Walawi. Watu wote wa Israel walitembea nyuma (Yoshua 6:8-9). Kama Mungu alivyoamuru, waisrael walitembea kuzunguka mji kwa siku sita, wakifanya msafara (ziara) mmoja kila siku, na siku ya saba, ziara saba. Na hapo kwa kelele za Yoshua na watu wake, kuta zilisambaratika (Yoshua 6:20). Kwa namna hiyo waisrael walianza kuiteka Kanaan, ambayo yalikuwa makazi waliyosubiria sana.

Sasa hebu tufupishe tulivyojifunza juu ya msingi wa matendo wa mlolongo wa tatu wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan. Kwa sababu ya ukosefu wa imani waisrael kwa Musa, msingi wa matendo haukuwekwa chini ya Musa, na kizazi cha kwanza cha waisrael akiwemo Musa wote isipokuwa Yoshua na Kalebi ambao walikuwa na imani thabiti-wote walikufa mbugani. Kizazi cha pili cha waisrael, kilichozaliwa mbugani, kiliingia Kanaan (Hes 14:29-38) chini ya Yoshua, wakikamilisha Msingi wa Matendo.

Ingawa Msingi wa kitaifa kwa ajili ya Masihi uliwekwa chini ya Yoshua, ilikuwa ni lazima kwa upande wa mbingu kuandaa msingi thabiti ili Masihi aje. Hii ni kwa sababu mtu wa anguko alishajenga falme kuu chini ya Shetani ambazo zingepinga toleo la mbingu la ukombozi.

Lakini pamoja na wajibu wao kuweka msingi wa mbingu, waisrael walitokomea katika kutokuwa na imani hata baada ya kuja katika nchi ya Kanaan, na hivyo, toleo la Mungu kwa mara ingine tena likarefushwa kwa kurudiwa rudiwa mpaka zama za Yesu.

Moses.

Home page.

## CHAPTER 13. JESUS IN THE DISPENSATION FOR RESTORATION

## SURA YA 13. YESU KATIKA TOLEO LA UKOMBOZI

Yesu alikuwa na wajibu wa kumtiisha (kumsambaratisha) Shetani. Ili kufanya hivyo ilimbidi kufuata mlolongo wa mfumo ambao Mungu aliuonyesha kama ishara na taswira katika milolongo ya Yakobo na Musa (Kumbukumbu la Torati 18:18, Yohana 5:19). Lakini kama Waisrael chini ya Musa walivyoanguka katika kukosa imani mwituni, Waisrael wakati wa Yohana Mbatizaji walitokomea katika ukosefu wa imani, kukiwa na matokeo ambayo yalisababisha mlolongo wa kiwango cha dunia nzima cha Yesu kwa ajili ya ukombozi wa Kanaan kuendelea kupitia majaribio matatu au milolongo.

### I MLOLONGO WA KWANZA WA UKOMBOZI WA KANAAN KATIKA KIWANGO CHA DUNIA NZIMA.

### A. Msingi wa Imani

*1. Kiongozi Mkuu wa kukomboa Msingi wa Imani*

Kiongozi mkuu mwenye wajibu wa kuandaa msingi wa toleo la ukombozi wakati wa Masihi ulikuwa "nyoosheni njia ya Bwana" (Yoh 1:23) huyu kiongozi mkuu alikuwa Yohana Mbatizaji, ambaye alikuwa mkuu sana kati ya waliozaliwa na wanawake (Math. 11:11). Kama ilivyoelezwa katika sura ya mlolongo wa Musa, kurudiwa ukosefu wa imani kwa Wasirael kulimpa nafasi Shetani kushambulia mwili wa Yesu, ambao ulikuwa ni mwilisho wa mwamba na tembe za jiwe. Kwa hiyo kipindi cha historia yao, Mungu aliwaelimisha watu wateule wasiwe wakosefu wa imani. Aliwatuma manabii wengi, hasa nabii

Eliya, kuwaelimisha watu kuungana kabisa, chini ya maadili ya hakalu ambalo kwalo ni taswira ya Yesu. Hata hivyo, Waisrael kwa sababu waliendelea kutokuwa na imani, lengo pekee la Eliya, ambalo lilikuwa kuwageuza Waisrael kutokana na ukosefu wao wa imani kurudi kwa Mungu halikutimizwa.  Kwa hiyo, Mungu alisema ya kuwa Eliya atarudi tena – ili kukamilisha jukumu lake (Mal. 4:5). Kurudi kwa Eliya kulitimizwa katika mtu Yohana Mbatizaji (Luka. 1:17; Math. 11:14, 17:13) alikuwa ni mtu aliyekuwa na wajibu wa kuweka msingi wa imani kwa ajili ya Masihi.

*2. Sadaka iliyohitajika ili kukomboa Msingi wa Imani:*

Kama ilivyofafanuliwa katika somo la "Musa katika toleo la ukombozi" kwa kuanza na toleo la zama za Musa, kipindi cha malipizi kwenye msingi wa hesabu ya arobaini (ambacho kinatajwa kama kipindi cha malipizi chenye msingi wa kipindi cha arobaini).  Kikawa kipindi tosha kutimiza sharti la kujitenga toka kwa shetani. Kwa maneno mengine, katika nafasi ya kutoa sadaka, kiongozi mkuu aliyekuwa aweke msingi wa imani angefanya hivyo akiwa ameunganika na Neno la Mungu baada ya kuweka kipindi cha arobaini cha malipizi cha kutenganishwa na shetani kwa kutimiza sharti hili, angetimiza sharti la malipizi ambalo linakomboa Msingi wa Imani.

Yohana Mbatizaji alikuwa anasimama katika msingi wa kipindi cha arobaini cha kutenganishwa na shetani, kipindi cha miaka mia nne cha maandalizi ya kumpokea Masihi, ambacho kilianza na nabii Malaki. Kupitia maisha yake ya kujinyima, Yohana aliweza kujitenga toka kwa shetani na kuweka msingi wa imani. Yohana aliishi mwituni akila nzige na asali, akijihusisha na kufikiria juu ya nia ya Mungu; hivyo makuhani na watu wa Israel waliyatazama maisha yake ya imani kwa heshima kuu.

**B.  Msingi wa Matendo**

*1. Kiongozi mkuu kwa ajili ya Msingi wa matendo*

Yohana mbatizaji alikuwa pia katika nafasi ya Abeli kwa ajili ya msingi wa matendo, ndiyo kusema, alikuwa kiongozi mkuu katika ujenzi wa msingi wa matendo. Jukumu la Musa lilipelekwa kwa Yoshua, na mwisho kwa manabii akiwemo Eliya, na mwisho kwa Yohana Mbatizaji. Kwa hiyo Yohana Mbatizaji alikuwa anasimama kwenye nafasi ya Musa. Musa alikuwa kiongozi mkuu kwa ajili ya msingi wa imani (katika nafasi ya wazazi) na kiongozi mkuu kwa ajili ya msingi wa matendo (katika nafasi ya mzawa wa pili). Vilevile, Yohana Mbatizaji alikuwa na majukumu mawili ya kuweka msingi wa imani na kusimama katika nafasi ya Abeli kama kiongozi mkuu kwa ajili ya Msingi wa Matendo.




*2. Kuweka Msingi wa Matendo*

Msingi wa kitaifa wa matendo ungekuwa umewekwa na Waisrael kwa upendo na utii kwa Yohana Mbatizajiambaye alikuwa Abeli wao wa taifa. Mungu alishawatayarisha wateule kumwamini kwa dhati Yohana Mbatizaji kama nabii maalum wa Mungu. Kila mmoja alijua ya kuwa nabii mkubwa wa Mungu, sababu walikwisha sikia utabiri wa Malaika juu ya kuzaliwa kwake, miujiza ya baba yake ya kuwa bubu

hekaluni, na miujiza na ishara zilizotokea wakati wa kuzaliwa kwake. Watu wote wa Yudea walimwangalia (mhusudu) kwa shauku kubwa tangu akiwa mtoto. Kama Luka 1:65-66 asemavyo, na hofu iliwaingia majirani wote. Na mambo yote haya yalizungumzwa kwenye eneo lile la milima ya nchi ya Yudea; na kila aliyeyasikia aliyaweka moyoni mwake kwa kusema, "je, mtoto huyu atakueje baadae? Kwani mkono wa Bwana u pamoja naye". Zaidi ya hayo, imani ya Yohana ilikuwa ya kipekee mno kwamba wengi wa makuhani wakuu na watu wa Israel walifikiri kuwa pengine hata anaweza kuwa Masihi (Yoh 1:19; Luka 3:15). Hivyo, watu wa Yudea waliokuwa katika nafasi ya Kaini walimwamini Yohana Mbatizaji na kumfuata kana kwamba alikuwa Masihi mwenyewe, na kwa jinsi hii waliweza kuweka msingi wa kitaifa wa matendo.

**C. Msingi kwa ajili ya Masihi**

Msingi wa Imani na Msingi wa Matendo iliowekwa na Yohana Mbatizaji yote kwa pamoja iliweka msingi kwa ajili ya Masihi. Msingi kwa ajili ya Masihi ni watu waliotayarishwa kumtumikia na kumhudumia Masihi ili kutimiza kusudio lake. Kwa hiyo, kama mwakilishi wa viongozi wote wakuu waliofanya kazi kwa bidii katika muda wote wa historia ya toleo la kuweka msingi kwa ajili ya MasihiYohana Mbatizaji angemtumikia Masihi zaidi ya mtu mwingine yeyote. Zaidi ya hayo, katika msimamo wa msingi huu kwa ajili ya Masihi, Yohana Mbatizaji alipaswa kuwaongoza Waisrael kumwamini Yesu na kumfuata; akiweka hali ambayo ingemwezesha Yesu kutekeleza kwa urahisi toleo la ukombozi. Hata hivyo, ingawa Yohana Mbatizaji alishaanzisha msingi huu na kumshuhudia Yesu kama Masihi hakumfuata Yesu (Yoh. 1:29-34). Zaidi ya hayo, Yohana baadae alikuja kuwa na mashaka kama Yesu alikuwa Masihi (Math. 11:3). Pia, pamoja na kwamba alikuja kama Eliya hakuelewa hili na alilikana (Yoh. 1:21). Kwa sababu watu waliamini utabiri wa Malaki kwamba Eliya atakuja kabla ya Masihi. Kukataa kwa Yohana kwamba

alikuwa Eliya kuliwachanganya watu na hivyo hawakujua wamwamini Yesu au Yohana na hali hiyo ikaziba njia kwa Waisrael kuelekea kwa Yesu. Kwa hiyo msingi kwa ajili ya Masihi ambao Yohana Mbatizaji alianzisha haukufanya kazi kama msingi kwa ajili ya Yesu, lakini ukaziba njia kati ya Yesu na watu wateule.
Msingi kwa ajili ya Masihi ni msingi ambao Mungu atatimiza kabisa dhumuni la toleo lake. Hata hivyo, msingi huu haukuweza kufanikisha kama msingi kwa ajili ya kumtumikia Masihi. Ambaye alipaswa kuwa kitofu cha toleo. Matokeo yake, msingi huu kwa kweli ulishindwa. Pamoja na kuwa Mungu alimtayarisha Yohasna Mbatizaji kwa uangalifu mkubwa kwa ajili ya Yesu, Yohana hakumfuata Yesu, na kwa jinsi hii akapoteza sifa yake ya kuwa mtu wa kihistoria katika nafasi ya Abeli. Na matokeo yake, mlolongo wa kwanza wa kiwango cha dunia nzima wa ukombozi wa Kanaan ukaishia katika kushindwa.

## II. MLOLONGO WA PILI WA UKOMBOZI WA KANAAN KATIKA KIWANGO CHA DUNIA NZIMA

A. Msingi wa Imani

*1. Kiongozi mkuu kwa ajili ya kukomboa msingi wa imani – Yesu arithi jukumu la Yohana Mbatizaji*

Kwa sababu ya ukosefu wa imani wa Yohana Mbatizaji kwa Yesu, Msingi wa Imani katika mlolongo wa kwanza wa ukombozi wa Kanaan katika kiwango cha dunia ulivamiwa na shetani. Masihi alikuja lakini msingi kwa ajili ya Masihi uliporomoka, bila kuacha nafasi kwa Yesu kusimama kama Masihi. Masihi huweza kutokea pale ambapo kuna msingi huru mbali na shambulio la shetani. Kwa hiyo Yesu alisukumizwa kutekeleza masharti ya malipizi ambayo yangeukomboa msingi kwa ajili ya Masihi yeye mwenyewe. Na wakati wakifanya hivyo hakuwa katika mamlaka ya masihi, bali katika ile nafasi ya Yohana Mbatizaji.
Kwa kuwa Yesu alikuwa mwana wa Mungu na alikuwa awe Bwana wa

utukufu, asingeenenda katika njia ya mateso (I Wakor 2:8). Hata hivyo, Yohana Mbatizaji, aliyezaliwa kwa ajili ya kunyoosha njia ya Bwana (Yoh. 1:23; Luka. 1:76), alishindwa kutimiza jukumu lake. Kwa hiyo, Yesu alilazimika kulirithi jukumu la (utume wa Yohana) Yohana Mbatizaji na yeye mwenyewe atayarishe msingi kwa ajili ya ujio wake kama Masihi. Hivyo, katika mlolongo wa pili wa ukombozi wa Kanaan katika kiwango cha dunia, Yesu alikuwa kiongozi mkuu ambaye ilimbidi alipe fidia ya kukomboa Msingi wa Imani.

*2. Sadaka iliyohitajika kwa ajili ya kukomboa Msingi wa Imani*

Kiongozi mkuu anayewajibika kukomboa msingi wa imani angeweza kuweka msingi huu kwa kuwa mmoja na Neno la Mungu baada ya kuweka kwanza kipindi cha msingi-wa arobaini cha kutengana na Shetani. Ili kufanya hili, Yesu alifunga kwa siku arobaini na kushinda (majaribu matatu) vishawishi vitatu toka kwa Shetani. Yesu alitimiza masharti haya siyo kama Masihi, lakini kama mtu anayerithi jukumu la Yohana Mbatizaji. Kwa maneno mengine, alitimiza masharti haya ili kukomboa Msingi wa Imani toka kwenye nafasi ya kiongozi mkuu aliyehusika katika kuweka Msingi kwa Ajili ya Masihi, na si kama Masihi mwenyewe.



Hebu tuangalie sababu za kipindi cha siku arobaini za kufunga kwa Yesu na kusali na kushawishiwa mara tatu. Katika mlolongo wa ukombozi wa kitaifa wa Kanaan chini ya uongozi wa Musa, mwamba uliyoashiria Yesu (I Wakor 10:4) ulishambuliwa na Shetani kwa sababu ya hasira za Musa kwa Waisrael kukosa imani. Uvamizi huu ulibaki kama msingi wa mbali kwa ajili ya kumshambulia Yesu moja kwa moja ambaye ni mwamba wa kweli kama wateule wangekosa imani tena wakati wa Yesu.
Yohana Mbatizaji alikuwa kiongozi mkuu ambaye angesitisha haya yasifanyike-kwa kupigana dhidi ya Shetani ili kujenga msingi wa imani. Hata hivyo, Yohana alishindwa kumwamini Yesu. Pamoja na kutokuwa na imani kwa Yohana Mbatizaji kuwa sababu ya moja kwa moja, Yesu asingeendelea mbele bila shambulio la Shetani la moja kwa moja na akawa mlengwa wa shabaha ya mashambulizi ya Shetani ya kila mara – kwa hiyo, Yesu mwenyewe ilimbidi atimize sharti la malipizi la kipindi cha msingi – wa arobaini kwa ajili ya kutenganishwa toka kwa Shetani kwa kufunga kwa siku arobaini na kulishinda shambulio la Shetani, ambalo lilijidhihirisha katika vishawishi vitatu.

*3. Majaribu matatu ya Shetani.*

Katika Mathayo 4:1-10 tunasoma kwamba Shetani alimjaribu Yesu kwa njia ya majaribu matatu. Dhumuni la awali la Shetani katika kumshambulia Yesu kwa kutumia majaribu haya, haikuwa kwa ajili ya kujaribu hali ya nje au nguvu ya Yesu ya kufanya miujiza, lakini kwa udhati yalilenga kumzuia Yesu katika kutimiza dhumuni lake kama Masihi. Kwa kuwa Masihi anakuja kukomboa dunia iliyokusudiwa wakati wa uumbaji, ambapo haikuweza kuanzishwa kwa sababu ya shetani, kwa mtazamo wa Shetani, kutimizwa kwa dhumuni lake Masihi kungemaanisha kumwangamiza Shetani milele. Kwa kuwa Ufalme wa Mbingu upo katika msingi wa *Kanuni*, na kwa kuwa Adam alishindwa kufuata *"Kanuni",* majaribu ya Shetani yalilenga *"Kanuni",*

na majibu ya Yesu yalipaswa kuwa katika *Kanuni.* Kwa upekee zaidi, dunia ambayo Masihi inabidi aiumbe ni ile iliyokusudiwa wakati wa uumbaji, ambayo ni dunia iliyo chini ya msingi wa kutimiza baraka tatu za Mungu. Hivyo, Yesu ilimlazimu adhihirishe Baraka Tatu, na jaribio la Shetani la kumzuia Yesu kutotimiza dhumuni lake lilikuwa ni kwa njia ya majaribu matatu ambayo msingi wake ulikuwa katika Baraka Tatu.

a. Jaribu la kwanza

Katika jaribu la kwanza, shetani alimtokea Yesu na kusema ".......Kama wewe ni Mwana wa Mungu yaamuru haya mawe yawe vipande vya mkate" (Math. 4:3). Mawe katika milki ya Shetani yaliwakilisha tembe (vipande) za mawe na mwamba ambao ulipigwa mara mbili na Musa. Kwa sababu ya ukosefu wa imani wa wateule Musa alivunja tembe za mawe na kupiga mwamba mara mbili, alitoa uwanja kwa Shetani kudai (kuchukua) mwamba. Mawe ambayo shetani aliyatumia kumjaribia Yesu yaliashiria Yesu mwenyewe kama mwamba wa kweli na tembe ya kweli ya jiwe. (I Wakor. 10:4; Ufu. 2:17).

Pale wateule walipokosa imani, kama walivyokuwa wakati wakiwa mwituni, shetani alikuwa katika nafasi ya kumshambulia Yesu, ambaye alikuwa umwilisho wa Neno ambalo liliashiriwa na tembe za mawe. Yesu ilimbidi ashinde hali hizi. Shetani alijua fika kwamba Yesu alikwenda mbugani kukomboa mwamba, hivyo shetani alimjaribu Yesu abadili mwamba kuwa mkate, sababu Yesu alikuwa na njaa kama Waisrael wasio na imani walivyokuwa wakati wa Musa. Kama Yesu angekosa imani na kuacha dhumuni lake la kukomboa mwamba achague kuamuru jiwe liwe mkate ili kujaza tumbo lake la njaa, hapo Shetani angekuwa amefanikiwa katika kumzuia Masihi asitimize dhumuni lake. Kwa kumuweka Yesu chini ya mamlaka yake, Shetani angepata kulimiliki jiwe milele (daima).

Jibu la Yesu kwa kishawishi hiki lilikuwa "......mtu hataishi kwa mkate

tu ila kwa kila neno linalotoka kwenye kinywa cha Mungu" (Math. 4:4). Hii ina maana kuwa hata kama mwili wa mtu utaishi kwa kula mikate, maisha yake hayatokuwa timilifu. Mtu atakuwa mzima pale tu, kwa kuongezea, ataishi kwa mkate wa uzima, ndiyo kusema kupitia kwa njia ya Kristo, ambaye ni Neno la Mungu lililofanywa mwili (Yoh. 6:35,51). Jibu la Yesu kwa kishawishi cha kwanza cha Shetani humaanisha kuwa hata kama atakuwa na njaa kali, mkate kwa mwili wa maungo si suala halisi. Yesu ilimbidi ashinde kishawishi cha shetani na kuwa mkate wa uzima wa Neno la Mungu, mkate utoao uzima kwa watu wote.

Kwa ushindi huu wa kishawishi cha kwanza, Yesu alitimiza sharti la kuweka tena umwilisho wa kweli wa mawe ambao ulipotelea kwa Shetani katika mwitu kwa sababu ya ukosefu wa imani wa wateule. Kwa maneno mengine, kwa kushinda kishawishi hiki (katika nafasi ya Yohana Mbatizaji), Yesu kiishara alikomboa nafasi ya Masihi, kielelezo cha mtu mkamilifu. Kwa kufanya hili, Yesu aliweka msingi wa kukomboa baraka ya kwanza ya Mungu kwa binadamu, hatua ya kwanza ya kukamilisha dhumuni la Mungu kwa ajili ya uumbaji.

b. Jaribu la pili

Katika jaribu la pili, Shetani alimweka Yesu katika mnara wa Hekalu na kusema, "......kama wewe u Mwana wa Mungu jitupe chini..." (Math. 4:6). Yesu alijitambulisha kama hekalu (Yoh. 2:19-21) na waumini pia wanaitwa mahekalu ya Mungu (I Wakor. 3:16). Waraka wa kwanza kwa Wakorintho 12:27 unatuambia kuwa waumini ni wanachama (viungo) wa mwili wa Yesu. Kwa hiyo, tunaweza kumuelewa Yesu kuwa ni hekalu kuu na waumini ni hekalu matawi. Kwa Shetani kumuweka Yesu mnarani mwa hekalu ina maana kuwa, kama matokeo ya ushindi wa Yesu wa jaribio la kwanza, Shetani ilimbidi atambue mamlaka ya Yesu kama Bwana wa Hekalu. Ombi la Shetani kwa Yesu la kumtupa chini toka juu ya kilele cha hekalu ilikuwa si kujaribu uwezo wa Yesu kufanya maajabu, lakini ilikuwa ni

kumjaribu aachie nafasi yake kama Bwana wa hekalu, kujirusha chini na kuwa kama mtu aliyeanguka, hivyo kukomesha ukombozi wake kwa watu ambao ni hekalu matawi. Kama Shetani alivyomiliki dunia kama Bwana batili baada ya kusababisha anguko la Adam (2 Wakor. 4:4; Yoh. 12:31), Shetani angekuwa bwana wa hekalu katika nafasi ya Yesu, kama Yesu (Adam wa pili) angekubali kishawishi hiki.
Kufikia hatua hii Yesu alisema, "...Usimjaribu Bwana Mungu wako" (Math. 4:7). Shetani ni malaika aliyeanguka; mtu wa kweli lazima awe na mamlaka juu ya malaika. Kwa hiyo, malaika aliyeanguka alikuwa kimaumbile chini ya mamlaka ya Yesu. Ingawa Shetani anaweza kuendesha dunia kwa muda kama bwana wake batili, jaribio lake la kusimama katika nafasi ya bwana wa hekalu lilikuwa ni tendo kinyume cha Kanuni. Shetani, malaika wa anguko, asingethubutu kumjaribu Mungu. Bado alifanya hivyo kwa kumjaribu Yesu, kwani Yesu aliposhinda kishawishi cha kwanza, alikuwa anakomboa nafasi yake kama mtu wa kweli na mtu binafsi, na hivyo alikuwa hekalu la kweli na mwili wa Mungu. Jibu la Yesu lilikuwa karipio kwa Shetani kwa tendo lake lisilo la Kikanuni, na ilimaanisha kuwa Shetani lazima amwache na aache kumjaribu mwakilishi wa Mungu na mwana wa kweli. Yesu alikuwa hekalu kuu na Baba wa Kweli wa watu. Kwa kushinda jaribio la pili, aliweka sharti ambalo litamwezesha kukomboa waumini kama hekalu – matawi, ndiyo kusema kama watoto wake. Kwa ushindi wa jaribu hili, Yesu alijenga msingi wa kukomboa Baraka ya Mungu kwa mtu, hatua ya pili kuelekea kutimiza dhumuni la Mungu kwa ajili ya kuumba.

c. Jaribu la tatu

Katika jaribu la tatu, Shetani alimpeleka Yesu mlimani kileleni na kumwonyesha tawala zote za dunia na utukufu wake. Na hapo alisema......... "vyote hivi nitakupa, kama utaanguka chini na kuniabudu mimi" (Math. 4:9). Ni wazi kwamba hakuna mlima (mrefu) ambapo tawala na falme zote za dunia zinaweza kuonekana, je,

kumpeleka Yesu kwenye mlima huu mrefu kunamaanisha nini?
Kwa sababu ya anguko Adam alipoteza mamlaka yake kama bwana wa uumbaji na akatokea kumilikiwa na Shetani; hivyo kimaumbile Shetani akawa mtawala wa uumbaji badala ya Adam (I Wakor. 8:20). Mungu alimtuma Yesu awe Adam mkamilifu, na kwa hiyo, Bwana wa Uumbaji (Mungu aliweka vyote chini ya Kristo) (I Wakor. 15:27). Shetani alijua hili, na kwa kuwa Yesu alikuwa mshindi katika kishawishi cha kwanza na cha pili, Shetani alilazimika kumweka Yesu katika nafasi ya bwana wa uumbaji.  Hii ndiyo maana ya Yesu kuongozwa mlimani ambapo falme zote za duniani na utukufu wake unaonekana.  Na hivyo, Shetani alimshawishi Yesu kuwa bwana wa uumbaji kama Yesu angemwabudu (Shetani).  Shetani alitaka Adam wa pili kumwangukia kama Adam wa kwanza alivyomwangukia katika Bustani ya Eden.
Yesu alijibu " '.....Mwabudu Bwana Mungu wako, na yeye tu, umtumikie' " (Math. 4:10). Malaika waliumbwa kuwa roho-tumikaji (Waheb. 1:14),  kuabudu na kumtumikia Mungu. Jibu la Yesu linakumbusha kanuni hii kwamba Shetani, malaika wa anguko, lazima amwabudu na kumtumikia Mungu. Kwa maumbile na kanuni hii, Shetani pia lazima amwabudu na kumtumikia Yesu, kwa sababu Yesu alikuwa hekalu la Mungu.
Kwa kushinda majaribio mawili ya kwanza, Yesu alishajenga msingi ambao ungemwezesha yeye kukomboa kwa ajili ya kila mtu Baraka ya Kwanza na ya Pili ya Mungu. Katika msingi huu ilibidi pia akomboe Baraka ya Tatu kwa ajili ya mtu, umiliki wa mtu kwa uumbaji.  Pamoja na kwamba Yesu angepata falme zote za dunia na utukufu wake kama angemwangukia (kumwabudu) Shetani, dhumuni lake kama Masihi lisingetimizwa. Yesu alijibu kuwa pamoja na kwamba Shetani angempa mamlaka juu ya uumbaji, hathubutu kuanguka chini na kumwabudu Shetani, kwani yeye (Yesu) alikuwa hekalu la Mungu. Majibu ya Yesu yalilenga kwenye "kanuni" na hivyo alikuwa mshindi.

Kwa kushinda kishawishi cha tatu, Yesu aliweza kutimiza masharti ya kumkomboa mtu juu ya mamlaka ya uumbaji. Kwa maneno mengine, aliweka msingi kwa ajili ya kumkomboa mtu ili apate Baraka ya Tatu.

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Jaribu la Kwanza** | Jiwe igeuzwe Mkate | **Baraka la Kwanza** | Kukamilishwa kwa mtu binafsi |
| **Jaribu la Pili** | Hekalu | **Baraka la Pili** | Kuzaa watoto wengi |
| **Jaribu la Tatu** | Mafalme za Dunia | **Baraka la Tatu** | Utawala juu ya Vitu vyote |
| **Mathayo 4 : 1-11** | | | |

Hivyo, kwa njia ya kuvumilia funga ya siku arobaini na kushinda vishawishi vitatu vya Shetani, Yesu katika nafasi ya Yohana Mbatizaji, alijenga msingi wa Imani.

**B. Msingi wa Matendo**

Siku arobaini za funga ya Yesu na kusali kwa ajili ya msingi wa imani na kumshinda shetani na vishawishi vyake vilimweka Yesu kuwa kiongozi mkuu na Abeli wa msingi wa kitaifa wa matendo. Matokeo yake kama watu wa Israel, waliokuwa katika nafasi ya Kaini, wangeamini, kutumikia, na kumtii Yesu, ambaye alikuwa katika nafasi ya Abeli alioibadili badala ya Yohana Mbatizaji, msingi wa kitaifa was matendo ungeanzishwa. Msingi huu wa matendo pamoja na msingi wa imani ungejumuisha msingi kwa ajili ya Masihi, na huo ungemwezesha Yesu kuondoka nafasi ya Yohana Mbatizaji kwenda nafasi ya Masihi.




Kama Yesu angeweza kupata msingi huu wa ushindi duniani hapo angeweza kufanikisha kuzaliwa mara ya pili kwa ukamilifu kwa watu na angeweza kwa utimilifu kutimiza dhumuni la Mungu la uumbaji. Kwa hiyo, Yesu alifunua siri za ufalme wa mbingu katika kuongea na kujishuhudia yeye mwenyewe kwa njia ya kutenda miujiza – yote ililenga ili watu wamwamini na kumtii (Yoh. 10:38). Kwa kuwa ilihusu msingi wa matendo kwa ajili ya msingi wa taifa kwa ajili ya Masihi, ilikuwa muhimu sana kwa viongozi wa Uyahudi na watu kumtumikia Yesu na kufuata kusudio lake, kwa kuwa alikuwa katika nafasi ya Abeli. Hata hivyo, viongozi wa watu, kama vile walawi, makuhani na wanasheria walikuwa mstari wa mbele kutomwamini Yesu. Na watu kwa ujumla walitokomea kutomwamini na hata walianza kumsingizia (kumpakazia) Yesu. Na hata toka hatua za mwanzo za huduma ya Yesu, mafarisayo walisema kuwa alikuwa mtenda dhambi (Yoh. 9:16,24) ingawa kwa kweli hakuwa na kosa lolote. Katika matukio mengi watu walichukua mawe na kumrushia Yesu, ingawa alikuwa akiwafundisha ukweli (Yoh. 8:59; 10:31). Yesu wakati mwingine ilibidi ajifiche, kwa sababu ya mipango ya siriya watu ya kutaka kumuua (Yoh. 7:1; 8:40). Wakati huo, Shetani ambaye alikuwa ameshindwa katika (zoezi lake la) vishawishi, aliondoka toka kwa Yesu "mpaka muda mwingine" (Luka 4:13). Kuondoka kwa shetani mpaka muda mwingine iliashiria kuwa shetani

hakuondoka kabisa kabisa na angeweza kurudi tena kwa Yesu. Kwa kuwa Yesu alishinda majaribu ya shetani, shetani hakuweza kumshambulia tena moja kwa moja. Hivyo shetani alikuwa ajaribu kumshambulia kupitia kwa watu, na aliwalenga viongozi waliotokomea katika ukosefu wa imani, na hatimae juhudi zake zilimlenga Yuda Iskarioti. Waraka wa kwanza kwa Wakorintho 2:8 unasema, "Hakuna hata mmoja wa watawala wa zama hizi waliolijua hili, na kama wangejua, wasingemsulibisha Bwana wa utukufu". Mtazamo wa watu kwa Yesu ulizidi hali ya kawaida ya kutomwelewa. Walijenga mtazamo mzito wa kutomwamini kwa kiasi kwamba walimwogopa na wakanuia kwamba aondoshwe na walimsulibisha. Kwa sababu ya ukosefu wa imani ya watu hawa, msingi wa matendo haukujengwa. Kutokana na hali hiyo msingi kwa ajili ya Masihi haukujengwa katika mlolongo wa pili wa ukombozi wa Kanaan katika kiwango cha dunia; kwa matukio hayo, mlolongo wa pili wa ukombozi wa kitaifa katika kiwango cha dunia pia ulishindwa.

## III. MLOLONGO WA TATU WA UKOMBOZI WA KANAAN KATIKA KIWANGO CHA DUNIA NZIMA.

### A. Mlolongo wa kiroho wa ukombozi wa Kanaan katika kiwango cha dunia nzima chini ya Yesu.

Kwa sababu ya ukosefu wa imani wa Yohana Mbatizaji, mlolongo wa kwanza wa ukombozi wa Kanaan katika kiwango cha dunia nzima ukaishia kushindwa. Kilichofuata, Yesu, yeye mwenyewe, alijaribu kuweka msingi kwa ajili ya Masihi. Hata hivyo, kwa sababu watu hawakuweza kumfuata, na hasa kwa kuwa wanafunzi wake walikosa imani, mlolongo wa pili wa ukombozi wa Kanaan katika kiwango cha dunia nzima pia ulishindwa. Kwa hiyo, Yesu ilimpasa alazimike kusulibishwa. Katika Yohana 3:14, Yesu anasema, na kama Musa alivyoinua nyoka nyikani, hivyo lazima na mwana wa mtu atainuliwa juu....." watu waliokuwa pamoja na Musa walipoumwa na nyoka na

kuanza kufa, Mungu alimwongoza Musa kuinua nyoka wa shaba ili kutoa njia ya wokovu kwa watu. Katika namna hiyo hiyo, nyakati za Yesu watu walipokosa imani, Mungu akalazimika kumwomba Yesu apitie njia ya msalabani.

Nini maana ya msalaba? Kama ilivyokwisha kufafanuliwa katika "dhumuni la Masihi", dhumuni la kimasihi la Yesu lilikuwa ni kutimiza toleo la wokovu, ambao ni, kukamilisha Dhumuni la Uumbaji. Mtu aliumbwa akiwa na mwili, na mwili wa kiroho na mtu alianguka katika mwili na roho. Hivyo wokovu lazima uwe wa sehemu zote mbili za mwili na mwili roho ya mtu. Tunaposema tunamwamini kwa dhati Yesu na kumtii hili lina maana kuwa tunatimiza maadili ya kuwa mwili mmoja na yeye. Yesu alisema haya pale alipojilinganisha na mzabibu na waumini kama matawi (Yoh. 15:5), na pale aliposema, "siku hiyo mtajua kuwa mimi ni ndani ya Baba, nanyi ndani yangu na mimi ndani yenu. (Yoh. 14:20). Kwa bahati mbaya, watu hawakumwamini Yesu na hawakuwa mwili mmoja naye (hawakuungana kimwili) matokeo yake, Mungu ilimlazimu kumruhusu shetani auchukue mwili wa Yesu ili kulipia malipizi ya dhambi ya watu kukosa imani. Kwa jinsi hii, Yesu alikufa msalabani.

Kwa kuwa Yesu ndiye mzizi wa uzima wa watu wote, shambulio la shetani la mwili wa Yesu humaanisha kuwa hata watakatifu wanaomwamini Yesu na kuwa mmoja naye hawawezi kuepuka shambulio la miili yao (I Rom. 7:22-23). Haidhuru ni kwa kiwango gani wana imani, miili yao bado ipo katika ukanda wa shambulio la shetani. Hivyo, inawapasa wasali kila mara (I Wathesalonike 5:17), na watoto wao bado wana dhambi ya asili.

Kwa sababu ya usulibisho, watu walipoteza mwili wa maungo wa mwokozi na hivyo walipoteza mtendewa wao wa kimwili katika imani na hawakuweza kupokea wokovu wa kimwili. Kwa hiyo, mlolongo wa tatu wa ukombozi wa Kanaan katika upeo wa dunia yote haukuweza kuanzishwa kama mlolongo wa matendo kwa pande

zote mbili wa mwili na wa roho. Badala yake mlolongo huu wa ukombozi wa Kanaan katika upeo wa dunia yote ulikuwa wa kiroho na ulikuwa chini ya Yesu mfufuka.




*M = Mungu S=Shetani MR = Mtu wa Roho MM = Mtu wa Mwili*

*1. Msingi wa Imani wa Kiroho.*

Kiongozi mkuu mwenye wajibu wa kujenga msingi wa imani wa kiroho alikuwa ni Yesu mfufuka. Katika kutimiza wajibu huo, alisimama katika nafasi ya Yohana Mbatizaji. Ingawa M

ungu alimuacha shetani achukue mwili wa Yesu ili ukosefu wa imani wa mtu ukombolewe, msingi wa wokovu wa kiroho uliwekwa pale Mungu, alipoutumia utii wa dhati wa Yesu kama msingi, akaifufua roho ya Yesu na kumweka katika nafasi ambamo shetani hawezi kumshambulia.

Yesu alisema "vunja hekalu hili, na katika siku tatu nitalijenga tena" (Yoh. 2:19). Kwa hakika alikuwa anazungumzia kufufuka kwake

mwenyewe katika siku tatu. Yesu mfufuka akawa kiongozi mkuu wa kujenga msingi wa imani wa kiroho. Katika kipindi cha siku arobaini baada ya kufufuka kwake, Yesu aliweka msingi wa kiroho wa kutenganishwa na shetani. Hili pia lilijenga Msingi wa imani wa kiroho wa mlolongo wa tatu wa kiroho wa ukombozi wa Kanaan katika upeo wa dunia yote.

Ni wazi Yesu mfufuka hakuwa sawa na wakati alipokuwa anaishi na wanafunzi wake kabla ya usulibisho. Tayari alishakuwa nafsi-roho ambaye alipita mida na fursa na asingeonekana kwa macho ya kawaida ya maungo, (Luka 24:16). Kwa mfano: wakati fulani alitokeza ghafla katika chumba kilichofungwa ambamo wanafunzi wake walikutana (Yoh. 20:19) na katika tukio jingine alitokeza pwani ya bahari ya Tiberia na hakuweza kutambulika na wanafunzi wake (Yoh. 21:1-4); katika tukio jingine, ghafla aliwatokea wanafunzi wawili wakielekea Emmau na akaondoka nao kwa mwendo kitambo bila kumtambua (Lk. 24:15-16). Kama jambo la hakika, Maria, ambaye alikuwa wa kwanza kukutana na Yesu mfufuka hakuweza kumtambua (Yoh. 20:14). Wakati wa kipindi cha siku – arobaini duniani baada ya kufufuka, Yesu aliwatokea wanafunzi wake dhidi ya mida muda na fursa, na hivyo kuweka msingi wa imani wa kiroho.

*2. Msingi wa matendo wa kiroho*

Kwa kuweka msingi wa imani, katika msingi wa kiongozi mkuu kwa ajili ya kuweka msingi wa kiroho wa matendo, hii ndiyo kusema, pia alipata msingi wa nguvu za kiroho, hii ndiyo kusema pia, alipata nafasi ya kiroho ya Abeli.

Mungu hakuweza tena kuendelea kujihusisha moja kwa moja na wayahudi, kwani walimsaliti Yesu; hivyo alihitaji Israel mpya; hii ndiyo “Israel ya pili” ambayo itamfuata Yesu mfufuka kwa imani ya dhati. Israel mpya, katika nafasi ya Kaini, ilikuwa iamini na kumtii Yesu, Abeli wa kiroho, na hivyo kujenga msingi wa kiroho wa matendo. Yesu

alifanya juhudi kubwa ili kujenga msingi wa kiroho wa matendo, ambao ungejenga wateule wafufuka wapya ambao wangeunganika naye katika imani.




Matendo 1:3 huongea juu ya wanafunzi wa Yesu, kwa kusema kwao alijionyesha yu hai baada ya kuteswa kwake, kwa dalili nyingi, aliwatokea katika kipindi cha siku arobaini, na kuzungumzia juu ya ufalme wa Mungu. Yesu aliwakusanya wanafunzi wake, waliokuwa wametawanyika baada ya kupoteza imani, na kutokea mara nyingi mfululizo, akiwafundisha kuwa na imani ya dhati kwake kama Masihi.

> Na kwa kuanzia kwa Musa na manabii, aliwaelezea maandiko yote yanayomhusu. (Lk. 24:27). Na Yesu alikuja na kusema nao, “mamlaka yote mbinguni na duniani nimepewa mimi” enendeni basi na mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi wangu mkiwabatiza kwa jina la Baba, na la Mwana na la Roho Mtakatifu, mkiwafundisha kuzingatia yale niliyowaamuru; na

> tazama nipo pamoja nanyi kila wakati, mpaka mwisho wa zama. (Math. 28:18-20).
>
> Wakati akiwa anakaa nao aliwaasa wasiondoke Yerusalem lakini wasubiri ahadi ya Baba, ambayo, alisema, “mlisikia toka kwangu, kwamba Yohana alibatiza kwa maji, lakini kabla ya siku nyingi mtabatizwa kwa Roho Mtakatifu”. (Matendo. 1:4 -5)

Yesu alifanya miujiza mingi (mf. Yoh. 20:19; 21:6); alimtia imani Tomasi mkosa imani (Yoh. 20:26-29); alimfanya Petro aahidi ufuasi wa dhati kwake (Yoh. 21:15-18); na aliwafundisha wanafunzi wake kuwa mizizi ya Israel mpya. Wanafunzi walitoa maisha yao kuamini, kutumikia, na kumfuata Yesu mfufuka, tofauti na njia ya zamani ambayo walimwamini kwa udhaifu. Hivyo, waliweza kuweka msingi wa kiroho wa matendo.

*3. Msingi wa kiroho kwa ajili ya Masihi*

Msingi kwa ajili ya Masihi ni ule hasa msingi ambao kwake Masihi anaweza kuokoa namna zote mbili kimwili na kiroho. Lakini Yesu mfufuka aliyekuwa akichukua jukumu la Yohana Mbatizaji wa kiroho angeweza kukomboa tu msingi wa kiroho kwa ajili ya Masihi (Msingi kwa ajili ya Masihi katika dunia ya kiroho)kwanza akiweka msingi wa kiroho wa imani (Msingi wa Imani katika duinia ya kiroho) na baadae msingi wa kiroho wa matendo (msingi wa matendo katika dunia ya kiroho). Jukumu la awali la Yesu lilikuwa si kuchukua utume wa Yohana Mbatizaji. Hivyo, mara alipoweka msingi wa kiroho kwa ajili ya Masihi, alisimama kama Masihi wa kiroho.

Hakuna masharti ya madai toka kwa shetani katika ukanda wa ufufuo ambao Yesu aliuweka (kulingana na kanuni ya ukombozi kwa njia ya malipizi) kwa kumwachia shetani achukue maisha yake. Hivyo, msingi wa imani ambao Yesu mfufuka aliuweka katika upande wa kiroho hauharibiki kwa uvamizi wa shetani. Msingi wa kiroho wa matendo

unawekwa kwa kumwamini Yesu katika maisha ya mtu mwenyewe kwa hiyo haudhuriki kwa shambulio la kiroho la shetani, na msingi wa kiroho kwa ajili ya Masihi ni eneo ambalo shetani hawezi kuliingilia.

Jukumu muhimu sana la Masihi ni dhima (wajibu) wa Baba wa kweli. Yesu mfufuka alikuwa Baba wa kweli wa kiroho kwa kumkomboa Roho Mtakatifu. Kuja kwa Roho Mtakatifu kulikowekwa katika kumbukumbu ya matendo ni ujio wa Mama wa kweli wa kiroho. Yesu mfufuka, kama Baba wa kweli wa kiroho, na Roho Mtakatifu, kama Mama wa kweli wa kiroho, wanafanya kazi pamoja ili kuwazaa mara ya pili kiroho wote waaminio. Kwa hiyo yeyote anayemwamini Yesu na Roho Mtakatifu, ambao ni wazawa wa kweli wa kiroho, na akapandikizwa kiroho kwao anasimama katika msingi wa kiroho kwa ajili ya Masihi na atakuwa na wokovu wa kiroho (Yoh. 3:16).

Wokovu wa kiroho una maana waumini wanakombolewa tu kama watoto wa kiroho wa Mungu, kupitia kwa wazazi wa kiroho, hii ndiyo kusema, ni Kanaan ya kiroho tu imekombolewa. Kwa hiyo, wakristu wanaweza kupokea faida ya kuanzishwa kwa Kanaan ya kiroho, na bado wana miili inayoweza kushambuliwa na shetani, kama mwili wa Yesu, mpatanishi wa watu, mwili wake ulishambuliwa na shetani. Matokeo yake, Dhambi ya Asili bado ipo ndani mwa mtu (Warumi. 7:25).

Masihi lazima arudi tena ili atimize wokovu na kukomboa kanaan ya umbo ambapo mtu anaweza kukombolewa kwa namna zote mbili kiroho na kimwili kama watoto wa kweli wa Mungu, Waisrael wakiongozwa na Musa, kiroho waliingia kanaan, kizazi cha pili cha Waisrael, kilichoongozwa na Yoshua, kimwili waliingia Kanaan ya kitaifa. Hili limefafanuliwa katika “Musa katika Toleo la Ukombozi”. Vile vile, wakristo wakiongozwa na Yesu, walianzisha Kanaan ya kiroho katika upeo wa dunia, na wakati wa ujio wa pili, Masihi kama

Yoshua atawaongoza wakristo kujenga Kanaan ya  kimwili katika upeo wa dunia.

**B. Mlolongo wa kimwili katika upeo wa dunia wa kuikomboa Kanaan chini ya Bwana wa ujio wa pili.**

Kama, wakati wa ujio wa pili, wale wenye jukumu la Yohana Mbatizaji watashindwa kutimiza majukumu yao, Bwana wa ujio wa pili yeye mwenyewe atachukua dhima ya Yohana Mbatizaji na kuweka msingi wa imani wa awamu ya tatu ya kimwili ya mlolongo wa Kanaan upeo wa dunia. Haidhuru njia hiyo itakuwa ngumu kiasi gani ambayo atapitia Bwana wa ujio wa pili, watu wanyenyekevu watakusanyika kwake, wakimwamini na kumtumikia, wakijenga msingi wa matendo katika awamu ya kimwili ya tatu upeo wa dunia kwa Kanaan.

Bwana wa ujio wa pili lazima aje ili awakomboe watu wote na kuelekea ubini wa moja kwa moja wa Mungu, kama watoto wa Mungu. Vile vile, lazima azaliwe duniani, katika mwili kama Yesu alivyokuwa.  Lazima akomboe, kwa njia ya malipizi, mlolongo wa kutokwa machozi ambao Yesu ilimlazimu kuupitia, na katika kianzio cha msingi wa matendo kwa ajili ya Masihi, lazima apandikize watu wote kiroho na kimwili. Watu hatimae watakuwa katika ubini (nasaba) wa moja kwa moja na Mungu, kwa kuondoa dhambi ya asili kupitia kwa Bwana wa ujio wa pili.

Awamu ya kiroho ya mlolongo wa tatu upeo wa dunia kuelekea Kanaan, ambao ulianza na msingi wa kiroho kwa ajili ya Masihi, umepanua eneo lake kufikia kiwango cha dunia yote katika miaka elfu mbili ya mwisho iliopita.  Kama vile Yoshua alivyorithi utume wa Musa na kumaliza mlolongo wa




kitaifa kuingia kanaan, vivyo hivyo Bwana wa ujio wa pili atakamilisha ujenzi wa Ufalme wa Mbinguni kwa kukamilisha katika kiwango cha mwili, mlolongo wa tatu upeo wa dunia kuingia kanaan ambao ulianza chini ya Yesu.

Kama vile ambavyo Yesu alipitia njia ya mateso ya ukombozi wa kiroho ikiwa ni matokeo ya kukosa imani watu wateule wa Israel, vivyo hivyo Bwana wa ujio wa pili ataonja mateso ya aina hiyo hiyo kama na ikiwa Israel ya pili, wakristu, wataanguka katika kukosa imani. Na kama vile Yesu alivyoiacha Israel ya kwanza na kuanza mlolongo mpya, chini ya wakristu kama Israel ya pili, hivyo pia, kama Bwana wa ujio wa pili atakataliwa na wakristu, ataanza Israel ya tatu.

## CHAPTER 14 DISPENSATIONAL TIME - IDENTITY

## SURA YA 14 TOLEO LA UTAMBUZI WA NYAKATI

### I. MASHARTI YA MALIPIZI NA TOLEO LA UTAMBUZI WA NYAKATI

Dhumuni la Toleo la Ukombozi, ambalo ni kukamilisha dhumuni la Uumbaji, linatimizwa kupitia kwa Masihi. Jukumu la mtu wa anguko ni kutayarisha msingi muhimu kwa ajili ya ujio wa Masihi, yaani, msingi kwa ajili ya Masihi. Wajibu huu unahusisha kutekeleza masharti muhimu ya malipizi ili kukomboa msingi wa imani na msingi wa matendo.

Hutokea nini pale kiongozi mkuu wa Toleo ashindwapo kutimiza wajibu wake wa kutekeleza masharti ya malipizi? Lengo la Toleo la Ukombozi lilizaliwa katika akili ya Mungu, ambaye ni wa dhati, na kwa hiyo lengo la Toleo nalo pia ni la dhati na lazima litimizwe (Is. 48:11). Kwa hiyo, kama kiongozi mkuu atashindwa, Mungu huchagua mtu mwingine ili kuendeleza kusudio lake, ingawa hili hurefusha historia ya Toleo. Pale Mungu anapochagua kiongozi mkuu mpya, hali, matukio, na watu wanaomzunguka kiongozi mkuu mpya watakuwa sawia na wale waliokuwepo wakati Mungu anamchagua aliyemtangulia. Hata kama kuna miaka elfu mbili au nne ya mapengo hayo katika historia ya ukombozi, hali sawia matokeo na watu watatokea. Kutokea huku kwa hali zilizopita, matukio na watu huitwa Toleo la Utambuzi wa Nyakati. Tukio la Toleo la Utambuzi wa Nyakati hutokea kulingana na Toleo la Mungu la Ukombozi kupitia malipizi.

Ni vigezo vipi viumbavyo utambuzi wa nyakati katika historia ya Toleo? Jibu lake limo katika juhudi za Mungu na mtu kukomboa msingi kwa ajili ya Masihi kupitia mchakato wa malipizi. Kwa maneno mengine, yaliyomo katika kipindi cha utambuzi wa nyakati kuna kiongozi mkuu, kipindi cha muda (majira), sadaka inayohitajika, matendo ambayo kwayo kiongozi mkuu huanzisha msingi wa




imani, na mlolongo ambao kwake kiongozi mkuu hutekeleza sharti la malipizi la kuondoa hulka ya anguko na huanzisha msingi wa matendo.

Peo na yaliyomo katika msingi kwa ajili ya Masihi yameongezeka toka yale ya upeo wa familia mpaka yale ya taifa na upeo wa dunia yote. Ingawa Toleo la Ukombozi linaweza kurefushwa kwa sababu ya kushindwa kwa binadamu kutekeleza wajibu wake, Mungu hukomboa vyote vilivyopotezwa kwa kupanua upeo wake wa shughuli.  Kwa mfano, pale wateule waliokuwa na jukumu la msingi wa kitaifa kwa ajili ya Masihi waliposhindwa, Mungu hakuchagua taifa jingine kwa ajili ya toleo la kitaifa. Badala yake, Mungu alianza toleo la dunia yote.  Kama toleo la dunia litakamilishwa kwa mafanikio, kupitia toleo hilo, toleo la kitaifa litakombolewa wakati huo huo.




**II.   MGAWANYO WA ZAMA ZA TOLEO, KATIKA MSINGI WA UTAMBUZI WA NYAKATI**

**A.  Mgawanyo wa Zama**

Familia ya Abraham ilijenga msingi wa kifamilia kwa ajili ya Masihi. Kwa mara ya kwanza katika historia msingi wa ushindi ambao Mungu angeweza kufanya kazi duniani ulianzishwa. Hivyo, kwa familia ya Abraham Mungu angeweza kuanza toleo la Ukombozi. Halafu nini maana ya historia kabla ya wakati wa Abraham?

Kwa kuwa Abraham alishindwa katika sadaka ya kwanza ya kuteketeza, historia mpaka msingi wa ushindi wa Abraham ilikuwa imechukuliwa na shetani. Kwa hiyo, kipindi hicho cha historia kikawa tu cha msingi wa Toleo la ukombozi, wazawa wa Abraham wakawa watu wateule wa kutekeleza matakwa ya Mungu. Tukiangalia nyuma, kipindi toka Adam mpaka Abraham ni kipindi ambacho Mungu alianzisha msingi kwa ajili ya Toleo la Ukombozi na hivyo linaweza kuitwa zama za toleo la msingi kwa ajili ya ukombozi kupitia malipizi. Ukiangalia kwa mtazamo wa toleo la utambuzi wa nyakati ilikuwa ni zama za ishara za utambuzi wa nyakati.  Katika zama hizo, Mungu alipania kujenga msingi wa kifamilia kwa ajili ya Masihi.



Muda toka familia ya Abraham hadi Yesu ulikuwa ni zama za toleo la Mungu kukomboa kwa njia ya malipizi zama za toleo lililopotezwa la msingi kwa ajili ya ukombozi. Kipindi hiki kinaitwa zama za Toleo la Ukombozi. Kutokana na mtazamo wa toleo la utambuzi wa nyakati, zilikuwa ni zama za taswira za utambuzi wa nyakati.  Katika zama hizi, toleo la Mungu lilikuwa lijenge msingi wa kitaifa kwa ajili ya Masihi.




Yesu alikuja kutimiza toleo la ukombozi. Kama viongozi wa Waisrael wasio na walio na dini wakati wa siku za Yesu wangemfuata, toleo la Mungu la ukombozi lingekuwa limetimizwa kabisa wakati huo. Historia ya dhambi ingeisha, na historia mpya, chini ya Mungu, ingeanza, ikikamilisha maadili kwa ajili ya Uumbaji.  Mbingu mpya na nchi mpya ambayo Biblia huzungumzia vingeanzishwa wakati huo. Hata hivyo, kwa sababu ya ukosefu wa imani ya watu wateule kwa Yesu, alisulibishwa na toleo la Mungu halikuweza kuhitimishwa.  Yesu hakuweza kufanya lolote isipokuwa kuahidi kurudi tena, na wakristo iliwabidi wasubiri kwa matumaini ya ujio wa pili.

Vile vile, tangu wakati wa kusulibishwa kwa Yesu mpaka Ujio wa Pili, umekuwa ni muda wa zama za toleo la Mungu la kukomboa toleo la zama za toleo la ukombozi ambalo halikumalizwa kwa namna ya kulirefusha.  Hivyo, zama hizi zinaitwa zama za toleo la urefushwaji wa ukombozi. Kutokana na mtazamo wa toleo la utambuzi wa nyakati, hizi ni zama za matendo za utambuzi wa nyakati. Katika zama hizi, Mungu alilenga kuanzisha msingi wa upeo wa dunia nzima kwa ajili ya Masihi.



**B. Mifano sambamba miongoni mwa matoleo ya zama**

Kama ilivyoelezwa mwanzoni mwa sura hii, zama tatu za toleo zote zimeelekezwa kwenye dhumuni la kujenga msingi kwa ajili ya Masihi. Matokeo yake, masharti sawia, matukio, watu hutokea tena kwenye mlolongo wa historia ya watu, na zama tatu za toleo huonyesha moja kwa moja mifano sambamba au utambuzi wa nyakati miongoni mwao (nyakati).

Mifano sambamba kati ya taswira za utambuzi wa nyakati (Toka kwa Abraham hadi kwa Yesu) na utambuzi wa nyakati za matendo  (toka kwa Yesu hadi ujio wa pili) litaongelewa hapa, wakati mifano sambamba ya zama za utambuzi za nyakati kiishara (Adam mpaka Abraham) utaongelewa zaidi katika hatua ya juu zaidi katika kitabu cha *Mchanganuo wa Kanuni Daraja la Tano*.




Katika Zama za Toleo la Ukombozi, Taifa kiongozi lenye wajibu wa toleo la Mungu lilikuwa ni taifa teule la Israel. Historia kiongozi (kuu) bila shaka, ilikuwa ni historia ya taifa la Israel, chini ya utamaduni wa Uyahudi. Kumbukumbu fafanuzi ya historia hiyo imo katika Agano la Kale.
Katika zama za Toleo la Kurefushwa kwa Ukombozi, watu viongozi wenye wajibu wa toleo la Mungu, halikuwa taifa la Israel, ila wale walioamini na kumfuata Yesu, Wakristo. Kwa kuwa Wakristo walirithi jukumu la Israel, wakawa Israel ya Pili.  Matokeo yake, historia ya Ukristo inatoa historia  kiongozi yenye maelezo ya Zama za Toleo la Urefushwaji wa Ukombozi.
Zama za Toleo la Ukombozi zimegawanywa katika vipindi vidogo sita viitwavyo: Utumwa nchini Misri, Wanasheria (Waamuzi); Ufalme wenye Umoja; Falme Zilizogawanyika za Kaskazini na Kusini; Utumwa na Kurudi kwa Wayahudi; Matayarisho ya Masihi.
Zama za Toleo la Urefushwaji wa Ukombozi pia limegawanyika katika vipindi vidogo sita vya aina kama ya mpangilio hapo nyuma; ukitoa vipindi vidogo sita, viitwavyo: Shutuma katika Himaya ya Warumi, Makanisa ya Wakristo chini ya Mfumo wa Wazee; Ufalme wa Kikristu; Falme zilizogawanyika za Mashariki na Magharibi; Kutekwa kwa Upapa na Kurudi; na Maandalizi ya Ujio wa Pili wa Masihi.




Tofauti ya takriban miaka elfu mbili si tofauti hiyo tu kati ya historia za zama za Toleo la Ukombozi na Zama za Urefushwaji wa Ukombozi – tofauti katika historia za nyuma za taifa, mazingira, na mapokeo ya kiutamaduni pia vinahusishwa. Hata hivyo, kila kipindi cha vipindi vidogo sita katika zama za ukombozi ni kipindi cha utambuzi wa nyakati kulingana na ushabiiano wa vipindi katika zama za urefushaji wa ukombozi.

Kila utambuzi wa nyakati maelezo yake yako hapa chini. Mashabihiano muhimu huonyesha kuwa historia ya binadamu ilikuwa inaendelea kulingana na toleo la Mungu na lililo na msisitizo makini kwa ukombozi.

*1. Kipindi cha utumwa nchini Misri na kipindi cha shutuma katika himaya ya Warumi*

Kipindi cha utumwa nchini Misri kilianza kama matokeo ya kushindwa kwa Abraham kutoa sadaka. Ni kipindi ambacho watoto kumi na mbili wa Yakobo na wanaukoo – sabini waliingia Misri ambayo iliashiria dunia ya Shetani ambamo wazawa wao waliteswa sana na Wamisri.  Kipindi cha Shutuma katika Himaya ya Warumi kilianza kama matokeo ya kushindwa Waisrael kumwamini Yesu. Hiki ni

**I.  Kipindi cha Utumwa Nchini Misri (miaka 400)**

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Yakobo**<br><br>Watoto wanaume : 12<br><br>Wanaukoo : 70 | Sabbath<br><br>Kutahiri<br><br>Sadaka | Baada ya miaka 400, wahuingia Kanan | Sheria ya Musa |

**I. Kipindi cha Shutuma katika Himaya ya Warumi (miaka 400)** 0 - 392 B.K

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Yesu**<br><br>Wanafunzi 12<br><br>Wafuasi 70 | Sabato<br><br>Ushirika (Komunio Takatifu) na Ubatizo<br><br>Ushahidi | 392 Baada ya Kristo, Ukristo inatangazwa Dini la Taifa | Injili |

kipindi ambacho mitume kumi na mbili wa Yesu, wanafunzi sabini, na wakristo wa awali walikumbwa na shutuma kali katika Himaya ya Warumi, ambayo iliwakilisha dunia ya kishetani.

Wakati wa kipindi cha miaka mia nne ya kukandamizwa nchini Misri, wateule wa Israel walichunga nafsi zao kama watu waaminifu kwa Mungu katikati ya mateso yao kwa kutimiza ibada ya kutairi, sadaka za kuteketeza, na kushika sabato. Vile vile, kwa takriban miaka mia nne wakati wa kipindi cha shutuma katika himaya ya warumi, wakristo walichunga nafsi zao kama waumini wa Mungu kwa kushika sabato, kwa kuishi maisha ya kujitoa mhanga, na kufanya sadaka za masakramenti ya komunio takatifu na ubatizo.

Baada ya kipindi cha utumwa nchini Misri cha miaka mia nne, Mungu alimchagua Musa kumtiisha Firauni na kuwaongoza waisrael kuelekea mazingira mapya, nchi ya Kanaan. Vile vile, ukristo, uliokuwa unashutumiwa ulipata kutambulika kisheria mwaka 313 B.K na Himaya ya Warumi ilitangaza kuwa dola ya dini ya Kikristo mnamo 392 B.K (baada ya Kristo). Kwa njia hii, wakristo walikuja kukombolewa toka dunia ya Shetani kwenda Kanaan ya kiroho.

Baada ya utumwa nchini Misri, Musa alipokea Amri Kumi Mlimani Sinai, akiweka kiini cha Agano la Kale. Kwa kuheshimu tembe za mawe, Hema, na sanduku la agano, wateule wa Israel ya kwanza walijitayarisha wenyewe kumpokea Masihi. Vile vile, kuelekea mwisho wa kipindi cha shutuma katika Himaya ya Warumi, wateule wa Israel ya Pili, walikusanya maneno ya Yesu na maandishi ya mitume na kuweka Agano Jipya na makanisa yaliyoongozwa chini ya Neno, na kwa njia hiyo kuweka msingi wa muhimu kwa ajili ya Ujio wa Pili.

*2. Kipindi cha Wanasheria (Waamuzi) na Kipindi cha Makanisa ya Kikristo chini ya Mfumo wa Wazee*

Wakati wa kipindi cha miaka mia nne baada ya Yoshua na Kaleb kuwaongoza waisrael kuingia Kanaan, Taifa la Israel liliongozwa na wanasheria. Hawa wanasheria walichukua kila mmoja majukumu mengi ya kuwa Nabii, Kuhani Mkuu, na Mfalme.Wakati wa Kipindi cha Makanisa ya Kikristo chini ya Mfumo wa Wazee, Wakristo waliongozwa na Wazee, ambao kazi zao, kulingana na msimamo wa Toleo la Ukombozi, ziliendana na kushabihiana na zile za Wanasheria/Waamuzi.

**II. Kipindi cha Waamuzi (miaka 400)**

| | |
|---|---|
| Waamuzi — Nabii / Kuhani Mkuu / Mfalme | *Mfumo wa Kibakila* |

**Maskani**

**II.Kipindi cha Mfumo wa Wazee (miaka 400)** 392 - 800 B.K.

| | |
|---|---|
| Wazee — Nabii<br>Wazee — Kuhani Mkuu<br>Wazee — Mfalme | *Mfumo wa Kibakila* |

**Makanisa**

Katika Kipindi hiki cha Waamuzi, mfumo wa kikabila uliibuka nchini Israel, chini ya wanasheria na katika kigezo cha ardhi mpya iliyogawiwa kwa kila kabila. Vilevile, baada ya ukombozi wa Ukristo tokana na shutuma katika Himaya ya Warumi, injili ilisambazwa na makabila ya Kijerumani ambayo yalisogea Ulaya ya magharibi kwa sababu ya uvamizi wa karne ya nne wa WahunI kutoka Mongolia. Huko katika nchi mpya ya Ulaya magharibi, mfumo wa Kibakila uliibuka.

*3. Kipindi cha Ufalme Ulioungana na Kipindi cha Ufalme wa Kikristo*.

Kwa kuanza na mwanzo wa Muungano wa Ufalme wa Israel, kipindi ambacho Wanasheria waliongoza Israel kiliisha na jukumu la Wanasheria liligawanywa miongoni mwa manabii, kuhani mkuu, na mfalme. Vilevile, kwa kuanza kwa Kipindi cha Ufalme wa Kikristo, Kipindi cha Wazee

**III. Muungano wa Ufalme (miaka 120)**

| | |
|---|---|
| - Nabii<br>- Kuhani Mkuu<br>- Mfalme | *Samuel*<br>↓<br>*Saul*<br>*(Mfalme)* |

**Ufalme wa Kikristo (miaka 120)**

| | |
|---|---|
| - Watawa<br>- Papa<br>- Mfalme | *Papa Leo III*<br>↓<br>*Charlemagne*<br>*(Mfalme wa Wafaransa na Warumi)* |

kuongoza Israel ya Pili kikaisha, na majukumu ya Wazee yaligawanywa miongoni mwa watawa, mapapa na mfalme. Kama ufalme ulioungana wa Israel ulivyoanza wakati nabii Samweli alipompaka mafuta mfalme Sauli kama mfalme wa kwanza, kulingana na amri ya Mungu kile ambacho kingetokea katika toleo la Mungu kama himaya ya muungano wa kikristo kilianza pale Papa Leo III alipomtawaza Charlemagne mfalme wa Wafaransa na Warumi.

*4. Kipindi cha Falme Zilizogawanyika za Kaskazini na Kusini; na Kipindi cha Falme Zilizogawanyika za Mashariki na Magharibi.*

Umoja wa Ufalme za Israel, ambao ulianza na Mfalme Sauli, uliendelea chini ya Mfalme Daudi na Mfalme Suleimani (Solomon); baadae uligawanyika katika Ufalme wa Kaskazini mwa Israel, ukijengwa na makabila kumi katika nafasi ya Kaini, na Ufalme wa Kusini wa Yuda uliojengwa na makabila mawili, katika nafasi ya Abeli.

**IV. Mafalme Zilizogawanywa za Kaskazini na Kusini (miaka 400)**




**Mafalme Zilizogawanywa za Mashariki na Magharibi**

**(miaka 400)** *919 - 1309 Baada ya Kristo (BK)*




Ufalme wa Kikristo, ambao ulianza na Charlemagne nao uligawanywa, lakini katika sehemu tatu Ufalme wa Franka Mashariki (ufalme wa Louis Mjeremani), na Ufalme wa Franka Magharibi (ufalme wa Charles Kipara), na Ufalme wa Kati (Ufalme wa Lothair) kwa sababu ya ugomvi miongoni mwa wajukuu watatu wa Charlemagne. Hata hivyo, mara baada ya kipindi cha falme zilizogawanyika kuanza chini ya Henry wa I mwaka 919, Italia ikaja kuwa chini ya utawala wa Franka Mashariki, na hivyo kutengana kulikuja kati ya falme za Frank Mashariki, au himaya ya Rumi Takatifu, na Frank Magharibi, au Ufalme wa Ufaransa, pamoja na ufalme wa mashariki katika nafasi ya Abeli na ufalme wa magharibi katika nafasi ya Kaini.

*5. Kipindi cha kutekwa Wayahudi na kurudi na kipindi cha kutekwa na kurudi kwa Upapa*

Ufalme wa kaskazini wa Israel ulianza kukosa kwake imani mara tu baada ya ufalme wa mshikamano ulipogawanyika na uliteketea kama matokeo ya kutoamini kwake (takriban 722 K.K). Ufalme wa kusini wa Yuda pia ulikosa imani. Hivyo falme hizi zilikosa kuunganika chini ya maadili ya hekalu yaliyowekwa na Mungu, na kwa hiyo wakashindwa kuanzisha msingi kwa ajili ya Masihi. Kwa hiyo, Mungu aliruhusu wachukuliwe utumwani na kuteseka mikononi mwa waasiria na wababiloni, hii ina maana kuwa, mikononi mwa dunia ya shetani. Kusini, Babiloni ilidhibiti kuanzia mwaka 608 K.K, na ilianza na Daniel na kundi dogo la watawala (605 K.K), kulianza milolongo ya kuhamisha waebrania kwenda Babiloni, ambako walikaa kwa takriban miaka sabini (Dan. 1:1-6; Yer. 25:11-12; 29:10; 39:1-10; II Wafalme 24,25). Mwaka 539 K.K, Ajemi iliiteka Babiloni na mfalme Siras alitoa amri (azimio) la kuwaachia huru wayahudi ambao walirudi nchini kwao katika makundi (misafara) mitatu katika kipindi cha miaka tisini na nne (iliyoishia mwaka 444 K.K). Hata hivyo, mpaka mageuzi yaliyoongozwa

na Malaki, hawakuweza kujiweka kama taifa ambalo lilisimamiwa na sheria na hawakuweka mila na desturi zilizokubaliwa na Mungu. Kwa mtazamo wa toleo, ni pale tu ambapo wangebadili matendo yao kulingana na sheria ndipo wangekubalika kuwa wamerudi katika nafasi yao kama watu wa Mungu. Kukamilika kwa kipindi cha kurudi kulizindua kipindi cha Matayarisho kwa ajili ya Masihi.

Toka mwisho wa kipindi cha Ufalme wa Kikristo, ambacho kilikuwa kitayarishe msingi wa dunia yote kwa ajili ya Ujio wa Pili, mpaka pale upapa ulipoanguka katika uozo mkubwa, Mungu alituma ishara nyingi – kama vile kushindwa katika Krusedi – ili kuwafanya mapapa na makuhani kutubu – lakini hawakutubu, badala yake, kwa kupata nguvu hatua kwa hatua kwa nguvu za kifalme, kulitokea mtafaruku kati ya mapapa na wafalme. Papa Bonifasi wa nane (VIII) alifarakana na mfalme wa Ufaransa, Filipo wa nne (IV), na hata alifungwa kwa muda na huyo mfalme. Mnamo 1309, Klement V, ambaye kuchaguliwa kwake kama Papa wa kwanza mfaransa kulipangwa na Filipo IV, alihamisha upapa kutoka Roma kwenda Avignon Ufaransa ya kusini. Kule mapapa waliofuata walikaa kwa takriban miaka sabini chini ya uchagizo wa wafalme wa Ufaransa. Mwaka 1377, Papa Gregori wa XI alirudisha upapa huko Roma, na hili lilizindua kipindi cha kurudi kutoka ugenini. Kwa kipindi cha miaka mia moja na arobaini kulikuwepo mitafaruku mingi, wakati mwingine kulikuwepo na mapapa watatu wakiongoza kwa wakati mmoja. Kuelekea mwisho wa kipindi hiki papa huko Roma alishapata udhibiti wa dhati katika kanisa.

*6. Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Masihi na kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili*

Baada ya kurudi kutoka mateka katika Babiloni, Waisrael walijenga tena hekalu ambalo lilikuwa limevunjwa, na kwa ombi la nabii Malaki walitubu dhambi zao zilizopita za kuabudu miungu ughaibuni. Wakiongozwa na Sheria, walichochea harakati za mabadiliko na mwanzo wa kipindi cha miaka mia nne ya matayarisho kwa ajili ya Ujio wa Pili.

**Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Masihi (miaka 400)**

- Harakati za Mabadiliko / Malaki

**Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili (miaka 400) 1517 - 1918 BK**

- Harakati za Mabadiliko / Luther

Baada ya Papa kurudi Roma, harakati za mabadiliko zilizoamshwa na Mungu zilianza na makanisa ya kikristo yaliweka msingi wa imani wa upeo wa dunia yote kwa ajili ya ujio wa pili. Kupitia mageuzi, mawingu meusi ya zama za kati yalipenywa, na yakiamshwa na imani mpya na ya dhati, shirikisho la kueneza injili duniani kote likainuka. Kipindi cha miaka mia nne ambacho kilianza na mabadiliko (mageuzi) kinaitwa Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili.

Zama za Agano la Kale ni zama ambazo imani kwa Mungu ilionyeshwa kwa nje kwa kuitikia kutoa sadaka na kuzingatia sheria. Kwa hiyo, ili kukomboa historia yote tangu Abraham katika kipindi cha maandalizi ya Masihi, Israel ya kwanza ililazimika kuteswa na mitafaruku ya nje chini ya utawala wa Uajemi, Wagiriki, Misri, Syria na Roma.

Zama za Agano Jipya ni zama ambazo mtu alitakiwa kuonyesha imani yake kwa Mungu, kwa njia ya kuitikia kwa undani kwa sala na imani chini ya msingi wa maneno ya Yesu. Kwa hiyo, kipindi cha maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili, Israel ya pili lazima ikumbane na mateso ya ndani (kiroho).

Kwa kuibuka kwa utu (falsafa kiongozi ya Mwamsho kipindi cha Mageuzi) – falsafa za kutambua, na kwa kiasi fulani wakatumia uhuru wa imani baada ya mageuzi, Ukristo (Israel ya Pili) ulilazimika kukumbana na mitafaruku na vurugu. Wakristo katika kipindi hicho iliwabidi walipie mlolongo wote wa historia tangu wakati wa Yesu kwa kukabili na kushinda majaribu makali ya ndani katika maisha yao ya dini.

Wakati wa kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Masihi, Mungu aliiandaa Israel ya Kwanza kumpokea Masihi kwa kuchepua upya na kuifanya upya Uyahudi na kwa kumfanya nabii Malaki atabiri juu ya kuja kwa Masihi. Hata hivyo, pamoja na kwamba Mungu alilenga juhudi zake kuandaa kwa ajili ya Masihi katika Taifa la Israel, pia aliuandaa ulimwengu wote kwa ajili ya ujio wa Masihi. Miongoni mwa watu wa mataifa, Mungu alimpata Gautama Budha wa India (565-485 K.K), kujitokeza kuweka kianzio cha Ubudha kwa kuendeleza Uhindu, na alimpata Sokraites (470-399 K.K) kujitokeza kuweka kianzio cha kipindi wanafalsafa maarufu wa Ugiriki. Huko Mashariki, Mungu alimpata Konfusia (552-479 K.K) ambaye aliweka kiwango cha maadili ya binadamu na desturi kupitia Ukonfusia. Mungu kwa jinsi hii alihakikisha kila mmoja ameweka utamaduni na dini iliyokubalika katika sehemu yake na watu

**Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Masihi (miaka 400)**

| Jibu la nje kwa Mungu | Mateso na Mitafaruku ya nje |
|---|---|
| Sadaka | Uajemi, Ugiriki, Misri, |
| Sheria | Syria, Roma |

**Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili (miaka 400) 1517-1918 BK**

| Jibu la ndani kwaMungu | Mateso na Mitafaruku ya ndani |
|---|---|
| Imani, Maombi | Utu |
| Maneno ya Yesu | |

ili wafanye maandalizi ya muhimu kiroho ili kumpokea Masihi. Yesu alipokuja katika msingi huo wa maandalizi, alipania kuunganisha maeneo yote na dini mbalimbali na tamaduni katika kundi moja la utamaduni mmoja chini ya Mungu kwa kuondoa Uyahudi, Uheleni, Ubudha, Ukonfusia, na dini zote na tamaduni ambazo Mungu aliziandaa.

Mungu aliandaa dunia kwa ajili ya ujio wa Masihi kwa kuleta umoja wa nchi za dunia ya Mediteranian (Bahari ya kati) na kuendeleza Himaya ya Warumi, kwa urahisi wake wa mawasiliano katika pande zote na ukubwa wa utamaduni wake chini ya msingi wa kuwa na lugha moja (Kigiriki). Kukiwa na msingi huu wa nje tayari kupitia toleo la Mungu. Masihi alipokuja, fikra yake ingeweza kwa haraka kuenea toka Israel mpaka Roma, na kutoka Roma mpaka duniani kote.

Vilevile, mungu alifanya katika Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili kuiandaa dunia pamoja

**Kipindi cha Maandalizi kwaajili ya Masihi (miaka 400)**

| **Mazingira** | **- Buddha** |
|---|---|
| Himaya ya Warumi | - Sokraites |
| | - Konfusia |

**Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili (miaka 400)** 1517-1918

**Mazingira**

na kuwepo Ukristo. Kabla ya kuzaliwa Masihi (miaka elfu mbili iliyopita). Mungu alilazimika kutayarisha watu mbalimbali kupokea kile ambacho Masihi angefundisha. Matayarisho hayo yalifanyika katika Uyahudi, Ubudha, Ukonfusia na dini nyingine na maendeleo ya maadili ambayo Mungu aliyachochea na kusonga mbele. Maadili kiroho, na msingi wa moyo kwa ajili ya Ujio wa Pili unafanyika kupitia Ukristo. Kwa hiyo Mungu, aliitayarisha dunia kwa ajili ya Ujio wa Pili kwa kueneza Ukristo duniani kote.

Katika Kipindi cha Maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili hali ya mambo ya nje iliendelezwa sana kama Msingi kwa ajili ya Ujio wa Pili wa Masihi. Mungu ameifanya kazi ya kuendeleza hali ya nje kufikia kiwango ambacho Masihi anaweza kuitumia ili kujenga Ufalme wa Mbingu. Kutenganishwa tamaduni sasa kunaunganishwa na maendeleo ya mawasiliano mamboleo usafirishaji ambao unarahisisha mwingiliano wa haraka na wa mara kwa mara wa lugha, tamaduni na mila. Moja ya maendeleo ambayo yatamsaidia Masihi maadili na njia ya kimbingu ni maendeleo ya mfumo wa dunia nzima wa mtandao wa mawasiliano. Tokea Mapinduzi ya Viwanda, maendeleo makubwa kwa takriban kila kitengo kinachoshughulikia mambo ya binadamu kimeandaa kila kitu ambacho ni cha muhimu katika kuyaweka mazingira safi (Mf. Usindikaji chakula, nguo, madawa, kujali mazingira na umeme).

Tumerejea historia za Israel ya kwanza na ya pili kama zilivyotokea katika nyakati tofauti na katika maeneo tofauti na majukumu muhimu yaliyofanywa na watu tofauti. Na bado, tunaweza kuona utambuzi wa nyakati wa kushangaza tunapolinganisha historia hizi mbili tokea kwenye mtazamo wa Toleo. Utambuzi wa nyakati huu umetokea kwa sababu zote mbili ni historia za toleo kiongozi kwa kuandaa msingi kwa ajili ya Masihi na hivyo matokeo yote mawili yamechagizwa na kuongozwa na Mungu.

Chapter 14

Homepage

# MAANDALIZI KWA AJILI YA UJIO WA PILI

Sura hii inajikita toka kipindi cha zinduko mpaka siku hizi. Sura hii inahusisha kwanza kipindi cha maandalizi ya Ujio wa Pili ambacho zaidi kimegawanywa katika vipindi vidogo vitatu: kipindi cha mageuzi, cha toka 1517 hadi 1648; kipindi cha ukinzano kati ya dini na falsafa, toka mwaka 1648 hadi 1789; na kipindi cha kukomaa mfumo wa siasa, uchumi na itikadi, toka mwaka 1789 hadi 1918. Vilevile sura hii inazungumzia vita vya Dunia vya karne ya ishirini.

## 1. KIPINDI CHA MAGEUZI

Kipindi cha mageuzi kilidumu kwa takriban miaka mia moja na thelathini, toka wito wa Luther wa mageuzi ya kidini mnamo mwaka 1517 mpaka vita ya mapigano kati ya Roma – Katoliki na madhehebu mapya ya Waprotestanti (Wapinzani) na madola ambayo yaliishia kwenye mkataba wa Westphalia mnamo mwaka 1648.

Baada ya kipindi cha shutuma chiniya himaya ya Kirumi, Papa na viongozi wa kanisa la Roma – Katoliki walikuwa na jukumu kubwa kuweka msingi kwa ajili ya Masihi. Kwa sababu hiyo, Mungu aliwapa vyeo na madaraka ambavyo viliwafanya wakubalike zaidi katika taifa na jamii, lakini wakati wa zama za ukabaila ufisadi wao na kuingilia sana maisha ya watu vilizuia kuweka msingi kwa ajili ya Masihi.

Kutumika vibaya mamlaka ya kanisa la Kristo katika kipindi kikali cha ukabaila, ukiongezea ufisadi na maadili maovu miongoni mwa wafanyakazi kanisani, vilichochea hamasa ya mtu kutaka kutekeleza matamanio ya tabia ya asili ambayo aliwekewa ndani yake wakati wa kuumbwa kwake.

Harakati za kuvunja hali za utendajikatika jamii na mfumo wa ufisadi katika dini zilitokea kutokana na dhamira za watu ya (Hulka Asili). Harakati hii ilikuwa na tazamio la ndani (Sung Sang) na tazamio la nje (Hyung Sang) kulingana hali mbili za Hulka Asili ya mtu. Hivyo, binadamu alitafuta kuridhisha matamanio yake ya ndani, kama yale ya

maisha ya imani, heshima, wajibu, ucha Mungu, na uhusiano na Mungu, na matamanio yake ya nje, kama yale ya kuendeleza ujuzi wake (kupitia sayansi), nguvu yake ya kufikiri, na haki zake.

Kwanza kulikuja harakati za kuamsha ustaarabu wa Kigiriki – (Ulyunani) ambayo ilikuwa harakati ya Kikaini, ilizingatia matamanio ya nje ya binadamu. Halafu zikaja harakati za Kiabeli, zilizingatia matamanio ya mambo ya ndani ya mtu. Harakati za kuamsha ustaarabu wa kigiriki ukaja kuitwa.siku za kutafuta elimu na maarifa Ulaya.na kusisitiza kujihusisha na mambo ya utu kama uzuri wa viumbe, uhuru wa mtu binafsi na thamani ya maisha katika Dunia hii. Mageuzi yalitokea kutokana na dhamira ya mtu ya ndani kuyafanya upya maisha chiniya Mungu, na kwamba mageuzi yalisisitiza uhusiano wa mtu kwa Mungu kinyume na itikadi ya utu na sisitizo la duniani kote la uyunani tunaweza kukiita kipindi cha mageuzi ya uamsho wa Uebrania.

**A: Mwamko (Renesansi)**

Kwa rehema za Toleo la Ukombozi la Mungu, mtu amekuwa akikomboa Hulka yake ya Asili. Hali yake ya juhudi zake za mambo ya nje ili kukomboa Hulka yake ya Asili kulipelekea kuchipuka kwa mwamko.
Kulingana na "Kanuni za Uumbaji" mtu aliumbwa ili awe mkamilifu pale tu akamilishapo wajibu wake, kwa njia ya zoezi la utashi (Nia) huru. Mtu aliumbwa awe huru, na hivyo huendelea kuutafuta uhuru. Pia, mtu aliye na tabia kamilifu anapaswa kuwa na uhuru kama mtu binafsi mwenye mwili wa kweli. Hivyo mtu mwenye Hulka Asili, ana matamanio ya kujenga tabia ya ubinafsi.

Mtu aliumbwa kupitia Neno la Mungu ili kushabihiana na Hulka ya Mungu. Kwa sababu hii, mtu, kwa Hulka yake ya Asili, hutamani kuendeleza akili yake, na nguvu za kufikiri. Mtu vilevile aliumbwa ili awe na mamlaka juu ya Uumbaji. Hivyo, mtu, kwa Hulka yake ya Asili, huthamini sayansi, na uelewa wa maumbile na hutamani kuendeleza mazingira yake. Hata hivyo, tamanio la hali ya nje ya Hulka ya Asili ya mtu lilikuwa linakandamizwa na mfumo wa ukabaila wa zama za kati. Hili lilisababisha watu kuendelea kudai kwa nguvu vitu kama uhuru, ubinafsi wa mtu, heshima katika maamuzi.

Kuendeleza kwa matamanio haya ya nje kulipata kichocheo kwa kuingiza staarabu za Ugiriki ya zama za kale nyakati za Krusedi (vita vitakatifu). Mtu wa zama za kati alijifunza kuwa mtazamo wa Ugiriki ya ulimbwende {ustaarabu} wa zamani ulikuwa sawa na matamanio ya nje. Hivyo, harakati za kuamsha staarabu za Ugiriki {Hellenism} zilianza zikiendeshwa kwanza nchini Italia, na baadae kote nchi za Ulaya. Kutokana na mwamko wa staarabu za Ugiriki mtazamo wa falsafa juu ya utu uliibuka.

Mwamko ulianza kama harakati ya kuteka tena moyo wa Ugiriki wa zama za kale, lakini punde ikawa harakati iliyobadilisha mtazamo wa jamii nzima kimaisha ukiwemo utamaduni, mfumo wa siasa, uchumi na hata dini. Hizi zilikuwa ni kani mojawapo pamoja na mageuzi zilizopelekea kumomonyoka kwa utamaduni wa wakati wa zama za kati na kuzaa zama za siasa.

Kwa kuwa mwamko kimsingi ulijihusisha na matamanio ya hali ya nje ya hulka ya mtu, unaweza kuonekana kama kwamba unakinzana na na toleo la msingi la Mungu la kukomboa roho ya mtu. Hata hivyo ili kukamilisha lengo la kukomboa thamani ya awali ya mtu, awamu ya kukomboa hali ya nje ya mtu ni lazima.

Kwa njia yoyote ile, viwango vyote vya thamani ya mtu lazima vikombolewe. Hii ina maana kuwa kila mtu lazima akamilike kama mtu pekee binafsi, kwa kuunganisha hali ya mambo ya nje na ndani ya uwepo wake. Kwa mtazamo huu, Mungu alileta mageuzi katika msingi wa mwamko.

B: MATENGENEZO

Ufisadi wa Kanisa Katoliki wa zama za kati ulikuwa ni ukinzano dhidi ya toleo la Mungu kwa ujio wa pili, na utapanyaji wa madaraka ya umati wa kanisa na ibada zake, ulisababisha watu wengi kutoa miito ya mageuzi makubwa. Na kama matokeo ya vita vya dini.“Kupelekwa utumwani Babiloni”, mgawanyiko mkubwa wa mwamko, nguvu za upapa na madaraka yake yalipungua mno na kilio cha mageuzi kiliongezeka kwa nguvu. Kwa jinsi harakati za utu zilivyokua, upinzani dhidi ya hatua za kanisa za kuzuia uhuru wa watu na kujitawala ulianza kupata mafanikio miongoni mwa watu.

Mnamo karne ya 14, Yohana Wyklif, profesa {mwalimu} wa teolojia katika chuo kikuu cha Oxford cha Uingereza, alitafsiri Biblia katika

kiingereza, akisisitiza kuwa taratibu ambazo imani ya mtu inavyoweza kupimwa si kwa vigezo vya papa au makuhani {mapadre}, bali Biblia yenyewe tu. Aliendelea kutoa hoja kwamba ibada nyingi za kanisa, sheria na mapokeo hazina msingi wowote katika maandiko ya Biblia. Wengine wengi walihoji unyonyaji wa kanisa kwa watu na tabia isiyo ya kidini ya makasisi, na pia walidai kuwepo mabadiliko. Hata hivyo, hakuna aliyefanikiwa, na baadhi waliuawa.
Mnamo mwaka 1517, Papa Leo wa kumi {x} alianza kwa kuuza “indulgence”(msamaha masharti kama sehemu ya malipizi) ili kupanua mfuko wa fedha ili kujenga Basilika {kanisa kubwa} la Mtakatifu Petro.Majibu ya zoezi hili yalitokea kuchochea mageuzi kwa kuanza na Martin Luther, mwalimu {profesa} wa teolojia ya kibiblia, aliyekuwa chuo kikuu cha Wittenberg nchini Ujerumani. Harakati za mageuzi zilikua haraka nchini Ujerumani, Ufaransa na Uswisi, zikiongozwa na Luther, Kalvini na Zwingli.

Ukinzano uliotokea wakati wa harakati za Waprotestanti {wapinzani} haukuwa tu wa dini bali ulikua mpaka kuwa vita ya kimataifa miongoni mwa nchi zenye maslahi tofauti katika mafanikio au kushindwa kwa mageuzi. Ukinzani ulidumu kwa zaidi ya miaka mia nne, mpaka mapigano kati ya dini ya zamani na mpya na mapokeo yao yalipokwisha kwenye vita vya miaka thelathini. Vita hivi, vilipiganiwa nchini Ujerumani, na kumalizika mnamo mwaka 1648 kwa mkataba wa Westphalia. Viliishia kwa ushindi wa Waprotestanti Ulaya ya Kaskazini na mageuzi yalifanikiwa.

II: KIPINDI CHA UKINZANI KATI YA DINI NA FALSAFA
Kipindi cha ukinzani kati ya Dini na Falsafa kilidumu kwa karibu miaka mia moja na arobaini, tangu mkataba wa Westphalia, mwaka 1648, mpaka mwanzo wa mapinduzi ya Wafaransa ya mwaka 1789. Kwa ushawishi wa mwamko na mageuzi, mtu aliingia katika mwelekeo kamili wa kuridhisha mahitaji ya mambo ya nje na ya ndani ya hali yake ya hulka-asili, na kwa sababu ya uhuru uliotolewa katika fikra za kidini na falsafa mtu hakuweza kuzuia uitengano wa mafundisho na ukinzani miongoni mwa falsafa {fikra}

Toleo la ukombozi linajengwa na hali ya kutenganisha mtazamo wa maisha ya aina ya Kaini dhidi ya ile ya Abeli. Wakati wa kuisha kwa historia, kanuni hii ya kutenganisha lazima itumike tena, pale ambapo dunia iliyopo itakapotenganishwa kati ya aina za makundi ya Kaini na

Abeli. Dunia ya Kaini ni dunia ya kutokuwa na imani-ukomunisti, na dunia ya aina ya Abeli ni ya kidini –inayounga mkono dunia ya kidemokrasia, hizi mbili kwa kulinganishwa, katika upeo wa dunia, ni kama "mbuzi" na "kondoo" ni kama Yesu alivyosema kwenye Mathayo 25:35. Dunia hizi mbili zipo chini ya pande mbili tofauti za mtazamo wa maisha.

**A: Mtazamo wa maisha – aina ya Kaini .**

Sisitizo la kukamilisha matamanio ya mambo ya nje ya Hulka-Asili ya mtu yalipelekea kuchipuka kwa mtazamo wa maisha aina ya Kaini, ambayo hupunguza imani ya Mungu na kujitoa kwa ajili ya dini na umekuwa ukipelekea kufikiri kwa kila kitu kwa kigezo cha maumbile na mtazamo wa utu. Mwelekeo huu ulitokea kuenea kama matokeo ya mtazamo wa maisha wa kipindi cha zama za kati, ambamo watu walifikiri kuwa mwili wa binadamu na dunia ya vitu kwa ujumla kuwa ni duni na ulikuwa umetishwa na Mungu na kusalimishwa kwa viongozi wa dini kwamba wasitegemee akili {au fikra} zao.

Wakiwa wamechagizwa na hali hii, wengi walianza kuangalia maumbile na maisha katika mwanga wa fikra na ushuhuda wao wa moja kwa moja, wakiwa wamejinasua na mtazamo wa teolojia. Wanafikra, kama vile Descartes, na washuhudiaji {wahakiki} kama vile Locke, waliachana na mtazamo wa kumchukulia Mungu kama ndiye chanzo cha kila kitu na kuwa ukweli unaweza kujulikana kwa njia ya kufikiri au uzoefu. Ufikiriaji uliegemea kuidharau historia na mapokeo, isipokuwa kuthamini wazo la mtu pekee.

Uhakikishaji {ushuhudiaji}, kwa namna nyingine, uliendeshwa kwa fahamu tano za mtu na kudai kuwa ujuzi unapatikana kutokana na uzoefu na kuona moja kwa moja, bila ya aina yoyote ya masharti ya awali. Hivyo, ufikiriaji na uhakikishaji ulitokea kupuuza miujiza, maono na ufunuo.
Kwa jinsi falsafa hizi zilivyozidi kusisitiza ufikiriaji na uzoefu wa fahamu tano na kupunguza matazamio katika maumbile na mtu, ndivyo walivyozidi kumtenganisha mtu toka kwa Mungu.

Mnamo karne ya kumi na nane mtazamo wa aina -ya –Kaini wa maisha ulihusisha fikra hii katika nyakati za mwanga, ambacho kinawza kufikiriwa kama kipindi cha hatua ya pili ya

mwamko.  Nyakati za mwanga {nuru} zilithamanisha mambo ya mtu kutokana na mtazamo wa kufikiri na jinsi gani unafanana kwa karibu na mpangilio katika maumbile. Hali hii iliathiri kila hali ya maisha na kupelekea kuvunjika kwa tamaduni kuu nyingi zilizokuwepo.
Kwa sababu mapokeo hayo yalisisitiza juu ya ufikiriaji mambo ya maisha, wanafikra wakati wa nuru walikataa katakata chochote kilichoonekana hitimisho nje ya mchakato wa ufukiriaji au ambacho kilionekana kuwa si kweli katika maisha.  Matokeo yake, mtu alikwenda zaidi ya hatua ya kuwa huru mbali na Mungu na kufikia hatua kali ya kumkana.

Wakichagizwa na mtazamo wa maisha ya aina ya Kaini, mafundisho ya kuamini Mungu bila ufunuo yalianzishwa.  Wana-Imani bila ufunuo waliegemea kuamini katika theolojia yenye msingi wa kufikiri na kuondokana na mambo kama uzoefu wa ufunuo na miujiza.  Wana imani bila ufunuo walimchukulia Mungu kama muumbaji wa wote ambaye hakushirikishwa katika historia na kuamini kuwa mtu atapata viwango vya maadili kutokana na maumbile bila ufunuo toka kwa Mungu.
Uhegelia wa mlengo wa kushoto {Strauss na Feuerbach}, pamoja na falsafa ya usoshalisti wa Kifaransa, hawa walipelekea kuwepo msingi wa kuzaliwa kwa itikadi ya kikomunisti.  Ni kwamba chini ya chagizo la itikadi hizi, Karl Marx na Friedrich Engels waliendeleza mafundisho yao ya ukinzani wa vitu katika maumbo.  Ukomunisti unaweza kuchukuliwa kama matokeo ya kutoamini uwepo wa Mungu na mali, na itikadi kubwa ya mwisho inayomkana Mungu.

**B: Mtazamo wa maisha ya aina ya Abeli .**

Tunapochambua kwa juu juu kipindi cha mpito toka zama za kati hadi jamii ya dunia ya sasa kutapelekea kuamini na kuchukulia kuwa kipindi cha mpito ni cha mchakato wa kumtenganisha mtu kutoka kwa Mungu na dini. Hii ni kwa sababu ufafanuzi wa mtu wa hali ya nje ya Hulka – Asili ya mtu katika kipindi hiki cha mpito kilitoa maendeleo makubwa miongoni mwa wanajamii.

Hata hivyo, uchunguzi wa makini utatuwezesha kuelewa kuna hali nyingine kubwa katika mpito toka zama za kati hadi jamii ya leo. Ufafanuzi wa mtu wa zama za kati juu ya hali ya ndani ya Hulka Asili ilipelekea harakati kuibuka na kuamsha mtazamo wa maisha wa

kiebrania. Harakati hizi zilikomaa na kuwa mageuzi.
Kupitia harakati hizi, falsafa na dini viliendeleza mtazamo wima wa maisha, ambao ni wa aina ya Abeli ya mtazamo wa maisha, na kupelekea mtu wa zama za kati kuendelea kuwa na uhusiano wa karibu na Mungu.

Katika karne ya 17 na 18, harakati nyingine mpya ziliibuka, harakati hizi zilisisitiza juu ya ushuhuda wa maajabu, maisha ya kikristo, na maadili. Dunia ya dini, ambayo ilichagizwa na mtazamo wa jumla wa kufikiri, ilihitaji sana harakati hizi kusisitiza kujitoa kidini na maisha ya kiroho ya mtu dhidi ya mafundisho au ukiritimba. Uimarisho nchini Ujerumani (ukiongozwa na Spencer), umethodisti, ambao ulichagiza mwamko mkubwa nchini Uingereza (ukiongozwa na makaka Wesley), na Quaker (Quakerism), (dhana iliyoanzishwa na George Fox) ni mifano ya harakati hizo.

Wote walisisitiza imani chini ya mfumo wa uzoefu wa mtu binafsi katika dini na miujiza au maswala ya kiroho ya maisha ya mtu, ambayo hayawezi kufafanuliwa katika wazo au fikra kavu; walisisitiza mtazamo wa maisha kuongozwa na uhusiano wa Mungu. Katika ukanda wa falsafa, wana itikadi kama vile Kant, Fitche, Schelling, na Hegel, katika kupinga itikadi ya kulinganisha na maumbile mtazamo wa nyakati za nuru, walitoa mawazo ya maisha ambayo yalitoa msisitizo wa mambo ya kiroho na uadilifu – ni kwamba mitazamo ambayo kimsingi ni ya aina ya Abeli.

## III: KIPINDI CHA KUKOMAA MFUMO WA SIASA, UCHUMI NA ITIKADI .

Kipindi hiki cha tatu kilidumu kwa miaka mia moja na thelathini. Kilianza na mapinduzi ya Wafaransa 1789 na kuendelea wakati wa mapinduzi ya viwanda, na kuishia kwa hitimisho la vita kuu ya kwanza ya dunia. Katika msingi wa – mitazamo ya aina ile ya Kaini na Abeli ya maisha ambayo ilitokea kabla ya kipindi hiki, dunia ya mtazamo wa Kaini na dunia ya mtazamo wa Abeli kila moja peke yake zilianza kujitokeza.

Umuhimu wa kipindi hiki cha miaka mia moja na thelathini katika toleo umo katika sura ya maendeleo ya mfumo wa kisiasa, uchumi, na itikadi mpaka kufikia hatua ambayo Masihi anaweza kupokelewa na

ambapo anaweza kuwabadili ili kujenga dunia adilifu kama ilivyokusudiwa awali na Mungu.

**A. Maendeleo ya mifumo ya sasa ya siasa .**

Nguvu za kisiasa, ambazo ziliwekwa kuongozwa na makabaila wakati wa zama za kati, ziliimarishwa na wafalme ili kuanzisha tawala yakinifu mnamo katikati ya karne ya 17. Halafu kuanzia mwisho mwa karne ya 18, mfumo wa utawala yakinifu uligeuzwa kuwa mfumo wa aina ya demokrasia wa Kaini na Abeli, asili yake ilitokana na mitazamo ya aina ya maisha ya Kaini na aina ya maisha ya Abeli. Chini ya chagizo la uadilifu wa Nuru, watu walilenga kujenga ukombozi, udugu, na usawa kama ukweli katika maswala ya mtu – lakini ilitokea hivyo nchini Ufaransa kwa njia ya mapambano ya mambo ya nje na ya tabia ya ukatili, hivyo kujenga demokrasia aina – ya – Kaini. Demokrasia aina ya Abeli ambayo iliendelezwa nchini Uingereza na Marekani na nchi nyingine zilikuwa kwa wingi chini ya mtazamo wa maisha ya aina ya Abeli, ambao ni mfumo wa kiutu zaidi ulioendana na namna ya mapinduzi yao. Kutokana na tamaduni hizi mbili kumekuwepo na dunia ya ukomunisti na dunia ya demokrasia.

Kama ilivyoelezwa katika “Kanuni za Uumbaji” uumbaji ulifanyika ukiwa na mfumo wa mtu mkamilifu, kama mfano. Dunia adilifu, iliyo na watu wakamilifu, ingeshabiiana na kutenda kama mtu mkamilifu. Ni kama seli na viungo vya mwili wa mtu hutenda kulingana na amri ya ubongo, watu na mashirika katika dunia adilifu wangefanya kazi kulingana na matakwa ya Mungu. Kama ilivyo hakuna sehemu ya mwili ambayo inakataa matakwa ya akili, haitakuwa vigumu kwa mtu mwadilifu kufuata matakwa ya Mungu. Kama amri zitokazo akilini zinapelekwa sehemu zote za mwili kupitia njia za pembezoni za mfumo wa neva, zikiongozwa na uti – wa – mgongo, maelekezo toka kwa Mungu yataifikia jamii nzima kupitia watakatifu, wakiongozwa na Masihi, anayekuja kama mzazi wa kweli.

Katika jumuiya adilifu, muafaka miongoni mwa bunge, serikali na mahakama, matawi haya ya dola huendana na muafaka miongoni mwa viungo vya mwili – mapafu, moyo, na tumbo (na mifumo ya kupumua, kuzunguka na kula). Kama vilivyo viungo hivi vitatu (na mifumo) katika mwili wa binadamu hufanya kazi pamoja kwa ulaini vinapofanya kazi kulingana na amri ya akili. Katika dunia adilifu,

matawi matatu makuu ya dola pia yatafanya kazi kwa pamoja kwa sababu yatafanya kazi kulingana na Masihi na mapenzi ya Mungu.

Kwa kipindi katika maendeleo ya mfumo wa siasa ya Ulaya Magharibi, mfalme alidhibiti shughuli zote za dola; bunge, serikali, na mahakama. Hata hivyo, baada ya nyakati za mapinduzi ya Wafaransa, nguvu tatu hizi zilianza kutenganishwa. Hivyo, kwa nje, angalau mfumo adilifu wa mfumo wa kisiasa ulianza kuonekana. Hii ina maana kuwa baadhi ya mifumo ya siasa kwa nje inafanana na mfumo wa mwili wa mtu. Hata hivyo, kwa sababu viongozi wa siasa hawamjui Mungu wala kutekeleza matakwa ya Mungu, mfumo hauwezi kufanya kazi kimuafaka kama ulivyokusudiwa awali. Masihi lazima aje ili afundishe matakwa ya Mungu na kumwonyesha mtu namna ya kujighubika nayo

**B. Mapinduzi ya viwanda na kukomaa kwa uchumi .**

Kufuatana na "Kanuni ya Uumbaji" Mungu alimbariki mtu kutawala vitu vyote vya uumbaji (Mwa. 1:28) baada ya kupata ukamilifu, hivyo kuumba na kufurahia mazingira mazuri. Mungu amekuwa akielekeza toleo lake kuendeleza mazingira ya vitu kwa kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara, ambavyo vipo chini ya msingi wa maendeleo ya kisayansi. Pamoja na kuwa mtu ni wa anguko, lazima atumie uwezo wa kuumba aliopewa na Mungu kuendeleza ugunduzi ambao utaumba mazingira hai yafaayo kwa ajili ya Masihi ili ajenge jumuiya adilifu. Mapinduzi ya viwanda, yalioanzia Uingereza yalitokea kuumba msingi wa mazingira mazuri kwa ajili ya jumuiya adilifu ya Mungu.

Katika mfumo wa kiuchumi wa jumuiya adilifu, uzalishaji, ugawaji na ulaji utawekwa sawa chini ya matakwa ya Mungu. Kwa hiyo, uzalishaji kulingana na mahitaji ya mtu, ugawaji wa haki, na ulaji kulingana na dhumuni la wote utakuwepo. Ingawa sasa sayansi na uchumi vimeendelea sana katika dunia, uzalishaji bado hauwezi kukidhi mahitaji, ulaji mara kwa mara haujali hali ya baadae na kufikiria maadili, na madhara yatokanayo na upendeleo katika ugawaji ni makubwa. Ni pale tu watu wote au vitu vyote vitakapokuwa na uelewano na Masihi, kulingana na matakwa ya Mungu, ndipo mfumo wa uchumi adilifu utakapojengwa. Baada ya mapinduzi ya viwanda, uzalishaji mkubwa ulihitaji nchi zinazoendelea, kama vile Uingereza, kushika makoloni mengi ili

kukuza masoko na vyanzo vya malighafi. Hata hivyo, nchi nyingi zinazoendelea zilikuwa ni nchi za kikristo, na kuanzishwa huku kwa makoloni kwa faida za kiuchumi kulipelekea kuwepo msingi wa nje kwa ajili ya kueneza kiundani Injili. Mapinduzi ya viwanda yamekuwa na umuhimu mkubwa katika kutimiza utabiri wa Yesu kwamba Injili itahubiriwa mpaka mwisho wa mipaka ya dunia katika kuandaa ujio wa Masihi. (Mt 24 , 14)

**C. Hatua za mapinduzi katika Siasa, Uchumi, Itikadi na Dini.**

Kama ilivyojadiliwa hapo juu, harakati dhidi ya zama za kati kuamsha ustaarabu wa kigiriki, uliojulikana kama mwamko, ulikuwa mwelekeo namna ya Kaini ambao uliamsha utu. Mwamko zaidi uliendeleza hulka yake ya Kaini na kutokea kwenye Nuru (mwanga) ambayo imechukuliwa kama mwamko wa pili. Baadae Nuru ilikuza zaidi hulka yake ya aina ya Kaini na kuzaa zama za ukomunisti, mwamko wa tatu kutokea.

Shetani hujua mipango ya Mungu na kila mara husonga mbele kuanzisha vitu upande wake kabla ya Mungu kukamilisha. Hivyo, kile ambacho shetani amefanya kukikamilisha ni sawa (katika muundo, na siyo yaliyomo) kwenye toleo la Mungu lijalo baadae. Hivyo, kuanzia kipindi cha mwamko, vipindi vitatu vya mapinduzi aina ya Abeli vilifuatana na awamu tatu za mapinduzi aina ya Kaini katika dini, siasa na viwanda. Aina ya Abeli ya kipindi cha kwanza ilikuwa ni mageuzi ambayo yalianza na Lutheri, kutokana na mwamko. Halafu, wakati na kufuatia kipindi cha mwanga au nuru mwamko wa pili wa kiroho ukatokea, katikati ya shutuma kali zilizoegemea kwa Fox, Spencer, Yohana Wesley, na Jonathan Edwards, na kupanuka kufikia kuwa mageuzi ya pili. Chini ya matukio haya na katika kuelewa sheria ya hapo juu ya uovu  kutangulia wema, mageuzi ya tatu yanategemewa baada ya mwamko wa tatu. Kwa kweli katika hali ya Ukristo leo hii inaonesha wazi kuwa kuna haja ya kufanya mageuzi.

Hatua tatu za mageuzi zimetokea pia katika uwanja wa siasa. Jamii ya zama za kati ziliangamia chini ya chagizo la mwamko (wa kwanza), wakati tawala yakinifu za kitawa zilianguka chini ya chagizo la mwamko wa pili (kipindi cha nuru) na “mageuzi ya pili”mwisho, katika upande wa shetani chama cha kikomunisti kilianzishwa na mapinduzi ya kisiasa chini ya msingi wa mwamko wa tatu. Sasa ni

muhimu kwamba dunia ya demokrasia ambayo ipo upande wa mbingu itiishe dunia ya kikomunisti kwa kutumia itikadi ya mageuzi ya tatu. Hili litakapotimia, dunia hizi mbili zitaungana na kuwa ufalme mmoja wa mbinguni hapa duniani.

Pia tunaona mapinduzi ya viwanda yalipitia katika hatua tatu. Awamu ya kwanza ya mapinduzi ilitokea katika msingi wa maendeleo ya injini ya mvuke kutoa nishati. Mara baadae, awamu ya pili ya mapinduzi ya viwanda yalitokea katika msingi wa kuendelea kwa nishati ya umeme na injini chomea ndani. Sasa, mapinduzi ya tatu ya viwanda yanayofanyika yamejikita kwenye matumizi ya nishati ya Atomiki.

Mapinduzi haya matatu yanaelekea kukomaa katika kipindi hiki cha matayarisho kwa ajili ya ujio wa pili wa Masihi. Kwa pamoja yanaleta kuwepo kwa msingi ulioandaliwa ambao kwa huo Masihi anaweza kuja na kukamilisha dhumuni la Mungu kwa ajili ya uumbaji. Kukomaa kwa dini na itikadi ni kwa ajili ya toleo lililoelekezwa katika ukamilifu wa asili ya mtu, wakati kukomaa kwa siasa na uchumi ni kwa ajili ya toleo ambalo litaendeleza mfumo na mazingira kwa ajili ya dunia adilifu.

## IV. VITA VYA DUNIA .

### A. Sababu za mpango wa Mungu juuya vita vya Dunia .

Bila shaka, vita hutokea kwa sababu za kisiasa, uchumi na itikadi. Hata hivyo, kwa nyongeza ya sababu hizo za nje, kuna sababu za ndani, yaani sababu za mpango wa Mungu , kulingana na kanuni za ukombozi kwa njia ya malipizi. Sababu ya msingi ya vita vya Dunia ni ukinzano kati ya utawala mzuri wa Mungu ambaye anajaribu kumrudisha mtu katika upande wake, na utawala mwovu wa shetani ambaye anajaribu kulinda na kutunza umilki wake kwa mtu – ukinzano ambao mtu anabanwa katikati. Hebu tuchunguze hili kwa undani zaidi.

Awali ya yote, vita vya Dunia vinalipuka kwa sababu ya harakati za mwisho za shetani katika kutunza au kulinda milki yake dhidi ya mpinzani wake. Kwa sababu ya Anguko mtu alianzisha Dunia isiyoendana na kanuni, na kumtumikia shetani kama bwana wake badala ya Mungu. Hivyo Mungu amekuwa akifanya kazi ya toleo la kukomboa Dunia yake ya kanuni kwa kujenga eneo jema ndani ya

Dunia isiyofuata kanuni, chini ya milki ya shetani, na baadae hatua kwa hatua kupanua eneo hilo.

Kristo, yeye pekee nyakati za ujio wa pili, anakuja kumaliza Dunia ya utawala mbovu na kuanzisha Dunia ya utawala mwema inayoongozwa na Mungu. Kwa hiyo, wakati wa ujio wa pili ni nafasi ya mwisho ya shetani kuzuia kupoteza utawala wake, na vilevile, mapambano yake yatakuwa ya pupa na makubwa, yakiwa na matokeo ya vita vitatu vya Dunia.

Pili, shetani alianzisha Dunia chini ya msingi uliokosa mfumo wa kanuni ya Baraka Tatu; hivyo ili kukomboa Dunia ya anguko kulingana na kanuni ya ukombozi kupitia malipizi, Mungu yampasa amfanye mtu ayatimize, katika upeo wa Dunia yote masharti ya malipizi ya kupokea Baraka Tatu. Ingawa mtu alianguka, Mungu asingeweza kumkataza kuanzisha mfano wa Dunia iliyobarikiwa ambayo Mungu alipania kuijenga, na watu wa anguko wameendeleza Dunia chini ya shetani isiyo na kanuni chini ya msingi wa kuigiza Baraka Tatu za Mungu kwa mtu.

Hivyo dunia isiyo -ya -kanuni imejengwa ambayo tabia ya mtu binafsi ipo chini ya shetani, familia na jamii zipo chini ya shetani, na utawala wa dunia iliyoumbwa upo chini ya shetani.

Hivyo, ili kukamilisha, masharti ya malipizi, dunia yote, kwa ajili ya kupokea Baraka Tatu, hili haliepukiki kwamba mtu atapambana na aina tatu za mapambano dunia yote, ambapo upande unaowakilisha kanuni na mbingu lazima ushinde dhidi ya upande wa shetani usiokuwa na kanuni.

Tatu, vita vya dunia lazima vitokee ili dunia itimize masharti ya kumshinda shetani na vishawishi vyake vitatu kwa Yesu. Mlolongo wa Yesu ni mlolongo ambamo Wakristo lazima watapita. Kwa hiyo, vishawishi vitatu ambavyo Yesu alipambana navyo lazima vishindwe na watu wote katika kiwango cha mtu binafsi, familia, taifa na dunia yote. Mapambano ya tatu ya dunia lazima yatokee ili watu wote, katika upeo wa dunia, waweze kushinda vishawishi vitatu vya Yesu.

Nne, vita vya dunia lazima vichukue nafasi ili kukamilisha, katika upeo wa dunia, masharti ya malipizi ya kukomboa utawala wa mbingu. Mungu amekuwa akisogeza Toleo la Ukombozi kupitia malipizi mbele na kugawa dunia ya anguko katika aina mbili; ya

Kaini na ile ya Abeli. Mashambulizi ya aina -ya –Kaini, upande wa shetani dhidi ya aina -ya –Abeli, upande wa mbingu ni mchakato wa ukombozi. Upande wa mbingu wa aina ya Abeli huanzisha msingi wa wema, kupitia sadaka. Mapambano ya mwisho lazima yatokee ili kukomboa kwa njia ya malipizi. Katika upeo wa dunia kitendo cha Kaini kumuua Abeli dunia ya Kaini huishambulia dunia ya Abeli kwanza, lakini matokeo yake ni kwamba dunia ya Abeli hupata ushindi dhidi ya dunia ya Kaini.

**B: Vita vya Kwanza vya Dunia .**

Katika hatua ya mwisho ya maandalizi ya ujio wa pili, Mungu amefanya toleo(mpango ukombozi) lake kwa kuwagawa watu kisiasa, kiuchumi na kiitikadi katika dunia mbili. Ile ya aina ya Abeli, ya upande wa Mungu, na aina ya Kaini, ya upande wa shetani. Upande wa mbingu na ule wa shetani zinaeleweka kutokana na mwelekeo wao unavyojihusisha na Toleo la Ukombozi la Mungu, kuchukua mwelekeo ulio sawa na Toleo la Ukombozi la Mungu, au kujenga maelewano na mwelekeo huo, hata kwa namna ambayo si ya moja kwa moja huainisha kitu kwamba kiko upande wa kimbingu. Nafasi yeyote kinyume cha mwelekeo wa Toleo la Mungu, hata kama si moja kwa moja huainisha kitu kuwa kiko upande wa shetani.

Dini zote zilizo na wema kama dhumuni lao lipo upande wa kimbingu. Hata hivyo dini fulani inapozuia nyingine ambayo ipo karibu na Mungu, hiyo dini husimama upande wa shetani. Kwa kuwa Ukristo ulijengwa kama dini kiongozi kwa ajili ya kukamilisha lengo la dini zote katika Toleo la Ukombozi ndiyo pekee iliyo karibu na Mungu. Kwa hiyo katika vita vya kwanza vya dunia, nchi zilizoongoza nchi za Fungamano, Uingereza, Marekani, Ufaransa na Urusi zilikuwa nchi za wakristu. Hivyo, zilikuwa upande wa kimbingu.

Kinyume chake, nchi mbili zilizoongoza zile za “Nguvu – Kiongozi”, za Ujertumani na Austria-Hungary, siyo tu ziliunga mkono Uturuki, nchi ya Kiislam iliyokuwa inashutumu Ukristo lakini zilikuwa nchi mabavu kupindukia. Hivyo, walikuwa upande wa shetani. Katika vita vya kwanza vya dunia, upande wa mbingu ulishambuliwa na upande wa shetani, lakini hatua kwa hatua ukapata ushindi wa mwisho.

Kwa msingi huu wa ushindi, upande wa mbingu ulitimiza katika upeo wa Dunia, hatua ya kwanza ya sharti la malipizi la kukomboa Baraka Tatu za Mungu. Ukiangalia kwa msimamo wa Dunia kushinda jaribu la kwanza la shetani kwa Yesu, sharti la malipizi la kukomboa Baraka ya Kwanza ya Mungu kwa mtu ilikuwa imetimizwa. Kwa maneno mengine, sharti la malipizi la kukomboa baraka ya kujikamilisha mtu binafsi lilitimizwa.

Zaidi ya hapo, hatua ya kwanza ya msingi kwa ajili ya kukomboa madaraka ya mbingu ulijengwa. Pia kwa ushindi wa upande wa mbingu katika Vita ya Kwanza vya Dunia, msingi ulijengwa ambao kwa huo Masihi angeweza kuzaliwa (kama mfano wa kiumbe mtu wa kweli).

**C. Vita vya Pili ya Dunia .**

Vita vya Pili vya Dunia vilikuwa vita ambavyo demokrasi ilianzisha msingi wa ushindi wa hatua ya kukua kwa kuteka madaraka ya kifashisti. Katika Vita vya Pili, Marekani, Uingereza na ufaransa, kama nchi za demokrasia ziliwakilisha upande wa Mungu. Ujerumani, Japan na Italia, kama nchi zenye ukiritimba ambazo zilisimama kupinga Ukristo, zilisimama katika upande wa shetani.

Ilikuwa ni kwa sababu ya kuanguka viumbe watatu, Adam, Hawa na Malaika Mkuu, kwamba baraka za Mungu hazikutimizwa. Kushiriki kwa viumbe watatu wa aina ya Adam, wa aina ya Hawa na wa aina ya Malaika Mkuuni lazima ili kukomboa Baraka Tatu. Vile vile, vita ambavyo kwavyo dunia ilipaswa kulipa sharti la malipizi ya kukomboa Baraka, kulilazimika kuwepo mapambano kati ya mataifa matatu yakimwakilisha Adam, Hawa na Malaika Mkuu, wakisimama upande wa Mungu na mataifa matatu yakiwakilisha nafasi sawa hizo tatu za upande wa shetani.Katika Vita Vya Pili Vya Dunia, Adam, Hawa na Malaika Mkuu upande wa Mungu ambazo ziliwakilishwa na nchi za Marekani, Uingereza na Ufaransa, ambapo Ujerumani, Japan na Italia ziliwakilisha nafasi zile ambazo zilikuwa upande wa shetani.

Kwa nini umoja wa Soviet, ambao ulikuwa taifa upande wa shetani, ulishirikiana na mataifa ya upande wa kimbingu wakati wa vita vya pili vya dunia ? Pale ambapo mfumo fulani wa jamii au mfumo wa Serikali unapokuwa pingamizi katika kutimiza mpango wa Mungu wa ukombozi, hufanya kazi ya kuliharibu na kulivunja hilo pingamizi

{kizuizi}. Vivyo hivyo, ili kusonga mbele dhidi ya Mungu na Mungu kuhitimisha lengo lake la dhati, ambalo ni kujenga dunia isiyofuata kanuni, shetani hufanya kazi ya kuvunja vikwazo vyovyote katika njia yake. Wakati mwingine pingamizi huziba njia zote za Mungu na za shetani; wakati huo pande zote mbili, wa mbingu na wa shetani huja kuzivunja.

Pande zote za Kaini na Abeli kila upande ulifanya jitihada kuangamiza jamii ya zama za kati {za ukabila}. Pia, upande wa mbingu na ule wa shetani viliweka juhudi kuteketeza jumuiya ya kifalme(madaraka pekee ya utawala). Vile vile, wakati wa Vita Vya Pili Vya Dunia, ufashisti ulitokea kuwa kizuizi upande wa mbingu na upande wa shetani, na hivyo kila upande ulitafuta kuuangamiza. Mungu aliacha Umoja wa Soviet ushirikiane na mataifa ya upande wa mbingu katika kuvunja nchi nyingine za ukiritimba, hata kama ilimaanisha kuwa dunia ya Ukomunisti itajengwa.

Vita vya Pili vya Dunia viliisha kwa kupata ushindi mataifa ya upande wa kimbingu. Kwa njia hii, sharti la malipizi katika upeo wa dunia katika hatua ya kukua kwa ajili ya kukomboa Baraka Tatu za Mungu kwa mtu lilitimizwa. Kwa kuangalia katika msimamo wa ushindi, upeo wa dunia, vishawishi vya shetani kwa Yesu sharti la malipizi kwa ajili ya kukomboa dunia yote Baraka ya Pili ya Mungu, ambayo ni ya kunyumbulisha watoto wema, lilitimizwa. Hivyo, baada ya vita, kazi ya ujio wa pili iliendelezwa katika hatua ya kuendeleza maendeleo ya dini. Zaidi ya hayo, msingi wa hatua ya kukua kwa ajili ya kukomboa madaraka ya kimbingu uliwekwa.

**D: Vita Vya Tatu Vya Dunia .**

Mungu tangu mwanzo alitaka kuhitimisha mpango wake wa Ukombozi katika familia ya Adam, kupitia kwa Kaini na Abeli. Hata hivyo, kazi yake ya kutenganisha wema mbali na uovu iliishia kushindwa kutokana na Kaini kumuua Abeli. Tangu wakati huo, Mungu amejitahidi kwa mfululizo kutenganisha wema mbali na uovu, ikipanuka katika hatua, kuanzia upeo wa familia mpaka wa kabila, taifa na upeo wa dunia nzima.

Wakati wa hitimisho la historia ya mtu, pande zote, ule wa mbingu na ule wa shetani, pande hizo zinajishughulisha katika dunia yote. Kwa jinsi hii, dunia mbili, ya Demokrasia na ya Ukomunisti zinaishi kwa

kushirikiana.  Lakini baada ya mapambano ya tatu ya dunia, dunia hizi mbili zitaunganishwa.  Ukiangalia kwa mtazamo wa toleo la Mungu, vita vya tatu vya dunia havitazuilika, vitatokea.  Hata hivyo, kuna namna mbili za kupigana vita hivyo.

Kwanza dunia ya kishetani inaweza kutiishwa kwa kupigana kijumla kiundani kupitia itikadi.  Mungu hapendelei kuhukumu au kuteketeza {Ezek. 33:14 -16}, bali wokovu.  Hivyo, anapendelea kumshinikiza shetani kujisalimisha kiitikadi, na kwa gharama ndogo ya sadaka ya mambo ya nje.  Kama hili litashindwa, upande wa shetani bila shaka utashambulia upande wa mbingu.  Upande wa mbingu lazima baadae uutokomeze upande wa shetani kwa nguvu.

Namna vita vya pili vitakavyotokea vitategemea jinsi dunia hizi mbili, ambazo zinabeba jukumu katika siku za mwisho, zitakavyotekeleza majukumu yao.Kwa namna yoyote ambayo vita hivi vitapiganwa, lazimakuwepo itikadi muhimu ambayo mtu anaweza kuongozwa kwayo kuelekea dunia adilifu.  Hali iko hivyo, hata kama kujisalimisha kwa dunia ya shetani kutapatikana kwa kupigana vita vya mapambano ki nje kwa kutumia silaha, dunia adilifu itapatikana kwa itikadi ya mtazamo wa hali ya juu, ile ambayo watu wote wanaweza kuifuata kwa uhuru na kwa furaha.

Itikadi ni nguvu inayoendesha ambayo itajenga dunia adilifu ya familia ya mtu.  Hivyo, itikadi inayohitajika lazima iwe itikadi ya upendo wa kweli ambayo inaweza kuvunja vikwazo kati ya makabila, mataifa na kutatua matatizo makubwa miongoni mwa rangi na tamaduni.  Zaidi ya hayo, itikadi hii lazima iwape watu matumaini na uwezekano wa kuhitimisha dunia adilifu.  Lazima iwe ambayo inaleta mwamko wa kiroho na badiliko katika tabia na kuwapa vijana mtazamo chanya {mzuri} juu ya maisha.  Lazima ionyeshe ubatili wa itikadi nyinginezo na hasa ile ya ukomunisti, Umarx – Ulenin, ambao ni hitimisho la mitazamo yote ya maisha aina ya Kaini.

Kama vita vya tatu vya dunia vitaishia katika ushindi upande wa mbingu, sharti la malipizi la ukombozi wa baraka tatu za Mungu litakuwa limetimizwa.  Upande wa mbingu utakuwa katika upeo wa dunia, jaribu la tatu la shetani kwa Yesu, hivyo, kujenga msingi mtimilifu kupitia malipizi kwa ajili ya ukombozi wa mamlaka ya Mungu.

Kama hili litatokea, kazi ya Kristo wakati wa ujio wa pili italeta dunia adilifu ya utawala wa Mungu, na umiliki wa mtu juu ya uumbaji utakuwa umekombolewa kiukamilifu. Dunia hii adilifu ambayo Mungu aliidhamiria wakati wa kuumba, ambayo ameisotea akijaribu kujenga duniani kupitia historia ndefu tangu anguko la mtu, itakuwa ndiyo matokeo. Dunia hii adilifu ndiyo ambayo mtu na Ulimwengu wote hapa na mbinguni kote husujudu Mungu na kuwa na uelewano mzuri kwa kila mmoja. Dunia adilifu kama hii inaitwa Dunia Adilifu ya Itikadi ya Kimbingu na Dunia.

Chapter 15

Homepage

## UJIO WA PILI

Yesu kwa hakika alizungumzia juu ya Ujio wa Pili (Math. 16 : 27). Bado, hakujawa na ufahamu wa uwazi kuhusu Ujio wa Pili. Tunahitaji kujua ni vipi, ni lini, na wapi Ujio wa Pili utajitokeza. Watu wengine wanaamini ya kuwa Ujio waPili utatokana na pale Yesu atakapouingia moyo wa mtu binafsi (Yoh. 14 :20) kupitia kushuka kwa Roho Mtakatifu (Maten. 8 :16,19). Hata hivyo huu si mtazamo wa kikanuni. Tangu kushuka kwa Roho Mtakatifu wakati wa pentekoste (Maten. 2 :4), waumini wengi wampata uzoefu wa uwepo wa Yesu ndani yao. Kama huu ndiyo ulikuwa Ujio wa Pili, basi itatupasa tuseme ya kuwa Ujio wa Pili tayari umekwisha tokea miaka elfu mbili iliopita. Hata hivyo tunajua ya kuwa Ujio wa Pili hauji kwa njia hii kwa sababu wakristu wameendelea kumsubiri Bwana wa Ujio wa Pili hata baada ya kushuka kwa Roho Mtakatifu siku ile ya pentekoste.

Kwa upande mwingine, watu wengine wanaamini ya kuwa Yesu atarudi kiroho. Ukweli mwingine unatuonyesha kuwa haitakuwa hivi. Tangu kufufuka kwa Yesu, kutokea kwa Yesu katika Roho kumewezekana kwa wakati wowote ule, na imetokea mara kwa mara. Bado, wakristu wanasubiri kwa hamu siku ya Ujio wa Pili katika Roho. Yesu mara kwa mara alikutana na mtume Yohana katika Roho, bado Yesu alimwambia hivi, ‘naam ; naja upesi.’ (Ufun. 22 :20)

### 1. Kristu atakuja tena kwa namna ipi ?

***A. Mafundisho chini ya msingi wa Ujio wa Pili wa Eliya***

Sasa ni jinsi gani Ujio wa Pili wa Kristu utatokea ? katika kufikiria hili, hebu kwanza tuangalie Ujio wa Pili wa Eliya. Ujio wa Pili wa Eliya ni mfano wa wazi ambao Mungu ametupa unaohusiana na jinsi Kristu atakavyokuja tena.

Kupitia kwa nabii Malaki, Mungu aliahidi kumtuma Eliya tena, kabla

ya kuja kwa Masihi (Mal. 4 :5). Hivyo waisrael wa wakati ule ambao walikuwa wakimsubiri Masihi kwa kweli walikuwa wakimsubiri Eliya wa Ujio wa Pili, kwa sababu alikuwa amtangulie Masihi. Kwa sababu Ujio wa Pili wa Eliya ulikuwa ndiyo uwe kurudi kwa Eliya aliyekuwa amepaa kwenda mbinguni, watu waliamini ya kuwa Eliya angeshuka toka mbinguni. Bado Yesu kwa uwazi alitamka ya kuwa Yohana Mbatizaji, aliyezaliwa Duniani, ndiye Eliya (Math. 11 :14,17 :13). Hata hivyo, kwamba Ujio wa Pili wa Eliya ulitokea kupitia kwa Yohana Mbatizaji haina maana kuwa Eliya, yeye mwenyewe alizaliwa tena kama Yohana Mbatizaji. Eliya alikuwa katika Dunia ya kiroho, akimsaidia Yohana Mbatizaji, ambaye alikuwa hapa Duniani, kwa kuwa Yohana alizaliwa akiwa na utume sawa na wa Eliya (Lk. 1 :17). Hivyo, pamoja na kwamba utume ulikuwa ni sawia, haiba yake ilikuwa ni tofauti (mtu mwingine) kupitia somo hili tulilojifunza kutokana na Ujio wa Pili wa Eliya, tunaweza kuelewa kwamba Ujio wa Pili inawezekana ukatokea kwa Bwana kuzaliwa hapa Duniani. Tunaweza pia kuelewa ya kuwa pamoja na kwamba wakati wa Ujio wa Pili, Bwana, kama Masihi, atakuwa na utume sawa na ule wa Yesu, yawezekana asiwe na muonekano kama wa Yesu (Yoh. 14 :16,17 ; 16 :12 ; Ufun. 19 :12 ; 2 :17).

***B. Mafundisho chini ya msingi wa Ujio wa Kwanza***

Katika Agano la Kale, tunapata utabiri wa aina mbili unaogongana unaohusu kuja kwa Masihi. Katika Daniel 7 :13 tunapata utabiri unaotabiri kuwa Bwana atakuja juu ya mawingu : ‘nikaona katika njozi za usiku, na tazama, mmoja aliye mfano wa mwanadamu akaja pamoja na mawingu ya mbingu……..’ hata hivyo nabii Mika alitabiri ya kuwa Masihi angezaliwa katika Bethlehem (Mika 5 :2). Ni upi kati ya tabiri hizi mbili zinazogongana ambao waisrael waliuamini ? kwa kuelewa chagizo la manabii hawa wawili Daniel na Mika kwa waisrael, na kwa kuelewa ya kuwa waisrael walikuwa na imani kubwa katika Mungu, tunaelewa ya kuwa walikuwa wakimsubiri Masihi aje toka mbinguni. Ilikuwa ni kwa sababu hii kwamba hata baada ya usulubisho wa Yesu, kundi la jumuiya isioukubali ukristu likatokea likisema Yesu asingewezekana awe ndiye Masihi kwa sababu alizaliwa katika mwili hapa Duniani. Hili linaweza kueleweka katika onyo la mtume Yohana ‘kwa maana wadanganyifu wengi wametokea Duniani, wasiokiri Yesu Kristu yuaja katika mwili. Huyo ndiye yule

mdanganyifu na mpinga Kristu. Jiangalieni nafsi zenu msiyapoteze mliyoyatenda, bali mpokee thawabu timilifu. (2 Yoh. 7-8)

Kuna watu ambao wanasisitiza kwamba Daniel 7 :13 ni utabiri ambao utatokea katika Ujio wa Pili. Hata hivyo, kutoka aya zifuatazo, tunaweza kuona ya kuwa zama za kale ziishe kwa Ujio wa Yesu : 'kwa maana manabii wote na torati walitabiri mpaka wakati wa Yohana……..' (Math. 11 :13) na kwa maana Kristo ni mwisho wa sheria, ili kila aaminiye ahesabiwe haki. (Warumi. 10 :4). Hali ilikuwa katika namna ambayo, hakuna hata mmoja aliyefikiria Ujiuo wa Pili wa Masihi mpaka pale Yesu mwenyewe, karibu na mwisho wa huduma yake ya kuhubiri, aliposema ya kuwa Bwana atakuja tena. Matokeo yake, hakuna mwisrael katika wakati wa Yesu angefikiria ya kuwa utabiri katika Daniel 7 :13 unahusu Ujio wa Pili. Wangeamini kuwa unamhusu masihi ajaye, na wangetenda kama kwamba tayari umekwisha timia. (kwa maneno mengine, wangemtazama Masihi awasili juu ya mawingu).

Basi kwa nini, katika kumtuma huyu mmoja Masihi, Yesu Mungu akatoa utabiri huu wa Masihi kuja katika mwili ? Yesu alisema 'wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani mwana wa Adam.' (Yoh. 3 :13), akionyesha kwamba alishuka toka mbinguni. Bado, kama tujuavyo vyema, Yesu alizaliwa hapa Duniani kutoka kwa mamaye Maria. Kwa nini basi, alikuja toka mbinguni ?
Neno mbinguni limetumika mara kwa mara katika Biblia. Limetumika mara kwa mara kama fumbo la kuelezea ukuu wa thamani iliyomo, utukufu, au wema. Hivyo, tunaweza kutafsiri yale aliyoyasema Yesu kumaanisha nilizaliwa kama ninyi nyote, lakini niko tofauti sana katika msukumo na asili ya kuzaliwa kwangu ; nimezaliwa kwa njia ya Mungu. Kwa ufahamu huu wa neno 'mbinguni', utabiri wa kwamba Yesu anakuja juu ya mawingu hauna makosa. Hata hivyo, ni kosa kuutafsiri kama ulivyoandikwa.

Kwa njia hiyo hiyo, Yohana Mbatizaji, ambaye alizaliwa katika familia ya Zakaria kulingana na toleo maalum la Mungu, hakuzaliwa tu kutokana na desturi ya hapa Duniani, bali alikuwa na utume mkuu (Lk. 1 :15-17, 76). Bila kujali namna ya kuzaliwa kwake, Mungu ndiye mhusika moja kwa moja, chanzo, na kwa jinsi hii Yohana

alishuka hapa chini toka mbinguni, akimwakilisha Eliya, na alikuwa na utume kama wa Eliya.

Ujio wa Pili wa Masihi unatokea kupitia kuzaliwa kwake hapa Duniani. Kutokana na kile kilichoonyeshwa katika mfano wa Ujio wa Pili wa Eliya na Ujio wa Yesu, ambao wote ulikuwa ni kazi ya moja kwa moja ya Mungu, huwezi kujizuia bali utafikiria juu ya utabiri kwa ajili ya Ujio wa Pili.

Kwa kuchanganua, Agano Jipya sio tu lina utabiri usemao Kristu atakuja kama mhukumu kati ya utukufu juu ya wingu kutoka mbinguni, bali pia mwingine usemao atakuja tena kama alivyokuja mara ya kwanza, kinyume kabisa na aina ile ya utabiri mwingine wa yeye kuja juu ya mawingu.

Tunasoma katika Luka. 17 :24,25 ya kuwa Yesu, akitambua kile kitakachotokea  wakati wa Ujio wa Pili, alisema, 'hivi ndivyo mwana wa Adam atakavyokuwa katika siku zake. Lakini kwanza lazima ateseke kwa mambo mengi na akataliwe na kizazi hiki. Kama Bwana atakuja tena katikati ya nguvu na utukufu, na tarumbeta zikiita kutoka kwa Malaika Mkuu, nani atathubutu kumkataa na kumshutumu ?

Leo, wakristu wenye imani wengi na makanisa wanaangalia juu angani, wakilsubiri Bwana aje juu ya mawingu, kusingekuwa na sababu ya yeye kushutumiwa. Hata hivyo, kama haji juu ya mwingu kama ilivyoandikwa, na badala yake akaja katika mwili, kama ilivyokuwa wakati wa Ujio wa Kwanza, basi inakuwa wazi kwa nini Yesu alisema angeteseka kwanza kabla ya kutambuliwa mwishoni (Luk. 17 :24,25).

Ufunuo 12 :5 anasema, ……..naye akazaa mtoto mwanaume, yeye atakayewachunga mataifa yote kwa fimbo ya chuma, lakini mtoto wake akanyakuliwa hata kwa Mungu, na kwa kiti chake cha enzi. Mtu atakayeitawala Dunia kwa fimbo ya chuma ni Bwana ajaye. Katika aya hii, inasema ya kuwa atazaliwa kutoka kwa mwanamke. Wakati mafarisayo walipotaka kufahamu muda wa Ujio wa Pili, walimuuliza Yesu ni lini Ufalme wa Mungu utakuja, naye akawajibu, '…….Ufalme wa Mungu hauji kwa kuuchunguza……..', (Lk. 17 :20). Kila mmoja anaweza kuangaza juu mbinguni, lakini Yesu alisema ya kuwa Ujio wa Ufalme wa Mungu, kwa maneno mengine, Ujio wa Pili hautakuwa wa kuonekana. Kwa nini iwe hivyo ? Ni kwa sababu

Masihi haji juu ya wingu kama ilivyoandikwa. Katika Lk. 18 :8, Yesu alisema nawaambia atawapatia haki upesi. Pamoja na hayo, mwana wa Adamu ajapo, ataipata imani Duniani ? 'Yesu alikuwa anatabiri kuwa hataikuta imani Duniani katika Ujio wake wa Pili. Hii ina maana kwamba wakati atakapokuja, hakutakuwepo hata mmoja kabisa ambaye ataokolewa kwa imani yao timilifu. Kwa nini hili liwe hivi ?

Bila shaka, sio waumini wote Duniani wana imani kamilifu, lakini kuna watu Duniani kote ambao wanafuata njia ya imani ya kweli. Basi kwa nini Yesu, akatamka ya kuwa asingekuta imani ? zaidi ya hayo, ni nani ambaye atashindwa kumtambua Bwana ajaye juu ya wingu lionekanalo ?  kwa kweli, hata wasioamini wangemtambua na kuwa na imani kwake. Je, watu watakosa imani, kwa kuwa kutakuwepo mtu wa kuwazuia kwa kweli sio hivyo. Matatizo siyo lazima yaathiri imani ya mtu. Tunatafsiri kusema kwa Yesu kwamba asingekuta imani Duniani kumaanisha kuwa atakuja kwa namna ile kama ya Ujio wa Kwanza.

Yesu alipokuja miaka elfu mbili iliyopita, kulikuwa na imani kubwa ya aina fulani, miongoni mwa watu. Wengine walisali mchana na usiku katika hekalu, na walishika amri za Mungu. Walijitahidi kushika amri na sheria zote ambazo Mungu aliwaamuru kuzizingatia. Walitoa sehemu ya kumi ya mapato yao kwa uaminifu, na walifunga. Katika hali hii, walikuwa na imani kubwa kwa Mungu, bado hapakuwepo imani ya kweli. Kwa nini hawakuwa na imani ambayo ingewawezesha kumwamini Yesu kama Masihi aliyetumwa na Mungu ?

Kutokana na mtazamo huu, Yesu hakuweza kukuta imani yeyote Duniani ! vilevile, leo kuna mamilioni ya wakristu wema wakimsubiri Bwana atokeze juu ya mawingu ; lakinikama atakuja kama alivyokuja mara ya kwanza, je, ataikuta imani itakayowawezesha  wakristu kumtambua ? kwa kusisitiza kwa mara nyingine tena, chini ya msingi vyanzo vya aya katika Biblia vilivyonukuliwa hapo juu na juu ya masomo tuliojifunza kutokana na kazi ya Mungu katika historia, Ujio wa Pili utatokea kama ulivyotokea mara ya kwanza, kwa Masihi kuzaliwa katika mwili hapa Duniani. Kama ilivyo ada, anakuja kama mwana wa Adam.

***C. Mtazamo wa kikanuni.***

Kulingana na 'kanuni za uumbaji', dhumuni la Mungu katika

kumuumba Adam na Hawa lilikuwa lihitimishwe kupitia kukamilisha kwao Baraka tatu hapa Duniani. Katika maneno mengine, walipaswa kujikamilisha wao wenyewe kama watu binafsi wenye uadilifu, wawe wazazi wa kweli, ambao ndiyo kiini cha familia adilifu, na kujenga Ufalme wa Mbinguni hapa Duniani. Halafu, kama wawakilishi wa Mungu, walikuwa wautawale uumbaji katika upendo. Hata hivyo, kwa sababu walianguka, hawakuweza kuwa wazazi wa kweli na wakaumba Dunia ya uovu.

Yesu ambaye alikuja kama Adam wa Pili (1 Wakor. 15 :45) ilikuwa aibadilishe Dunia hii, iwe Dunia adilifu ambayo ilikuwa imepangwa wakati wa uumbaji (Math. 4 :17). Kwa kuwa Baraka tatu za Mungu mpaka sasa hazijakamilishwa bado, hata baada ya toleo la wokovu kupitia usulubisho wa Yesu na ufufuo, Masihi, Adam wa tatu asiye na dhambi, lazima aje kukamilisha dhumuni la Mungu kwa ajili ya uumbaji.

Masihi lazima azaliwe juu ya nchi kama uthibitisho wa kiumbe mwenye mwili, kwa kuwa lazima awe mfano wa mtu wa uadilifu, mtu ambaye amekamilisha tabia yake, na kwa hivyo, ambaye amekamilisha Baraka ya kwanza. Anaweza tu kutekeleza jukumu hili katika mwili. Lazima pia ajenge familia adilifu ambayo Mungu anaitaka, na kwa jinsi hii aweze kuwa mzazi wa kweli, mmoja ambaye atakuwa ametimiza Baraka ya pili ya Mungu. Moyo wake wa uzazi utapandikiza moyo wa Mungu na upendo katika mioyo ya wote watakaomfuata na atawasaidia kujikamilisha mwenyewe kwa kuwapa uzaliwa wa pili na kwa kumuonyesha kila mmoja jinsi yeye mwenyewe anavyoweza kutekeleza dhumuni la kweli la maisha. Atakuwa mtu mkamilifu na atakuwa Bwana atawalae Dunia ya kiroho na Dunia ya umbo katika upendo mtimilifu akikamilisha baraka ya tatu ya Mungu. Watu watapandikizwa kwake (War. 11 :17) na kuwa kitu kimoja naye kwa kuamini na kumtumikia. Kwa jinsi hii, Bwana atawaongoza kuwa watu wawezao kudhibiti vitu kupitia upendo, wakitimiza baraka ya tatu ya Mungu. Kwa hiyo, lazima azaliwe katika mwili, hapa Duniani, kama wakati wa Ujio wa Kwanza.

Utume mkuu wa uyahudi haukuwa tu kumpokea Yesu bali pia kumfuata na kumsaidia akamilishe nia yake baada ya kuja. Vivyo hivyo, utume wa ukristu, katika zaida ya kujenga msingi wa upeo wa

Dunia nzima kwa ajili ya Ujio wa Pili, ni kumsaidia Bwana atimize kazi yake atakapokuja.

Ufalme wa Mbinguni hapa Duniani ambao Kristu anakuja kuujenga hautakuwa Ufalme wa Mbinguni katika mauzauza. Ufalme wa Mbinguni hauwezi kutimizwa kwa miujiza ya kimaumbile yasiyo ya kawaida bali tu kwa mtu kutimiza wajibu kutatua matatizo yoyote katika njia ya kweli, kulingana na mwongozo wa Mungu.

Wokovu hauwezi kutokea kwa wale wasioitikia kazi ya Mungu. Hata hivyo, ni matakwa ya Mungu kwamba watu wote waokolewe kwa sababu yeye ni Mungu wa haki na upendo. Kwa kuwa maadili ya Mungu kwa ajili ya uumbaji hayajatimizwa kwa pamoja kutimizwa kwa tabia ya mtu binafsi. Kwa hiyo, Kristu ambaye katika wakati wa Ujio wa Pili atakamilisha kwa utimilifu maadili ya Mungu, hatafungwa na dhehebu lolote lile la kikristu, bali atakuwa zaidi ya madhehebu yote. Atatenda kwa kujenga Dunia moja chini ya Mungu, kuvuka mipaka ya ukabila, utaifa na ubaguzi wa rangi.

***D. Maana ya mawingu.***

Kama Bwana atatokea hapa Duniani katika mwili, basi kuja juu ya mawingu ina maana gani ? ina maanisha nini juu ya mawingu ? mawingu ni maji katika hali ya mvuke. Bila kujali maji ni machafu kiasi gani, yanapobadilika na kuwa mvuke halafu wingu, yanakuwa yametakasika. (yamechujika)

Kulingana na aya katika Ufun. 17 :15, maji yanaashiria anguko au mtu mwenye dhambi. Halafu, mawingu yanathibitisha watu waliofufuka au k uzaliwa mara ya pili kama watakatifu miongoni mwa wenye dhambi. Maelezo kwamba kristu atakuja juu ya mawingu yanamaanisha kuwa atakuja tena miongoni mwa watakatifu ambao Mungu atawaandaa.

Basi, kwa nini Yesu alisema atakuja tena juu ya mawingu ? kwanza ya yote, ilikuwa ni kuwazuia wale wote wasioamini katika Kristu kuwadanganya watu. Mpaka wakati halisi wa ujio wake, ilikuwa bora kuwafanya watu waamini kuwa angekuja juu ya mawingu. Kama ingeelezwa wazi kwamba Kristu angetokea katika mwili Duniani, mtafaruku ambao ungesababishwa na madai ya wapinga kristu wengi ingekuwa vigumu kuuzuia. Hata hivyo, muda utakapowadia, Mungu kwa kweli atatuambia jinsi gani Masihi angekuja (Amosi. 3 :7).

Pili, ilikuwa ni kuwatia nguvu wanafunzi katika maisha yao ya kidini, ambayo yangekuwa ya mlolongo mgumu.  Kwa kweli, Yesu alizungumzia mambo kadha wa kadha juu ya Ujio wa Pili ambayo hayaeleweki kikamilifu. Ufun. 22 :20 anasema, ‘naam naja upesi’. Math. 10 :23, Yesu alisema, ‘ kwa maana ni kweli nawaambia hamtaimaliza miji ya Israel, hata ajapo mwana wa Adam.’ Katika Math. 16 :28, alisema, ‘amin, nawaambieni, pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata watakapomwona mwana wa Adamu akija katika Ufalme wake.’ Katika Yohana 21 :18-22, alizungumzia pia kama kwamba angekuja tena katika kile kipindi cha Yohana. Katika aya hizi zote Yesu alisisitiza ya kuwa Ujio wa Pili utatekelezwa upesi (karibu na wakati wake). Bado, haikutokea hivyo. Basi, kwa nini Yesu alisema ingetokea ? Yesu, alikuwa na sababu gani ya kusema vile ?

Yesu aliona kwa mbali shutuma toka kwa himaya ya Roma, hivyo ilimlazimu kuwaelimisha, kuwatia nguvu, na kuwapa matumaini wanafunzi wake katika njia ambayo ukristu ungeweza kusalimika katika kipindi chote cha shutuma za kuhuzunisha na haraka waandae msingi katika upeo wa Dunia nzima kwa ajili ya Ujio wa Pili. Wakristu wa mwanzo waliweza kubaki na shauku na hamasa kwa sababu waliamini kuwa ujio wa Yesu mara ya pili ulikuwa w muhimu na kwamba angekuja kutoka Mbinguni juu ya mawingu katika nguvu na utukufu wa Mungu. Kwa sababu ya imani hii, walipata nguvu za kustahimili mateso na shutuma za himaya ya Roma na kwa jinsi hii waliweza kujenga kanisa la ukristu la awali.

## II. Kristu atakuja tena lini ?

Basi Kristu atakuja tena lini ? katika Math. 24 :36, Yesu alisema, ‘walakini habari ya siku ile na saa ile hakuna aijuaye, hata Malaika walio Mbinguni, wala mwana, ila baba peke yake ; ikionyesha kuwa itakuwa kazi bure  kung’ang’ania kujua juu ya wakati wa kurudi kwake.

Hata hivyo, aya hiyo hiyo katika Math. Inasema kuwa Baba anajua, na Amosi, 3 :7 anasema ‘hakika Bwana Mungu hatafanya neno lolote, bila kuwafunulia watumishi wake manabii siri yake’. Hivyo tunaweza kuelewa kuwa kupitia kwa manabii Mungu kwa kweli lazima atawafahamisha watu juu ya kuja tena Kristu mara ya pili. Mifano

mingi ya Mungu kubashiri yale atakayoyafanya yanaweza kufuatiliwa katika mlolongo wa ukombozi. Mungu alimuasa Nuhu juu ya hukumu ya gharika na Lutu juu ya kuiteketeza Sodoma na Gomora ; na Mungu alifunua juu ya kuzaliwa kwake Masihi mara ya kwanza. Mungu amifunua juu ya kuzaliwa Yesu kwa familia ya Yohana Mbatizaji (Lk. 1 :41-45) ; kwa wachunga kondoo malishoni (Lk. 2 :8-12,15) ; kwa mamajusi kutoka mashariki (Math. 2 :1-12) ; kwa Simeoni (Lk. 2 :26-32) ; kwa Anna (Lk. 2 :38) ; kwa Yusuf (Math. 1 :20-22) ; na kwa wengine. Katika historia ya toleo la Mungu yote, kunaweza kukawa na wakati muhimu zaidi ya ule wa ujio wa Masihi kwa Mungu ? itawezekana vipi Mungu asiwafahamishe watu, wakati ambao mwana wa Mungu mwenyewe, ajapo Duniani kutimiza dhumuni lililopotea la uumbaji ?

Kwa upande mwingine, Yesu pia alisema atakuja kama mwizi (Ufun. 3 :3). Lakini basi, alisema pia hatakuja kama mwizi kwa wale watakaokuwa katika nuru (1Wathes. 5 :4 -6) na kwa wale watakaokuwa macho (1Wathes. 5 :4 –6, Ufun. 3 :3). Hivyo ni wazi kuwa wale waumini ambao siku zote huomba na ambao wako macho na wako katika nuru, Mungu atabashiri kuja kwa Bwana ili kwamba waweze kuandaa kwa ajili yake (Lk. 21 :34,35).

Kwa kuwa toleo la ukombozi la Mungu linahitimishwa kwa kupitia kwa Masihi, Masihi ni tunda la thamani mno la historia yote ya toleo la ukombozi la Mungu. Msingi ulioandaliwa kwa ajili ya Masihi huyu wa thamani, ulikuwa katika imani ya kiyahudi na waisrael, ambao ulianzia katika familia ya Yakobo. Hata hivyo, kama ilivyoelezwa, huko nyuma, watu wa Israel hawakuwa na imani na Yesu, na kwa hivyo Mungu akandaa Israel ya pili yenye mchanganyiko wa watu wa aina zote wale wamwaminio Yesu.

Njia ya toleo la Mungu inayopatikana katika historia ya waisrael lazima pia ipatikane katika historia ya ukristu, kwa sababu Mungu ameuandaa ukristu kuwa Israel ya pili katika upeo wa Dunia nzima badala ya Israel ya kwanza, ambayo ilianza na Yakobo, na historia ya Israel ya pili , ukristu, iliyoanza wakati wa Yesu, lazima zote zifuate mchakato uleule kwa ajili ya kutimiza madhumuni ya maandalizi kwa ajili ya kumpokea Masihi Duniani.

Historia ya Israel na historia ya ukristu zinatofautiana katika makosa na matukio ya kihistoria na mkao wa kijiografia na asili ya utamaduni. Hata hivyo sehemu kuu ya historia ya toleo la Mungu la ukombozi ilipitishwa kutoka moja mpaka nyingine. Kwa kuwa matoleo haya yote yalikuwa yaandae msingi kwa ajili ya Masihi, madhumuni yaliyopelekea kuwepo kwa kila toleo ni mamoja na yaliyo sawa. Tayari tumelinganisha historia hizi mbili kutokana na mtazamo wa toleo la Mungu la ukombozi. Hebu tufikirie wakati wa ujio wa ukristu kuzingatia ulinganifu huo.

Historia ya Israel kutoka kwa Yakobo mpaka kwa Yesu iligawanyika katika sehemu kuu sita ya vipindi vidogo vidogo ; kipindi cha utumwa katika Misri ; kipindi cha majaji ; kipindi cha ufalme ulioungana ; kipindi cha ufalme uliogawanyika wa kaskazini na kusini ; kipindi cha kutekwa kwa wayahudi na kurudi ; na kipindi cha maandalizi kwa ajili ya Masihi. Vipindi hivi sita vidogo vidogo kwa kweli vinajumuisha zama za toleo moja la miaka 1930, kipindi ambacho Mungu alitaka kuhitimisha toleo la ukombozi. Lakini pale ambapo Israel ya kwanza ilishindwa kutimiza wajibu wake kwa kumwamini Masihi, Mungu akawa hana njia nyingine ila kurefusha toleo la ukombozi.

Kipindi kutoka enzi za Yesu mpaka Ujio wa Pili pia kimeganyika katika sehemu kuu sita ya vipindi vidogo vidogo : kipindi cha shutuma katika himaya ya Roma ; kipindi cha makanisa ya kikristo chini ya mfumo wa wazee (kipindi cha wazee) ; kipindi cha ufalme wa kikristu ; kipindi cha falme zilizogawanyika za mashariki na magharibi ; kipindi cha kutekwa Upapa na kurudi ; na kipindi cha maandalizi kwa ajili ya ujio wa Pili. Vipindi hivi vidogo vidogo pia vilijumuisha kipindi cha jumla ya miaka 1930.

Mwaka 1930 sio wakati ambao tunapaswa kusubiria kwa matumaini na mtazamo – tayari umekwisha pita. Basi, kwa nini, sisi tulio hapa Duniani hatujashuhudia hukumu ya mwisho na utukufu wa Ujio wa Pili ? kama Ujio wa Pili unapaswa kutokea hewani, basi utukufu wa Bwana tayari ungekuwa umesambazwa kwa nuru kote Duniani. Hata hivyo kama ilivyokwisha elezwa awali, Bwana hatakuja juu ya mawingu kama tunavyofahamu, Ujio wa Pili utatokea kwa Masihi kuzaliwa katika mwili hapa Duniani. Basi, mwaka 1930 ndio mwaka hasa aliozaliwa Masihi ? mwaka hauwezi kuonyeshwa kwa kuwa

kulikuwa na tofauti ya miaka 10 kwa kipindi chote cha historia ya toleo. Kwa mfano, kipindi cha shutuma katika himaya ya Roma kilikuwa kiwe cha miaka mia nne, lakini kwa kweli, kilidumu kwa miaka iliofikia 392 tu baada ya kufa Kristu. Kipindi cha maandalizi kwa ajili ya Ujio wa Pili kilianza kwa mageuzi katika mwaka 1517 na kikakisha miaka mia nne baadae. Chini ya msingi huu, Ujio wa Pili ulipaswa kutokea mwaka 1917. Kwa jinsi hii kuzaliwa kwa Kristu kungetokea kati ya mwaka 1917 na 1930.

Yesu, alipokuja miaka elfu mbili iliyopita, hakutangaza Umasihi wake kwa haraka na hapo hapo kuanza kuhukumu. Kulikuwa na kipindi ambacho hakikuonekana wala kusikika lakini  imara, cha maandalizi cha maisha yake binafsi, halafu na kipindi cha huduma ya mahubiri kwa watu, kuandaa msingi kwa ajili ya kuhitimisha madhumuni ya Masihi. Wakati wa Ujio wa Pili, Bwana itampasa lazima kupitia mlolongo wa aina hiyo hiyo ya maandalizi baada ya kuzaliwa kwake.kwa kuelewa kile kilichotokea wakati wa toleo kwa ajili ya ukombozi, tunaweza kutambua ya kuwa wakati huu ni kipindi cha maandalizi kwa ajili ya kutokea Bwana.

Tunauita wakati wa Ujio wa Pili wa Kristu siku za mwisho. Tayari imekwisha elezwa katika maelezo ya ‘hitimisho la historia ya mtu (binadamu)’ ya kuwa siku za leo ni siku za mwisho. Vivyo hivyo, inaweza kuzungumziwa kuwa siku za leo ni wakati ambao Kristu anaweza kutokea.

## III Kristu atakuja tena akitokea wapi ?

Basi, kama Kristu kwa mara ingine tena atazaliwa kama mtu katika mwili, lazima atakuwa anakuja akitokea mahali fulani pa pekee katika taifa  pekee. Ni taifa lipi hilo ? miaka elfu mbili katika Yudea, Yesu alisema kuwa angekuja tena, lakini je atarudi tena miongoni mwa watu wa Israel ? katika Math. 21 :33 – 43 katika hadithi ya shamba la mizabibu, Yesu kwa uwazi alionyesha  ya kuwa asingerudi tena katika nchi ya Israel. Katika hadithi hii, Mungu ndiye mmiliki wa shamba la mizabibu, shamba la mizabibu linawakilisha kazi ya Mungu kuhitimisha maadili kwa ajili ya uumbaji, wapangaji ni taifa teule la Israel, watumishi ni manabii, mtoto wa mwenye shamba ni Yesu, na taifa litakalozaa matunda inamaanisha taifa litakalompokea Bwana wakati wa Ujio wa Pili. Yesu alisema hatarudi tena kwa watu

waliomuua. Zaidi ya hayo, alsiema atachukua haki yao ya kuwa taifa teule na kutoa kwa taifa lingine na watu watakaokuwa tayari kuzaa matunda kwa ajili ya Ujio wa Pili.

Basi, tuichukulieje aya inayozungumzia juu ya ujio wa wana wa Israel katika Biblia Ufun. 7 :4 anasema, wakati wa Ujio wa Pili, watu laki 144,000 watatolewa kutoka makabila ya Israel na kupigwa muhuri hii ina maana gani ?
Jina Israel kwa mara ya kwanza  alipokea Yakobo baada ya kumshinda Malaika katika bonde la Yakobo (Mwa. 32 :28) na lina maana ya 'yeye yule aliyeshindana na Mungu.' Kwa maneno mengine, 'Israel ina maana ya watu wa Mungu walioshinda katika imani  na haimaanishi kwa lazima kuwa ina maana ya wazawa wa ukoo wa Yakobo. Hili linatokana na maneno ya Yohana Mbatizaji katika Math. 3 :9……..wala msiwaze mioyoni mwenu kwamba, tunaye baba, ndiye Ibrahim ; kwa maana nawaambia ya kwamba Mungu aweza katika mawe haya kumwinulia Ibrahim watoto. Inatokana pia na maneno ya mtume Paulo aliposema katika Warumi. 9 :6 'maana hawawi wote waisrael walio wa uzao wa Israel.

Basi, ni nani watakuwa wateule wa 'Israel' baada ya kifo cha Yesu msalabani ? ni wakristu wenye imani kubwa waaminio katika Bwana. Warumi. 11 :11 anasema, '…..lakini kwa kosa lao wokovu umewafikilia mataifa, ili wao wenyewe watiwe wivu.' Hii inaonyesha kuwa kitofu cha toleo la Mungu kwa ajili ya ukombozi limehamia mahali pengine mbali na waisrael.

Basi Mungu atashughulikia toleo lake kuu si miongoni mwa wazaliwa wa ukoo wa Ibrahim, bali miongoni mwa wakristu wenye imani kubwa ambao wamerithi imani ya Ibrahim. Lakini kwa uhakika kabisa Bwana atakuja toka nchi gani ?

Alipoulizwa na mwanafunzi wake ni wapi atakakofikia ajapo tena, Yesu alijibu kwa fumbo katika Lk. 17 :37, 'ulipo mzoga, ndipo watakapokutanika tai'. Yesu hakuonyesha wazi ni nchi gani angefikia. Lakini Ufun. 7 :2 – 4 anasema Malaika atapanda kutoka maawio ya jua, katika maneno mengine, kutoka mashariki na atawapiga muhuri watu laki 144,000 elfu  watumishi wa Mungu wateule katika paji la uso la kila mmoja wao. Basi ni nchi ipi yenye kuashiria hili ?

Taifa lile la mashariki ni Korea. Mkulima anapohamisha mti kwa kuupanda tena, kwa uangalifu huchimba shimo na kulimwagia maji kwa ajili ya matayarisho ya kuupanda mti. Mungu angewezaje, anayetazamia tunda la historia ya mwanadamu, kumtuma Masihi bila matayarisho ? kwa matazamio ya msingi aliouandaa Mungu, hebu tufikirie zaidi wazo la kwamba Korea ni nchi ambayo itampokea Bwana.

Kwa yeyote, taifa ambalo Masihi atafikia lazima liwe mtendewa wa moyo wa Mungu. Chini ya msingi wa mtazamo huu, Korea ndiyo nchi ambayo Mungu ameiandaa. Kutoka anguko la mwanaume wa kwanza na mwanamke wa kwanza mpaka hivi leo, Mungu ameishi katika kukata tamaa na amehisi kutokamilika. Mara kwa mara tumemsema Mungu kuwa mwenye utukufu wa hali ya juu kabisa, ambaye yuko mbali sana juu yetu. Lakini hii ni kwa sababu hatuujui moyo wa Mungu ; kwa sababu ya kuanguka Adam na Hawa, ambao walikuwa watoto pekee wa Mungu, Mungu amekuwa akisononeshwa kwa moyo wa mzazi, aliyepotelewa na watoto wake, na amekuwa akihangaika kupitia Dunia ya dhambi ya Jehanam, akiwatafuta, akipania kuwaokoa watoto wake waasi. Kwa hiyo, mtu binafsi, familia au taifa ambaye ama ambayo au ambalo, atapigana, itapigana au litapigana dhidi ya shetani, katika nafasi ya Mungu hawezi, haiwezi au haliwezi kukwepa njia ya machozi na mateso. Watoto wanyenyekevu na wenye imani, watawezaje kuishi katika raha, ambapo watashiriki maombolezo ya moyo wa mzazi wao ? kwa Masihi ndiye abebaye moyo wa huzuni wa Mungu, na ndiye atakayemuondolea Mungu sikitiko, hawezi kuja kwa watu ambao wameridhika kwa mali waliyo nayo. Kwa kuwa taifa linalopaswa kumpokea Masihi lazima liwe mtendewa wa moyo wa Mungu, ndiyo kwamba, kwa kuwa watu wake lazima wawe wana na mabinti ambao wana moyo ufananao na moyo wa Mungu. Taifa lile haliwezi kuepuka njia ya mateso.

Israel ya kwanza na ya pili, zote zililazimika kupitia njia ya mateso na maisha magumu. Kama taifa ambalo litampokea Masihi, Korea pia ililazimika kuenenda katika njia sawa na ile ya kwanza. Kwa jinsi hii, katika historia yake ya hivi karibuni, Korea imebidi kupitia mlolongo wa njia ya mateso mno. Hata wakati ikiendelea kupata mateso na huzuni, Korea imeendelea kwa utii kuendeleza utamaduni mwema wa

kumcha Mungu kwa unyenyekevu na uaminifu. Hata katika kilele cha kuwa na mamlaka yenye nguvu kitaifa, haijawahi hata siku moja kuichokoza au kuanza kulishambulia taifa lingine. Mkakati wa Mungu umekuwa kushinda ushindi baada ya kushambuliwa ; tofauti kabisa na mkakati wa mashambulizi ya shetani. Kudhibiti kwa wakorea nyanja za ukoo, lugha ya kipekee, na utamaduni wa umoja wa kitaifa, na werevu wa utamaduni pekee wao mbali na kuvamiwa mara kwa mara zaidi ya karibu miaka elfu tano ni kumbukumbu ambayo haiwezi kulinganishwa vizuri na historia yeyote Duniani. Hata katikati ya historia yake ya kusikitisha, taifa la Korea liliheshimu haki na amani na lilikuwa likielimishwa ili lipate kuwa mtendewa wa Mungu.

Pili, ni dhahiri kwamba Korea ni taifa lenye matunda ya dini nyingi. Wakorea wana mvuto wa nguvu katika mwelekeo wa maisha ya kidini ; wanamwabudu Mungu na kufuata maisha ya njia ya kiroho. Kwa jinsi hii, mengi ya mafundisho makuu ya kiroho na kijadi, kama vile Ubudha na ukonfusia, umeshamiri katika nchi hii, na ni kutokana na utamaduni huu wa kiroho kwamba utamaduni wa taifa la Korea uliweza kuzaa matunda. Katika kipindi cha karne chache za mwishoni, Ukristu uliwasili na kufaulu kufikia kilele cha juu kabisa katika Ukristu. Dini imeshabihiana vyema na maisha ya kila siku kwa furaha isio kifani. Taifa lifananalo na maelekezo hayo ni vigumu kupatikana popote Duniani.

Bwana haji kuwaokoa wakristu peke yao. Wakati wakristu ni taifa teule katika toleo la Mungu, watu wote wanapaswa kuwa watoto wa Mungu, na Mungu, mwenyewe, ameziunda na kuziongoza dini zote kuu kuelekea katika ukombozi wa watu kulingana na mwelekeo wa majimbo yao, katika kipindi maalum, na kulingana mazingira. Kwa hiyo Masihi, ambaye atahitimisha madhumuni kamili ya toleo la Mungu, lazima kwa wakati mmoja ahitimishe madhumuni ya dini zote nyingine. Katika mwanga huu, taifa litakalostahili kuandaliwa kumpokea Bwana litakuwa taifa ambalo lina matunda ya dini zote kubwa.

Tatu, taifa ambalo kwalo Bwana wetu, atafikia lazima liwe mstari wa mbele katika mapambano ya Mungu na shetani. Mungu alimwambia Adam na Hawa, '…….usile tunda……..kwa kuwa siku utakayokula utakufa'. Katika maneno haya, tunaweza kuelewa kwamba hatua

waliyofikia kuanguka ikawa ndiyo mstari wa kutenganisha kati ya mbingu na nchi, kati ya uzima na kifo, na kati ya mema na mabaya. Kwa hiyo, Bwana lazima afikie katika hatua ya aina hiyo hiyo, ambapo uzima na kifo na mema na mabaya kwa mara ingine tena vinapambana kila kimoja. Halafu, anapaswa kwenda mbele zaidi kuwaondolea kwa uhakika matatizo ya Duniani na kuhitimisha historia ya toleo la Mungu.

Toleo la Mungu kuirudisha kwa kuikomboa Dunia upande wake, iliyoanza na shetani liko chini ya msingi, na linaweza kufupishwa kimaelezo kama utenganisho wa Kaini na Abeli. Utenganisho wa Dunia ya aina ya Kaini na Abeli kabla ya kuja kwa Masihi umethibitika katika Ulimwengu wa kikomunisti na Ulimwengu wa kidemokrasia. Haya ni maendeleo mlalo ya toleo wima ambalo Mungu amekuwa akishughulikia katika historia yote. Kwa hiyo, Bwana atatokea wakati ambapo ukomunisti na demokrasia , nguvu mbili zitakapokuwa zikipambana kati yao, ni kwamba, katika hatua ya njia panda kati ya upendo wa Mungu na chuki ya shetani. Mstari huo wa mapambano ni makubaliano yanayofahamika kama mstari sambamba wa 38 katika penisula ya Korea. Mstari sambamba wa 38 Korea una maana hiyo katika toleo la Mungu kwa ajili ya ukombozi. Sio tu mstari wa mbele wa demokrasia na ukomunisti ; pia ni mstari wa mbele wa Mungu na shetani.

Mungu anaposhughulika kuhitimisha nia yake, shetani hushughulika kupinga na kuzuia kazi ya Mungu. Kwa jinsi hii, mstari wa mbele wa Mungu unakuwa mstari wa mbele wa shetani. Katika jitihada zote za Mungu, shetani atapinga zaidi maandalizi ya taifa litakalompokea Masihi.

Kwa kuwa chembechembe kiini katika mchakato wa ukombozi ni dini, katika upeo wa Dunia nzima wa toleo la ukombozi, Mungu anashughulika kufanya maandalizi ya kumpokea Masihi kwa kuzingatia matunda ya dini za Duniani, na shetani hushughulika kuzivunja dini zote.

Katika kuiandaa Korea kwa ajili ya Masihi, Mungu alitafuta kukuza dini kote nchini Korea – shetani alitaka kuzipukutisha zote kabisa. Kwa jinsi hii, vita iliyozuka Korea kwa kuzingatia mstari sambamba wa 38, na matokeo ya kugawanyika kwa Korea, hayakuwa tu matokeo ya mgongano wa kiraia katika taifa kugombea mipaka ya

kutenganishwa. Yalikuwa ni mapambano kati ya kundi la ukomunisti na kundi la demokrasia na zaidi ya hayo, kati ya Mungu na shetani. Ukweli kwamba mataifa mengi (16) hayakujihusisha na ugomvi huo mara moja hata hivyo yalishiriki na kusaidia toleo kwa ajili ya ukombozi yana uthibitisho wa kiroho.

Nne, taifa ambalo Bwana atafikia lazima lijenge msingi wa kitaifa kwa ajili ya toleo la ukombozi. Ili Korea liwe taifa litakalompokea Masihi, lilipaswa kujenga msingi wa kitaifa wa kujitenga na shetani, kama vile ilivyokuwa kwa waisrael na wakristu wa awali – walivyofanya. Waisrael walipaswa kutekeleza sharti la kujitenga na shetani kwa mateso ya muda wa miaka mia nne katika Misri, ambayo iluwakilisha Ulimwengu wa kishetani. Israel ya pili ilitimiza sharti la kujitenga na shetani kwa kuvumilia shutuma kwa takriban karne nne chini ya himaya ya Roma, ambayo pia iliwakilisha Dunia ya kishetani. Kwa hiyo, wakati wa Ujio wa Pili, ili kujitenga na shetani, Korea pia ililazimika kuvumilia mateso mikononi mwa taifa ambalo liko upande wa shetani. Katika hoja hii, taifa lililokuwa upande wa shetani ni Japan, na kwa miaka arobaini lilileta mateso yasiofikirika juu ya Korea. Kwa kisingizio cha makubaliano ya EULSA PROTECTION TREATY, Japan kwa kulazimisha iliidhulumu Korea haki zake za kidiplomasia na utaifa wao kutoka mwaka 1905 mpaka 1945, Japan iliposhindwa katika vita vya pili vya Dunia.

Katika kipindi hiki, wakorea walinyimwa uhuru wao kabisa na Japan, na idadi isiyohesabika walitiwa gerezani na kuchinjwa na kupata mateso ya aina mbalimbali makali mno. Kuanzia katika mwaka 1910, Japan ilipotwaa Korea, shutuma za ukristu, ambazo ndizo zilikuwa msingi wa jumuiya ya uhuru wa Korea, hazikuwa na mfano kwa ukatili wake. Ukiwa chini ya toleo la Mungu ukristu ulikuwa ukifurahia uhuru wake kote Ulimwenguni, taifa la Korea, na wakristu wake wakiwa mstari wa mbele, waliteseka mno, na kwa jinsi hii walilipa malipizi ya kitaifa yaliowapa sifa ya kuwa taifa litakalompokea Masihi.

Tano, taifa hili lazima liwe na historia ya utabiri husika. Mungu atakapomtuma mwanaye mpendwa, atawezaje kufanya hivyo kimya kimya ? kwa hakika atawafunulia wale wote Duniani ambao wamejiandaa kiroho ; hakika atawapa habari njema na atawafanya wajiandae kumpokea Masihi. Kama vile waisrael walivyotambua

kupitia kwa manabii ya kuwa Masihi yuaja kama mfalme na kuwaokoa, watu wa Korea wamekuwa wakimsubiri mfalme mwenye haki. Kwa muda wa miaka mia tano, Korea pia imekuwa na matazamio ya nguvu ya kimasihi kama matokeo ya Chung – Gam – Nok, ambacho ni kitabu cha utabiri. Ni tabia ya kawaida tu kwa watu wa Korea kuwa na mawazo haya ya kipekee ya kumtazamia Masihi hata kabla ya kupokea mafao ya nyakati katika toleo la wokovu la Mungu kupitia kwa Yesu. Wengi walio na kipaji cha roho miongoni mwa watumishi wa Mungu na watu wa kawaida wamepata ufunuo wa kipekee unaohusu Ujio wa Pili wa Bwana katika nchi ya Korea ; na wengine wengi wenye hisia nzito za kidini wamepata ufunuo huo wa kwamba Korea itakuwa kituo cha wokovu Duniani.

Kukamilika kwa toleo la ukombozi la Mungu kumelenga kimsingi katika kumkomboa mtu na kwa upana zaidi kumelenga katika kuyakomboa mazingira ya Ufalme wa Mbinguni. Mungu ameshughulika ndani ya dini ili kumkomboa mtu ; Mungu ameuendeleza ustaarabu ili kuyakomboa mazingira ya Ufalme wa Mbinguni. Ameshughulikia kuwepo kwa utamaduni wenye maadili halisi na ustaarbu kwa ajili ya Ujio wa Pili. Ujio wa Pili utaleta muungano kati ya dini na sayansi, kati ya mambo ya kiroho na mambo ya ustaarabu katika maumbile, na kati ya mashariki na magharibi. Yote yataungana kwa furaha, yakizaa utamaduni mpya wa U – mungu. Peninsula ya Korea ilikuwa ni sehemu iliyojificha ya mashariki ya mbali kwa muda mrefu ; hata hivyo, utamaduni wa magharibi ukaja mashariki na mwisho ukafika Korea.

Mungu amewafundisha wakorea kwa muda wa miaka elfu tano kuwa na imani nzito na upendo, na katika msingi huo ukristu ukapokelewa. Mungu alipotuma ukristu kwa watu wa Korea, alifanya maandalizi yake ya mwisho kwa ajili yao ili waweze kumpokea Bwana wa Ujio wa Pili, na akaifanya Korea kuwa mwakilishi wa ukristu Duniani. Pamoja na kwamba Korea ni taifa dogo, imejihusisha mara kwa mara kwa uthabiti katika historia ya kisasa, kama kwamba yenyewe ndiyo kiini cha mwenendo kiongozi wa siasa ya kimataifa.

**Zama za Yesu na zama za sasa kwa mtazamo wa utambuzi wa nyakati .**

Zama za Yesu na wakati wa Ujio wa Pili ni vipindi vya toleo la utambuzi wa nyakati. Hivyo, toleo la Ujio wa Pili la Mungu, ambalo lipo chini ya ukristu, linafanana na lile la nyakati za Yesu.
Kwanza, hebu tuziangalie hizo nyakati mbili kwa mtazamo wa taifa teule (kiongozi) kwa ajili ya toleo. Mpango wa Mungu ulikuwa kupanua toleo lake kutoka kwa Yesu mpaka kufikia taifa la Israel, kutoka Israel mpaka Roma, na kutoka Roma kufikia kote Ulimwenguni.
Kwa kutambua kuwa dini kiongozi wakati wa Ujio wa Pili ni ukristu, na ya kuwa Israel ni Korea, basi taifa gani litakuwa katika nafasi ya Roma ? Roma ya leo ni taifa ambalo Mungu ameliandaa kuwa taifa kiongozi Duniani, chini ya ukristu. Kwa zaidi ya miaka mia mbili, Amerika imeandaliwa na Mungu kukamilisha madhumuni ya Ujio wa Pili. Vilevile, uhusiano kati ya Korea na Amerika katika nyakati za zetu ni sawa na uhusiano kati ya Roma na Israel nyakati za Yesu.

Pili, hebu tulinganishe ukristu wa leo na uyahudi wa nyakati za Yesu. Wakati wa Yesu, uyahudi katika Israel ulishirikishwa kwenye mamlaka ya makuhani na kwenye miiko ya Hekalu ; maisha yao ya kiroho yalirubuniwa. Viongozi wa dini ya kiyahudi walisahau utamaduni wa unyenyekevu ambao ulipita toka kwa Ibrahim mpaka kwa yakobo na Musa na manabii. Badala yake, uhusiano wao na Mungu ukawa wa kawaida tu, na kama matokeo ya hilo, Yesu aliwakosoa juu ya tabia yao ya kuwa na imani bila matendo mara nyingi (Math. 23 :1-39).

Leo, ukristu lazima utubu ya kwamba umepoteza lengo na sasa imekuwa ni mazoea tu. Tunapofikiria shauku na imani waliyokuwa nayo wakristu wa kanisa la awali, tunasema ya kuwa kanisa la leo limekuwa la mazoea zaidi kuliko na limeacha kwa ukubwa mno madhumuni ya awali ya imani. Watu wengi hujifikiria ya kuwa ni wakristu, lakini kwa kweli wanaishi maisha ambayo yako mbali na mafundisho ya Yesu.

Kama vile Yesu alivyomwaga nguvu zake zote kufanya mageuzi katika uyahudi uliorubuniwa katika nyakati zake, katika nyakati za Ujio wa Pili, atafanya mageuzi ya kimsingi katika ukristu pia ili kufanya kanisa la kweli linalomuabudu Mungu na atawatia nguvu wakristu pia kuwa watu watakaotekeleza matakwa ya Mungu na mafundisho ya Yesu.

Wakati wa Yesu, uyahudi haukuitambua thamani ya kweli ya Yesu ; viongozi wa kiyahudi waliyapa mgongo matakwa ya Mungu na mageuzi ambayo Yesu alikuwa akifundisha na wakamshutumu. Vivyo hivyo, nyakati za Ujio wa Pili, mafundisho mapya na shughuli za kimageuzi za Kristu zitapingwa na waumini ambao watakataa kufanya juhudi ya mageuzi ya ukristu, na kwa kanisa ambalo limefunganishwa kwenye utamaduni wa mamlaka yake na miiko.

Wakati wa Yesu, maneno ya Masihi hayakupokelewa na viongozi wa kiyahudi. Bali, yalipokelewa na wayahudi wa daraja la chini na mataifa waliokuwa na kiu ya maisha ya kiroho, au waliosumbuliwa na kujishuku juu ya uovu wao. Hivyo hivyo, wakati wa Ujio wa Pili, watu wa chini, ambao wanajaribu kwa bidii kuishi kwa kuzingatia neno la Mungu, au hata wasio wakristu, wanaweza kuwa wa kwanza kuyapokea mafundisho ya Kristu, kuliko viongozi wa kikritsu. Hii ndiyo sababu Yesu, kwa huzuni, alisema ya kuwa wale watakaofurahia tafrija ya ndoa ambayo ataiandaa wanaweza wakawa sio waalikwa, bali wale walioitwa ghafla kutoka mitaani (Math. 22 :8 – 10).

Watu wa nyakati za Yesu walizaliwa kuishi maisha ya uthibitisho wa toleo, kwa kuwa wangepaswa kumtumikia Masihi na kumsaidia kukamilisha matakwa yake. Hawakuwa watu binafsi wa kawaida tu, bali walikuwa na majukumu ya kihistoria ya kuishi katika kipindi muhimu katika historia ya toleo. Vivyo hivyo, watu wote leo, na hasa wakristu, wana jukumu la kumtumikia Bwana na kuanzisha Dunia ambayo itatambua maadili kwa ajili ya uumbaji. Tunaishi katika hatua ambayo katika nyakati haifanani na yoyote tangu mwanzo wa historia.

Wakati wa Ujio wa Pili, Kristu atatangaza matakwa ya Mungu, ambayo lazima yakamilishwe, Duniani, na atawaelimisha watu kuyatekeleza. Watu wa kweli wa imani wanapaswa kumtafuta na kumtumikia ; na kufuata matakwa ya Mungu, ambayo yatafunuliwa kupitia kwake. Katika Math. 2 :3 Biblia inasema ya kuwa baada ya kusikia habari za kuzaliwa kwa Masihi, Yerusalem yote ilifadhaika. Hata hivyo, kulikuwepo yeyote aliyemjali Yesu akiwa mtoto, au mbele za uuma akamuunga mkono baada ya kuanza kazi ya utume wake ?

Hebu tusikilize kwa unyenyekevu sauti itokayo ndani ya akili yetu asilia na tutafute kutangazwa kwa Masihi. Hebu tutulize akili yetu na tutege masikio kwenye habari za kutupa matumaini ambazo zitatangaza zama mpya.